

# Agape

## Ufunuo wa Tabia ya upendo ya Baba

Adrian Ebens

# Agape

*Ufunuo wa Tabia ya Baba ya Upendo*

Ari kwa wazee wenzangu,
Ndugu wa thamani katika njia nyembamba: Craig Jacobson,
Eddie Perez, Craig Jones, Colin Nicolson, na Gavin Devlin.

Shukurani za kipekee kwa mke wangu Lorelle, Danutasn
Brown, Tony na Anna Pace, Gary Hullquist, na Frank Klin.

MARANATHA
MEDIA

Kwa ujumbe zaidi:
fatheroflove.info
adrian@life-matters.org

Copyright © Adrian Ebens, 2019
ISBN: 978-0-6482290-4-9

# Yaliyomo

Utangulizi ............ 3
1. Ufunuo wa Baba ............ 6
2. Unasoma kwa jinsi gani? ............ 12
3. Kifo cha Msalaba ............ 21
4. Mwanangu Mpendwa ............ 30
5. Wapende Adui zako ............ 36
6. Moto kutoka Mbinguni ............ 43
7. Usiufanye Moyo Wako kuwa Mgumu ............ 53
8. Mbona Kuwaamuru Wadhambi wa Kupiga Mawe? ............ 64
9. Sheria kama Kioo ............ 75
10. Kutia Hofu ya Mungu ndani yako ............ 86
11. Hasira ya Bwana ............ 94
12. Kuweka Upanga Pahali pake ............ 104
13. Taji la Miiba ............ 118
14. Nguvu za Mauti ............ 129
15. Amri za Baba Yangu ............ 140
16. Tajiri na Lazaro Kwenye Kioo ............ 153
17. Malaika Wanao Piga Sana ............ 165
18. Kauli Wazi ............ 181
19. Alijeruhiwa kwa Makosa Yetu ............ 190
20. Nyoka Aliyewekwa Wazi Kwa Msalaba ............ 205
21. Agano la Milele na Utumishi wa Kifo ............ 230
22. Musa Mtu Mnyenyekevu Sana ............ 246
23. Eliya na Mpaka wa Mwisho ............ 265
24. Ibrahimu na Chukizo la Ukiwa ............ 281

# Utangulizi

Ni swala ambalo limefanyiwa utafiti wa kina kwamba watoto hutwaa mambo mengi, kama sio yote, katika sifa za wazazi wao. Kupitia kwa kutazama na kutagusana sifa na tabia za baba na mama, chanya au hasi, huakisiwa kwa maisha ya mtoto. Ni sheria ya urithi.

Ulimwengu umejaa vurugu na ukatili licha ya kuwa kuna wito mwingi wa kudumisha usalama. Roho ya uchokozi kuelekeza vitisho, halisi au hata kukisiwa, mara nyingi hupelekea mchakato wa kujikinga dhidi ya uharibifu wa maisha ya binadamu.

Ndani ya roho zetu kila mtu ana hamu ya amani, utulivu na kuhakikishwa kuwa anapendwa. Je, wanadamu watasongea vipi karibu na jambo hili bora? Pamoja na uvumbuzi wetu katika teknolojia ulimwengu unazidi zaidi na zaidi katika ubinafsi na ukatili.

Maisha ya kristo aliye tembea katika dunia miaka 2000 iliyopita yanatupa mfano wa kujikana nafsi, upendo wa kudumu unaoleta amani kwa mamilioni wasiyoweza kuhesabika. Kwa watu wengi, mfano wa maisha haya ya kupendeza huangamizwa na hata kuharibiwa na na hadithi nyingi zilizonakiliwa kwenye kurasa za Bibilia zikieleza kwa kina mwingiliano wa Mungu na mwanadamu katika historia yote ya binadamu.

Mungu wakati mwingine huonekana kuwa katili sana na kuua halaiki akiamuru sio tu kifo cha majeshi ya adui bali pia watoto wao wachanga. Bibilia inaonyesha utaratibu wa kuogofya kuwa amekasirika na amejawa na ghadhabu. Zaidi ya hili kifo cha msalaba ni kwa wengi waliochafuliwa na mawazo kuwa Mungu huhitaji kifo cha wale wanaomuasi.

Mitazamo hii ya Mungu ni maarufu katika dini nyingi za ulimwengu ikiwemo ya ukanaji wa Mungu, ambao sana umezuka karibuni katika mapinduzi ya Ufaransa yalisakifu kupitia kwa uchinjaji wa maelfu ya watu.

Kwa wale ambao wanamvuto katika neno la Mungu, tofauti kati ya maelezo ya Mungu katika Bibilia na maisha ya Kristo imeleta baadhi ya madai ya Kristo kuwa magumu zaidi kutatua. Ila katika kipindi fulani akizungumza na mmoja wa wafuasi wake Yesu alisema, “iwapo umeniona umemwona Baba.”

Hili linawezekanaje? Inaweza kuwa ukweli kuwa Mungu kwa kweli ni mwengi wa rehema, neema na mkarimu kama anavyoonyeshwa katika maisha ya Yesu? Katika moyo wa sheria ya Mungu anasema “usiue.” Hili ni onesho la tabia ya Mungu? Ama ni kesi ya kanuni fulani kwa mpangilio wa chini wa viumbe na mkusanyiko mwingine tofauti kabisa wa wale walio kwenye uongozi, yaani Mungu? Ni athari gani hili linao juu ya viongozi wanaoweza kujipanga katika mfano kama huo? Linaweza watoa viongozi wanaotenda kwa njia sawa na hii wakiingia uongozini?

Katika tambo hili inapatikana hatima ya utafiti wa miaka kumi na sita kwa mwanga wa swali hili. Safari ilianza nilipokuwa nikinong’oneza kuhusu kuzaliwa kwa kifungua mimba wangu. Nilifikiria juu ya wakati nilimshika mikononi mwangu mara ya kwanza na kina cha hisia za upendo niliohisi kwake. Kuwa na ladha kama hiyo ya hisia za kiungu kulinileta katika kukutana na Mungu  kuliko athiri kwangu fikira kuwa hisia niliyokuwa nayo kwa mwanangu ilikuwa onyesho la upendo wa Mungu kwa Mwanawe, na hivyo upendo wake kwa wanawe wote wazaliwao duniani.

Safari imekuwa ndefu na wakati mwingine ya kuchosha.  Bibilia kwa mara nyingine ilionekana ikifanya kuwa haiwezekani kupatanisha utata dhahiri iliyoweka mbele zangu.

Nashiriki nanyi hapa hitimisho ya utafiti huu.  Kupitia kwao nimefika inchi kadha kukutana na watafiti wengine juu ya jitihada sawa, na ni mbaraka gani umekuwa kwetu sote.

Nashuhudia kwako kweli Mungu ukweli ni upendo. Sio mtu wa vurugu. Hatutishi na tishio la kukaanga  watoto wake wanaoenda kinyume naye katika kuzimu kwa milele kama mamilioni wanavyoamini.

Nagundua kuwa wengi hawajaamini, lakini nakukaribisha uchukue safari hii na ujionee mwenyewe na ugundue ukweli kuwa Mungu ni upendo.

# 1. Ufunuo wa Baba

*Mungu ni upendo* ni maneno yaliyoandikwa na Yohana baada ya uhusiano wa karibu na Yesu alipokuwa akihudumu hapa ulimwenguni. 1 John 4:16. Yohana alipoketi juu ya kilima akisikiza jinsi alivyohubiri, alipomtazama akiyafungua macho ya kipofu, alivyowakemea watenda dhambi kwa machozi machoni mwake, Yohana aliifahamu huduma ya kweli ya Yesu.

> Hakuna mtu ye yote aliyemwona Mungu wakati wo wote, ila ni Mungu Mwana pekee, aliye kifuani mwa Baba ndiye ambaye amemdhihirisha. Yohana 1:18

Sura ya Mungu kama inavyofunuliwa katika maisha ya Yesu ilijitokeza kwa namna tofauti kabisa na vile binadamu alikuwa amemuelewa Mungu kuwa hapo awali. Yesu na wanafunzi wake walipokuwa wakipita karibu na mtu kipofu wakamuuliza:

> …Rabi, ni nani aliyetenda dhambi, ni huyu mtu au wazazi wake hata azaliwe kipofu?" Yohana 9:2

Swali lao lilidhihirisha kwamba binadamu walimjua Mungu kama dikteta katili anayetoa adhabu kwa wasio mtii. Kuinuka na kuanguka kwa falme za kilimwengu hadi wakati wa kristo kulighushiwa kupitia umwagikaji wa damu na kuongoza kwa nguvu za chuma, kuonyesha mtazamo wa binadamu wa tabia za Mungu kama asiyekuwa na huruma na mwenye kulipiza kisasi.

Kulikuwa na shahidi aliyetangaza ujumbe tofauti. Uzuri wa maumbile umahiri wa vazi la maua na harufa nzuri, ndege walioijaza anga na nyimbo zao tamu, na miti mikuu ya kijani hai vyote vilishuhudia kweli Mungu ni muumbaji wa ajabu na Baba mwenye upendo. Bidii na ari ya pendo la wazazi kwa wanao, kujali kwa ukaribu na kifungo cha mume kwa mkewe pia kunatangaza moyo tefu wa Muumbaji.

Miaka elfu moja na mia tano iloyopita Musa, akitaka kutaka kumjua muumbaji wake, alimwagiza Mungu kudhihirisha utukufu wake.

> Bwana akashuka ndani ya lile wingu, akasimama pamoja naye huko, **akalitangaza jina la Bwana. (**6) Bwana akapita mbele yake, akatangaza, Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli. Kutoka 34:5-6

Licha ya haya na ushahidi mwingine mwingi mtazamo uliotawala ulikuwa kwamba Mungu ni katili na mkali na bila shaka huwaadhibu wale wanao mkosea.

Mbona mtazamo huu ulienea? kwa sababu shetani alikuwa na shuku na upendo wa Mungu tangu mwanzo.

> Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa, (5) kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya. Mwanzo 3:4-5

Shetani aliwafanya Adamu na Hawa kuamini kwamba Mungu hakuwa nao Moyoni. Aliwafanya kuamini kwamba Mungu hawezi kuaminiwa. Kwa kuwaambia kwamba hawatakufa watakapokula tunda, alifungua njia kwa maonyo ya Mungu, yaliyopeanwa kwa upendo, na kueleweka visivyo.

> Walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika. Mwanzo 2:17

Kama kula tunda kutoka kwa mti hakungeleta kifo kwa Adamu na Hawa basi nini kingewaletea kifo? Hitimisho ambalo lingeweza kupatikana ni kuwa ni Mungu pekee, na wakati Adamu aliisikia sauti ya Mungu bustanini tunaona zao la fikara kama hizo.

> Akasema, Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha. Mwanzo 3:10

Mbona Adamu alikuwa akimwogopa Mungu? Ni kwa sababu aliogopa kifo na kwamba Mungu angewaua kwa kutomtii. Ni kutokana na uwoga huu wa kifo kutokana na fikira kuwa Mungu angewaua, shetani aliendelea kuwahifadhi katika utumwa. Lakini Mungu alitaka:

> …kuwaweka huru wale waliokuwa utumwani maisha yao yote kwa sababu ya kuogopa mauti. Waebrania 2:15

Shetani alipendekeza kwa wazazi wetu wa kwanza kuwa Mungu alikuwa muuaji ambaye angewaua walioenenda kinyume naye nakwamba aliwadanganya kwa kuwaambia kuwa wakila matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya watakufa. Lakini hizi zilikuwa sifa za shetani mwenyewe. Katika mazungumzo na mafarisayo, Yesu anaeleza sifa hizi kupitia kwa matendo yao.

> Ninyi ni watoto wa baba yenu Ibilisi, nanyi mnataka kutimiza matakwa ya baba yenu. Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo, wala hakushikana na kweli maana hamna kweli ndani yake. Asemapo uongo husema yaliyo yake mwenyewe kwa maana yeye ni mwongo na baba wa huo uongo. Yohana 8:44

Kupitia kwa maelezo haya, shetani ameuteka ulimwengu; Amewakilisha visivyo tabia ya Mungu ili kuwafarakanisha naye. Mwana wa Mungu alishuka kutoka mbinguni ili kudhihirisha tabia halisi ya Baba yake; Alikuja kuondoa wingu jeusi la wasiwasi na kuonyesha sura halisi ya Baba. Wakati mmoja wanafunzi walitoa ombi, "Tuonyeshe Baba," Yesu akajibu:

> Akamwambia, "Bwana, tuonyeshe Baba yako yatosha." (9) Yesu akamjibu, "Filipo, nimekaa nanyi muda huu wote hata usinijue? Mtu ye yote aliyeniona Mimi, amemwona Baba. Sasa wawezaje kusema, 'Tuonyeshe Baba?' Yohana 14:8-9

Katika kuelezea hudumu yake ya duniani Yesu alisema:

> Roho wa Bwana yu juu Yangu, kwa sababu amenitia mafuta kuwaletea maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao na vipofu kupata kuona tena, kuwaweka huru wanaoonewa Luka 4:18.

Kwa mawazo takatifu tunatazama mjane wa Nain Yesu alipodakiza gari la mazishi na kumfufua kijana wake. Mioyo yetu inaguswa tunapotazama hadithi ya Jairo na faraja iliyochukua nafasi ya uchungu wake Yesu alipomfufua msichana wake. Yesu angepita kijiji kizima na hakuna mgonjwa hata mmoja angesalia. Aliwapa chakula watu 5000 kwenye mlima kutokana na kuwahurumia, na akawambia upendo wa baba kwao.

Uwepo wa Kristo ulikuwa wakukaribisha kiasi kwamba kina mama wangemletea watoto wao ili awabariki. Katika vitendo vyake vyote utukufu wa Baba ulidhihirishwa. Katika kila neno alilolitamka, pande za giza zilizokuwa zimefunga ulimwengu katika utumwa ziliondolewa na nuru ya utukufu wake. Mungu hakutumia nguvu za fikra chanya au jeuri; daima angesema ukweli katika upendo na hakuogopa kuanika uongo na kutoamini. Lakini machozi yalikuwa machoni mwake alipokuwa akiwakemea waliokuwa katika hatia. Aliishi kwa ajili ya wengine na kila nafsi ilikuwa ya thamani kubwa kwake.

Tabia ya Kristo duniani inadhihirisha kwetu tabia ya Mungu. Kristo alisema kwa maana sifanyi kwa ajili Yangu mwenyewe. Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake mwenyewe. 2 Wakorintho 5:19. Tabia zima ya Baba ilidhihirishwa kwa Mwanawe.Yesu duniani alidhihirisha kwa mwanadamu kwa kueleza sura ya Baba.

> Kwa maana sisemi kwa ajili Yangu mwenyewe, bali Baba aliyenituma aliniamuru ni nini cha kusema na jinsi ya kukisema. (50) Nami ninajua amri Zake huongoza hadi kwenye uzima wa milele. Hivyo lo lote nisemalo, ndilo lile Baba aliloniambia niseme" Yohana 12:49-50 (NKJV)

Alipokuwa akiomba kwa bidii kwa baba yake, Yesu aliyasema maneno haya:

> Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma. (4) **Nimekutukuza Wewe duniani** kwa kuitimiza ile kazi uliyonipa niifanye. (5) Hivyo sasa, Baba, unitukuze mbele Zako kwa ule utukufu niliokuwa nao pamoja na Wewe kabla ulimwengu haujakuwako. (6) **"Nimewajulisha Jina Lako wale ulionipa kutoka katika ulimwengu.** Walikuwa Wako, ukanipa Mimi, nao wamelitii Neno Lako. Yohana 17:3-6

Yesu anatwambia kuwa alimtukuza Baba alipokuwa duniani. Utukufu wa Baba ni tabia yake, na hili ndilo Yesu alidhihirisha kwetu katika huduma yake duniani. Anamwambia Babake pia kuwa Amejulisha jina la Baba au tabia kwa wanafunzi waliokuwa naye. Hii ndio sababu mbona Yesu angesema kwa ujasiri kwa Filipo kuwa kama umeniona umemuona Baba. Filipo hakupaswa kushuhudia matendo yote ya Yesu ulimwenguni kote ilikujua jinsi Baba alivyo. Katika kipindi cha miaka mitatu Yesu alituonyesha kwa kila kipengele jinsi Baba alivyo.

Ufunuo mkuu wa upendo huu ulidhihirishwa msalabani.

> Hivi ndivyo Mungu alivyoonyesha upendo Wake kwetu, kwa sababu Mungu alimtuma Mwanawe wa pekee ulimwenguni, ilitupate uzima kwa Yeye. (10) Huu ndio upendo, sikwamba tulimpenda Mungu, bali Yeye alitupenda, akamtuma Mwanawe, ili Yeye awe dhabihu ya kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu. (11) Wapenzi, kama Mungu alitupenda sisi hivi,imetupasa na sisi kupendana. 1 Yohana 4:9-11

Kama Yesu angeangushwa na majaribu ya shetani basi angepotea milele, na jamii yote ya Mwanadamu ingepotea kwa sababu hiyo. Baba wa mbinguni hakumkopa Mwanawe kwa ulimwengu kwa miaka thelathini na mitatu tu, alimtoa kwetu. Kulikuwa na hatari kuwa wote wangepotea, lakini bado Baba kwa upendo wake mkuu kwa ulimwengu alikuwa tayari kumtoa mwanawe wa pekee ili aweze kutukomboa.

> Mungu hakumhurumia Mwanawe, bali alimtoa kwa ajili yetu sote, atakosaje basi kutupatia vitu vyote kwa ukarimu pamoja Naye? Warumi 8:32

Hatari inadhihirishwa katika ombi la Yesu katika bustani. Kulikuwa na wasiwasi kuwa hangevumilia majaribu; lakini bado aliamini mapenzi ya Mungu bila kuzingatia gharama.

> Akaenda mbele kidogo, akaanguka kifudifudi akaomba, akisema, “Baba yangu, kama inawezekana, kikombe hiki na kiniepuke, lakini si kama nitakavyo mimi bali kama utakavyo Wewe.” Mathayo 26:39

Tunawezaje fahamu upana wa upendo huo? Ni maneno gani yanaweza elezea ajabu ya upendo wa Mungu? Adamu hakuwa tayari kukitoa kile

kilichokuwa cha thamani kubwa kwake, lakini Baba alikuwa tayari. Hakumuepusha hata mwanawe.

Yesu kwa upole alipokea kichapo, kejeli na mzaha wa umati uliokuwa unafurahi katika kuteseka kwake. Alijaribu kuubeba msalaba wake kwa uaminifu hadi wakati uzito ulipomzidi. Alimwagiza Yohana kumtunza mamaye alipokuwa msalabani na akamwomba Babake kuwasamehe wale waliokuwa wakimuua.

Ulimwengu haukuwa umeshuhudia upendo wa kushangaza namna hii hapo mwanzo. Tabia ya Baba iliangaza kutoka kwa Mwanawe katika mwanga mtukufu. Kweli Baba huwapenda adui zake na huwasamehe wale ambao wanatafuta kumuangamiza. Haya yote yaliwekwa wazi kwa tabia za Mwana wa Mungu. Kupitia kifo Mwana wa Mungu alidhihirisha muuaji ambaye alikuwa shetani na akadhihirisha matendo ya joka. Msalabani muuaji na aliye uawa walionyeshwa kikamilifu. Roho aliyemshawishi Kaini kumuua Habeli nduguye aliwekwa wazi kwa mwanga mkamilifu msalabani, na mbingu ingeweza kuona kikamilifu kwa mara ya kwanza kile muongo na muuaji ambaye shetani alikuwa. Athari yake mbinguni ilianguka kama umeme, na mahali pake hapakupatikana tena mbinguni katika mioyo ya malaika.

Katika mwanzo wa safari hii tunataka tuwe na uwezo wa kupata miwani nzuri ili tuweze kusoma hadithi za Bibilia. Kwa  mwanga wa msalaba wa Kalvari tabia za Mungu ambazo hutujaza hofu katika Agano la Kale ziliweza kuwa nzuri na za kuvutia zaidi. Upole na upendo wa mzazi unaonekana kushikamana na utakatifu, haki na uweza. kwa kuangaziwa na hadithi kutoka Agano Jipya tunaweza anza kuona ukweli wa matendo ya hukumu katika Agano la Kale. Hiki ni chombo katika msururu huu – kuonyesha kwamba maisha ya Yesu hapa duniani ni sawa leo jana na hata milele na kwamba ndivyo hivyo Baba yetu alivyo.

## 2. Unasoma kwa jinsi gani?

Yesu alikuwa mwalimu wa ajabu sana. Wakati wale maakida waliokuwa wametumwa na wakuu wa kanisa kwenda kumkamata waliulizwa mbona hawakuja naye, waliweza kujibu tu:

> …"Kamwe hajanena mtu ye yote kama Yeye anenavyo." Yohana 7:46

Licha ya ukweli huu Agano Jipya hunakili kwamba watu wengi walikuwa na shida kumuelewa.

Akizungumza na wayahudi kuhusu kifo chake na kufufuka kwake alisema, "Haribu hekalu hili nami nitalisimamisha kwa siku tatu." Walidhani alikuwa anazungumzia Hekalu halisi la Yerusalemu, Lakini alikuwa anazungumzia hekalu la mwili wake wenyewe. Yesu alimwambia Nikodemu kwamba lazima azaliwe tena; Nikodemu alidhani kwamba Yesu alikuwa akizungumzia kuzaliwa kimwili lakini Yesu alikuwa akizungumzia kuzaliwa kiroho. Wakati Yesu alimpa mwanamke maji ya uhai katika kisima alidhani alimaanisha maji ya kimwili ilihali alimaanisha maji ya kiroho. Tena yesu aliwaonya wanafunzi kuhusu chachu ya Mafarisayo; walidhani analizungumzia mkate halisi. Lakini Yesu akawaambia:

> Inakuwaje mnashindwa kuelewa kwamba nilikuwa sisemi nanyi habari za mikate? Jilindeni na chachu ya Mafarisayo na Masadukayo." Mathayo 16:11

Wakati Yesu aliwalisha watu 5000 alianza kwa kuwafunza maana ya muujiza huu ambao aliufanya. Aliwaelezea kwamba mkate ni maisha yake ambayo ulimwengu ulihitajika kuwazia na kufikiria. Aliwaambia:

> Mtu ye yote aulaye mwili wangu na kunywa damu yangu, anao uzima wa milele. Nami nitamfufua siku ya mwisho. Yohana 6:54

Maneno haya yaliwashangaza wasikilizaji wake. Walinung'unika wakisema, "Huu ni msemo mugumu; Nani awezae kuusikia?" Wengi waliokuwa na mvuto katika huduma yake walimgeuka na wakaacha kumfuata tena.

> Alikuwepo ulimwenguni na ingawa ulimwengu uliumbwa kwa Yeye, haukumtambua.(11)Alikuja kwa walio Wake, lakini wao hawakumpokea. Yohana 1:10-11

Mambo haya yote yalikuwa ni utimizaji wa utabiri wa nabii Isaya:

> Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta? Na mkono wa Bwana amefunuliwa nani?(2) Maana alikua mbele zake kama mche mwororo, Na kama mzizi katika nchi kavu; Yeye hana umbo wala uzuri;Na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani.(3) **Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko;** Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu. Isaya 53:1-3

Majibu asili ya moyo wa mwanadamu kwa Mwana wa Mungu ni kumkataa yeye pamoja na mafunzo yake.

> Mtu ambaye hana Roho wa Mungu hawezi kupokea mambo yatokayo kwa Roho wa Mungu, kwa kuwa ni upuzi kwake, naye hawezi kuyaelewa kwa sababu hayo yanaeleweka tu kwa jinsi ya rohoni. 1 Wakorintho 2:14

Mtu asilia anaposoma neno la Mungu hawezi kulielewa. Bibila inatwambia;

> Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana. (9) Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu. Isaya 55:8-9

Isipokuwa tuzaliwe kwa Roho wa Mungu na tuje kwa Bibilia kwa unyenyekevu kuagiza uongozi tutaelewa visivyo neno la Mungu ni nini.

> Mtu ye yote anayedhani kwamba anajua kitu, hajui kama impasavyo kujua. 1 Wakorintho 8:2

> Ndugu zangu wapendwa, fahamuni jambo hili: Kila mtu awe mwepesi wa kusikia, lakini asiwe mwepesi wa kusema wala wa kukasirika. Yakobo 1:19

> Yeye ajibuye kabla hajasikia, Ni upumbavu na aibu kwake. Methali 18:13

Ni rahisi kujibu jambo kabla ya kulisikia. Tazama mfano ufuatao:

> Kisha Yesu akawauliza, "Nilipowatuma bila mfuko, wala mkoba, wala viatu, mlipungukiwa na kitu cho chote?" Wakajibu, "La, hatukupungukiwa na kitu cho chote." (36)Akawaambia, "Lakini sasa, aliye na mfuko na auchukue na aliye na mkoba vivyo hivyo. Naye asiye na upanga, auze joho lake anunue mmoja. Luka 22:35-36

Lakini baadaye anaoneka kubadili mawazo yake?

> Ndipo Yesu akamwambia, "Rudisha upanga wako mahali pake, kwa maana wote watumiao upanga watakufa kwa upanga Mathayo 26:52

Kwani Yesu aliwaagiza wanafunzi wake kununua Upanga, na kisha wakati Petro anautumia anamkemea? Kwani Petro aliutumia katika tukio mbaya? kama ndivyo, Yesu alimwambia wakati wa kuutumia na wakati usio wa kuutumia? Maneno, "wote watumiao upanga watakufa kwa upanga," Yanaoneka ya haki kwa wote. Kama hayo hayakutosha tunaongezea kwa zaidi mwelekeo huu:

> Vaeni chapeo ya wokovu na mchukue upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu. Waefeso 6:17

> Kwa maana Neno la Mungu li hai tena lina nguvu tena lina makali kuliko upanga uwao wote wenye makali kuwili, tena linachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, viungo na mafuta yaliyo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. Waebrania 4:12

> Katika mkono wake wa kuume alishikilia nyota saba na kinywani mwake ulitoka upanga wenye makali kuwili. Uso wake kama jua kali linalong'aa kwa nguvu zake zote. Ufunuo 1:16

Bibilia hutumia neno *Upanga* kurejelea Neno la Mungu. Tutajuaje wakati wa kutumia kuelewa huku na wakati wa kuelewa upanga halisi? Fikiria pia mfano wa moto.

> Eliya akajibu, akamwambia yule akida wa hamsini, Ikiwa mimi ni mtu wa Mungu, na ushuke moto kutoka mbinguni, ukuteketeze wewe na hamsini wako. Moto ukashuka, ukamteketeza, yeye na hamsini wake. 2 Wafalme 1:10

> Wakati ulipokaribia wa Yeye kuchukuliwa mbinguni, alikaza uso Wake kwenda Yerusalemu. (52) Akatuma watu wamtangulie, nao wakaenda katika kijiji kimoja cha Samaria kumwandalia kila kitu, (53) lakini watu wa kijiji kile hawakumkaribisha kwa sababu alikuwa anakwenda Zake Yerusalemu. 54Wanafunzi Wake, yaani, Yakobo na Yohana walipoona hayo, wakasema: "Bwana, unataka tuagize moto kutoka mbinguni ili uwaangamize?" (55)Yesu akageuka na kuwakemea, (56) nao wakaenda kijiji kingine. Luka 9:51-56

Kwa kukemea wanafunzi Yesu alikuwa akimkemea pia Eliya? Je, ilikuwa tu kwamba hawakujua wakati mwafaka wakuita moto? Tena maneno ya Yesu ni ya haki kwa wote. Anasema kwamba hakuja kuangamiza maisha ya wanadamu bali kuwakomboa. Je, hili linatumika alipokuwa hapa ulimwenguni tu, Lakini ataangamiza maisha ya binadamu baadaye?

Haya ni baadhi ya maswasali ambayo huibuka wakati mtu anaposoma Bibilia. Hutuletea swali muhimu ambalo yesu alimuuliza mtaalamu wa sheria aliye mswali.

> Yesu akamjibu, "Imeandikwaje katika Torati? Kwani unasoma nini humo?"? Luka 10:26

Yesu hakumuuliza tu unasoma nini bali ni jinsi gani unaisoma? Ni kanuni zipi unatumia kusoma Neno la Mungu? Hili ni swali muhimu sana ambalo linahitaji jibu kama tunataka kuunganisha kurasa ambazo zinaonekana kukinzana.

Mapema katika karne ya 19 mtu ambaye alikuwa aongoze moja wapo ya mkutano mkubwa wa injili kule Marekani kaskazini alikuwa anakabiliwa na

swali hili. Katika maisha yake ya awali William Miller alikuwa amekufa moyo na Bibilia,na kuhitimisha kwamba imejaa mambo yanayopingana. Bali baada ya kushuhudia tukio la kustaajabisha la jinsi Marekani walivyoshinda dhidi ya majeshi ya Waingereza katika vita ambavyo Waingereza wangeshinda virahisi, aliamini kwamba nguvu kuu kuliko za mwanadamu zilikuwa kazini, na akaja kuangalia upya Bibilia. Hili lilikuwa jambo la kufedhehesha kabisa kwake ambalo angelifanya, kwa sababu alikuwa amewaekea wakristo wengi kauli dhahiri ambazo zinakizana katika Biblia ambazo hawakuweza kupata majibu. Alipozifanya upya hisia zake kuhusu Bibilia alikumbwa na mjadala sawa na aliokuwa amewaekea wenzake.

> "Punde tu baada ya kukataliwa kwa Deism, akizungumza na rafiki kwa tumaini na la utukufu milele kupitia kwa kuhalalishwa na maombezi ya Kristo, aliulizwa alijuaje kuna mkombozi kama huyo. Alijibu, "imedhihirishwa katika Bibilia." – "Unajuaje kuwa Bibilia ni kweli?" ulikuwa mwitikio, kwa kurudia majadiliano yake ya awali kuhusu pingamizi na upagani ambao alikuwa amedai kuwa yamefunikwa, Bw. Miller alihisi kauli kama hiyo kwa nguvu zake kamilifu, alikuwa ameshangazwa kwanza; lakini kwa onesha, alizingatia kuwa ikiwa Bibilia ni ufunuo wa Mungu, lazima iwe na uthabiti ndani yake; sehemu zake zote lazima zipatane, lazima ilipeanwa kwa mafundisho ya watu, na, hivyo, lazima ichukuliwe kwa kueleweka kwake. Kwa hivyo, alisema, "Nipe muda, na nitaunganisha utata huo wote unaoonekana kwa maridhisho yangu mwenyewe, au nitasalia kuwa Deist." Kisha akajitoa kwa kusoma neno kwa maombi. Aliweka kando ufafanuzi wote, na akatumia marejeleo ya mwisho na marejeleo yake mwenyewe kama yalivyomsaidi. Aliona kuwa lazima atafautishe Bibilia na usaidizi wote wa kuifafanua. Bibilia ilikuwa kongwe kuyaliko yote, na lazima ingekuwa juu ya yote na aliiweka hapo. Aliona kwamba lazima isahihishe ufafanuzi wote; na, katika kuusahihisha, nuru yake safi iangaze bila ukungu ambao imani za utamaduni zilikuwa zimehusishwa ndani yake. Aliazimu kuweka kando mawazo ya awali, na kupokea, kama urahisi wa mtoto, halisi na dhahiri maana ya maandiko." Sylvester Bliss, *Memoirs of William Miller* (1853) p 68.

Hili ndilo hasa alilolitenda. Katika kipindi cha miaka miwili alijifunza Bibilia jalada hadi jalada.

"Niliamua kuweka kando umilikaji wangu wa awali, kwa kulinganisha andiko kwa andiko, na kujiingiza katika uchunguzi wake katika mara kwa mara na kwa njia ya mpangilio. Nilianza na Mwanzo, na nikasoma fungu baada ya fungu, nikiendelea polepole kwa kuwa maana ya mafungu kadhaa haikuwa imefunuliwa ili kuniacha huru kutoka kwa aibu kwa kuzingatia upagani au utata. Nilipopatana na chochote kisichoeleweka, kitendo changu kilikuwa kulinganisha na mafungu yote ya dhamana; na, kwa usaidizi wa Cruden, niliweza kuyachunguza mafungu yote ya Maandiko ambayo kwayo kulipatikana maneno yoyote maarufu yakiwa katika kiwango chochote kisichoeleweka. Kisha, kwa kuruhusu kila neno kuwa na mwelekeo wake halisi katika mada ya fungu, kama mtazamo wangu wa kwayo uliunganika na kila fungu la dhamana katika Bibilia, liliacha kuwa gumu. Kwa njia hii nilifuata mafunzo ya Bibilia, katika somo langu la kwanza, kwa miaka kama miwili hivi, na niliridhishwa kikamilifu, kuwa inajieleza yenyewe. Sylvester Bliss, *Memoirs of William Miller* (1853) p 69.

Kwa wakati huu alianzilisha mfumo wa kanuni ambazo kwazo aliweza kuunganisha pingamizi ambazo alikuwa amekumbana nazo awali. Huu ni muhtasari wa kanuni alizotumia:

1. kila neno lazima liwe na zao sahihi juu ya mada inayowasilishwa katika Bibilia.
2. Kila andiko ni muhimu, na linaweza fahamika kwa kutumiwa kwa uangalifu na kutafitiwa.
3. Hukuna kilichodhihirishwa katika Bibilia kinaweza fichwa kwa wale wanaoomba kwa imani, na wala sio kwa kusita.
4. Kuelewa mafundisho, leta maandiko yote pamoja juu ya mada unayotaka kujua; kisha ruhusu kila neno kuwa na athari sahihi, na kisha iwapo unaweza jenga nadharia yako bila pingamizi, hauwezi kuwa katika kosa.
5. Bibilia lazima ijieleze yenyewe, kwa kuwa ni kanuni yake binafsi, kama nitategemea mwalimu kunifafanulia, na atakisia maana yake, ama atake iwe katika misingi ya imani yake, au kujifikiria mwenye hekima, kisha kukisia, matamanio, imani au hekima, ni kanuni yangu, na sio Bibilia.

6. kama neno linaleta maana sawa jinsi lilivyo, na halikiuki sheria rahisi za maumbile, lieleweke sawasawa; kama sivyo, mfano.
7. Kanuni muhimu kwa zote ni, kama lazima uwe na imani. Lazima iwe ni imani inayohitaji kujitolea, na, kama itajaribiwa, inaweza wacha kitu cha dhamani duniani, ulimwengu na tamaa zake, tabia, kuishi, kazi, marafiki, nyumba, faraja na heshima za ulimwengu. Kama moja ya haya litazuia sehemu yoyote katika kuamini neno la Mungu, itaonyesha imani yetu kuwa bure. Wala hatutawahi amini mradi tu moja ya nia hizi inaishi mioyoni mwetu. Lazima tuamini kuwa Mungu hawezi liacha neno lake, na tuwe na ujasiri kuwa Yule achukuae andiko la anguko la shomoro, na huhesabu nywele za vichwa vyetu, ataongoza utafsiri wa neno lake, na kuweka kwa kizuizi kwake, na kuzuia wale ambao wanamtumainia Mungu kwa dhati, na kuweka imani thabiti kwa neno lake, kutokana na kupotoshwa kutoka katika ukweli.

kanuni hizi za kufasiri hutoa chombo cha kukuza ujumbe, uongozi wa moja ya ufufuo mkuu ambao ulimwengu umewahi shuhudia.

Tunagundua kwa makini kuwa ili tufahamu mafundisho tunahitaji kuchukua maandiko yote tunayoweza kupata juu yake na kuyaleta pamoja kabla ya kutoa hitimisho letu. Kila neno liwe mahali pake halisi na athari. Hili ni jambo ambalo sio rahisi kwa watu wengi kwa sababu tunataka kupata majibu kwa upesi, lakini inahitaji bidii na nidhamu kutafuta mafungu yote juu ya mada, chukua kwa mfano neno la Kigiriki *monogenes* linatafsiriwa kama pekee katika Yohana 3:16. Watu wengi huamini kuwa neno hili humaanisha kipekee, lakini Bibilia inajisemea nini?

| | |
|---|---|
| Huyu aliyekufa alikuwa **mwana pekee** wa mwanamke mjane, Luka 7:12 | Mwana pekee |
| kwa kuwa **binti yake wa pekee**, mwenye umri wa miaka kumi na miwili, alikuwa anakufa. Luke 8:42 | Mwana pekee |

| | |
|---|---|
| Mtu mmoja miongoni mwa ule umati wa watu akapiga kelele, akasema, “Mwalimu, naomba umwangalie mwanangu, ndiye **mtoto wangu wa pekee**. Luke 9:38 | Mwana pekee |
| Neno alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu, nasi takauona utukufu Wake, utukufu kama wa **Mwana pekee** atokaye kwa Baba, amejaa neema na kweli. Yohana 1:14 | Mwana wa pekee |
| Hakuna mtu ye yote aliyemwona Mungu wakati wo wote, ila ni Mungu **Mwana pekee**, aliye kifuani mwa Baba ndiye ambaye. Yohana 1:18 | Mwana wa pekee |
| ‘Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa **Mwanawe wa pekee**, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Yohana 3:16 | Mwana wa pekee |
| Ye yote amwaminiye hahukumiwi, lakini asiyeamini amekwisha kuhukumiwa,kwa sababu hakumwamini **Mwana pekee** wa Mungu. Yohana 3:16 | Mwana wa pekee |
| Kwa imani Abrahamu, alipojaribiwa na Mungu, alimtoa Isaki kuwa dhabihu.Yeye aliyekuwa amezipokea ahadi za Mungu alikuwa tayari kumtoa mwanawe,aliyekuwa **mwanawe pekee** awe dhabihu. Waebrania 11:17 | Mwana wa pekee |
| Hivi ndivyo Mungu alivyoonyesha upendo Wake kwetu, kwa sababu Mungu alimtuma **Mwanawe wa pekee** ulimwenguni, ili tupate uzima kwa Yeye.1 Yohana 4:9 | Mwana wa pekee |

kuna watu watano tu wametajwa katika Agano Jipya kama *monogenes* au pekee. Mafungu matano yanamrejelea Yesu kama Mwana wa Mungu. Kuna rejeleo moja kwa Isaki na kisha marejeleo mengine ni ya watoto wa pekee ambao Yesu aliponya. Katika muktadha huu wa watoto wengine ambapo neno linatumika maana ni wazi kuwa inamaanisha mtoto ambaye amezaliwa peke yake. Kwa kuzingatia Isaka,tunajua hakuwa mwana pekee wa Ibrahimu lakini alikuwa mwana pekee aliyezaliwa na Sara ambaye alipokea ahadi na Ibrahimu. Tunapoweka mafungu haya yote pamoja tunaona kuwa neno hili linapotumika kwa Yesu lazima limaanishe jambo sawa, mwana pekee wa kuzaliwa kwa Baba.

Ikiongezwa, kwa hili ni kanuni ambayo inaorodheshwa kama nambari sita hapo juu inayosema kuwa tunapaswa kuchukua maana sawasawa ya kifungu iwapo hakikiuki maumbile. Haikiuki maandiko kuelewa kuwa Yesu ni mwana wa pekee wa Baba. Hivyo kupitia kwa mchakato huu tunaweza tambua maana ya neno monogenes bila kutafuta kutoka kwa ufafanuzi au kwa mtu mwengine. Bibilia, yenyewe, hujieleza.

Tutahitaji kuzitumia kanuni hizi kwa makini tunapotafuta kupatanisha maisha ya Yesu na hadithi zingi za kikatili za Agano la Kale. Itachukua bidii nyingi kudhibitisha ukweli madai ya Bibilia; kuwa Yesu ni ule ule jana, leo na hata milele.Waebrania 13:8. Kwa hivyo, kama habadilika, wakati wa huduma yake duniani alikuwa ufunuo kamili wa Baba yake.

## 3. Kifo cha Msalaba

Kazi ya Mwana wa Mungu hapa duniani ilikuwa kudhihirisha tabia ya Baba yake. Namna gani ni jambo la thamani kusoma kuhusu mkombozi mwenye upendo na tefu, aondoae mizigo, kutibu magonjwa na kuguza mioyo ya waume, wake na watoto. Mama wanatafuta kwa hamu na bidii kuwaleta watoto wao kwake ili awaguze na awabariki. Kamwe sikusikia ulimwengu ulishuhudia kujikana nafsi na upendo wa kujali kama huo. Kadiri wakati ulivyopita ndivyo sura ya Baba yake ilivyorejeshwa kwa uzuri wa Edeni. Kwa watu, uso wa kwanza walioona ni ule wa Yesu alipoyafungua macho yao; Sauti ya kwanza waliosikia ilikuwa sauti ya kimuziki ya Mwana wa Mungu iliyojawa neema na ukweli.

Picha ambayo Yesu alituchorea ilikuwa ikilingana barabara na maneno yaliyonenwa na Musa takriban miaka 1500 mbeleni.

> Bwana akashuka ndani ya lile wingu, akasimama pamoja naye huko, akalitangaza jina la Bwana. (6) Bwana akapita mbele yake, akatangaza, Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; Kutoka 34:5-6

Lakini maisha ya Yesu yalichorwa kwenye turubai yalibadilika kwa damu. kama miaka kumi na miwili yesu alisimama hekaluni na kutazama mwana kondoo akiuawa, Alijua hii ndio hatima yake. Wabaptisti walipomtangaza

ulimwenguni, ilikuwa na andiko “mwana kondo wa Mungu aziondoae dhambi za Ulimwengu” Yohana 1:29. Mshahara wa dhambi lazima ulipwe, haki lazima ihudumu kama maandiko yasemavyo.

> wanahesabiwa haki bure kwa neema Yake kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu. (25) Yeye ambaye Mungu alimtoa awe dhabihu ya upatanisho kwa njia ya imani katika damu Yake. Alifanya hivi ili kuonyesha haki Yake, kwa sababu kwa ustahimili Wake aliziachilia zile dhambi zilizotangulia kufanywa. (26) Alifanya hivyo ili kuonyesha haki Yake wakati huu, ili Yeye awe mwenye haki na mwenye kumhesabia haki yule anayemwamini Yesu. Warumi 3:24-26

Mungu alihitaji msalaba? Je, hii ilikuwa adhabu yake kwa kuasi sheria zake? Maswali haya lazima ni muhimu. Kama hasira ya Mungu iliridhishwa kwa kifo cha Mwanawe na kifo kilikuwa jambo ambalo Mungu mwenyewe alikuwa ameamua,basi hatimaye picha ya kupendeza iliyochorwa na Yesu kuhusu Baba yake imebadilishwa kwa damu ya Mwana asiyekuwa na hatia. Maneno ya Kristo “imekwisha” hayawezi kukamilisha sura ya Baba mwema, lakini badala yake milele hutoa uaminifu kuwa alihitaji kifo ili kukidhi hasira yake dhidi ya dhambi. Hili litamfanya mwanzilishi wa kifo na pia mwanzilishi wa ukatili wa kulipisha kisasi.

Nabii Isaya alinena kuhusu msalaba miaka 700 kabla yakutokea na akaonyesha mwitikio wa wanadamu kwake.

> Ni nani aliyesadiki habari tuliyoileta? Na mkono wa Bwana amefunuliwa nani? (2) Maana alikua mbele zake kama mche mwororo, Na kama mzizi katika nchi kavu; Yeye hana umbo wala uzuri; Na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani. (3**) Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu. (4) Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa**. (5) Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Isaya 53:1-5

Yesu alipokuja kukomboa mwanadamu mwitikio wetu wa asili ulikuwa kumkataa. Alileta uzima wa milele, lakini majibu asili ya mwanada yalikuwa kupuuza zawadi hii.

> Ndani Yake ndimo ulimokuwa uzima na huo uzima ulikuwa nuru ya watu. (5) Nuru hung'aa gizani nalo giza halikuishinda.Yohana 1:4-5

Mwana wa Mungu alikuwa akibeba dhambi zetu juu yake, na bado mwitikio wetu kwake ulikuwa kuamini kuwa amepigwa na Mungu. Maneno kupigwa na kuteswa yanamaana kuwa kupiga na kuua kwa ukatili. Lakini sio Mungu aliyempiga mwanawe kwa ukatili ngumi ya kifo; Hili ndilo mwanadamu huliamini, lakini sio kweli. Basi nini kilichosababisha kifo cha Yesu msalabani? Mfumo ulikuwa umewekwa tangia mwanzo wakati Adamu aliulizwa kama alikuwa amekula tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya.

> Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia,Uko wapi? (10) Akasema, Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha. (11) Akasema, Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! Umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale? (12) Adamu akasema, Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala. Mwanzo 3:9-12

Adamu hakuomba msamaha wala kuhurimiwa.Dhambi zake zilikuwa zimepofusha mtazamo wake kiasi ya kwamba hakutaka kuagiza msamaha na kuhurimiwa. Badala ya kuitikia kuwa alikuwa ameasi na kuomba kuhurumiwa alianza kuweka lawama kwa Mungu kwa kumuumbia mwanamke aliye mjaribu baadaye. Alifikiria Mungu ni mkali na mwenye asili ya kuadhibu, na kwa hivyo tabia ya kweli ya Mungu ilifichika kutoka kwake kwa uwongo huu. Katika hadithi ya Kaini tunaona kanuni hiyo hiyo ikitenda kazi.

> Kaini akamwambia Bwana, Adhabu yangu imenikulia kubwa, haichukuliki. Mwanzo 4:13 (Tafsiri ya Wycliffe, Tazama pia Tafsiri ya Luther 1912)

Kaini alikataa kutubu kwa sababu aliamini kuwa Mungu hangemsamehe. Hii ni nguvu ya dhambi juu ya jamii ya mwanadamu; Ni dhambi ya kuamini kwamba Mungu hawezi tusamehe dhambi zetu. Hata mwana mpotevu haombi msamaha lakini badala yake anatafuta kulipia vitendo vyake kwa kufanya kazi.

> Nitaondoka na kurudi kwa baba yangu na kumwambia, 'Baba, nimetenda dhambi mbele za Mungu na mbele yako. (19) Sistahili tena kuitwa mwanao, nifanye kama mmoja wa watumishi wako. Luka 15:18-19

Njia ya pekee ya kumwezesha mwanadamu kutubu ni kwa Roho wa Kristo kupeanwa kama zawadi ili kutuwezesha kufika mbele ya mtazamo wetu na kuagiza na pia kupokea msamaha.

> Mungu wa baba zetu aliyemfufua Yesu ambaye ninyi mlimwua kwa kumtundika kwenye msalaba. (31) Mungu alimtukuza akamweka mkono wake wa kuume **kuwa kiongozi na Mwokozi ili awape Israeli toba na msamaha wa dhambi.** Matendo 5:30-31

Adamu alipofanya dhambi aliweza kuweka uadui kwa Mungu. Moyo wake ulikuwa vitani naye, tunasoma:

> Kwa maana kuwa na nia ya mwili ni mauti, bali kuwa na nia inayoongozwa na Roho ni uzima na amani. (**7) Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui na Mungu**, kwa maana haiitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii.. Warumi 8:6-7 (NIV)

Ili Mungu ampe Adamu uwezo wa kutubu na kuagiza msamaha, Alituma Roho wa Mwanawe ndani ya Moyo wa Adamu na ndivyo Adamu aweze kulia "Abbaa Baba." Roho wa Yesu moyoni mwa Adamu tu ndiye angewezaa kumpa neema ya kumwezesha kulia hivi.

> Kwa sababu ninyi ni watoto wa Mungu, Mungu amemtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, anayelia, "Abbaa! Yaani, Baba.". Wagalatia 4:6

Katika kuja kwa Adamu alipokuwa hampokei kabisa,Yesu alilazimika kuvumilia uadui moyoni mwa Adamu ili kumpa neema. Chuki hii hudunga moyo wa Kristo na kusababisha kuyasikia mateso.

> Maana alisema, Hakika ndio watu wangu hawa, wana wasio na hila; akawa Mwokozi wao. (9) Katika mateso yao yote yeye aliteswa, na malaika wa uso wake akawaokoa; kwa mapenzi yake, na huruma zake, aliwakomboa mwenyewe; akawainua, akawachukua siku zote za kale.. Isaya 63:8-9

Hivyo basi ni kwa njia hii Kristo ndiye mwana kondo aliyeuawa tangia mwanzo wa ulimwengu. Ufunuo 13:8. Ili kumpa mwanadamu hamu na

msukumo wa kuomba msamaha na rehema Yesu lazima ateseke kwa machungu. Kukataliwa na kuchukiwa na mwanadamu. Hudharauliwa na kukataliwa kwa wanadamu na mwana wa huzuni ajuaye sikitiko Kila wakati waume na wake wanapokataa wito wa Kristo kwa Moyo, Kukataliwa humchoma kwa kina cha upendo wake kwa nafsi zao. Kila udhihirisho wa uovu kutoka kwa moyo wa wanadamu husababisha Kristo kuhuzunika isivyoelezeka kwa wahusika na mwathiriwa. Kutokana na mtazamo huu kweli Kristo alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu katika siku ambazo Isaya aliandika maneno hayo miaka 700 iliyopita kabla ya Kristo kuja duniani. Hivyo basi leo anabeba huzuni sawa kama msalaba begani mwake ili kumpa mwanadamu muda zaidi kugeuka kutoka kwenye ukatili na njia za ukatili na kujifunza ukweli kuhusu Baba yake.

Kama wanadamu wameamua kutokuamini kuwa Mungu anaweza samehe, hii ni zawadi ambayo Kristo lazima angelipa ili kumkomboa mwanadamu. Ili kuchukua nafasi yetu lazima angekufa jinsi wanadamu hufa. Kifo hiki ni kile ambacho wanadamu huamini kuwa Mungu hawezi wasamehe. Udanganyifu kwamba Mungu hawezi samehe ndio ambao humpa shetani nguvu za mauti. Hivyo basi, ni kupitia kwa kifo tu ndio mwanadamu anaweza mshinda shetani.

> Basi kwa kuwa watoto wana nyama na damu, Yeye pia alishiriki katika ubinadamu wao, ili kwa kifo **chake, apate kumwangamiza huyo mwenye nguvu za mauti, yaani, Shetani**; Waebrania 2:14

Kifo cha msalaba ni kifo ambacho dhambi huhitaji sio Mungu. Wakati mtu anapovuka mstari ndani ya dhambi inakuwa vigumu kurudi nyuma, kama mtazamo wote wa rehema na neema umeondoka, na uwezekano pekee wa matokeo ni kifo. Mwanadamu anapoitazama sheria kamilifu kama kioo na kutaka kuhusisha kifo kwa Mungu, uakisi huja kwa mwanadamu kwa wakati huo na kumuangamiza.

> Kwa maana kama mtu ni msikiaji tu wa Neno wala hatendi kile linachosema, **yeye ni kama mtu ajitazamaye uso wake kwenye kioo**; Yakobo 1:23 (NKJV)

> Kwa maana kwa jinsi ile unavyowahukumu wengine, ndivyo utakavyohukumiwa na kwa kipimo kile utakachotoa ndicho utakachopokea. Mathayo 7:2

Adamu alipolila tunda la mti alichagua kuamini kuwa Mungu hakumtakia mema moyoni mwake. Alichagua kuamini nyoka, kwamba Mungu alikuwa muongo mwenye kujipenda. Mawazo haya, yanaweza kuonyeshwa kwenye kioo kikamilifu cha sheria, alikuja moja kwa moja kwake na kumuhukumu kama alivyojua. Dhana yake ya uongo kuhusu Mungu ilipoozesha mkono wake ambao ungeweza kufikia rehema na neema. Ilikuwa vigumu kwake kurejea kutoka kwenye nafasi hii. Kifo kikawa tu ndio tokeo, kwa maana hii ndio hukumu yeye mwenyewe alikuwa amejiamulia.

Ili kutangaza kanuni hizi kwa ulimwengu, Kristo alikuja ili aweze kuweka msalaba wazi ili tuweze kutambua ukweli asili wa dhambi. Yesu alinena maneno ya mtu aliye na mzigo wa dhambi:

> Ilipofika saa tisa Yesu akapaza sauti akalia, "Eloi, Eloi lama sabakthani?" Maana yake, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" Mathayo 27:46

Mungu hakumuacha Mwanawe hata kidogo, lakini Kristo alipokuwa akibeba dhambi zetu juu yake yeye mwenyewe, alikufa kama mwanadamu ambaye hawezi samehewa kwa kuwa haya ndio *mapenzi* ya mwanadamu – mwanadamu ambaye, wakati ambao dhambi zake zimewekwa juu yake, hudhani kwamba hawezi samehewa au hajafikia hakikisho la kusamehewa atahisi mapenzi ya kuachwa na Mungu. Katika maneno haya ya Kristo tunaona laana ya dhambi juu yake, laana iliyo onyeshwa na Kaini.

> Tazama, umenifukuza leo katika uso wa ardhi, nitasitirika mbali na uso wako, nami nitakuwa **mtoro** na mtu asiye na kikao duniani; hata itakuwa kila anionaye ataniua. … Mwanzo 4:14

Neno mtoro linaweza maanisha kuyumba na kutetemeka. Kristo anaonyesha kuwa alibeba laana ya Kaini. Alihisi kuwa uso wa Mungu ulikuwa umejificha na alitetemeka kwa sababu ya hatia yetu. Maandiko yanadhihirisha kinachoficha uso wa Mungu.

> Maana kwa ajili yako nimestahimili laumu, Fedheha imenifunika uso wangu.. Zaburi 69:7

> Lakini maovu yenu yamewafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeuficha uso wake msiuone, hata hataki kusikia.. Isaya 59:2

Kwa kulemewa na mzigo wa dhambi Yesu analia:

> Kwa maana mabaya yasiyohesabika Yamenizunguka mimi. **Maovu yangu yamenipata, Wala siwezi kuona.** Yamezidi kuliko nywele za kichwa changu, Na moyo wangu umeniacha. Zaburi 40:12 (NIV)

Kwa kumrejelea Baba tunasoma:

> Maana hakulidharau teso la mteswa, Wala hakuchukizwa nalo; Wala hakumficha uso wake, Bali alipomlilia akamsikia. Zaburi 22:24

Aibu ya dhambi zetu ilimfunika Kristo kiasi ya kwamba hangeweza kuuona uso wa Baba. Alikabiliana na kifo kama jinsi kila mwenye dhambi atakavyo kabiliana na kifo katika hitimisho ya pambano kuu. Kristo alihisi makaa ya moto nafsini mwake.

> Kamba za kuzimu zilinizunguka, Mitego ya mauti ikanikabili. (6) Katika shida yangu nalimwita Bwana, Na kumlalamikia Mungu wangu. Akaisikia sauti yangu hekaluni mwake, Kilio changu kikaingia masikioni mwake. (7) Ndipo nchi iliyotikisika na kutetemeka, Misingi ya milima ikasuka-suka; Ikatikisika kwa sababu alikuwa na ghadhabu. (8) Kukapanda moshi kutoka puani mwake, Moto ukatoka kinywani mwake ukala, Makaa yakawashwa nao. Zaburi 18:5-8

Kristo aliteseka kifo cha waovo. Moto ulikuja kutoka katikati mwa Kristo na ukammeza. Dhambi zetu juu ya kristo zilimfanya kuteseka jinsi shetani na waovu wote watakavyo teseka wakati wa mwisho.

> Kwa wingi wa maovu yako, katika uovu wa uchuuzi wako, umepatia unajisi patakatifu pako; basi nimetokeza moto kutoka ndani yako, nao umekuteketeza, nami nimekufanya kuwa majivu juu ya nchi, machoni pa watu wote wakutazamao… Ezekieli 28:18

Kama mbadala wetu patakatifu pa Kristo au mwili hekalu uliharibiwa na mkusanyiko wa dhambi zetu. Alijeruhiwa kwa kosa letu na kupondwa kwa maovu yetu. Kifo cha kutisha ambacho shetani atakufa tayari Kristo amekipitia katika Msalaba. Moyo wa Kristo ulilipuka kutoka kwa moto ulioletwa kutoka kwa maji na damu. Kristo alikufa ndani ya moto wa jehanamu hai na hivi ndivyo wenye dhambi watakavyo kufa hasa. Na pumzika na kuakisi kwa mshangao kwa haki kama Baba hakumuacha Mwanawe lakini akateseka naye kupitia kwa kifo chake msalabani hivyo basi Baba yetu na mkombozi atakuwepo pale akiteseka na waovu ndani ya ndimi za jehanamu. Maandiko yanatwambia:

> Katika mateso yao yote yeye aliteswa… Isaya 63:9

Hakuna Baba ambaye atafurahia kumpoteza mwanawe, ni uchungu kwake na kwa hivyo Baba yetu na Mwanawe watateseka tena machungu ya msalaba na waovu katika mauti yao. Kama watakatifu wakisimama juu ya kuta za sayuni  na kuwaona wapendwa wao kwenye ndimi za moto, Mkombozi atawabeba na kuwapitisha juu ya ule msalaba na itachukua miaka elfu moja  kuwaandaa juu ya tukio hilo. Kama Maria na wanafunzi walipokuwa wakimtazama Mwana wa Mungu msalabani wakalia kwa uchungu, ndivyo watakatifu watachomwa na kuwapoteza milele wapendwa wao walioikataa neema ya Mungu. Wakati huo ndio tu tunaambiwa Mungu atafuta kila chozi machoni mwetu.

> Atafuta kila chozi, kutoka katika macho yao. Mauti haitakuwepo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu, kwa maana mambo ya kwanza yamekwisha kupita." Ufunuo 21:4

Hili linatokea baada ya kifo cha waovu katika Ufunuo 20:

> Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake, nayo mauti na kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake. Kila mtu akahukumiwa kulingana na yale aliyotenda. (14)Kisha Mauti na Kuzimu zikatupwa katika ziwa la moto. Hii ndio Mauti ya pili, yaani, hilo ziwa la moto. (15)Iwapo mtu jina lake halikuonekana katika kile kitabu cha uzima, alitupwa ndani ya lile ziwa la moto. Ufunuo 20:13-15

Jinsi kristo alivyofufuka katika kaburi la mateso miaka 2000 iliyopita ndivyo atakavyofufuliwa kutoka kwenye uchungu wake wa kupoteza mabillion ya wana wake waliomtemea mate,waliomdharau na kukataa rehema za pendo lake. Yesu atakapokuwa akifufuliwa kwa mibaraka ya Baba nasi pia tutafufuliwa juu pamoja naye tuingie katika nchi mpya bila hata kivuli cha huvuni kusalia.

Kwa kurejea kwenye mateso ya Kristo msalabani tunataka tugundue jambo. Tunatazama kwamba licha ya kuwa Kristo alikuwa mwisho wa kukata tamaa alipohisi upweke na kuachwa kabisa, kwa imani alimwomba Baba kuwasamehe waliokuwa wakimuua;

> Yesu akasema, "Baba, wasamehe, kwa maana hawajui walitendalo!" Wakagawana nguo Zake kwa kupiga kura. Luka 23:34

Kifo cha msalaba kinaufunua uongo wa shetani kwamba Mungu hawezi tusamehe. Tunaona Mungu alimtoa Mwanawe kwa hiari ili tuweze kuhesabiwa haki. Aliruhusu afe bila tumaini, ili takapoona kwamba amefufuka kutoka kaburini, tunaweza kuchagua kuamini kwamba tunaweza samehewa dhambi zetu na kupokea mibaraka ya kufanywa upya maishani.

Roho wa Mwana wa Mungu huja ndani ya mioyo yetu na kuinua mikono yetu ya kiroho iliyopooza ili kupokea rehema za Mungu.

Ni ajabu jinsi gani kujua kwamba Mungu hakuhitaji kifo. Hasimami mbele ya mwenye dhambi kama mnyongaji wa adhabu ya kifo. Baba yetu kwa hiari aliruhusu Mwanawe atuonyeshe hatima ya watakao kataa kuamini rehema za Mungu. Hakumuua Mwanawe ili kulipiza kisasi cha hasira yake, bali alimtoa mwanawe kwa hasira yetu ili tuweze kuona upendo wa Mungu.

Onyo ambalo Mungu alitoa katika bustani ya edeni kuwa ile siku ambayo Adamu atakula kutoka kwenye mti wa ujuzi wa mema na mabaya atakufa, hakika, halikuwa tishio la kumuua; Ilikuwa ni onyo la hukumu ambalo mwanadamu atajiletea juu yake kwa kuchagua kuamini kwamba Mungu ni mbinafsi, na kwa hivyo, hawezi samehe. Ni ukweli mzuri Kwamba Kristo pekee aliyeelewa urefu na kina na upana wa upendo wa Mungu, alijua kwamba inawezekana kumuagiza Mungu rehema na msamaha. Mathayo 11:27. Hivyo basi ilikuwa wazi kwamba Mwana wa Mungu ndiye afikiaye mioyo ya wanadamu na kuwa na ujasiri wa kuamini kuwa wanaweza samehewa.

Ni jinsi gani inavyostajabisha ufunuo wa msalaba. Basi tusiendelee kumtazama Kristo kuwa “alipigwa na Mungu na kuteswa lakini

alidharauliwa na kukataliwa na wanadamu” – kupigwa na kuteswa kupitia kwa kuelewa vibaya kwa tabia ya Mungu.Mungu hakuhitaji kifo kama Adhabu ya dhambi; bali kifo ni tokeo dhabiti la kuamini kuwa Mungu hawezi tusamehe.

# 4. Mwanangu Mpendwa

Kulikuwa na kimya kirefu wote wakitazamana. Uzito wa hisia ulikimbia kwa ndani, lakini wote walijuwa kuwa wakati umewadia. Tangia siku za kuwepo kwao, Baba na Mwana walikuwa katika uhusiano wa karibu wao wenyewe, lakini sasa uhusiano ulikuwa uvunjwe baada ya kitambo kidogo. Mwana wa Mungu alikuwa aje kwa huduma ya duniani ya kuwaokoa wanadamu wake wake kwa waume. Wote Baba na Mwana wanaelewa hatari na gharama iliyohusishwa , lakini upendo unawaongoza wote.

kwa muda mfupi, Baba na mwana walitazama siku za usoni na kuangalia huduma akijifunua. Madharau, kukataliwa, kuchukiwa, kutemewa mate, mateka, viboko na misumari vyote havikuonekana chochote ikilinganishwa na wakati mbingu na inchi zilikaa kimya na kutazama kutengana kwa Baba na Mwana. Mwana anaona millenia ya makosa, mateso, uasi na kukosa maana viliyovilingishwa juu yake akitetemeka kama jani, akivutwa na kuraruliwa na hali ya dhambi iliyouficha uso wa Baba yake.

kwa kuondoka kati maeneo haya ya usoni, Baba na mwana walikubaliana – jinsi gani Baba anaweza mtoa Mwana hadi kwa hatima yake? Kabla ya kuweka msingi wa ulimwengu Baba alikuwa katika vita na uwezekano wa kutofaulu kwa mpango huu na hatari ya kumpoteza Mwanawe kwa nguvu za dhambi. Mwana wa Mungu angechukua uhalisia wa binadamu juu yake na kutoa fursa wazi kwa mpizani wake, shetani, kumshinda. Kabla ya kuanza

hakuwa na uhakika wa mafanikio. Baba alijiweka katika nafasi ambayo angempoteza Mwanawe milele katika juhudi za kuukomboa ulimwengu. Huruma nyingi ya Baba ikirithiwa na Mwanawe iliwekwa wazi katika ombi la Mwana kwa Baba amruhusu aje duniani kutuokoa. Je Baba angemruhusu Mwanawe kutenda hivyo? Angemruhusu ajihatarishe?

Kina cha upendo wa Baba kwetu kinapimwa na upendo wake kwa Mwanawe na hatari iliyochukiliwa ili kutuokoa. Tunapata sura ya upendo wa Baba alipozungumza wakati wa ubatizo wa Mwanawe.

> Nayo sauti kutoka mbinguni ikasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa sana naye." Mathayo 3:17 (Tyndale)

Baba anapendezwa na Mwanawe. Hakuna hazina nyingine kubwa katika maisha ya Baba kuliko Mwanawe. Kwa kuzungumza kuhusu kuzaliwa kwake mbinguni Mwana wa Mungu alishangaa:

> Kabla milima haijawekwa imara, Kabla ya vilima nalizaliwa. (26) Alipokuwa hajaiumba dunia, wala makonde Wala chanzo cha mavumbi ya dunia; (27)Alipozithibitisha mbingu nalikuwako; Alipopiga duara katika uso wa bahari; (28) Alipofanya imara mawingu yaliyo juu; Chemchemi za bahari zilipopata nguvu; (29) Alipoipa bahari mpaka wake, Kwamba maji yake yasiasi amri yake; Alipoiagiza misingi ya nchi; (30) Ndipo nilipokuwa pamoja naye, kama stadi wa kazi; Nikawa furaha yake kila siku; Nikifurahi daima mbele zake; Methali 8:25-30

Tunapata taswira ya mkono tefu wa Baba juu ya bega la Mwanawe wakishirikiana pamoja katika kuumba ulimwengu. Mungu aliumba vitu vyote kwa mwanawe, na ilimpendeza Baba kumwona Mwanawe akitenda kwa nguvu zake na akili alizokuwa amempa.

> Zamani Mungu alisema na baba zetu kwa njia ya manabii mara nyingi na kwa njia mbalimbali, (2) lakini katika siku hizi za mwisho amesema nasi kwa njia ya Mwanawe, ambaye amemweka kuwa mrithi wa vitu vyote, ambaye kwa Yeye aliuumba ulimwengu. (3) Mwana ni mng'ao wa utukufu wa Mungu na mfano halisi wa nafsi Yake, akivihifadhi vitu vyote kwa neno Lake lenye uweza… Waebrania 1:1-3a

> Baba anampenda Mwana, naye ametia vitu vyote mikononi Mwake. John 3:35

kwa ukaribu ndivyo ulivyokuwa uhusiano kati ya Baba na Mwana hadi Kristo angesema:

> "Nimekabidhiwa vitu vyote na Baba yangu: hakuna mtu amjuaye Mwana ila Baba, wala hakuna amjuaye Baba ila Mwana na ye yote ambaye Mwana anapenda kumdhihirisha Baba kwake." Mathayo 11:27

> Kama vile Baba anavyonijua Mimi, nami ninavyomjua Baba; Yohana 10:15

> Baba ampenda Mwana na kumwonyesha yale ambayo Yeye Baba mwenyewe anayafanya, naye atamwonyesha kazi kuu kuliko hizi ili mpate kushangaa. Yohana 5:20

Kama Yuda alivyoelezea kwa Yusufu kuhusu upendo wa baba yao Yakobo kwa Benjamini, hivyo tunaweza ona kuwa maisha ya Baba wa mbinguni yalikuwa "imeshikamana na roho ya kijana." Mwanzo 44:30. Kama mzazi yeyote apendaye anajua, hakuna chochote unaweza kosa kufanya kwa sababu ya upendo, kulea na ulinzi wa mtoto. Huu ndio upendo wa Baba kwa Mwanawe. Ni katika muktadha huu tunatafakari fungu kuu katika Maandiko:

> 'Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele. Yohana 3:16

Maneno haya mawili "kwa maana" yanatuzungumzia kuhusu upendo ambao hauwezi kueleweka kikamilifu. Baba alipomsikiza Mwanawe akimsihi aje atuokoe, Baba alikuwa katika hali ya kitisho cha giza kuu ambalo hakuna kiumbe kilichoumbwa kinaweza thamini kwa kweli. Baada ya mapambano makubwa Baba katika upendo kwa Mwanawe nasi alikubali ombi la Mwanawe la kukomboa jamii ya mwanadamu. Upendo wa kustajabisha huo, ajabu hiyo, upendo wa ajabu – huu unafaa kuwa wimbo wetu hadi mwisho wa umilele.

kama tulivyoonyesha hapo mbeleni, kuteseka kwa Kristo hakukuwa kumefungwa tu kwenye huduma yake duniani. Mara tu dhambi ilipotokea kukawaa na Mkombozi. Ni Roho wa Kristo aliyekuwa ameendeleza jozi

takatifu edeni. Walipokula tunda kulingana na mapendekezo ya shetani aliyekuwa ndani ya joka, Kristo alivunjwa kwa kumkataa yeye na Baba yake. Baada ya yote waliokuwa wamepewa, ubinafsi wao na kutokuwa na shukurani kulimsababishia Kristo uchungu mkubwa kama mzazi yeyote ajuavyo wakati watoto wao wanapowageuka. Lakini bado Kristo hakuwaacha. Njia pekee ambayo wangekuwa na uzima ilikuwa ni kwa yeye kukakaa nao katika Roho na Kuendelea kuwapa uzima kila wakati walipoikanyaga sheria na tabia ya Baba yake.

Kila wakati Waisraeli walipotenda dhambi walifaa kuleta mwanakondoo kama sadaka.

> Na mtu awaye yote katika watu wa nchi akifanya dhambi pasipo kukusudia, kwa kufanya neno lo lote katika hayo ambayo Bwana alizuilia yasifanywe, naye akapata hatia; (28) akijulishwa hiyo dhambi yake aliyoifanya, ndipo atakapoleta mbuzi mke mkamilifu, awe matoleo yake kwa ajili ya dhambi yake aliyoifanya. (29) Naye ataweka mkono wake kichwani mwake hiyo sadaka ya dhambi, na kumchinja sadaka ya dhambi mahali hapo pa sadaka ya kuteketezwa. Kisha atayaondoa mafuta yake yote, kama vile mafuta yanavyoondolewa katika hizo sadaka za amani; kisha kuhani atayateketeza juu ya madhabahu, iwe harufu ya kupendeza kwa Bwana; na kuhani atafanya upatanisho kwa ajili yake, naye atasamehewa.(32) Naye akileta mwana-kondoo kuwa sadaka ya dhambi, ataleta wa kike mkamilifu. (33) Naye ataweka mkono wake kichwani mwake sadaka ya dhambi, kisha atamchinja awe sadaka ya dhambi, mahali hapo wachinjapo sadaka ya kuteketezwa. Walawi 4:27-29, 31-33

Mpangilio huu unadhihirisha ukweli wa kuhuzunisha kuwa kila dhambi husababisha mateso kwa Mwana wa Mungu. Tangu kwa dhambi ya kwanza hadi leo hii, Kristo anateseka kwa uchungu wa kukataliwa na huzuni ya kina kwa yale amabyo wana wake waliopotea wanawafundisha wengine duniani. Kila dhambi humfanya kusulubiwa mara ya pili na kumfedhehesha kwa dhahiri. Waebrania 6:6. Kiwango hiki cha kuteseka ni zaidi ya ufahamu wetu; inaonekana kwetu haiwezekani kabisa kuwa kuteseka kwa Kristo sio saa arobaini tu, kupelekea na kuhusisha msalaba, au hata miaka thelathini na mitatu duniani, lakini kwa kweli miaka elfu sita ya kuteseka na kukataliwa kila siku. Kama ingewezeka kwetu kufahamu mateso yote jinsi yanafika katika

moyo wa Baba, tunaweza ona kwa kweli mateso ya Baba sio tofauti na yale ya Mwanawe, kwa kuwa kila mzazi huteseka mwanawe anapoteseka.

Kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na nafsi Yake mwenyewe, akiwa hawahesabii watu dhambi zao. Naye ametukabidhi sisi ujumbe huu wa upatanisho 2 Wakorintho 5:19

Tunaweza lakini kwa umbali tambua mateso ya Baba alipokuwa akitazama kwa makini jinsi ulimwengu ulivyomfanya Mwanawe? Tunaweza fikiria sikitiko moyoni mwa Baba Mwanawe alipomuuliza:

> …"Baba yangu, kama inawezekana, kikombe hiki na kiniepuke, lakini si kama nitakavyo mimi bali kama utakavyo Wewe." Mathayo 26:39

Tunaweza pata faraja kiasi katika kujua kuwa kuteseka kwa Kristo kulitendeka miaka elfu mbili iliyopita, lakini sasa hivi Kristo anateseka kwa watoto wote ambao shetani amenasa katika biashara ya kuwauza watoto kwa ngono; anateseka kwa wote wasio na makao na wana ambao wanaangamia kwa njaa, yaliyofanywa hivyo kwa ubinafsi wa mwanadamu; kwa waathiriwa wa ukatili wa kinyumbani na ubakaji; kwa mamilioni walioshikwa katika matumizi ya dawa na kilio; kwa mamia ya watu ambao wanatafuta kujiua kila siku — Kristo anayahisi yote na ndivyo ilivyo pia kwa Baba. Mateso haya hayajafungwa kwa waaathiriwa wa ukatili tu mbali pia kwa wahusika. Roho wa Kristo anatafuta kuwabadilisha wanyanyasaji wa wenzao kwa kuwatia hatiani kwa dhambi zao. Hatia inayohisika inatumwa kwao, sio kuwahukumu lakini kuwaokoa kutoka kwa kuifanya mioyo yao kuwa Migumu na kupoteza nafsi zao. Makosa yanayohisiwa hutumwa kuwakomboa, sio kuwahukumu tu. Nafsi inapozima kosa kwa kileo na dawa au chochote ili kuzuia akili kufikiria kuhusu kile ambacho kimetendwa, hivyo Kristo anadharauliwa, anakataliwa na kunyamazishwa. Hili linatendeka kwa mabillioni ya nafsi kila siku, wanapogeuka kutoka kwa upendo wa kujitoa nafsi wa msalaba huu, sura inayometameta sana na yenye kungaa kwa kutazama.

Katika kiwango hiki tunaweza jaribiwa kulia kama Mafarisyo:

> …"Wewe ambaye utalivunja hekalu na kulijenga kwa siku tatu, jiokoe mwenyewe basi! Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, shuka kutoka msalabani."(41)Vivyo hivyo, viongozi wa, makuhani, walimu

> wa sheria na wazee wakamdhihaki wakisema,(42) "Aliwaokoa wengine, lakini hawezi kujiokoa mwenyewe!. Yeye ni Mfalme wa Israeli! Ashuke sasa kutoka msalabani, tutamwamini. Mathayo 27:40-42

Tunaona mwitikio wa kweli katika maisha ya Maria Magdalena. Alifahamu kile Kristo angeteseka msalabani kwa ajili yake, na aliamini kuwa kupitia kwa matendo yake alisamehewa. Kwa shukurani alijaza pomoni hadi ya kamwagika manukato ya fedha za tajiri ambayo yalikuja kutoka kwa chupa ya sanduku iliyotengenezewa mfalme.

Bado swali linaweza ulizwa: kama Mungu ni mwenye nguvu nyingi mbona basi anaruhusu yeye mwenyewe na Mwanawe kukabiliwa kwa mateso mengi na uchungu mwingi? Pili, mbona haingilii kati na kumaliza tu mateso haya yote? Hii ni mada yetu ya sura ifuatayo. Tazama Mwana wa Mungu azichukuae dhambi za ulimwengu, na ushangae kwa upendo na ustahimilivu wa Baba yetu wa mbinguni kuvumilia mateso haya kwa miaka elfu sita iliyopita. Kwa kweli, Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee.

# 5. Wapende Adui zako

Wakati Yohana mbatizaji alimwasilisha Yesu kama Masihi, tumaini la taifa kuu lililotengenezwa upya lilifufuka. Mawazo ya Mshindi kama Yuda Maccabees aliyetupilia mbali nira ya ufalme wa Seleucid yalichochea nguvu za taifa la Wayahudi walipofikiria hatima yao ya sasa chini ya mikono na nguvu za Roma. Umati mkubwa ulipoanza kumzingira mwalimu huyu mpya na wakaona jinsi alivyoonyesha nguvu zake kupitia kuwaponya wagonjwa, hisia za matarajio zilianza kujitokeza.

> Yesu akapita katika Galilaya yote, akifundisha katika masinagogi yao, akihubiri Habari Njema za Ufalme wa Mungu, akiponya kila ugonjwa na kila aina ya maradhi miongoni mwa watu. (24) Kwa hiyo sifa zake zikaenea sehemu zote za Shamu, nao watu wakamletea wote waliokuwa na magonjwa mbalimbali na maumivu, waliopagawa na pepo, wenye kifafa na waliopooza, naye akawaponya. (25) Makutano makubwa ya watu yakawa yanamjia kutoka Galilaya, Dekapoli, Yerusalemu, Uyahudi na kutoka ng'ambo ya Mto Yordani. Mathayo 4:23-25

Baada ya Yesu kuwateua wanafunzi kumi na wawili, Yesu alienda nao kwenye ufuo wa bahari. Umati ulianza kukusanyika, wengine kusikiza na wengine kuponywa. Umati ulipokuwa mkubwa Yesu aliwaongoza mlimani alipoanza

kuzungumza. Mibaraka iliyokuwa ikitoka midomoni mwake ilikuwa sio kama chochote ubinadamu umewahi sikia. Alianza mjadala wake kwa kauli kama:

Heri wenye upole, heri rehema na heri wapatanishi. Mathayo 5:5,7,9. Badala ya kuwapa mibaraka chungu nzima kwa mashujaa wanaotumia upanga wao kwa ustadi kwa minajili ya ukweli. Alinena mibaraka juu ya walioudhiwa kwa ajili ya haki na waliovumilia shutuma na kuudhiwa kwa ajili yake. Mathayo 5:10,11. Hakunena maneno kama ya Generali mweye kisasi akiandaa majeshi yake kwa vita, lakini badala yake upole, utulivu na upendo wa Baba yake aliotaka uonekani ndani ya wafuasi wake wote.

Maneno haya yaliyonenwa na Kristo, hakuyafunza tu bali aliishi kila nukta katika maisha yake ya duniani. Huruma zake, na uvumilivu wake kwa watu wote ulikuwa kwenye maonyesho. Katika kumalizia huduma yake uvumilivu dhidi ya kukejeliwa, kupigwa na kifo haukuonyesha hata uzi mmoja wa kutisha na kulipiza kisasi. Kile alichofunza siku hiyo kilionyesha yeye ni nani hasa, na kama mwakilishi wa Baba yake, alidhihirisha jinsi Mungu alivyo. Ni muhimu kuelewa kwamba Yesu hakutwambia tufanye jambo ambalo halifanyi yeye mwenyewe, kwa sababu yeye ni Mungu anatumia kanuni tofauti kwake na zetu. Hapana. Ni kwa sababu yeye ni Mungu kuwa anaishi jinsi hasa aliyozungumza kwetu pale mlimani.

Maneno ya Yesu yalikata kwa kina matarajio na kiburi cha Wayahudi, na kwa vile maneno haya yanazungumzwa kwa jumla kwa wanadamu wote basi pia yanakata kwa kina kiburi na matarajio yote ya mwanadamu. Tunagundua ukweli kuwa uzuri wa Mungu kwa mtazamo wa mtu mwenye dhambi humwelekeza kwa toba na kumfunulia maana ya maneno ya ufunguzi ya Yesu katika mahubiri yake – Heri walio masikini wa kiroho na heri wenye huzuni kwa sababu ya ubinafsi wa kiburi na matarajio yao.

Mwana wa Mungu hukata kwa kina na bado kwa kina, matatizo ya mwanadamu anapozidi kunena:

> "Mmesikia walivyoambiwa watu wa zamani kwamba, 'Usiue, ye yote atakayeua atapasiwa hukumu.' 22Lakini mimi nawaambia kwamba, ye yote atakayemkasirikia ndugu yake wa kiume au wa kike, atapasiwa hukumu. Tena, ye yote atakayemwambia ndugu yake wa kiume au wa kike, 'Raca' a , yaani kumdharau na kumdhihaki, atapasiwa kufanyiwa baraza. Lakini ye yote atakayesema 'We

> mpumbavu ulaaniwe!' Atapasiwa hukumu ya moto wa jehanam. Mathayo 5:21-22

Yesu anapanua maneno yaliyopeanwa na Musa karne nyingi zilizopita. Hatangui hata yodi au nukta ya torati lakini badala yake kuongeza ukuu na utukufu wenye mwanga.

> Usimchukie ndugu yako moyoni mwako; ni lazima kumkemea jirani yako, wala usichukue dhambi kwa ajili yake. (18) Usifanye kisasi, wala kuwa na kinyongo juu ya wana wa watu wako; bali umpende jirani yako kama nafsi yako; Mimi ndimi Bwana. Walawi 19:17-18

Nani asiyekasirika na mtu anayemtende mabaya? Nani hajawahi kuwa na fikira za kulipiza wale ambao kwa wakati fulani walitudunisha au kutuaibisha? Nani ambaye ameweza kutochukia kabisa kwa mtu yeyote kwa wakati fulani? Baadaye mtume Yohana kwa kupanua maneno ya Yesu aliandika maneno haya:

> Ye yote amchukiaye ndugu yake ni mwuaji, nanyi mwajua ya kwamba mwuaji hana uzima wa milele ndani yake. 1 Yohana 3:15

Ni ufalme wa namna gani huu ambao Yesu anazungumzia? Kumchukia mtu inamaanisha kuwa wewe ni muuaji anayestahili kifo? "Jehanamu ya moto" au moto wa jehenamu katika Mathayo 5:22 ambao Yesu anazungumzia kuhusu? Uliza Kaini alaivyolia kwa dhiki – adhabu yangu imekuwa kubwa, haichukuliki! Mwanzo 4:13 (Wycliffe). Uliza Yesu alipokuwa msalabani akibeba uovu wa wanadamu wote chuki, kisasi na ubinafsi; mulize kuhusu - "Jehanamu ya moto" ambayo huja kwa wanaoishi jinsi hii.

Kweli mtu aliye karibu nawe amewahi kukasirisha kwa kina? Umewahi hisi hasira dhidi yao? Umewahi pambana na kuacha kufikiria jinsi wamekujeruhi na namna gani unataka kuwaona wakiletwa kwenye haki? Je, hii sio Jehanamu ya kudumu? Je, fikira kama hizo hazituchomi mioyoni mwetu? Ni kwa namna gani moyo unavyokabiliana na fikira mawazoni mwetu kuhusu kweli ya kumtaka mtu afe? Ni namna gani Roho wa Yesu, akaae karibu Zaidi kuliko ndugu, anahisi tunaporuhusu mawazo ya kuazia wengine kifo? Pengine tunajua kuwa kuwawazia kifo ni hatia lakini tunahisi kwamba hatutaki kuwaona tena. Ila hili sio tunda la mti huo huo lililopakwa rangi tofauti? Ni namna gani yesu anateseka katika moto huu wa jahanamu tunaporuhusu mawazo kama hayo kututawala?

Maneno ya Yesu ni mashambulizi ya moja kwa moja kwa mambo ya kawaida ya jinsi wanadamu wanahusiana wao kwa wao. Wito wa upole, unyenyekevu na uvumilivu machoni pa unyanyasaji na kutendewa maovu kunahitaji kwa wasikilizaji zaidi ya yale wanayoweza kupeana, na hili ndilo kusudi. Kama yesu anavyosema:

> Yesu aliposikia haya akawaambia, "Walio wazima hawahitaji tabibu, bali walio wagonjwa. Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi." Marko 2:17

Yesu anaendelea na hotuba yake ya usahihi kama wa wembe, ili kuunda mioyo ya wanadamu kupokea neema yake: Katika sentensi moja anaanika ubinafasi wa kila mtu.

> "Mmesikia kwamba ilinenwa, 'Usizini'. (28) Lakini mimi nawaambia: kwamba ye yote amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake. Mathayo 5:27-28

Mtu awaye yote ambaye ni mwaminifu kwake yeye mwenyewe anajua kuwa maneno haya yanazungumza moja kwa moja juu kwa misingi ya shida zake na kumkemea kabisa. Yesu anatangaza shida kuwa *ubinafsi* ambao moyo wa mtu binafsi unapaswa kufanyiwa marekebisho. Mungu analenga kupanda kanuni mpya ndani ya mtu, kanuni ambayo hana na hawezi kuipata yeye mwenyewe. Mungu mwenyewe anatupa Imani ya Kristo, "ufalme wa mbinguni ndani yako," ambao ukipokewa basi "Mambo yote huwa mapya." Mtu wa maisha ya imani na vitendo ni kielelezo tu cha kanuni hiyo, mibaraka ambayo huanza ndani na kutiririka nje kwa watu wengine wanaomzunguka, bila kuzingatia serikali au utamaduni ulio ndani yake. Ulimwengu unadhani kuwa Mungu atatenda nje kisha afanye ndani. Mwanadamu hudhani kuwa Mungu atarekebisha ulimwengu kwanza, kuangamiza waovu na kisha kuanzisha taifa la wanaostahili. Lakini mpango wa kuanza nje kisha kujaribu kufanya ndani, umeanguka daima na daima utaanguka. Mara tena kile ambacho Yesu anaagiza hakitawezekana kwa mwanadamu, lakini na Mungu na Neema ndani ya Kristo mambo yote yanawezekana.

Iwapo kuna yeyote ambaye anaamini moyoni mwake kuwa hajawahi tenda lolote mbaya, maneno yafuatayo kutoka kwa Kristo huvunja uwezekano isipokuwa kwa kutambua dhambi na kuukubali msalaba.

> “Mmesikia kwamba ilinenwa,‘Jicho kwa jicho na jino kwa jino.’ (39) Lakini mimi nawaambia, msishindane na mtu mwovu. Lakini kama mtu akikupiga kwenye shavu la kuume, mgeuzie na la pili pia, (40) Kama mtu akitaka kukushtaki na kuchukua shati lako, mwachie achukue na koti pia. (41) Kama mtu akikulazimisha kwenda kilometa moja, nenda naye kilometa mbili. (42) Mpe yeye akuombaye,wala usimgeuzie kisogo yeye atakaye kukukopa.” (43“Mmesikia kwamba ilinenwa,‘Mpende jirani yako na umchukie adui yako.’ (44) Lakini mimi ninawaambia:Wapendeni adui zenu na waombeeni wanaowatesa ninyi, (45) ili mpate kuwa watoto wa Baba yenu aliye mbinguni. Kwa maana Yeye huwaangazia jua lake watu waovu na watu wema, naye huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki. (46)Kama mkiwapenda wale wanaowapenda tu, mtapata thawabu gani? Je, hata watoza ushuru hawafanyi hivyo?(47)Nanyi kama mkiwasalimu ndugu zenu tu, je, mnafanya nini zaidi ya wengine? Je, hata watu wasiomjua Mungu, hawafanyi hivyo?(48)Kwa hiyo iweni wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu.” Mathayo 5:38-48

Umewahi sikia mtu akisema mambo yasiyokuwa yako na kukupiga? Yesu anasema mgeuzie shavu la pili pia. Orodha ya mambo yanayoagizwa hapa hayawezekani kabisa kuimarishwa katika maisha ya mtu, lakini bado Yesu anadhihirisha kwetu hati ya utambulisho wa ufalme wake. Inawezekanaje kumpenda adui yako? Uwapende wanaotaka kukuua? Uwapende wale wanaotaka kukudhuru na uwapende wale ambao daima wanatafuta kukuumiza? Yesu anatuagiza tuwapende? Kwa sababu gani?

“Ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni.”

Umeelewa hilo? Iwapo wewe ni mpole, mwenye huruma, mngwana na mtulivu na unawapenda adui zako basi unadhihirisha kuwa wewe ni mwana Baba yako aliye mbinguni. Hilo lina maana gani? Lina maana kuwa hivi ndivyo Baba alivyo! Kama hufanya jua kuwaangazia waovu na wema, basi kama wana wake tutaweza kuangaza upendo wetu kwa uovu na wema kwa sababu hivi ndivyo Baba yetu wa mbinguni alivyo. Haya ndio mahubiri makuu kuwahi kuhubiriwa kwa sababu yanazungumza juu ya uwepo wa Utu mkuu wa ajabu ulimwenguni, Baba yetu wa mbinguni. Anadhihirishwa kwetu kupitia kwa Mkombozi wetu wa thamani sana, Mwana wa Mungu aliyehai, Ajuae jinsi alivyo hasa. Hakuna kiumbe mwingine ulimwenguni kwote ajuae jinsi Baba alivyo na katika mahubiri haya tunaona tabia ya Baba ikidhihirishwa kwetu.

Hoja ya kutia muhuri ukweli huu ni katika maneno ya mwisho ya sura ya tano ya Mathayo.

> Kwa hiyo iweni wakamilifu kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu."  Mathayo 5:48

Hili linatudhibitishia kuwa kila kitu ambacho Yesu amesema katika mahubiri yake ni ufunuo wa tabia yake ya upendo. Maneno haya yanatuzungumzia kuhusu jinsi Baba yetu hushughulikia hali. Kitabu cha Luka kinaongezea neno ukamilifu ambalo Mathayo analitumia kwa njia hii:

> Iweni na huruma, kama Baba yenu alivyo na huruma. Luka 6:36

Hivyo ukamilifu unapatikana katika huruma. Swali ambalo lazima liulizwe ni. Kama Mungu huwapenda adui zake na anadhihirisha kwetu kupitia kwa Mwanawe ambaye yuko radhi kuyatoa maisha yake kwa wale wamchukiao, basi mbona Biblia inaonekana kufundisha kuwa Mungu anawachukia adui zake na chuki kamilifu na katika joto ya hasira yake yuko tayari, kwa ajili ya kuwaokoa wenye haki, kuwapendua waovu kwa kuita moto na kibiriti ushuke, kuwatazama wakifa tu katika kilio cha hofu na masumbuko makali?

Hili ni swali ambalo lazima tuligeukie aidha, kwa vile kuna hadithi nyingi katika agano la kale ambazo zinaonekana kutuonyesha kuwa Mungu yuko tayari kuwapenda adui zake kwa kiwango, lakini kisha huachilia hasira yake ya ndani ambayo hupasuka kama moto na kuwalipuwa kutoka kwenye uso wa dunia.  Baadhi hupendekeza kuwa huu ni ukumbusho muhimu kuwa tusicheze na Mungu na kuwa hata ana mipaka ambayo tukiivuka, tutalipa na maisha yetu na kwa namna ya makali. Jinsi tunavyopatanisha ukamilifu wa Mungu kuhusu yale Yesu aliyanena katika mahubiri juu ya mlima na hadithi tunazosoma katika Agano la Kale ni lengo la kitabu hiki kwa sababu kwa watu wengi kuna utengano mkubwa kati ya Yesu katika injili na Mungu katika Agano la kale, ila linalostajabisha vya kutosha ni Musa aliyeagizwa kuyaandika maneno hayo katika Walawi, umpende adui yako na chuki dhidi yake.

Utengano huo huo ulikuwepo bado na wale waliomsikia Yesu miaka 2000 iliyopita. Kwa wale walio amini kuwa ufalme ambao Yesu alielezea  ni ule wa Mungu na kwamba uliwakilisha tabia yake, Maneno ya Yesu na Huduma yalikuwa halufu ya maisha kwa maisha. Kwa wale ambao hawa kuruhusu matarajio yao yaondoke ulimwenguni huu na kuamini kuwa yesu

hakuonyesha tabia yake hasa ya Mungu wala jinsi ufalme wa Mungu unapaswa kuwa, Mbegu zilikuwa pale za kumchukia, Kristo kwao alikuwa mzushi. Hawakuwahi kumjua Mungu ambaye Yesu alielezea. Kwa hivyo, hawangemuona Yesu kama Mwana wa Mungu waliyeabudu. Iwapo yale Yesu alisema ni kweli, pengine hawakumjua Mungu wa kweli ama Mungu wao alikuwa amebadilisha mwenendo wake.

Je, Mungu hutimiza ahadi zake asemapo:

> Kwa kuwa mimi, Bwana, sina kigeugeu; ndio maana ninyi hamkuangamizwa, enyi wana wa Yakobo. Malaki 3:6

Mungu wa injili ni sawa na Mungu wa Musa, Ibrahimu na Nuhu? Yesu Kristo ni yule jana, leo, na milele? Waebrania 13:8. Haya ni maswali ambayo huhitaji uamuzi. Kwa sasa, hebu na tufurahi kwa ufunuo wa Baba ambao Kristo alitupa juu ya mlima na tutiwe moyo kuwa tukiwa na Kristo hatutapenda rafiki zetu tu bali adui zetu pia.

# 6. Moto kutoka Mbinguni

Kadri wanafunzi walikaa na Yesu, walishangazwa na maneno na matendo yake. Mwanga wa ufalme aliokuwa ameutangaza katika mahubiri ya mlimani ulikuwa unatafuta kupenya kwenye pa la giza la akili zao. Bado wakichafuliwa na ukuu wa duniani, wanafunzi waligeuza mawazo yao kwa nafasi wanazoweza kushikilia katika ufalme wa Mbinguni. Hili kwa kiasili lilipelekea kuwepo kwa majadiliano mengine:

> Kukazuka mabishano miongoni mwa wanafunzi kuhusu ni nani miongoni mwao atakayekuwa mkuu kuliko wote. Luka 9:46

Mbona mawazo yao yaligeuka kwa umuhimu wa nafsi zao wenyewe? Walisisimuliwa na nguvu za Mungu zilizokuwa wazi ndani ya Yesu, lakini bado hawakuukumbatia msalaba wake. Walihofia kumuuliza kuhusu maana ya msalaba kwa sababu ilipendekeza kuwa ungekatisha tamaa matumaini yao.

> Watu wote wakastaajabia uweza mkuu wa Mungu. Wakati bado watu wanastaajabia hayo yote aliyokuwa akiyafanya Yesu, Yeye akawaambia wanafunzi Wake: (44) "Sikilizeni kwa bidii haya nitakayowaambia sasa: "Mwana wa Adamu atasalitiwa na kutiwa mikononi mwa watu." (45) Lakini wao hawakuelewa alimaanisha nini. Maana ya maneno hayo ilifichika kwao,hivyo hawakuyaelewa, nao wakaogopa kumwuliza maana yake. Luka 9:43-45

Yesu alijua mawazo yao ya ukuu na akamchukua mtoto mdogo na kumkumbatia mikononi mwake kisha akawaambia:

> Kisha akawaambia, "Ye yote atakayemkaribisha mtoto huyu mdogo kwa Jina langu, atakuwa amenikaribisha Mimi na ye yote atakayenikaribisha Mimi, atakuwa amemkaribisha Yeye aliyenituma, kwa maana yeye aliye mdogo miongoni mwenu, ndiye aliye mkuu kuliko wote." Luka 9:48

Mtoto asiye na hatia hakuwa na hamu ya kitaifa. Katika unyenyekevu wa uelewa wake alijibu ukunjuvu na mguzo tefu wa Bwana. Huu ulikuwa ufafanuzi wa ukuu katika ufalme wake – Upendo rahisi, wa kudumu na wa kuaminiwa wa Bwana. Unyoofu wa wanafunzi ulikuwa umeondolewa na matarajio na kukatishwa tamaa na maisha, lakini Yesu alikuwa amekuja kuwarejeshea unyoofu wa utotoni ukiunganishwa na hekima ya miaka.

Katika uhusiano wao na Yesu, wanafunzi walimpenda. Kila siku waliona huruma na upendo kwa watu na wakasikia mambo mazuri alionena kuhusu Baba yake? Siku moja, baaada ya kipindi kirefu cha kazi aliwatuma wanafunzi katika kijiji cha Samaria kutafuta jumba kwa ajili ya usiku.

> Wakati ulipokaribia wa Yeye kuchukuliwa mbinguni, alikaza uso Wake kwenda Yerusalemu. (52) Akatuma watu wamtangulie, nao wakaenda katika kijiji kimoja cha Samaria kumwandalia kila kitu, (53) lakini watu wa kijiji kile hawakumkaribisha kwa sababu alikuwa anakwenda Zake Yerusalemu. Luka 9:51-53

Wanafunzi wake walipoona jinsi Wasamaria walivyomtenda Bwana wao, walichukizwa na ukosefu wao wa ukarimu. Katika joto za hisia zao walidhihirisha kina cha giza linalopatikana Moyoni mwa mwanadamu.

> Wanafunzi Wake, yaani, Yakobo na Yohana walipoona hayo, wakasema: "Bwana, unataka tuagize moto kutoka mbinguni ili uwaangamize kama Eliya alivyofanya?" Luka 9:54

Ingeonekana kuwa walikuwa na kinga ya Kibibilia kwa mpango wao wa mauaji ya kuwachoma Wasamaria. Walitaja hadithi ya Eliya ambaye alikuwa ameitisha moto kutoka mbinguni juu ya baadhi ya waliokuwa wameamua kumuumiza. Wakiwa wamejihami na hadithi hii, wanafunzi walijihisi wamejikinga kikamilifu kwa kuagiza kifo cha Wasamaria hawa wasio na shukurani. Jibu ambalo yesu aliwapa liliweza kuwajia kama mshtuko kabisa.

> Yesu akageuka na kuwakemea, 56kwa maana Mwana wa Adamu hakuja kuziangamiza roho za watu, bali kuziokoa. Luka 9:55-56

Maneno haya yanadhihirisha moyo wa huruma na tabia ya Yesu. Yesu sio muangamizaji lakini badala yake mkombozi. Kwa wakati huo huo pia ingionekana kuwa Yesu hakuwakemea wanafunzi wake tu bali pia matendo ya Eliya.

> Ndipo mfalme akatuma akida wa askari hamsini pamoja na hamsini wake, wamwendee Eliya. Akamwendea, na tazama, ameketi juu ya kilima. Akamwambia, Ewe mtu wa Mungu, mfalme asema, Shuka. (10) Eliya akajibu, akamwambia yule akida wa hamsini, Ikiwa mimi ni mtu wa Mungu, na ushuke moto kutoka mbinguni, ukuteketeze wewe na hamsini wako. Moto ukashuka, ukamteketeza, yeye na hamsini wake 2 Wafalme 1:9-10

Kusoma kwa juu kwa hadithi hii kutaonekana kukiashiria kuwa ingawa Yesu alikuja duniani kukomboa maisha ya watu, Mungu katika Agano la Kale alikuwa tayari kuwateketeza watu wakiwa hai kwa kujaribu kumshika nabii wake. Yesu alikemea chuki ya wanafunzi ya kutaka kuwateketeza Wasamaria tu ama pia alikemea matendo ya Eliya pia? Jibu ambalo Yesu anawapa wanafunzi wake kuhusu huduma yake linaashiria kuwa alimkemea Eliya pia. Ni namna gani Yesu angewakemea wanafunzi akisema kuwa huduma yake ilikuwa kuwaokoa watu na aonyeshe kuwa katika wakati fulani atawaangamiza? Kama ni hivi, Yesu angewaambia sasa sio wakati wa mambo haya au tuwaombee kwa muda kiasi. Yesu hapeani dalili yoyote ya kuchelewesha adhabu. Anazungumzia tu kuokoa maisha ya watu kinyume na kuwaangamiza.

Taarifa hii ya Yesu katika toleo la king James inaonekana kuwa aibu kabisa sana kwa tafsiri nyingi za sasa za Bibilia kwa sababu maneno haya hayuko pale.

> Yesu akageuka na kuwakemea, (56) nao wakaenda kijiji kingine. Luke 9:55-56 (NIV)

> Akageuka na kuwakemea, (56) nao wakaenda kijiji kingine. Luke 9:55-56 (RV)

Uwepo wa  kuondolewa kwa maneno hayo katika tafsiri mbalimbali una matokeo mengi ya kuelewa tabia ya Mungu. Swali moja kuu ambalo lazima

lizuke ni hili: Nani aliyeleta moto kutoka mbinguni ukawachoma hao watu? Tunahitaji kurejelea kidogo katika hadithi ya Eliya kwa jambo muhimu ambalo Mungu alimwonyesha baada ya ushindi wake mkuu juu ya mlima Karmeli

> Akasema, Toka, usimame mlimani mbele za Bwana. Na tazama, Bwana akapita; upepo mwingi wa nguvu ukaipasua milima, ukaivunja-vunja miamba mbele za Bwana; lakini Bwana hakuwamo katika upepo ule; na baada ya upepo, tetemeko la nchi; lakini Bwana hakuwamo katika lile tetemeko la nchi; (12) na baada ya tetemeko la nchi kukawa na moto; lakini Bwana hakuwamo katika moto ule; na baada ya moto sauti ndogo, ya utulivu. 1 Wafalme 19:11-12

Ni wazo lipi ambalo Mungu alitaka kuonyesha kwa Eliya? Kanuni sawa inaonyeshwa kwingineko katika maandiko:

> Akajibu akaniambia, akisema, Hili ndilo neno la Bwana kwa Zerubabeli, kusema, Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa roho yangu, asema Bwana wa majeshi. Zakaria 4:6

Mungu alikuwa akimwambia Eliya kuwa hatumi nguvu kuwalazimisha watu kumtii na kuongeza utawala wake lakini badala yake ni sauti yake ndogo tulivu inayotenda mioyoni mwa watu na kuwageuza kwa ukweli. Inapingana kwa Mungu kumwambia Eliya kuwa hakuwa katika moto na kisha kugeuka na kuwateketeza watu 102 waliotafuta kumshika Eliya. Walikuwa 102 kwa sababu moto ulishuka mara mbili kwa vikosi viwili vya hamsini na viongozi wao. Ni ukweli kuwa Mungu alituma moto kula dhabihu juu ya madhabahu lakini moto huyu haukutumwa kuwaangamiza watu mbali kuwaokoa. Eliya alipoita moto ushuke juu ya watu hawa, tayari alikuwa ameonyeshwa kuwa Mungu hakuwa katika moto huo kuwalazimisha watu kutii. Utiifu wa kutambaa wa akida wa kikosi cha tatu haukuwa utiifu ambao Mungu alikuwa anatafuta.

> Tena akatuma akida wa hamsini wa tatu, pamoja na hamsini wake. Yule akida wa hamsini wa tatu akapanda, akaenda akapiga magoti mbele ya Eliya, akamsihi sana, akamwambia, Ee mtu wa Mungu, nakusihi, roho yangu, na roho za watumishi wako hawa hamsini, ziwe na thamani machoni pako. 2 Wafalme 1:13

Mtu huyu alipiga magoti kwa heshima kwa Mungu wa Eliya kwa sababu alimpenda na alitaka kuabudu? Bila shaka hapana! Aliogopeshwa kuwa

angeuawa  na alikuwa akisihi kwa uhai wake. Kama ibada ya jinsi hii ilikuwa imekubalika kwa Mungu, basi Yesu angeitisha moto ushuke juu ya mafarisayo wachache na Warumi wachache, na kila mtu angekuwa akimwabudu mara moja – sio kwa sababu ya upendo kwake, lakini badala yake kwa hofu.

Kwa hivyo sio Mungu aliyekuwa katika moto huo uliowala watu hao. Basi tuna kadiriaje yaliyotendeka hapo?

> Ndipo mfalme akatuma akida wa askari hamsini pamoja na hamsini wake, wamwendee Eliya. Akamwendea, na tazama, ameketi juu ya kilima. Akamwambia, Ewe mtu wa Mungu, mfalme asema, Shuka. (10) Eliya akajibu, akamwambia yule akida wa hamsini, Ikiwa mimi ni mtu wa Mungu, na ushuke moto kutoka mbinguni, ukuteketeze wewe na hamsini wako. Moto ukashuka, ukamteketeza, yeye na hamsini wake 2 Wafalme 1:9-10

Akida na watu wake walikuwa chini ya mamlaka ya mfalme wa Israeli ambaye alikuwa ameagiza msaada kutoka kwa Baalzebub, mungu wa Ekroni. Mungu wa Ekroni alikuwa mungu wa uongo aliyeongozwa na shetani. Kwa kutafuta msaada kwa mungu huyu, alikuwa anajifungua kwa mamlaka ya shetani.

> Je, hamjui kwamba mnapojitoa kwa mtu ye yote kama watumwa watiifu, ninyi ni watumwa wa yule mnayemtii, aidha watumwa wa dhambi, ambayo matokeo yake ni mauti, au wa utii ambao matokeo yake ni haki? Warumi 6:16

Hata kama watu hawa waliokuwa wakimwakilisha mfalme walikuwa wamejiweka katika utawala wa shetani, akida bado alimtambua Eliya kama mtu wa Mungu. Waisraeli walikumbuka kilichotendeka katika Mlima karmeli walipoona kuwa Mungu alikuwa na Eliya. Kama akida aliamini kuwa Eliya alikuwa mtu wa Mungu mbona Eliya alitafuta ishara kuthibitisha? Tunagundua jibu baadaye kidogo katika sura hii:

> Malaika wa Bwana akamwambia Eliya, Shuka pamoja naye; **usimwogope**. Akaondoka, akashuka pamoja naye hata kwa mfalme.  2 Wafalme 1:15

Eliya aliambiwa asihofu. Mbona Eliya akahofu? Tatizo linatokea tu baada ya matukio ya Mlima Karmeli.

> Eliya akawaambia, Wakamateni hao manabii wa Baali, asiokoke hata mmoja. Wakawakamata; na Eliya akawachukua mpaka kijito cha Kishoni, akawaua huko. 1 Wafalme 18:40

Kabla ya Eliya kuwaua manabii wa Baali alikuwa amesimama kwa ujasiri mbele ya mfalme na watu wake. Kabla ya hili, Eliya alikuwa ametafutwa kwa zaidi miaka mitatu baada ya kuenda kwa ujasiri mbele za mfalme kumwambia kuwa hakutakuwa na mvua. Haijatajwa kuwa Eliya alikuwa na hofu katika haya yote aliyoyapitia. Ilikuwa tu baada ya Eliya kuwaua manabii wote wa Baali *kwa upanga* ndivyo akawa na hofu.

> Ndipo Yezebeli akampelekea Eliya mjumbe, kusema, Miungu wanifanyie hivyo na kuzidi, nisipokufanya roho yako kesho, panapo wakati huu, kama roho ya mmojawapo wa hao. (3) Naye alipoona hayo, aliondoka, akaenda aihifadhi roho yake, akafika Beer-sheba, mji wa Yuda, akamwacha mtumishi wake huko. 1 Wafalme 19:2-3

Itaonekana kuwa kuna kanuni ya kinyumenyume inayohusiana na kanuni ya dhahabu na inaenda hivi. "mambo mabaya unayowatendea wengine utahofu kuwa yatatendwa kwako." Hili lilikuwa hakika kwa yale Kaini aliyoyapitia:

> Kaini akamwambia Bwana, Adhabu yangu imenikulia kubwa, haichukuliki. 14 Tazama, umenifukuza leo katika uso wa ardhi, nitasitirika mbali na uso wako, nami nitakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani**; hata itakuwa kila anionaye ataniua.** Mwanzo 4:13-14

Baada ya Eliya kutoroka mikono miovu ya Yezebeli alisema maneno ya kustajabisha.

> Lakini yeye mwenyewe akaendelea katika jangwa mwendo wa siku moja, akaenda akaketi chini ya mretemu. Akajiombea roho yake afe, akasema, Yatosha; sasa, Ee Bwana, uiondoe roho yangu; kwa kuwa mimi si mwema kuliko baba zangu. 1 Wafalme 19:4

Eliya alikimbilia uhai wake lakini kisha anamwomba Mungu kuyachukua uhai wake. Mbona hangeacha Yezebeli amuue? Kisha anaongeza maneno ya maombolezo "kwa kuwa mimi sio mwema kuliko baba zangu" alimaanisha nini kwa hili? Ungamo lake kwa Mungu baadaye linadhihirisha nia yake.

> Akafika kunako pango, akalala ndani yake. Na tazama, neno la Bwana likamjia, naye akamwambia Unafanya nini hapa, Eliya? (10) Akasema, Nimeona wivu mwingi kwa ajili ya Bwana Mungu wa majeshi; kwa kuwa wana wa Israeli wameyaacha maagano yako, na kuzivunja madhabahu zako, na kuwaua manabii wako kwa upanga; nami nimesalia, mimi peke yangu; nao wanitafuta roho yangu, waiondoe 1 Wafalme 19:9-10

Eliya alimwaga kwa Mungu masikitiko yake na kukatizwa tamaa kwa maanguko ya Israeli, na mauaji ya manabii wa Mungu kwa upanga. Eliya alitarajia kuwa taifa lingefanya mkutano na kuwa upande wake na kumsaidia kufanya mabadiliko katika ufalme. Wakati Yezebeli alimtisha, alitarajia kuwa kila mtu angesimama naye katika kushinda kusudi lake lakini aliachwa peke yake. Ilionekana kuwa kila kitu kilikuwa bure. Pia nia yake ya kuwaua manabii wa Baali kunadhihirishwa. Walikuwa wamewaua manabii wa Mungu kwa upanga. Adhabu ya ibada ya sanamu inayotolewa katika sheria za Musa ilikuwa kuuawa kwa kupigwa mawe, sio kuwaua kwa upanga. Tunaangazia adhabu ya kupiga kwa mawe katika sura nyingine, lakini hoja ni kuwa Eliya hakufuata mtindo unaoainishwa katika maandiko wa kukabiliana na waabudu sanamu. Hili linadhihirisha kuwa ingawa Eliya alitaka kuheshimu Mungu wa kweli, alilishughulikia kwa njia ya makosa. Hili linatuunganisha na hadithi ya nyuma ya wanafunzi. Walimpenda na kumheshimu Bwana, lakini upendo wao ulipotoshwa na shetani wakati mambo hayakuenda kama walivyotarajia na roho wa kisasi alifunuliwa. Hivyo basi ilifaa kuwa wanafunzi katika roho yao wanapatana na hadithi ya Eliya kwa sababu inaonesha roho sawa. Tunakumbushwa kuwa:

> Eliya alikuwa mwanadamu kama sisi… Yakobo 5:17 (NKJV)

Eliya alijua kuwa manabii wa Baali walistahili kifo, lakini jinsi ya kushughulikia jambo hili ilimfanya kuenda kwa njia ambayo haikuwa katika mpangilio wa Mungu. Hili linadhibitishwa katika hofu yake ya ghafla ambayo hakuwa ameishuhudia kabla. Hofu hii bado ilikuwa na Eliya aliposogelewa na askari wote. Kama Eliya alivyokuwa ameua kwa upanga, alihofu kuwa angeuawa kwa upanga. Ingawaje akida hakuwa na shaka kuwa Eliya alikuwa mtu wa Mungu, Eliya alikuwa akipambana na hofu yake ya kifo na kama hakuwa mwema kuliko baba zake. Shetani alipata mtaji katika shaka ya Eliya, kumsababisha kuieleza kwa kusema:

> **Ikiwa** mimi ni mtu wa Mungu, na ushuke moto kutoka mbinguni, ukuteketeze wewe na hamsini wako. 2 Wafalme 1:10

Ni sawa na maneno yaliyotamkwa na shetani:

> "**Kama** Wewe ndiye Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yawe mikate." Mathayo 4:3

Kutumia nguvu za kiungu kuhakikishia mtu kuhusu msimamo wao na Mungu ni ukosefu wa imani. Tunafaa kuamini kwa imani kuwa sisi ni watoto wa Mungu kwa kile ambacho tayari Mungu ametwambia. Watu wale hamsini walifaidikaje kwa maonyesho haya ya nguvu? Hili liliwasiadiaje kuamini yale ambayo tayari walikuwa wameungama kuhusu Eliya kuwa mtu wa Mungu? Ambaye alikuwa na uhakika kuhusu hili alikuwa Eliya. Uhakika huu ulimfanya Eliya kusahau kuwa Mungu hakuwa katika moto, na alishindwa na pendekezo la shetani la kuitisha moto kutoka mbinguni juu ya watu hao. Je tunaushahidi kuwa shetani anawezaitisha moto kutoka mbinguni na kuwateketeza watu?

> Bwana akamwambia Shetani, Tazama, yote aliyo nayo yamo katika uwezo wako; lakini usinyoshe mkono wako juu yake yeye mwenyewe. Basi Shetani akatoka mbele za uso wa Bwana… (16) Huyo alipokuwa akali akinena, akatokea na mwingine, na kusema, Moto wa Mungu umeanguka kutoka mbinguni na kuwateketeza kondoo, na wale watumishi, na kuwaangamiza; mimi peke yangu nimepona, mimi tu, kukuletea habari. Ayubu 1:12,16

Baadhi ya maswali bado yanabaki. Iwapo shetani alimdanganya Eliya kupitia kwa shaka yake binafsi inawezekanaje kuwa kwa sura ifuatayo Eliya angefasiriwa kwenda mbinguni? Inaonekana ajabu sana kufikiria kuwa kufanya kosa kubwa kama hilo karibu na mwisho wa maisha yake ya duniani kungezawadiwa na ufunguo wa kuingia mbinguni moja kwa moja na uzima wa milele. Tunapoangazia Yohana Mbatizaji kweli alishuku kuwa Yesu ni Masihi kabla ya kifo chake.

> Yohana Mbatizaji aliposikia akiwa gerezani mambo ambayo Kristo a alikuwa akiyafanya, aliwatuma wanafunzi wake (3) ili wakamwulize, "Wewe ndiye yule aliyekuwa aje, au tumngojee mwingine?" Mathayo 11:2-3

Bibilia haitwambii jinsi Yohana alijibu: Lakini kwa njia Yesu alizungumza Inaonekana dhahiri kuwa Yohana alishinda shaka yake na alikuwa ameandaliwa kwa kuuawa. Yesu alisema;

> Kama mko tayari kukubali hilo, yeye Yohana ndiye yule Eliya ambaye manabii walikuwa wamesema angekuja. Mathayo 11:14

Tunaambiwa pia:

> Naye atatangulia mbele zake katika roho ya Eliya,… Luka 1:17

Yohana mbatizaji alifanya kazi kubwa sana Kwa Mungu lakini wakati ule alikuwa na mgogoro mkubwa wa imani ambao aliushinda, uliompelekea kuandaliwa kwa kifo. Hili ni katika hali sawa na Eliya aliyefanya kazi kubwa kwa Mungu na kisha akawa na mgogoro mkubwa wa imani kuelekea mwisho wa huduma yake. Eliya alishinda shaka yake binafsi iliyosababisha kifo cha moto cha watu mia, na ilifasiriwa. Hili ni funzo la thamani kwetu sote, kuwa wenye haki wataishi kwa imani na wala sio kwa uhalali wa matendo yao. Kufasiriwa kwa Eliya baada ya anguko kubwa kama hilo kunatupa sote tumaini kuu kuwa hata nasi tunaweza fasiriwa baada ya kuona jinsi wadhaifu na wanyonge tulivyo. Natufurahi kwa kuwa wokovu ni kwa uhalali wa Kristo pekee, sio kwa kutakiwa kwa matendo ya manabii shujaa wanaoweza kuwaangamiza wengine kwa jina la Mungu kwa ajili ya kujilinda wao wenyewe.

Swali lingine linalofaa kufikiriwa ni, kwa nini Mungu akaruhusu watu hawa waangamizwe na shetani kwa moto. Kwa vile watu hawa walikuwa watumishi wa Mfalme wa Israeli aliyekuwa amejipeana kwa Baal-zebub mungu wa Ekroni, watu hawa hawakuwa na ulinzi dhidi ya muangamizi. Shetani alipowezeshwa kuwafikia hawa watu, alihitaji kuweza kuwaua kwa njia ambayo ingeonyesha kuwa Mungu aliwaua. Hili lilikaribia uongo mkamilifu, fanya jambo na kuushawishi ulimwengu kuwa ni Mungu alilifanya. Uoga wa Eliya ulitumiwa vibaya na shetani kumpa lengo alilolitaka. Mpango huu umefanikiwa zaidi kwa sababu watu wengi wameamini kuwa Mungu aliwateketeza watu hao, lakini kwa kushiriki Yesu anatwambia kuwa hii sio roho yake. Ni mkombozi na wala sio muangamizi.

Ni jambo la kupendeza namna gani kujua kuwa Mkombozi wetu wa thamani aliyemchukua yule mtoto mdogo mikononi mwake na kutudhihirishia ukuu wa ufalme wake, ni Mkombozi ambaye tunaweza kupumzisha uhakikisho

wetu kwake. Hawezi tuumiza kwa njia yeyote, kwa kuwa yesu ni mchungaji wa kondoo, sio muuaji; Huongoza kondoo wake kwenye maji matulivu na hawatesi hadi kifo. Bado kuna mengi katika somo la moto ambayo tunafaa kufikiria kabla ya kuwa na uyakini kuwa kweli Baba wa mbinguni ni mtu ambaye tunapaswa kutokuwa na hofu kwake.

## 7. Usiufanye Moyo Wako kuwa Mgumu

Katika sura ya tatu tuliangazia kifo cha msalaba na upendo wa ajabu kilichoonyesha. Katika sura ya nne tukatazama kina cha ndani ya Baba na uhusiano wake na Mwana. Ukweli huu unatupa msingi mkuu juu ya kuelewa tabia ya Mungu na jinsi ufalme wake ulivyo. Sura ya tisa ya Luka inatupa hadithi bora sana inayotuonyesha kinachotendeka tukiukataa msalaba. Inatupa sura ya jinsi wanadamu hutamani Mungu kuwachoma watu wakiwa hai kwa adhabu ya dhambi zao wakiamini kuwa hili ni kwa ulinganifu na tabia yake.

| | | |
|---|---|---|
| Luka 9:18-20<br><br>Matt 16:13-17<br><br>Marko 8:27-29 | Uhusiano wa Baba na Mwana kudhihirishwa | Petro alikili kuwa Yesu ni Kristo wa Mungu. Mathayo anarekodi kuwa Petro alieleza kuwa alikuwa Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai . Yesu anamwambia Petro kuwa ufahamu ni ufunuo wa kiroho kutoka kwa Baba na hakuna mtu anaweza jifunza hilo mwenyewe isipokuwa Mungu amfunulie. |

| | | |
|---|---|---|
| Luka 9:21-22<br><br>Matt 16:21-23<br><br>Marko 8:31-33 | onyo la kwanza la msalaba. | Yesu anatoa onyo la kwanza kuhusu chuki ya Mwanadamu katika kumtii Mwana wa Mungu na namna atakavyouawa Petro anaitikia hili kwa hisia kali na anaeleza Kwa msisitizo kwamba hili halitatendeka! Petro anakataa kuruhusu tamaa zake za ukuu wa utawala zisulubiwe. Huku ni kuukataa msalaba. Yesu anakemea roho wa shetani aliye Ongoza kauli ya Petro. |
| | Ugumu wa<br><br>kwanza | Hakuna rekodi ya Petro au wanafunzi kuitikia msalaba ujao na ya kuwa wanaweza jiandaa. Hili linaanza kuifanya migumu mioyo ya wanafunzi na hata kwa mateso ya Kristo msalabani. |
| Luka 9:23-27<br><br>Matt 16:24-28<br><br>Marko 8:34-38 | Wito wa Kuubeba msalaba wa Kujikana nafsi | Yesu anawaonya wanafunzi kuwa tamaa zao za kidunia lazima ziwachwe kama wanataka kumfuata. Hakuna heshima ya kilimwengu kwa njia aiendayo. Kuna kujikana nafsi tu na huduma kwa watu wengine. |
| Luka 9:28-36<br><br>Matt 17:1-8<br><br>Marko 9:1-6 | Baba anawaamuru kumsikiliza Mwanawe | Kwa rehema Baba anadhirisha utukufu wa Mwanawe na kuwasihi wasikilize anachosema Kukataa kwa kwanza kwa msalaba kuna maana kuwa wanafunzi hawana upendo mkamilifu na wanahofu sauti ya Baba. Hofu imewaadhibu. “Na mwenye hofu hakukamilishwa katika upendo.” 1 Yohana 4:18. |
| Luka 9:37-42<br><br>Matt 17:14-21<br><br>Mark 9:14-29 | Kutokuamini kunawekwa Wazi | Ukataa wa kuukubali msalaba unaanza kujionyesha katika ukosefu wa imani. wanafunzi hawawezi kuyaondoa mapepo kwa sababu mioyo yao bado imeadhirika kwa tamaaa zao za ukuu wa utawala. Yesu anataja ukosefu wao wa imani kama onyo. |

| | | |
|---|---|---|
| Luka 9:44-45<br><br>Matt 17:22-23<br><br>Marko 9:31-32 | Onyo la Pili la msalaba. Mioyo Inafanywa migumu Hata zaidi. | Kwa upendo, Yesu tena anawambia juu ya msalaba ili kuwasaidia kuyaacha tamaa zao lakini tena wanakataa wito huu wa kutubu na Wanahuzunika tu kwa kile ambacho anasema. Mioyo yao inakuwa migumu hata zaidi kwa sababu hiyo. |
| Luka 9:46-48<br><br>Matt 18:1<br><br>Marko 9:33-38 | Tamaa ya ubinafsi inakua. | Wanafunzi walimfungulia shetani mlango ambaye anawajaribu kujadiliana nani aliye mkuu kati yao. Yesu anawajibu kwa kumweka mtoto mchanga kati yao na kuwaonya kuwa isipokuwa wamekuwa kama mtoto huyo mchanga hawawezi kuridhi ufalme wa mbinguni. |
| Luka 9:49-50<br><br>Marko 9:38-39 | Roho wa utawala anatokea. | Kwa kuwa wanafunzi walikuwa wakitafuta nafasi hawakutaka mtu mwingine yeyote achukue nafasi hiyo na kuitumikisha roho ya nguvu kwa waliowaona kama wapinzani wao. |
| Luka 9:51-54 | Roho wa mauaji anatokea na kuhalalishwa kupitia kwa Maandiko. | Kwa kukataa msalaba wa kujikana nafsi mioyo ya wanafunzi ililemewa na roho wa kiburi kupelekea kwa utawala na mauaji. Kuifanya mioyo yao kuwa migumu kuliwafanya kuona kuwa hakuna ubaya wowote katika kuua kwa jina la Mungu. |

Wanafunzi hawakutaka kukubali onyo la Yesu kuhusu kifo kilichomngojea mikononi mwa viongozi wa taifa wakatili. Walikuwa wamelaza matarajio yao yote kwa ukuu wa taifa juu yake; Walimjua Yesu sio jinsi alivyo lakini walivyotaka awe. Matarajio yalikuwa Yesu awe Barabbas[1], na ukweli wa msalaba ulisulubisha ndoto zao na kuwageuza kuwa vumbi. Walichagua kutokumbatia msalaba na kuanza kufahamu mateso makubwa ya uhusiano

[1] Barabbas alikuwa kiongozi wa kisiasa katika wakati wa Yesu ambaye alitetea mageuzi ya uongozi wa Roma kwa Israeli. Alitetea vurugu ili kuafikia lengo hili na alidai kuwa na umbo la kimasyia. Jina lake Barabbas linamaanisha “mwana wa baba” na alikuwa Kristo bandia kabisa kwa Kristo aliye Mwana wa kweli wa Mungu.

ambayo Kristo alishuhudia kila siku kwa kuona karibu kila mtu anakana na kuupuuza ujumbe wake, kazi, na yeye mwenyewe kama mwakilishi wa Baba. Badala yake walichagua kupuuza mateso hayo jambo ambalo lilifanya mioyo yao migumu.

Wakati wa ubatizo wa Yesu Baba wa mbinguni alitangaza kwa ulimwengu upendo wake wa kina kwa Mwanawe; mlango ulifunguliwa kwa kweli kuelewesha upendo, huruma, na makini ya Mungu na Mwanawe. Ni makini hii inayowafanya kubeba msalaba huu wa kutisha wa uchungu kupitia kwa kujikana nafsi. Kila siku mioyo yao inalia kwa ubinafsi wa wanadamu, majivuno, na anasa. Tabia ya uhuru wa kupenda ya Mungu huruhusu watu kuendelea kumpuuza na kumkataa kwa miaka na halipizi kamwe. Huruhusu mioyo yao kuwa migumu na kwa huzuni huwatazama wakijiangamiza wakati daima akiwatafuta watoke katika kutenda hivi. Wanafunzi walikaribishwa waanze kufahamu mwangaza wa upendo huu, lakini msalaba sio ambao walikuwa wakitaka na, Israeli walivyokuwa wamemwambia Musa kuuficha mwangaza wa uso wake, wanafunzi waliweka pazia juu ya mioyo yao na kuzuia ukweli kuwafanya wepesi.

Wakati Kaini na Habeli waliangalia kifo cha mwana kondoo, Kaini aliweka pazia juu ya moyo wake iliyochujuka maana ya mateso, na kwa hivyo mwana kondoo kwa kweli akawa kichocheo cha kuufanya moyo wake mgumu uliomwandaa kwa mauaji ya ndugu yake. Habeli alipomtazama mwana kondoo alitetemeka alipotafakari maana yake. Alifikiria juu ya mwana kondoo wa Mungu kuvunjwa kwa ajili yetu na akalia kwa moyo uliovunjika. Mwana kondoo sawa alitoa matokeo kinyume kabisa katika watu hao wawili.

Huu ndio mwanga wa msalaba. Mwanga huo ni mwangafu sana kiasi ya kwamba aidha tuanguke kwa mwamba na tuvunjike au tupinge na tuwe wagumu kama mwamba na hivyo tuangamizwe na hatia zetu wenyewe wakati hatimaye tutakapokabiliana na ukweli wa upendo wa Mungu.

Kanuni hizi ni muhimu kwetu katika kuelewa hadithi za Bibilia kwa usahihi. Isipokuwa tuukubali upendo wa upole wa Baba kwa Mwanawe mioyo yetu haiwezi fanywa miepesi kweli katika kutafsiri hukumu za Mungu. Baba mwenye upendo hawezi mchoma mwanawe akiwa hai, kuwamwagia moto wa kibiriti wakilia katika kifo cha uchungu. Kuamini kuwa Mungu anaweza fanya hivi nikutoelewa uhusiano wa Baba na Mwana na neema imwagikao ulimwenguni kutoka kwao. Kutoelewa msalaba huwafanya watu kuusahau

uchungu aupitiao wakati anapodharauliwa, kuchukiwa na kukataliwa; lakini hukataa kuchoka na wale ambao wanamkataa. Huuacha moyo wake wazi hadi wakati wa mwisho, akitarajia kuwa wenye dhambi watamgeukia. Iwapo mwishoe watamkataa na kutanga mbali naye kabisa, kukataliwa kwote humsababishia uchungu mwingi. Ni uchungu ambao sisi kama wadhambi hunywea kutoka kwa huzuni, hasira na karaha. Ingekuwa kamwe tusiruhusu mtu kufanya hili kwetu mara kwa mara. Kuacha moyo wake wazi kwa kukataliwa ni msalaba wa kweli wa Baba ukiwekwa wazi kwa mwanawe.

Nguvu na ajabu ya msalaba inaelezea maajabu mengine yote kuhusiana na hukumu ya Mungu. Popote tuonapo hukumu ikianguka juu ya watu katika Maandiko lazima tuielezee kwa mwanga wa msalaba kwa kuwa hapa ndipo mahali ambapo huruma na haki hupigana busu.

> Kristo alitukomboa kutoka katika laana ya sheria kwa kufanyika laana kwa ajili yetu, kwa maana imeandikwa, "Amelaaniwa yeye aangikwaye juu ya mti." Wagalatia 3:13

> Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Isaya 53:5

Yesu amelipa mshahara na akateseka laana ya dhambi. Alikufa kifo cha wale ambao katika mwisho wa wakati wanakataa ukombozi na kuchagua afadhali kufa. Kama yesu angekufa kifo tofauti na kile cha mwisho wa wakati basi hakulipa mshahara wa dhambi. Swali basi ni, Yesu aliteseka moto wa jehanamu? Iwapo kifo cha mwisho cha waovu kinadai wachomeke katika moto wa jehanamu, na Yesu hakulipa deni hilo, basi hakulipa adhabu ya dhambi. Je, Yesu alipitia moto juu ya msalaba? Zingatia jinsi Paulo anaunganisha kutenda mema kwa wale ambao hawastahili makaa ya moto kwa nafsi.

> Badala yake: "adui yako akiwa na njaa, mpe chakula, akiwa na kiu, mnyweshe. Maana ukifanya hivyo, utampalia makaa ya moto yanayowaka kichwani pake. Warumi 12:20

Wana wa Israeli walipouona utukufu wa Mungu katika mlima Sinai, ulionekana kama moto uteketezao.

> Na kuonekana kwake ule utukufu wa Bwana kulikuwa kama moto uteketezao, juu ya mlima machoni pa wana wa Israeli. Kutoka 24:17

Upendo wa kutokuwa na ubinafsi wa Mungu unapodhihirishwa kwa mtu mwenye ubinafsi, hisia za hatia wanazoshuhudia huchoma moyoni zaidi kiasi cha kusababisha uchungu unaoonekana. Hali ya Yesu msalabani imetabiriwa katika zaburi kadhaa.

> Mungu wangu, Mungu wangu, Mbona umeniacha? Mbona U mbali na wokovu wangu, Na maneno ya kuugua kwangu? Zaburi 22:1

> Nalikuwa sisemi, nalinyamaa kimya, Sina faraja, maumivu yangu yakazidi. (3) **Moyo wangu ukawa moto ndani yangu, Na katika kuwaza kwangu moto ukawaka;** Nalisema kwa ulimi wangu, Zaburi 39:2-3

> Kamba za mauti zilinizunguka, Mafuriko ya uovu yakanitia hofu. (5) Kamba za kuzimu zilinizunguka, Mitego ya mauti ikanikabili. (6) Katika shida yangu nalimwita Bwana, Na kumlalamikia Mungu wangu. Akaisikia sauti yangu hekaluni mwake, Kilio changu kikaingia masikioni mwake. (7) Ndipo nchi iliyotikisika na kutetemeka, Misingi ya milima ikasuka-suka; Ikatikisika kwa sababu alikuwa na ghadhabu. (8) **Kukapanda moshi kutoka puani mwake, Moto ukatoka kinywani mwake ukala, Makaa yakawashwa nao.** Zaburi 18:4-8

Mshahara wa dhambi ni mauti. Kwa kweli kile kiletacho hicho kifo ni hatia ambayo wenye dhambi hushuhudia wanapokabiliana na jinsi uovu ulivyo. Njia pekee ambayo uovo unaanikwa ni wakati tabia ya Mungu inadhihirishwa kuwa tofauti. Tabia ya Mungu inapodhihirishwa ni moto uteketezao kwa waovu kwa sababu, kama wenye dhambi wajuavyo usafi, kutokuwa na ubinafsi na neema ya Mungu kwa ulinganisho na ubinfsi wao,hali ya uovu, maana ya hatia ni kama kaa la moto mioyoni mwao. Wakati wakuja kwa Kristo waovu wataangamizwa na mwanga wa kuja kwa Kristo.

> wala hatukula chakula cha mtu ye yote pasipo kukilipia. Badala yake tulifanya kazi kwa bidii usiku na mchana, ili tusimlemee mtu ye yote miongoni mwenu. 2 Wathesalonika 2:8

Kristo ni mwanga wa utukufu wa Baba, Waebrania 1:3 na utukufu wa Baba ni tabia yake. Kutoka 33:18; 34:6,7. Kupendeza na uzuri wa tabia ya Kristo utadhihirishwa kikamilifu katika kuja kwake na ufunuo wake utakuwa moto ambao ni furaha kwa wenye haki na kifo kwa waovu.

> yeye naye, atakunywa mvinyo wa hasira kali ya Mungu ambayo imemiminwa katika kikombe cha ghadhabu yake pasipo kuchanganywa na maji. Naye atateswa kwa moto uwakao na kiberiti mbele ya malaika watakatifu na mbele za Mwana-Kondoo. Ufunuo 14:10

Neno la kiberiti ni *theion* linalotokana na theos ambalo humaanisha Mungu na hubeba maana ya uvumba wa uungu. Pia humaanisha kumurika ghafla. Tunapotazama uvumba katika patakatifu ukielezewa mbinguni tunagundua uhusiano kwa moto.

> Malaika mwingine aliyekuwa na chetezo cha dhahabu, akaja na kusimama mbele ya madhabahu. **Akapewa uvumba mwingi** ili autoe pamoja na maombi ya Watakatifu wote, juu ya ile madhabahu ya dhahabu iliyoko mbele ya kile kiti cha enzi. (4) Ule moshi wa uvumba pamoja na yale maombi ya watakatifu, vikapanda juu mbele za Mungu, kutoka mkononi mwa huyo malaika. (5) **Kisha yule malaika akachukua kile chetezo, akakijaza moto kutoka kwenye ile madhabahu,** akautupa juu ya dunia. Pakatokea sauti za radi, ngurumo, umeme wa radi na tetemeko la nchi. Ufunuo 8:3-5

Uvumba unawakilisha uwepo wa Uungu wa Mungu ambao ni kama moto. Hili ndilo linamaanishwa na kiberiti. Tena tunaona hili katika Isaya:

> Tazama, jina la Bwana linakuja kutoka mbali sana, linawaka kwa hasira yake, kwa moshi mwingi sana unaopaa juu; midomo yake imejaa ghadhabu, **na ulimi wake ni moto ulao**; (28) na pumzi yake ni kijito kifurikacho, kifikacho hata shingoni, kupepeta mataifa kwa ungo wa ubatili; na lijamu ikoseshayo itakuwa katika taya za watu. (30) Naye Bwana atawasikizisha watu sauti yake ya utukufu, naye atawaonyesha jinsi mkono wake ushukavyo, na ghadhabu ya hasira yake, na **mwako wa moto ulao, pamoja na dhoruba, na tufani, na mvua ya mawe ya barafu**. (33) Maana Tofethi imewekwa tayari tokea zamani, naam, imewekwa tayari kwa mfalme huyo; ameifanya kubwa, inakwenda chini sana; tanuru yake ni moto na kuni nyingi; **pumzi ya Bwana, kama mto wa kiberiti, huiwasha**. Isaya 30:27-28,30,33

> Kwa sababu hiyo Bwana, Mungu wa majeshi, asema hivi, Kwa sababu mnasema neno hili, tazama, **nitafanya maneno yangu**

**katika kinywa chako kuwa moto, na watu hawa kuwa kuni, nao moto utawala.** Yeremia 5:14

.. Kwa maana upendo una nguvu kama mauti, Na wivu ni mkali kama ahera. Mwako wake ni mwako wa moto, Na miali yake ni miali ya Yahu. Wimbo ulio bora 8:6

Upendo wa Mungu ni moto na kwa wenye haki kuchomwa na huo upendo moyoni ni kuzuri. Hili ndilo wanafunzi walishuhudia siku ya pentekosti.

Ghafula sauti kama mvumo mkubwa wa upepo uliotoka mbinguni, ukaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi. (3) **Zikatokea ndimi kama za moto zilizogawanyika** na kukaa juu ya kila mmoja wao. Matendo 2:2-3

Maandiko yanatwambia wazi kuwa kuna wale wanaoweza kuishi katika moto huu wa tabia ya Mungu; wenye haki ambao watachomeka milele katika moto wa upendo wa Mungu, kwa kuwa Mungu ni moto ulao. Waebrania 12:29. Waovu watakapo kuwa wanavunjwa na hatia ya dhambi zao, wale wanaoamini katika uhalali wa Kristo mioyo yao itachomeka kwa upendo na shukurani.

Wenye dhambi walio katika Sayuni wanaogopa; tetemeko limewashika wasiomcha Mungu; **Ni nani kwetu sisi awezaye kukaa na moto ulao; ni nani kwetu sisi awezaye kukaa na moto uteketezao milele?** (15) Ni yeye aendaye kwa haki, anenaye maneno ya adili; ni yeye anayedharau faida ipatikanayo kwa dhuluma; akung'utaye mikono yake asipokee rushwa; azibaye masikio yake asisikie habari za damu; afumbaye macho yake asitazame uovu. Isaya 33:14-15

Mwisho wa wakati mdhambi atapokea mshahara wake, na ni nani analipa mshahara huu?

Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti… Romans 6:23

Dhambi hulipa mshahara. Ni uzito uvunjao wa hatia na utambuzi wa kujua kuwa wakati kupitia maisha yao yote, mdhambi alikuwa anakataa ombi la roho ya Kristo, alikuwa akimchoma Kristo kwa maneno yake ya ukatili na tabia zao mbovu kwa wengine. Wakati mdhambi anagundua yote ambayo amemfanyia Kristo kupitia maisha yake, hisia zake mwenyewe za haki zitadai

kifo. Kama Kaini mwenye dhambi atalia, "Dhambi zangu ni nyingi haziwezi chukulika."

Hali zima ilibebwa na Kristo msalabani. Aliteseka moto wa jehanamu. Alifanywa mdhambi kwa ajili yetu na akahisi uzito wa kuvunja wa dhambi juu yake alipokuwa akiimaliza laana. Alichopitia msalabani ni ambacho waovu watashuhudia wakati wa mwisho.

> Nao walitembea katika eneo lote la dunia, wakaizunguka kambi ya watakatifu na ule mji uliopendwa. Lakini moto ukashuka kutoka mbinguni na kuwateketeza. (10) Naye Ibilisi aliyewadanganya akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti alipo yule mnyama na yule nabii wa uongo. Nao wakateswa huko mchana na usiku, milele na milele. Ufunuo 20:9-10

Tena maandiko yanatwambia jinsi shetani atakufa:

> Kwa wingi wa maovu yako, katika uovu wa uchuuzi wako, umepatia unajisi patakatifu pako; **basi nimetokeza moto kutoka ndani yako, nao umekuteketeza,** nami nimekufanya kuwa majivu juu ya nchi, machoni pa watu wote wakutazamao. Ezekieli 28:18

Andiko hili linaweka wazi mpangilio wa jinsi hili linatendeka:

1. Shetani anajitia unajisi kwa wingi wa maovu na kupitisha hizo dhambi kwa wengine .
2. Neno lifuatalo ***basi*** linatokea matokeo yanayotokea.
3. *Nimetokeza moto kutoka ndani yako* – moto wa hatia. Mungu analetaje moto huu? Ufunuo wa tabia yake ya upendo kama ilivyorekodiwa katika sheria.
4. ***Nao*** *umekuteketeza*. Basi ni moto unaotoka ndani ya shetani unaozaliwa na hatia yake ya dhambi utakao mteketeza.
5. **Na** kisha shetani anafanywa majivu juu ya nchi **baada ya** kuteketezwa.

Shetani hawezi epuka kutazama maovu ambayo ndiye yeye na maovu yote ambayo ametenda akiwa machoni pa Mungu. Usafi wakupendeza na utakatifu wa Mungu hauna ubinafsi, huleta na kutoa hukumu ya nafsi ambayo hutoka moyoni kama moto uchomao. Mchakato huu humla shetani. Baada ya kuliwa na kufa anageuzwa majivu juu ya nchi kwa moto wa utakaso.

Kuangamizwa kwa waovu kunaelezewa katika kitabu cha historia cha Esdras wa pili:

> Na huyu mwanangu atakemea uvumbuzi muovu wa mataifa hayo, ambayo kwa maisha yao ya uovu yameanguka katika dhoruba; (38) Na ataweka mbele yao mawazo yao maovu, na adhabu ambayo kwayo wataanza kuadhibiwa, ambayo ni kama moto: na atawangamiza bila kazi kwa sharia ambayo ni kama mimi. 2 Esdras 13:37-38

Sheria ambayo huwasababishia waovu adhabu kama hiyo ni sheria moto lakini ilipeanwa kwa upendo. Mkombozi wetu hakuja kuukemea ulimwengu lakini ulimwengu ukombolewe kupitia kwake. Sheria ni sheria ya upendo lakini waovu huhisi wamekemewa nayo kwa kuwa ni uakisi wa tabia ya Mungu.

> Akasema,Bwana alitoka Sinai,Akawaondokea kutoka Seiri;Aliangaza katika kilima cha Parani,Akaja Meribath-Kadeshi.**Upande wake wa kuume Palikuwa na sheria ya moto-moto kwao.**(3)**Hakika awapenda hayo makabila ya watu;** Watakatifu wake wote wamo mkononi mwako; Nao waliketi miguuni pako; Watapokea kila mmoja katika maneno yako. Kumbukumbu 33:2-3

Nini kuhusu ukweli ambao Bibilia hutwambia kuwa waovu watakuwa majivu?

> Nanyi mtawakanyaga waovu; maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu; katika siku ile niifanyayo, asema Bwana wa majeshi. Malaki 4:3

Wakati ambao hatimaye dhambi imelipa mshahara wake kwa waovu kupitia kwa laana ya hatia ambayo huwaangukia wakitazama usafi wa uzuri wa tabia ya Mungu, miili yao iliyokufa italala juu ya dunia. Kisha wakati huo tu, miili ya waovu itageuzwa majivu.

> Mkingojea na kuhimiza kuja kwa hiyo siku ya Mungu, ambayo siku hiyo mbingu zitachomwa moto na kutoweka na vitu vya asili vitayeyuka kwa moto 2 Petro 3:12

Kuna wengi ambao wanaeleza kifo cha mwisho cha waovu kama kuweka chini mbwa aliyegonjeka yule awekae maisha ya wengine hatarini;kwa hivyo, mnyama huyo lazima awekwe chini. Tatizo na mfano huu ni kuwa mwenye mbwa hawashi moto uchomao polepole, umchomao mbwa huyo kwa siku

kadhaa akiwa angali hai, kumsababishia kilio na kuomboleza katika uchungu kabla ya kufa hatimaye. Wazo hili linatoka kwa moyo mgumu. Baba yetu aliye mbinguni hawezi fanya jambo kama hili. Mara ujuavyo upendo wa Mungu, haiwezekani tu kumshtaki na mateso ya polepole na mauaji binafsi ya mabilioni ya watoto wake.

Sababu kwa nini wazo hili ni karibu linakubalika na kila mtu na kufunzwa katika ulimwengu wa wakristo ni kwa sababu ya kukataa kuruhusu ukweli wa msalaba kuingia moyoni. Moyo kwa upande wake unakuwa mgumu kwa ukweli wa hali ya makini na huruma ya Mungu, na kama ilivyokuwa na wanafunzi, hapo huingia wazo la Mungu kutuma moto kutoka juu na kuwachoma watu wakiwa hai.

Basi tujifunze funzo kutoka kwa wanafunzi na tuangazie amri ya Baba wakati mwanawe aligeuzwa sura – "msikilize" basi tusikilize ombi la sauti yake akiweka mtoto mdogo wa thamani katikati yetu na kumshika mtoto huyo karibu na kifua chake na kutuambia "isipokuwa mmekuwa kama mtoto asiye na hatia hamuwezi kuurithi ufalme wa mbinguni." Msiifanye mioyo yenu migumu kama Waisraeli walivyofanya waliomsihi Musa kuweka pazia juu ya uso wake injili ilipotangazwa kwao.

> Hiyo ndiyo sababu nilikasirikia kizazi kile, nami nikasema, 'Siku zote mioyo yao hupotoka, nao hawajazijua njia Zangu'. (11) Hivyo nikaapa kwa hasira Yangu, 'kamwe hawatainingia rahani Mwangu.' (12) Ndugu zangu, angalieni, asiwepo miongoni mwenu mtu mwenye moyo mwovu usioamini, unaojitenga na Mungu aliye hai. (13) Lakini mtiane moyo kila siku mtu na mwenzake, maadam iitwapo 'leo', **ili asiwepo hata mmoja wenu mwenye kufanywa mgumu kwa udanganyifu wa dhambi.** (14) Kwa kuwa tumekuwa washiriki wa Kristo, kama tukishikamana tu kwa uthabiti na tumaini letu la kwanza hadi mwisho (15) Kama ilivyonenwa: "Leo, kama mtaisikia sauti Yake**, msifanye mioyo yenu migumu kama mlivyofanya wakati wa kuasi.**" Waebrania 3:10-15

Iwapo utachagua kutokukubali kujikana nafsi kwa msalaba, uko katika hatari ya kuufanya moyo wako kuwa mgumu unaposoma Bibilia kwa namna sugu na kuhusisha kwa Mungu uchungu na vifo vya mamillioni ya watu katika historia ya mwanadamu. Iwapo leo utaisikia sauti yake, usiufanye moyo wako kuwa mgumu.

## 8. Mbona Kuwaamuru Wadhambi wa Kupiga Mawe?

Upinzani wa wanafunzi kwa binafsi kukataa msalaba kuliwapelekea kutamani kuuwawa kwa Msamaria ambaye hakuwa na heshima. Upinzani uo huo, ukiishi mioyoni mwa viongozi wa Wayahudi, ulisababisha wao kutaka kumuua Yesu. Wayahudi waliwekeza nguvu nyingi katika kutafuta kumnasa Kristo kwa maneno yake na matendo ili waweze kumtangaza mzushi na aweze kuuawa. Moja wapo ya mitego mingi iliyowekewa Yesu umeelezwa katika injili ya Yohana:

> Alfajiri na mapema Yesu akaja tena hekaluni, watu wote wakakusanyika, akakaa akaanza kuwafundisha. (3) Walimu wa sheria na Mafarisayo wakamleta mwanamke mmoja aliyefumaniwa akizini. Wakamsimamisha katikati ya umati wa watu wote. (4) Wakamwambia Yesu, "Mwalimu, huyu mwanamke amekutwa akizini. (5) Katika sheria, Musa alituamuru kuwapiga kwa mawe wanawake wa namna hii, mpaka wafe. Sasa Wewe wasemaje?" Yohana 8:2-5

Kwa Mafarisayo ulionekana kama mtego barabara. Kama Yesu alitafuta kumwokoa mwanamke kutoka kwenye kifo wangemuhukumu kwa kuvunja sheria ya Musa. Kama angemuhukumia kifo wanaweza kumshtaki kwa Gavana wa Roma kama muasi. Yesu alikuwa tayari amesema hakuja

kuitangua torati wala manabii na kuwa hata Jodi moja ya sheria ilitafutika. Musa aliandika katika sheria:

> Na mtu aziniye na mke wa mtu mwingine, naam, yeye aziniye na mke wa jirani yake, mtu mume aziniye, na mwanamke aziniye, hakika watauawa. Walawi 20:10

> Watoeni nje katika lango la mji ule, mkawapige kwa mawe hata wafe; yule kijana, kwa kuwa hakupiga ukelele, naye yu ndani ya mji; na yule mume, kwa kuwa amemtweza mke wa mwenzake; ndivyo utakavyoondoa uovu katikati yako. Kumbukumbu la Torati 22:24

Mwanamke huyu alipatikana katika tendo halisi la kuzini. Kulingana na sheria anapaswa kupigwa mawe hadi kufa. Mwanamke sasa alikuwa ametupwa miguuni mwa mwenye kupeana sheria ili aweze kupeana hukumu yake. Ni muhimu kukumbuka kuwa Mwana wa Mungu ndiye aliyepeana sheria katika Mlima Sinai.

> Kwa nini basi iwepo sheria? Sheria iliwekwa kwa sababu ya makosa mpaka atakapokuja yule mzao wa Abrahamu, ambaye alitajwa katika ile ahadi. **Sheria iliamuriwa na malaika kwa mkono wa mpatanishi.** Wagalatia 3:19

> Kwa maana kuna Mungu mmoja na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, yaani, mwanadamu Kristo Yesu,1 Timotheo 2:5

Yesu, kama neno la Mungu, ndiye aliyenena maagizo "usizini." Sasa kwa kuwa mwanamke alikuwa miguuni pake, washtaki wa mwanamke walisubiri kuona atakachofanya. Yesu akainama na kuanza kuandika, kuwapuuza inavyoonekana. Kisha akanena akisema:

> "Kama kuna mtu ye yote miongoni mwenu ambaye hana dhambi na awe wa kwanza kumtupia jiwe. Yohana 8:7

Tangazo hili linavutia sana na linalipua dhana ambayo ilikuwa ikiwaendesha Mafarisayo. Hili halikuwa inavyoonekana ulimwenguni wa fikira. Lakini Yesu alikuwa anaonyesha tu kanuni sawa iliyopeanwa na Musa kuhusu kesi nyingine ya kupiga mawe mtu aliye mkufuru Mungu.

> Na yeye atakayelikufuru jina la Bwana hakika atauawa; mkutano wote watamwua kwa kumpiga kwa mawe; kama ni mgeni, kama ni

mzalia, hapo atakapolikufuru jina la Bwana atauawa. (17) Na mtu ampigaye mtu hata akafa, lazima atauawa; Walawi 24:16-17

Nena na mkutano wote wa wana wa Israeli, uwaambie, Mtakuwa watakatifu; kwa kuwa mimi Bwana, Mungu wenu, ni mtakatifu. Walawi 19:2

Nini kinachoendelea hapa? Mtu atakayekufuru lazima auawe kwa kupigwa kwa mawe lakini yeyote atakayeua lazima auawe. Iwapo mtu atampiga mwingine kwa mawe hadi kifo basi si anaua mtu mwingine? Si hivyobasi anahitimu kwa kuuawa pia? Hili linaweza unganishwa na wazo ambalo Yesu alikuwa anaeleza kuwa mtu mtakatifu pekee na asiye na dhambi ana hati ya utambulisho ya kumuua mtu mwengine. Yesu ndiye mtu tu asiyekuwa na dhambi na basi yeye alifanya nini?

Yesu alipokuwa akiandika katika mavumbi ya sakafu ya hekalu alikuwa akipeana ukweli wa kiroho wa yale yaliyokuwa yameandikwa katika sheria. Kama mtu alishuku kuwa mke wake amezini, angemleta mbele ya kuhani ili kuitekeleza sheria kuhusu wivu.

Basi kuhani atamleta mwanamke akaribie, na kumweka mbele za Bwana; (17) kisha kuhani atatwaa maji matakatifu katika chombo cha udongo; kisha kuhani atatwaa katika vumbi lililo pale chini ya maskani, na kulitia katika hayo maji; (18) kisha kuhani atamweka mwanamke mbele za Bwana, naye atazifungua nywele za kichwani mwa huyo mwanamke, kisha atampa hiyo sadaka ya unga ya ukumbusho mikononi mwake, ambayo ni sadaka ya unga ya wivu, naye kuhani atakuwa na hayo maji ya uchungu yaletayo laana mkononi mwake; (19) tena kuhani atamwapisha huyo mwanamke, naye atamwambia mwanamke, Kwamba hakulala mtu mume pamoja nawe, tena kwamba hukukengeuka kuandama uchafu, uli chini ya mumeo, maji haya ya uchungu yaletayo laana yasikudhuru; (20) lakini kwamba umekengeuka uli chini ya mumeo, na kwamba u hali ya unajisi, na mtu mume amelala nawe, asiyekuwa mumeo; (21) hapo ndipo kuhani atamwapisha mwanamke kwa kiapo cha kuapiza, kisha kuhani atamwambia huyo mwanamke maneno haya, Bwana na akufanye wewe uwe laana na kiapo kati ya watu wako, hapo Bwana akufanyapo paja lako kupooza, na tumbo lako kuvimba; (22) na maji yaletayo laana yatakuingia matumboni mwako, na kukuvimbisha tumbo, na kukupoozesha paja lako; na mwanamke ataitika, Amina, Amina. (23) **Kisha kuhani**

> **ataziandika laana hizo ndani ya kitabu, na kuzifuta katika maji ya uchungu;** Hesabu 5:16-23

Watu hawa waliokuwa wamemshika mwanamke huyu akiwa kwenye kitendo cha uzinifu, walikuwa wamemdanganya na kumdhalilisha. Jinsi Yesu alivyoandika katika mavumbi ya sakafuni, Roho Mtakatifu (Aliye ashiriwa kwa maji) alileta hatia kwa watu hao iliyosababisha tumbo zao kufura na miguu yao kuoza kupitia kwa hatia ya dhambi. Walikuwa na wivu kwa Kristo na uliwala. Jinsi zaburi inasema:

> Niliponyamaza mifupa yangu ilichakaa Kwa kuugua kwangu mchana kutwa. Zaburi 32:3

Badala ya kuungama dhambi zao na kusamehewa,watu hawa waliondoka bila kusema chochote wakibeba hatia ambayo ilisababisha mifupa yao kuwa nta zee.

> Yesu akainuka na kumwambia, "Wako wapi wale waliokuwa wanakuhukumu kuwa mwenye hatia?" (11) Yule mwanamke akajibu, "Hakuna hata mmoja Bwana."Yesu akamwambia, "Hata Mimi sikuhukumu. Nenda zako, kuanzia sasa usitende dhambi tena." Yohana 8:10-11

> Na kama mwanamke hakuwa na unajisi lakini yu safi; ndipo ataachiliwa, naye atazaa wana. Hesabu 5:28

Yesu alimsamehe mwanamke huyu dhambi zake; Alifuta maandishi yote ya dhambi zake kwa maji machungu ambayo angeyanywa msalabani, na kwa hivyo hakuwa najisi kamwe. Alikuwa amekuwa huru na mbegu ya kweli ilikuwa imezaliwa ndani yake. Alidhihirisha Roho wa Kristo ndani ya moyo wake.

Yesu alipowaambia mafarisayo "Yeye asiye na dhambi miongoni mwenu na awe wa kwanza wa kumtupia jiwe" Alitangaza hukumu ya kifo juu yake. Hakujaribu kumuondolea mashtaka dhidi yake. Alifunga shtaka, na mwanamke alikuwa na uhakika kuwa angekufa. Kupitia kwa kuandika sakafuni, Yesu aliwakumbusha mafarisayo kuwa hawakuwa bila dhambi, na wakaondoka. Washtaki wote wa mwanamke walipoondoka, mpaji wa sheria alimuuliza wahukumu wake walipo. Aliashiria kuwa walikuwa wameondoka, na kwa hivyo hukumu yake ilikuwa mikononi mwa mpaji wa sheria. Alisema "wala mimi sikuhukumu," enenda na usitende dhambi tena. Mpaji wa sheria

alituonyesha jinsi analenga kutumia sheria kutupa rehema. Kama angemwachilia huru mwanamke hangehitaji rehema, hivyo alitoa hukumu ili kumpa rehema. Hilo ndilo kusudi nzima la sheria. Sheria inakusudia kutupeleka kwa Kristo ili tuhesabiwe haki kwa imani. Wagalatia 3:24.

Ni huzuni kubwa namna gani kufikiria kuwa Viongozi wa Wayahudi kweli waliamini kuwa ilikuwa kusudi la Mungu kuwa mwanamke huyu anafaa kuuawa kwa mawe. Hatutaki kumetameta kwa ukweli wa jambo hili. Kama Waroma hawakuwa wanaongoza na watu hawa walikuwa huru kuitii sheria kama walivyotaka wangechukua mawe na kumuua mwanamke huyu. Hili kwa kweli lilitendeka kwa kesi ya Stephano.

> Lakini wao wakapiga kelele kwa sauti kubwa, wakaziba masikio yao, wakamrukia kwa nia moja. (58) Wakamtupa nje ya mji, wakampiga kwa mawe. Nao mashahidi wakaweka nguo zao miguuni mwa kijana mmoja aitwae Sauli. (59) Walipokuwa wakimpiga mawe, Stefano aliomba, "Bwana Yesu, pokea roho yangu" Matendo 7:57-59

Watu hawa waliamini katika Mungu ambaye alikuwa ameamua kuwaadhibu wadhambi kwa kuwaua kwa mawe. Hebu tufikirie juu ya mwanamke huyu mchanga akiwa amepigwa kichwani kwa jiwe kubwa na kuanguka ardhini kwa hofu? Kisa kitakapoisha kungekuwa na mwili uliopondwa na kujazwa damu kama onyo kwa wale ambao Mungu hana huruma nao; ukifanya dhambi utalipa na maisha yako. Je sura hiyo inakujaza na uelewa wa kina wa upendo wa Mungu kama huyo? Ungependa kufurahia daima mbele ya Kiumbe kama huyo ambaye huwakamata wadhambi kama wadudu wasiokuwa na thamana?

Mbona basi sheria ya Musa inaamuru watu kuuawa kwa mawe? Sheria inaakisi tabia ya Mungu. Kama Mungu aliamuru sheria hii basi hili linamaanisha kuwa alitaka iwekwe hapo itumike ikihitajika? Kuna kanuni muhimu sana tunapaswa kuzingatia hapa kama inavyoelezewa na Kristo.

> "Usihukumu ili usije ukahukumiwa.(2)Kwa maana kwa jinsi ile unavyowahukumu wengine, ndivyo utakavyohukumiwa na kwa kipimo kile utakachotoa ndicho utakachopokea. Mathayo 7:1-2

Mungu wetu aliye mbinguni ameanzilisha mfumo ambao utaruhusu watu kuhukumiwa kulingana na hukumu zao wenyewe. Wacha tuchunguze mahali

ambapo kupiga kwa mawe kulianzia. Hii ndio mara ya kwanza kupiga kwa mawe kunatajwa katika Bibilia.

> Musa akasema, Haitupasi kufanya hivyo; kwa kuwa tutamchinjia sadaka Bwana, Mungu wetu, na hayo machukizo ya Wamisri; je! Tutachinja sadaka ya hayo machukizo ya Wamisri mbele ya macho yao, **wasitupige kwa mawe?** Kutoka 8:26

Kupiga kwa mawe ilikuwa tabia ya Wamisiri. Hivi ndivyo walivyokabiliana na walioasi dhidi ya miungu yao. Moja wapo ya sababu ambayo Waisraeli walitaka kwenda jagwani kutoa kafara ni kwa kuwa wanyama ambao wangetoa kafara waliabudiwa na Wamisiri kama miungu. Inawezekana kuwa Farao alijuwa vizuri kuwa kama Waisraeli wangetolea kafara katika nchi, ingewachochea Wamisri kuwapiga kwa mawe. Kuwa Waisraeli walipokea tabia hii kutoka kwa Wamisiri ni dhahiri kwa kile walitaka kumfanyia Musa.

> Musa akamlilia Bwana, akisema, Niwatendee nini watu hawa? Bado kidogo nao watanipiga kwa mawe. Kutoka 17:4

Kalebu na Yoshua walipowasihi watu kuwa wangeenda mbele na wainyakue nchi ya Kanani, majibu yao yalikuwa kuwapiga kwa mawe.

> Ikiwa Bwana anatufurahia, atatuingiza katika nchi hii atupe iwe yetu, nayo ni nchi yenye wingi wa maziwa na asali. (9) Lakini msimwasi Bwana, wala msiwaogope wale wenyeji wa nchi, maana wao ni chakula kwetu; uvuli uliokuwa juu yao umeondolewa, naye Bwana yu pamoja nasi; msiwaogope. (10) **Lakini mkutano wote wakaamuru wapigwe kwa mawe.** Ndipo utukufu wa Bwana ukaonekana katika hema ya kukutania, mbele ya wana wa Israeli wote. Hesabu 14:8-10

Basi mbona Mungu angeruhusu tabia hii ya Wamisiri ya kupiga kwa mawe katika sheria kwa Waisraeli?

> kwa sababu hawakuzitekeleza hukumu zangu, bali walizikataa amri zangu, nao walizitia unajisi sabato zangu, na macho yao yaliandama vinyago vya baba zao. (25) **Tena naliwapa amri zisizokuwa njema, na hukumu ambazo hawakuweza kuishi kwazo;** Ezekieli 20:24-25

Amri na hukumu hii kuhusu kupiga kwa mawe haikuwa nzuri, na zilikuwa adhabu ambazo ziliingizwa au kuongezwa kwa sheria, iliyoadhibu kosa. Bila

shaka sio jambo nzuri kupigwa kwa mawe hadi kifo! Adhabu hizi zilikuwa kwa mujibu wa mawazo yao wenyewe ya kuhukumu kosa na iliangaza mafikira yao wenyewe na jinsi walivyokuwa wamejifunza kutoka kwa Wamisiri. Kama Yesu anavyoeleza:

> Unachukua ambapo hukuweka kitu na unavuna mahali ambapo hukupanda kitu.' (22) **"Bwana wake akamjibu, 'Nitakuhukumu kwa maneno yako mwenyewe, wewe mtumishi mwovu! Kama ulifahamu kwamba mimi ni mtu mgumu**, nichukuaye mahali ambapo sikuweka kitu na kuvuna mahali ambapo sikupanda, Luka 19:21-22

Waisraeli waliamini kuwa Mungu ni mtu mkali. Walipouona utukufu wake kwao ulikuwa kama moto uteketezao.

> Na kuonekana kwake ule utukufu wa Bwana kulikuwa kama **moto** uteketezao, juu ya mlima machoni pa wana wa Israeli. Kutoka 24:17

Kumbuka kuwa ni Waisraeli wenyewe walioianzisha tabia hii ya kuwapiga kwa mawe wadhambi ili kukabiliana nao. Waisiraeli walipoamua kumpiga Musa kwa mawe Kutoka 17:4, walidhihirisha roho ya kuhukumu bila huruma. Bibilia inasema:

> Kwa kuwa hukumu itakuwa haina huruma kwa mtu ye yote asiyekuwa na huruma. Huruma huishinda hukumu. Yakobo 2:13

Kwa kuwa Waisraeli hawakuonyesha huruma katika hukumu yao, utaratibu huu wa hukumu uliakisiwa kwao. Walichagua kuamini kuwa Mungu alitaka kuwaua jagwani, na walitaka Kumuua Musa kwa kumpiga kwa mawe. Mungu hadhihakiwi kwani Waisraeli walipopanda mbegu hii walivuna mazao yake. Kutoka kwa vinywa vyao wenyewe, Israeli walijihukumia kifo jagwani kulingana na imani yao kumhusu Mungu.

Waisraeli mara kwa mara walionyesha uwoga wao kuwa Mungu angewaua jangwani:

> Wakamwambia Musa, Je! Kwa sababu hapakuwa na makaburi katika Misri **umetutoa huko ili tufe jangwani?** Mbona umetutendea haya, kututoa katika nchi ya Misri? Kutoka 14:11

> wana wa Israeli wakawaambia, **Laiti tungalikufa kwa mkono wa Bwana katika nchi ya Misri**, hapo tulipoketi karibu na zile sufuria za nyama, tulipokula vyakula hata kushiba; kwani mmetutoa huko na kututia katika bara hii, ili kutuua kwa njaa kusanyiko hili lote. Kutoka 16:3

> Kisha wana wa Israeli wote wakamnung'unikia Musa na Haruni; mkutano wote wakawaambia, Ingekuwa heri kama tungalikufa katika nchi ya Misri, au, ingekuwa heri kama tungalikufa katika jangwa hili. (3) **Mbona Bwana anatuleta mpaka nchi hii ili tuanguke kwa upanga? Wake zetu na watoto wetu watakuwa mateka**; je! Si afadhali turudi Misri? Hesabu 14:2-3

Kwa hivyo walipokea hukumu kulingana na hukumu yao wenyewe:

> Kisha Bwana akanena na Musa na Haruni, na kuwaambia, (27) Je! Nichukuane na mkutano mwovu huu uninung'unikiao hata lini? Nimesikia manung'uniko ya wana wa Israeli, waninung'unikiayo. (28) Waambieni, **Kama niishivyo, asema Bwana, hakika yangu kama ninyi mlivyonena masikioni mwangu, ndivyo nitakavyowafanyia ninyi;** (29) mizoga yenu itaanguka katika jangwa hili, na wote waliohesabiwa miongoni mwenu, kama jumla ya hesabu yenu, tangu waliopata umri wa miaka ishirini na zaidi, hao walioninung'unikia, Hesabu 14:26-29

Katika wakati wa Kristo tunaona Mafarisayo walijichanganya kwa mfumo wa hukumu wao wenyewe ambao baba zao wa kwanza walipokea kutoka kwa Wamisiri. Unadhihirisha uwoga wa daima ambao Waisraeli waliishi chini yake na utumwa ulioleta.

> Je, ubatizo wa Yohana ulitoka mbinguni au kwa wanadamu?" (5) Wakasemezana wao kwa wao wakisema, "Kama tukisema, ulitoka mbinguni, atatuuliza, 'Mbona hamkumwamini?' (**6) Lakini tukisema, ulitoka kwa 'wanadamu', watu wote watatupiga mawe** kwa sababu wanaamini kwamba Yohana alikuwa nabii." (7) Basi wakajibu, "Hatujui ulikotoka." Luka 20:4-7

Ni dhahiri kuwa japo Waisraeli waliondoka Misri, Misri haikuwatoka. Mafarisayo waliishi katika ulimwengu wa kuhukumu, hasira, na kulipisha kisasi, wakimiliki sifa zote za Farao, Mkuu wa utumwa. Roho hii ni zao la jinsi walivyoitazama tabia ya Mungu. Kwa kweli, mungu waliyeabudu alikuwa

sawa na Farao. Taifa la Waisraeli lilipotengenezwa Mungu aliruhusu mawazo yao yawekwe katika sheria. Ingewezekanaje Mungu aruhusu sheria yake ichafuliwe na mawazo ya watu waovu? Ni kwa sababu kusudi la sheria ni kuleta hatia ya dhambi ili kwamba aweze kupeana rehema.

> Zaidi ya hayo, sheria ilikuja, ili uvunjaji wa sheria uongezeke. Lakini dhambi ilipoongezeka, neema iliongezeka zaidi. Warumi 5:20

Baba yetu aliye mbinguni angeruhusu adhabu ya namna yeyote iongezewe kwa sheria yake kwa maana kifo chochote kingeamuriwa kilikuwa tu ni kwa lengo la kutoa rehema kwa walioiagiza. Tunakumbuka ambacho maandiko yanasema kuhusu tabia ya Mungu:

> Bwana akapita mbele yake, akatangaza, Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa **huruma, mwenye fadhili**, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; Kutoka 34:6

> Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema, Kwa maana **fadhili zake ni za milele.** Zaburi 107:1

Mungu daima ni mwingi wa rehema na daima ni mapenzi yake kuonyesha rehema. Rehema hutoweka tu watu wanapokataa kuiamini na kuitamani hukumu. Ni watu ndio ambao huilazimisha rehema kutoweka, na kujificha kutoka kwake kwa kuamini kuwa Mungu ni kama wao. Wanataka kuamini kuwa Mungu huwageuka watu na huwangaamiza wanapoacha kumpendeza. Kama hili lilikuwa kweli basi hatuwezi sema kuwa rehema za Mungu hudumu milele. Tunakumbuka kwamba mtu ambaye huhukumu bila huruma hapokei rehema kwa sababu hili ndilo ameamua yeye mwenyewe. Hii ndio maana mtu aliyemkufuru Mungu alipigwa kwa mawe hadi kifo bila huruma.

> kisha huyo mwana wa mwanamke wa Kiisraeli akalikufuru hilo Jina, na kuapiza; nao wakamleta kwa Musa. Na jina la mamaye alikuwa akiitwa Shelomithi, binti ya Dibri, wa kabila ya Dani. (12) Nao wakamtia kifungoni, ili wapate kuambiwa neno litakalotoka kinywani pa Bwana. (13) Na Bwana akasema na Musa, na kumwambia, (14) Mtoe huyo aliyeapiza nje ya marago; na wale wote waliomsikia na waweke mikono yao kichwani mwake, kisha mkutano wote na wamwue kwa kumpiga kwa mawe. Walawi 24:11-14

Mungu aliweka hukumu ya kifo ambayo Israeli wenyewe waliamua kupitia uhusiano wao na adhabu ya kukufuru miungu ya Wamisiri. Mungu wetu alimtaka mtu huyu atiwe hatiani kuwa dhambi yake ilikuwa chungu na kweli alistahili kifo, lakini kwa lengo la kumpa rehema. Tunajua hili ni kweli kwa sababu ya maneno ya aliyepeana sheria mwenyewe:

> Kwa hiyo nawaambia, kila dhambi na kufuru watu watasamehewa, lakini mtu atakayemkufuru Roho Mtakatifu hatasamehewa. Mathayo 12:31

Yesu alisema kuwa kila dhambi inaweza samehewa isipokuwa moja – kumkufuru Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu hufanya kazi katika mawazo yetu na kutusihi tutubu na kuomba rehema. Mtu ambaye huendelea kukataa kuisikiza sauti inayomwagiza atubu hataipokea rehema, na kwa hivyo, atahukumiwa kulingana na adhabu ambayo watu wake wameweka. Laiti mtu katika Walawi 24 angaliomba rehema angalipewa. Alimkufuru Roho Mtakatifu aliyemsihi atubu kwa kuwa Baba yetu hapendelei mtu yeyote akipotea. Lakutisha aliinyamazisha sauti na kwa hivyo akafa kulingana na imani yake kuwa Mungu hangemsamehe.

Ni wangapi miongoni mwetu huchukua mawe na kuwapiga watoto wetu hadi kifo kwa sababu ya dhambi ambazo hawajatubu na kuwaponda kwa hiari na kufanya damu kutapaka sakafuni? Wazo lenyewe ni la kuchukiza haliwezi elezeka kwa maneno. Bado mamillioni ya watu wanaamini kuwa Baba yetu wa mbinguni alidai hili kutoka kwa Waisraeli. Watu wangapi wameenda kaburini wakimchukia huyu Mungu ambaye walimdhania kuwa alipendzwa watu wakipigwa mawe hadi kufa? Wakristo wengi wanamshukuru Mungu kwa kuwa katika Agano Jipya mambo yamebadilika, lakini hili halijabadilisha kwa vyovyote kuamini kwao kuwa Mungu alikuwa hivyo katika Agano la Kale. Mara nyingine tena tunakumbushwa kuwa Yesu alisema kuwa hakuja kuitangua sheria. Sheria bado inasimama, lakini kama tulivyo jifunza, Baba yetu kamwe hatamani kumuua mtu yeyote.  Anawahurumia watu wote.

“Naomba kwamba uufungue moyo wako kwa Mungu wetu mbinguni. Anakupenda sana. Kamwe hajawai taka kukuumiza au kukuua kwa ajili ya dhambi zako. Anataka tuone kuwa dhambi zetu zinatuangamiza na kuwa tunaweza omba msamaha wakati wowote. Utakapojua kuwa Mungu hajakukasirikia na kuwa anakupenda kweli basi unaweza mkimbilia na kuungama dhambi zako zote na kuwa na hakika kuwa atakusamehe zote.

Kama Yesu alivyomwambia mwanamke aliyeshikwa akizini – “wala mimi sikuhukumu. Enenda zako; wala usitende dhambi tena.”

Lakustajabisha wale ambao hukana ukweli kuwa Mungu huwapenda kweli na daima yuko tayari kuwaonea huruma, hawatapokea huruma yoyote; kwa sababu wanaamini kwa Mungu ambaye hana huruma kwa wadhambi, na kwa hivyo wanapoteza tumaini la kusamehewa. Kama Kaini wanalia – “Uovu wangu ni mkubwa, hauchukuliki.”

> Kwa kuwa walichukia maarifa, Wala hawakuchagua kumcha Bwana. (30) Hawakukubali mashauri yangu, Wakayadharau maonyo yangu yote. (31) Kwa hiyo watakula matunda ya njia yao, Watashiba mashauri yao wenyewe.(32) Maana kurudi nyuma kwao wajinga kutawaua, Na kufanikiwa kwao wapumbavu kutawaangamiza. Methali 1:29-32

Lisikize neno la Mungu na uamini lisemalo:

> Bwana alinitokea zamani, akisema, Naam nimekupenda kwa upendo wa milele, ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu. Yeremia 31:3

> Haya, njoni, tusemezane, asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu. Isaya 1:18

> …na kuzifuta katika maji ya uchungu; Hesabu 5:23

## 9. Sheria kama Kioo

Tunapoangalia hadithi za Yesu katika injili tunamtazama Baba. Yesu alimwambi Filipo, "Aliyeniona mimi amemwona Baba." Yohana 14:9. Kuna hadithi muhimu katika injili ambayo inaangazia kipengele muhimu cha tabia ya Baba yetu ambayo mara nyingi ni kuielewa visivyo kabisa. Yesu aliifanya karibu hudumu yake yote katika himaya ya taifa la Wayahudi. Wakati mchache akichagua kutembelea maeneo ya wapagani ya Phoenicia.

Kiburi na chuki ilikaa kwa kina kwa Wayahudi ilishika mioyo ya wanafunzi na kupofusha macho yao kwa uhusika wao katika dhambi za taifa la ubaguzi wa rangi na chuki ya kiroho. Israeli walikuwa wameitwa kuwa nuru kwa watu wa Mataifa, hata hivyo, waliigeuza fadhila hii kuwa giza kupitia madharau yao kwa majirani wao ambao hawakupendelewa.

Mwanamke aliyeishi katika eneo hili, pamoja na watu wengi wa jamii yake, alikuwa amesikia juu ya mwalimu huyu wa Kiyahudi ambaye angetibu watu. Binti wake alikuwa "amepagawa na pepo" na alikuwa ameijaribu miungu yake imsaidie binti yake lakini bila mafanikio. Alihofia kama mwalimu wa Kiyahudi angemsaidia binti yake. Aliamua kumsihi Yesu kuhusiana na hali yake huku akishikilia shuku ya kile ambacho Myahudi huyu angekitenda, au angefanya, kwa ajili yake.

Kilio cha moyoni cha mama huyu kilifika kwenye masikio ya Mkombozi.

> “Nihurumie,Ee Bwana, Mwana wa Daudi, binti yangu amepagawa na pepo na anateseka sana.” Mathayo 15:22

Kama Mwana wa Mungu wa kujitoa kafara, moyo wake ulijawa huruma. Alikuwa amekuja hasa katika eneo hili kwa ajili yake, lakini jambo ambalo Yesu anafanya baadaye linadhihirisha jambo muhimu kuhusu tabia ya Mungu.

> Lakini Yesu hakumjibu neno. Mathayo 15:23

Sababu yake ya kufanya hivi ni dhahiri kataki sentensi inayofuata.

> Hivyo wanafunzi wake wakamwendea na kumsihi sana, wakisema, “Mwambie aende zake, kwa maana anaendelea kutupigia kelele.” Mathayo 15:23

Kama Yesu angemtimizia ombi lake mara hiyo, ugumu wa wanafunzi haungedhihirishwa. Hivyo basi, Mkombozi alikaa kimya kuona vile wangejibu. Walitafsiri kunyamaza kwake kama uthibitisho wa chuki yao kwa kuzingatia rangi na taifa. Pia wakati huo huo, kunyamaza kwake kulijaribu shaka kuwa mwanamke huyu wa kigeni alikuwa anajishughulisha na huyu mwalimu wa Kiyahudi. Tunaona vitendo vya Yesu vikitenda kama kioo kwa kudhihirisha kilicho mioyoni mwa wale waliomzunguka.

Mfano mwengine wa hili ni pamoja na wakati yesu alipo “alifanya kama anataka kuendelea mbele” alipokuwa akitembea na wale wawili kwenda Emmau. Luka 24:28. Na wakati Yesu alipokuja “akitembea juu ya maji; akataka kuwapita.” Marko 6:48.

Kama ambavyo tumejifunza, wanafunzi walikuwa wanakataa wito wa kuubeba msalaba wao wenyewe machoni pa kukataliwa kwa Mwana wa Mungu na ulimwengu. Hili liliwapofusha kwa mambo mengi ambayo Yesu alijaribu kuwaambia. Kwa vile walikuwa wasikizaji wa sheria walimtazama yesu kwa namna ifuatayo:

> Basi iweni watendaji wa Neno wala msiwe wasikiaji tu, huku mkijidanganya nafsi zenu. (23)Kwa maana kama mtu ni msikiaji tu wa Neno wala hatendi kile linachosema, **yeye ni kama mtu ajitazamaye uso wake kwenye kioo**(24)na baada ya kujiona alivyo, huenda zake na mara husahau jinsi alivyo. Yakobo 1:22-24

Wanafunzi walikuwa wamejibu wito wa Kristo wa ufalme mpya, lakini mioyo yao haikuwa imetii kanuni ya kujikana nafsi, wala kukataliwa kwa Masihi wao mpendwa na taifa lao. Hili liliwafanya wasikilizaji wa sheria ikitoka kinywani mwa Yesu. Yesu alipokuwa kimya kwa mwanamke wa kigeni waliona sura zao wenyewe ndani yake na wakafasiri vitendo vyake kama ubaguzi wa rangi. Walikuwa wakionyesha mitazamo yao wenyewe na tamaa zao kwake iliyopelekea wao kumsihi Kristo kumfukuza mwanamke huyu mbele yake. Hili lilikuwa linavunja kiasi gani kwa mwanamke kuwasikia wakizungumza namna hii. Dhiki yake kwa binti yake lazima ilimchoma ndani alipogeuka kusikiliza kile Yesu angesema.

> Yesu akajibu, "Nimetumwa tu kwa ajili ya kondoo wa Israeli waliopotea." Mathayo 15:24

Jibu hili lilimjaribu kila mtu kuona kama kweli walikuwa wakisikiliza. Yesu alitambulishwa na Yohana mbatizaji kwa maneno haya:

> "Tazama, Mwana Kondoo wa Mungu aichukuaye **dhambi ya ulimwengu!"** Yohana 1:29

Yesu alikuwa Mkombozi wa ulimwengu wote, sio tu wa Wayahudi halisi. Ukweli huu ulikuwa umebainishwa na mwanamke Msamaria kisimani na wale waliotoka nje ya mji:

> Wakamwambia yule mwanamke, "Sasa tunaamini, wala si kwa sababu ya maneno yako tu, bali kwa kuwa tumemsikia sisi wenyewe. Tumejua hakika kweli ya kwamba huyu ndiye Kristo, Mwokozi wa ulimwengu." Yohana 4:42

Yesu alikuwa Mkombozi wa ulimwengu lakini ufalme wake kwa hakika haukuwa wa ulimwengu:

> Yesu akajibu, "Ufalme Wangu si wa ulimwengu huu. Ufalme Wangu ungekuwa wa ulimwengu huu wafuasi Wangu wangenipigania ili nisitiwe mikononi mwa Wayahudi. Lakini kama ilivyo Ufalme Wangu hautoki hapa ulimwenguni." Yohana 18:36

Neno *Israeli* linarejelea wale wote ambao watakubali karama ya Ukombozi. Kama waraka wa mtume Paulo unavyoielezea:

> Kwa maana mtu si Myahudi kwa vile alivyo kwa nje, wala tohara ya kweli si kitu cha nje au cha kimwili. (29) Lakini mtu ni Myahudi

> alivyo ndani na tohara ya kweli ni jambo la rohoni, ni la kiroho, wala si la kimwili. Mtu wa namna hiyo hapokei sifa kutoka kwa wanadamu bali kwa Mungu. Warumi 2:28-29

Mkombozi alikuwa akiwazungumzia kuhusu ufalme wake wa kiroho wa moyo. Kwa kuja kwa Yesu, mwanamke alikuwa akijibu wito wa Roho. Alidhibitisha kuwa, kweli, alikuwa wa nyumba ya Israeli. Sio Israeli kimwili, lakini Israeli Kiroho. Jina Israeli lilipewa Yakobo kwa ushindi wa Imani aliyoweka wazi katika kupigana na malaika katika hali yake ya kukata tamaa. Sasa mwanamke huyu alionyesha kuwa, kweli, alikuwa mshindi Mwisraeli wa kweli.

> Lakini yule mwanamke akaja, akapiga magoti mbele ya Yesu, akasema, "Bwana, nisaidie!" Mathayo 15:25

Imani ya mwanamke haizai matunda. Anashikila katika imani. Mkombozi alikuwa na hamu ya kumsaidia lakini bado mtihani wake haujaisha.

> Yesu akajibu, "Si haki kuchukua chakula cha watoto na kuwatupia mbwa." Mathayo 15:26

Hapa neno *lakini* halimaanishi kuwa yesu alikuwa anakabiliana na ombi la mwanamke huyu. Neno la Kiyunani *de* pia humaanisha *na* katika hali ya kuendelea kwa wazo. Yesu alikuwa akimuuliza kuamua sasa kama kweli alikuwa Mwisraeli. Maneno yake yamewekwa kwa njia ambayo ni kama jaribio la chuki kwa msingi wa rangi na taifa la wanafunzi na pia shuku yake juu ya mwalimu huyu myahudi. Mwanamke huyu angesema "Bwana mimi ni mmoja wa wana wako, na ninaamini utanisaidia." Hili ndilo jibu kuu ambalo mwanamke angelitoa. Lakini jibu lake linastajabisha kwa kuwa ijapo anamwita mbwa, bado anaishikilia imani.

> Yule mwanamke akajibu, "Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo yanayoanguka kutoka kwenye meza za bwana zao." Mathayo 15:27

Hata kama alifikiria kuwa Yesu alimwita mbwa bado alishikilia imani akiamini kuwa Yesu angemsaidia, akimfanya Mwisraeli wa kweli mshindi. Upendo wa mwanamke huyu kwa bintiye na jibu lake kwa Mvuto wa Roho ulimpa ushindi wa Imani.

> Ndipo Yesu akamwambia, “Mwanamke, imani yako ni kubwa! Iwe kwako kama unavyotaka.”Naye binti yake akapona tangu saa ile ile. Mathayo 15:28

Jibu hili liliwakemea wanafunzi. Walikuwa wakiyasikia maneno ya Yesu na mioyo yao ya kibinadamu na walikuwa wakionyesha ubaguzi wao kupitia kwake. Yesu alipojibu ombi la mwanamke huyo walishangazwa na mtazamo wao ulivunjwa. Kwa hatua hii wangefikiria vitendo vya Yesu kuwa vya ajabu au wangeanza kuhoji chuki na ubaguzi wao.

Yesu ana jina katika andiko “hekima ya Mungu.” 1wakorintho 1:24. Hekima hii itokayo kwa Baba yake humruhusu kuingiliana na wanadamu na kudhihirisha kilicho mioyoni mwao bila kukabiliano nao moja kwa moja, jambo ambalo hutoa upinzani tu. Mbona Yesu hakuwaambia kuwa, “Mnashida ya ubaguzi na chuki na lazima muiepuke”? Hili halingekuwa limefanikisha chochote. Badala yake, Yesu anazungumza kwa namna ambayo inaruhusu neno lake kutenda kama kioo na kudhihirisha kilicho moyoni.

Mara tu unapoelewa kanuni hii, unaweza soma andiko kama mtendaji wa sheria na wala sio kama msikizaji tu ukitazama uso wako halisi. Jaribu ambalo Yesu aliwapa wanafunzi linamkabili kila msomaji wa Bibilia. Mambo yanayoonyeshwa katika maandiko ili kudhihirisha kilicho moyoni mwa msomaji. Kama wanafunzi walivyosoma katika vitendo vya Yesu chuki yao ya kitaifa, Wengi husoma maandiko wakielezea Mungu kupitia uelewa wao wa kibinadamu badala ya kulingana na tabia ya kweli ya Mungu. Kifungu kifuatacho kinasikika kama Mungu anasahau kuhusu watu wake na kuwageukia.

> Nami nitawatawanya mbele ya adui, kama kwa upepo wa mashariki; **nami nitaviangalia visogo vyao,** wala si nyuso zao, siku ya msiba wao Yeremia 18:17

Tunatumia neno kugeuza nyuma kwa watu kuonyesha kuwakataa kwetu. Zingatia muktadha wa jinsi Mungu anaonyesha nyuma yake katika kifungu hiki:

> kisha itakuwa wakati unapopita utukufu wangu, nitakutia katika ufa wa ule mwamba, na kukufunika kwa mkono wangu hata nitakapokuwa nimekwisha kupita; (23) nami nitaondoa mkono

wangu, **nawe utaniona nyuma yangu**, bali uso wangu hautaonekana. Kutoka 33:22-23

Katika muktadha huu Mungu anaonyesha mugongo wake ili kumchunga Musa kutoka kwa utukufu kabisa wa tabia yake. Upendo wa Mungu kwa wanawe ni mkubwa sana, hivyo basi kuifia nafsi na utunzaji ambao mwenye dhambi aonapo upendo huu kikamilifu, mara moja huleta maana ya kukwaruzana na kujihukumu kwa nafsi na hatia.

Maana watu wangu wamenisahau, wameufukizia ubatili uvumba; nao wamewakaza katika njia zao, katika mapito ya zamani, ili wapite katika njia za kando, katika njia isiyotengenezwa; Yeremia 18:15

Israeli walikuwa wamemsahau Bwana na wakazigeukia njia zingine. Bwana alificha utukufu wake na akawageuzia mgongo ili wasiharibiwe kabisa. Pia, aligeuza uso wake ili kwamba wasiweze kuona mateso na huzuni yake kwa kuona watoto wake wakivuna walicho kipanda.

Naliwatolea wapigao mgongo wangu… Isaya 50:6

Vitendo vya Waisraeli vilikuwa vikimuumiza mkombozi wetu. Ibada ya sanamu ilimuumiza Zaidi. "Katika mateso yao yote yeye aliteswa, na malaika wa uso wake akawaokoa; kwa mapenzi yake, na huruma zake, aliwakomboa mwenyewe; akawainua, akawachukua siku zote za kale." Isaya 63:9. Basi aligeuza uso kwa mapigo yao. Kirai hiki kinaweza eleweka kama Bwana akiwa anajeruhiwa kwa makosa ya watu wake katika kumkata kwao na pia kulinda watu wake kutoka kwa utukufu kamilifu wa tabia yake ili wasivunjwe kikamilifu na hatia yao. Moyo wa ubinadamu utasoma kifungu hiki kama Mungu kuwakataa tu watu wake kwa sababu hivyo ndivyo hasa jinsi binadamu wataitikia na wakati tunasoma Bibilia kihalisia hivyo ndivyo tutakavyoelewa. Kwa shukurani mawazo ya Mungu sio mawazo yetu. Isaya 55:8-9.

Wacha tutazame mfano mwingine wajinsi Neno la Mungu hutenda kama kioo nafsini mwetu. Katika hesabu 13 tunasoma yafuatayo:

Kisha Bwana akanena na Musa, akamwambia, (2) Tuma watu, ili waende wakaipeleleze nchi ya Kanaani, niwapayo wana wa Israeli; katika kabila ya baba zao mtamtuma mtu mmoja, kila mtu na awe mkuu kati yao. Hesabu 13:1-2

Lakini tunasoma katika Kumbukumbu 1:22

> Tazama, Bwana, Mungu wako, ameiweka nchi mbele yako; haya panda, itamalaki, kama Bwana, Mungu wa baba zako, alivyokuambia; usiogope wala usifadhaike. (22) Nanyi mkanikaribia kila mmoja wenu, mkasema, Na tupeleke watu mbele yetu, ili watupelelezee nchi na kutuletea habari za njia itupasayo kuipandia, na za miji tutakayoifikia. (23) Neno hili likanipendeza sana; nikatwaa watu kumi na wawili, mtu mmoja wa kila kabila. Kumbukumbu 1:21-23

Kifungu katika Hesabu 13 hakitoi muktadha wote wa kile kilitendeka. Kinawakilishi amri ya Mungu ya kupeleleza nchi. Vifungu viwili vilivyowasilishwa namna hii katika maandiko hutoa radha ndogo kwa msomaji. Kama msomaji anashikilia moyoni mwake hamu ya kukanusha Bibilia, vifungu hivi vinaweza wekwa pamoja na kutumika kuthibitisha kuwa Bibilia hujipinga yenyewe. Utata unaopatikana ndani ya msomaji unaonyeshwa kwenye Bibilia. Mtendaji wa sheria angejua kwa haraka kuwa amri ya kupanda juu na kuchukua nchi ilimaanisha kuwa hakuna haja ya kupeleleza nchi, na ombi la kupeleleza lilidhihirisha ukosefu wa imani. Mungu hujibu maombi kwa amri kulingana na hamu yao. Habari za kuogofya ambazo wengi wa wapelelezi walileta zinadhihirisha ukosefu wa imani ulikuwa mioyoni mwao jambo ambalo lilisababisha ombi la kupeleleza nchi. Hivyo Bibilia imeandikwa kwa njia ambayo mtu anayeishi katika utata anaweza kusoma Bibilia na kupata utata anaoutafuta ili kutetea madai yake. Mtendaji wa sheria anazidi kushikilia imani na anatafuta kutatua mapambano wazi na kuunganisha Bibilia.

Wacha tuangazie hadithi ya Daudi kuwahesabu Waisraeli.

> Tena hasira ya Bwana ikawaka juu ya Israeli, akamtia Daudi nia juu yao, akisema, Nenda, ukawahesabu Israeli na Yuda. 2 Samweli 24:1

Sasa linganisha hii na 1 Mambo ya Nyakati 21:1

> Tena shetani akasimama juu ya Israeli, akamshawishi Daudi kuwahesabu Israeli. 1 Mambo ya Nyakati 21:1

Mara nyingine pale inaonekana, kwa uso, utata. Hili ni sawa na wakati Yesu alikuwa amewasilishwa kama Mkombozi wa ulimwengu na kisha akasema

kwa mwanamke, “si kutumwa ila kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli.” Tunajaribiwa tunaposoma kifungu hiki. Katika sura ya mbele tutaangalia kwa undani kuhusu hasira ya Bwana. Kwa sasa tutaangazia tu katika kusoma maneno ya Kiebrania katika nuru ya maisha ya Yesu Kristo. kuhesabu huku kwa wana wa Israeli kulipelekea kwa kifo cha watu 70,000.

> Basi Bwana akawaletea Israeli tauni tangu asubuhi hata wakati ulioamriwa; nao wakafa watu toka Dani mpaka Beer-sheba sabini elfu. 2 Samweli 24:15

Baadhi ya watafsiri wanaashiria kuwa Mungu alikuwa na hasira sana na Israeli, alitengeneza kisingizio cha kuyaangamiza maelfu ya watu:

> Tena hasira ya Bwana ikawaka juu ya Israeli, akamtia Daudi nia juu yao, akisema, Nenda, ukawahesabu Israeli na Yuda 2 Samweli 24:1

Tunaposoma kuwa hasira ya Bwana ikawaka juu ya Israeli ni taswira gani hili linajenga katika mawazo yako? Tunawaza mtu aliye na uso mwekundu akienda juu na chini, tayari kuripuka katika hasira? Inawezekana kuwa watafsiri walikuwa wakisoma Kiebrania kulingana na uelewa wao wenyewe? Kinachoshangaza kuhusu tofauti ya maana katika maneno ya Kiebrania ni kuwa msomaji au mtafsiri ataamua lahaja. Kwa baadhi ya maneno tofauti ya maana hubadilika kwa kiasi kikubwa maana ya kile kinachosomwa. Unapo angalia neno *hasira* na *ikawaka* katika 2 samueli 24:1 yanaweza fasiriwa kama *kuteseka* na *kuhuzunishwa*. Neno *akamtia* linamaana ya *kushawishi*, hivyo tunaweza soma kifungu ifuatavyo.

> Tena hasira ya Bwana ikawaka juu ya Israeli, akamtia Daudi nia juu yao, akisema, Nenda, ukawahesabu Israeli na Yuda 2 Samuel 24:1

Hili basi liko katika uelewana na 1 mambo ya Nyakati 21:1 linalosema shetani akasimama juu ya Israeli. Mbona Daudi akashawishiwa? Ni kwa sababu Israeli walimhuzunisha Roho wa Mungu, hasira ya bwana inaelezewa katika Bibilia akiruhusu malaika wa shetani kuchukua uongozi.

> Akawapelekea ukali wa hasira yake, Ghadhabu, na uchungu, na taabu, Kundi la malaika waletao mabaya. Zaburi 78:49

Tena neno kutuma linaweza tafsiriwa kama kuachilia. Ghadhabu ya Mungu inaelezewa kama hatimaye kuruhusu watu wake kumtupilia mbali, jambo ambalo linamfanya shetani kusimama na kuchukua uongozi wa hali hiyo. Baba yetu wa thamani anawapenda watoto wake, na Mkombozi wetu na Mchungaji wetu ambaye anatunza kondoo wake bila kuchoka. Watu wake wanapoendelea kupuuza na kukataa wito wake, hatimaye lazima awaruhusu wapate matamanio yao wenyewe. Israeli walitamani ukuu wa kitaifa chini ya Daudi. Roho wa Mungu aliwasihi wasitafute vitu hivi, lakini roho huyo aliyekuwa akitaka mfalme sasa alikuwa anataka kupanua himaya. Hivyo Bwana akamruhusu shetani kumpotosha Daudi kwa kuwahesabu watu.

Watafsiri wengi wa Bibilia wanachagua kufasiri neno la Kiebrania *aph* kama *hasira* katika 2 samueli 24:1. Ambapo katika Kutoka 34:6 neno sawa linalohusishwa na neno la *muda mrefu* linafasiriwa ifuatavyo:

> Bwana akapita mbele yake, akatangaza, Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; Kutoka 34:6

Mungu ameruhusu neno hili la Kiedbrania kutumika kama kioo nafsini mwetu. Tunaweza lisoma kama hasira au kuteseka. Hii ni kwa sababu neno la kiebrania linamaanisha pua au kupumua kwa haraka kupitia kwa pua. Kupumua kwa haraka kunaweza tokana na hasira au huzuni kubwa. Wakati Yesu aliwaambia wanafunzi kuwa lazima angeteseka kwa ajili ya mambo mengi mikononi mwa viongozi, hawakutaka kulisikia hili. Hivyo tunapata katika sehemu nyingi watu afadhali wafikirie Mungu kama mwenye hasira kwa wale ambao wanatenda dhambi dhidi yake kuliko kumuona kama Baba atesekae na kuvunjwa moyo. Kama wangeruhusu nafsi zao kuona hili, linaweza leta imani ya kuacha kumjeruhi Baba yetu. Kumuona kama mwenye hasira huruhusu watu wengi kuhalalisha kutenda dhambi kwao. Kama vile tu wanafunzi walivyotafsiri kunyamaza kwa Yesu kama ubaguzi wa kikabila watafsiri wengi wa Bibilia, na kwa hivyo, wasomi, wanasoma hisia zao wenyewe kuelekea udhalimu katika tabia ya Mungu.

Mfano wa mwisho wa kuangazia :

> Basi Sauli alikufa kwa sababu ya kosa lake alilomkosa Bwana, kwa sababu ya neno la Bwana, asilolishika; na tena kwa kutaka shauri kwa mwenye pepo wa utambuzi, aulize kwake, (14) asiulize kwa

> Bwana; kwa hiyo akamwua, na ufalme akamgeuzia Daudi, mwana wa Yese. 1 Mambo ya Nyakati 10:13-14 (NKJV)

kama mtu alikuwa anatafuta ushahidi wa kuonyesha kuwa Mungu huwaua watu hili litaonekana kuwa swala rahisi. Inasema kuwa Mungu alimuua Sauli. Fungu hili ni kioo. Msikiaje wa sheria ataona sura yake mwenyewe katika fungu hili. Sauli alikuwa amependelewa sana na Mungu na Sauli akaasi dhidi yake. Mtu halisi atakuwa na hisia za kulipiza kisasi katika hali kama hiyo na kumhukumu Sauli kuwa anafaa kuuawa. Kwa upande mwingine, mtu halisi anaweza kuwa na hisia sawa za uasi kwa mamlaka na kusoma fungu hili kama Mungu kumuua Sauli moja kwa moja kunakupa ushahidi wa kuthibitisha kuwa mamlaka ni katili na isiyotaka kufikiria. Kwa wale ambao husoma Bibilia kupitia kwa tabia ya Yesu, watatafuta majibu zaidi ili kuelezea fungu hili kwamba Mungu kwa kweli alimuua Sauli. Katika hali hii jibu linapatikana katika mafungu kumi ya mwanzo katika sura hiyo.

> Tena vita vilikuwa vikali sana juu ya Sauli, na wapiga upinde wakampata; hata akafadhaika sana kwa sababu ya wapiga upinde.(4) Ndipo Sauli akamwambia yule mchukua silaha zake, Futa upanga wako, unichome nao, wasije watu hawa wasiotahiriwa wakanisimanga. Lakini huyo mchukua silaha zake akakataa; kwa sababu aliogopa sana. Basi Sauli akautwaa upanga wake, akauangukia. 1 Mambo ya Nyakati 10:3-4

Sauli alijiua. Sauli alikuwa ametanga mbali na Mungu na hili lilimaanisha kuwa Mungu hakuwa na uwezo wa kumlinda vile angetaka kufanya. Sauli hakuwa akilindwa katika vita na matukio yalitendeka kwa njia ambayo Sauli aliyamaliza maisha yake. Hili linatupa muktadha wa mafungu.

Kuna funzo muhimu hapa kwa wasomi wa Bibilia. Kama unao uhakika kuwa huduma ya Kristo duniani ni ufunuo wa Baba na kufahamu kuteseka kwa Kristo kupitia kwa kukatiliwa kila anakoshuhudia kwa jamii ya mwanadamu, basi kama mwanamke wa Syrophoenicia tutashikilia katika imani na kuamini kuwa kweli ni mwingi wa rehema hata inapoonekana kuwa hana. Hii ni sheria ikitenda kama kioo kwa nafsi zetu ilikutoa kilicho mioyoni mwetu ili tuweze kutubu uonyesho wetu wa hamu zetu na mwelekeo juu ya Kristo na Baba yake.

> …Iwe kwako kama unavyotaka. Mathayo 15:28

## 10. Kutia Hofu ya Mungu ndani yako

> Ilipokaribia wakati wa Pasaka ya Wayahudi, Yesu alipanda kwenda Yerusalemu. (14) Huko hekaluni aliwakuta watu wakiuza ng'ombe, kondoo na njiwa. Nao wabadilisha fedha wakiwa wameketi kwenye meza zao. (15) Akatengeneza mjeledi kutokana na kamba, akawafukuza wote kutoka kwenye eneo la hekalu pamoja na kondoo na ng'ombe. Akazipindua meza za wale waliokuwa wakibadilisha fedha na kuzimwaga fedha zao. (16) Akawaambia wale waliokuwa wakiuza njiwa, "Waondoeni hapa! Mnathubutuje kuifanya Kipipa kimoja kidogo chenye ujazo wa lita.Hivyo kila mtungi ulikuwa na ujazo wa nyumba ya Baba yangu kuwa mahali pa biashara?" (17) Wanafunzi wake wakakumbuka kuwa imeandikwa: "Wivu wa nyumba Yako utanila." Yohana 2:13-17

> Ndipo akaingia hekaluni akaanza kuwafukuza wale waliokuwa wakiuza vitu humo. (46) Naye akaawaambia, "Imeandikwa, 'Nyumba Yangu itakuwa nyumba ya sala, lakini ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi.' " Luka 19:45-46

Pasaka ilitengenezwa ili kufunza wenye dhambi kuhusu upendo wa ajabu wa Mungu katika kumtoa Mwanawe afe kwa ajili ya ulimwengu.Viongozi wa Israeli walikuwa wamegeuza hili kuwa nafasi ya kujitajirisha kwa gharama ya watu wengine. Dhabihu ilihitajika kwa kila familia na ili kununua mwana kondoo mtu alihitaji kubadilisha sarufu za ndani kwa shekeli ya hekalu.

Ubadilishaji huu wa fedha ulitoa fursa ya kuuza mnyama wa kutolewa kafara kwa bei ya juu. Masikini na waliokuwa katika mazingira magumu walikuwa na wakati mgumu wa kuweza kupata dhabihu iliyohitajika, jambo ambalo liliwaacha wakifikiria kuwa wamedanganywa na watu wale ambao walihitajika kuwafunza kuhusu wingi wa neema ya Mungu.

Yesu alipozuru eneo la hekalu, moyo wake ulihuzunishwa. Kama vitendo hivi vingebaki bila kupingwa vingewapeleka mamilioni kaburini bila Kristo na bila wokovu kwa sababu ukweli wa injili ulikuwa ukigeuzwa kuwa tamaa za kibinafsi. Hapa tunatangulizwa katika kipengele cha tabia ya Mungu ambayo hueleweka vibaya kwa urahisi. Mungu aliwapenda kwa kina hawa watu waliokuwa wakitenda maovu haya kadri alivyowapenda wale ambao walikuwa wakidanganywa na makuhani. Ili kuwafikia viongozi hawa walihitaji kukabiliwa kwa mwendo wao wa dhambi ili kuwaokoa. Huu ndio mtindo ambao ukombozi hufuata:

> Zaidi ya hayo, sheria ilikuja, ili uvunjaji wa sheria uongezeke. Lakini dhambi ilipoongezeka, neema iliongezeka zaidi. Warumi 5:20

Kubadilishana kwa hasira na machungu ya shughuli katika hekalu yalikuwa udhihirisho wa hali za mioyo ya watu walioliongoza taifa. Kama hawangetubu kwa vitendo hivi wangekufa.

Mkombozi wa ulimwengu anauwezo wa kusoma nafsi za wanadamu, kama Baba ajuavyo hesabu ya nywele katika kila kichwa, hivyo anajua kwa ukaribu sana mawazo ya kila mtu. Kama Uungu umlikavyo ubinadamu, Kristo husoma siri za ndani kabisa za wale wote wamzungukao. Hiki kilikuwa kipindi cha hukumu; waliokuwa mbele ya Kristo walitambua kuwa Mkombozi angesoma kila kitu cha nafsi zao. Kwa waovu hili lilikuwa jambo la kutisha zaidi waliloshuhudia. Vitendo vya kuchukua viboko vya kamba haikuwa kuwapiga watu na kuwaumiza kwa nje, bali kuwavutia juu ya uovu waliokuwa wakiutenda. Hakuna mtu aliyeuawa, hakuna mtu aliyejeruhiwa, lakini bidhaa za biashara ziliangushwa chini kama onyo la kuwa vitu hivi vilikuwa vinawaangamiza.

Mkombozi alikuwa anawatia hatiani kwa dhambi, sio kuwaangamiza bali kuwaokoa. Alikusudia waone hatari, watubu, na waokolewe. Roho wa Mungu alipochunguza mioyoni mwao alikuwa kuwahimiza wageuke kutoka kwa dhambi zao na waombe msamaha kwa matendo yao maovu. Badala

yake, watu waliamua kuukimbia uso wake na kuchagua kuzishikilia dhambi zao badala ya kuziacha. Walifukuzwa hekaluni kwa sababu ya kukataa kutubu. Kama wangetubu wangepokea neema na amani nafsini mwao ambayo ingewaruhusu kuzidi kukaa machoni pake. Ingawa wengi walitoroka kutoka kwa Kristo, wengi walibaki na kusikiliza mafundisho yake.

> Kila siku alikuwa akifundisha hekaluni. Lakini viongzi wa makuhani, walimu wa sheria na viongozi wa watu walikuwa wakitafuta njia ili kumwua. Luka 19:47

Kama Yesu angejawa na hasira na fujo kwa watu, hakuna mtu angesalia; wote wangekimbia. Wale waliotubu kwa unyenyekevu hawakuhitaji kuondoka kwa sababu hawakuhisi hukumu yoyote machoni pake.

> Kwa hiyo, sasa hakuna hukumu ya adhabu kwa wale walio ndani ya Kristo Yesu, wale ambao hawaenendi kwa kuufuata mwili bali kwa kufuata Roho. Warumi 8:1

La kuhuzunisha, makuhani na watawala walikata kumruhusu Roho wa Mungu kuitakasa mioyo yao. Hekalu halisi liliwakilisha moyo wa taifa. Hekalu lingetakaswa kwa machozi ya kutubu, lakini badala yake, lilitakaswa kwa uovu wa kuukimbia uso wake. Roho alikuwa akiwakaribia katika hukumu ili kuwaokoa, lakini kadiri Roho alivyowakaribia zaidi ndivyo walishtuka zaidi.

> **Nami nitawakaribieni ili kuhukumu;** nami nitakuwa shahidi mwepesi juu ya wachawi, na juu ya wazinzi, na juu yao waapao kwa uongo; na juu yao wamwoneao mwenye kuajiriwa, kwa ajili ya mshahara wake, wamwoneao mjane na yatima, na kumpotosha mgeni asipate haki yake, wala hawaniogopi mimi, asema Bwana wa majeshi. Malaki 3:5

Mawazo yetu halisi tunaposoma fungu hili ni kudhani kuwa Mungu atawaua na kuwaangamiza waovu kwa hasira yake. Mara nyingine neno la Mungu linatenda kama kioo. Fungu linasema “ Nami nitawakaribieni ili kuhukumu.” Baba yetu anataka kutukaribia ili tusemezane kuhusu dhambi zetu. Kumjia mtu bila ubinafsi na upendo humwacha bila uchaguzi mwingine ila kutubu au kuikimbia nuru. Haiwezekani kuwa batili machoni pa Mungu. Wale ambao wanashikilia dhambi zao hukimbia kwa kile wanafikiria ni uzima wao, lakini wanaonyesha kuwa kweli wanapenda kifo na wanakimbia kutoka uzimani.

Kutakaswa kwa hekalu kunaonesha maeneo yaliyotendeka Mbinguni wakati Lucifer na malaika wake waliasi dhidi ya Mungu. Roho wa Mungu aliwahukumu kwa mtendo yao mabaya, lakini la kuhuzunisha walikataa kukubali msamaha. Zingatia namna mbili matukio haya yanaonyeshwa katika andiko:

> Nao malaika ambao hawakulinda nafasi zao, lakini wakayaacha makao yaliyokuwa yao hasa, hawa amewaweka katika giza, wakiwa wamefungwa kwa minyororo ya milele kwa ajili ya hukumu siku ile kuu. Jude 1:6

> Kwa maana kama Mungu hakuwasamehe malaika walipotenda dhambi, bali aliwatupa kuzimu a, katika vifungo vya giza wakae humo mpaka ije hukumu, 2 Petro 2:4

Unasomaje fungu hili? Katika Yuda tunaambiwa kwamba malaika waliacha makao yao mbinguni. Katika 2 Petro 2:4 tunaambiwa kuwa Mungu hakuwasamehe malaika walipotenda dhambi bali aliwatupa katika kuzimu na giza.

Mwana wa Mungu alipowakaribia hukuwa akiwakilisha Baba yake, hawangeweza kuvumilia uso wake. Kristo, ambaye ni Mikaeli Malaika mkuu, alipigana na malaika hawa akiwasihi waigeukie nuru, watubu mienendo yao, na wamrudie Baba.

> Basi palikuwa na vita mbinguni: Mikaeli na malaika zake wakapigana na hilo joka, nalo joka pamoja na malaika zake likapigana nao. (8) Lakini joka na malaika zake wakashindwa na hapakuwa tena na nafasi kwa ajili yao mbinguni. Ufunuo 12:7-8

Vita mbinguni vilimwangazia Lucifer akitafuta uchukuzi wa bidhaa zake katika hekalu la Mungu.

> Kwa wingi wa uchuuzi wako watu walikujaza udhalimu ndani yako, nawe umetenda dhambi; kwa sababu hiyo nimekutoa kwa nguvu katika mlima wa Mungu, kama kitu kilicho najisi; nami nimekuangamiza, Ewe kerubi ufunikaye, utoke katika mawe hayo ya moto. Ezekieli 28:16

Tena Bibilia inatuzungumzia kama kioo. Inadhihirisha kilicho moyoni. Inaposema, " Nami nimekuangamiza, Ewe Kerubi ufunikaye." Tunapatwa na changamoto ya kujijazia jinsi hili litakavyotendeka. Kama Lucifer angekubali

makosa yake kabla ya kujiingiza katika vita dhidi ya serikali ya Mungu, angeokolewa. Juhudi za Mwana wa Mungu za kutakasa hekalu la moyo wake zilipeleka jambo hilo hadi kichwani, na wakti Yesu alimtia hatiani kwa makosa yake, alikataa, akaufanya moyo wake kuwa mgumu na akaanguka dhambini kabisa. Matendo ya Kristo yalimpa Lucifer jukwaa la kuikataa nuru na kujiangamiza mwenyewe. Katika mpangilio huu Bibilia inaashiria kuwa Mungu alianza mpango ambao ungepelekea kwa uangamizo wa Lucifer. Hili ni sawa na wakati Bibilia inaposema kuwa Mungu aliufanya mgumu moyo wa Farao. Mungu alimsihi Farao atubu lakini uchaguzi wa Mfalme ulikuwa kuufanya mgumu moyo wake. Ni matendo ya jua ambayo hufanya udongo kuwa mgumu, ama ni viungo katika udongo ambavyo huitikia jua, na kuufanya kuwa mgumu?

Shetani na malaika zake hawakutupwa kutoka mbinguni. Shetani alitupwa kupitia kwa kukataa kwake kuitikia hukumu ya Roho wa Mungu na kutaka kuutoroka uso wake. Mchakato sawa ulitendeka hekaluni yesu alipolitakasa. Aliwaonyesha watu makosa yao, aliwahukumu kwa dhambi zao, Roho aliwakaribia na kuwapa wito wa kutubu, lakini walikataa. Kukataa huku kuliwaweka wengi katika minyororo ya giza kama malaika walioasi. Wakati Roho anafanya juhudi ya moja kwa moja kufikia nafsi na anakataliwa kwa nguvu, mara moja giza huingia ndani na kuishika mateka nafsi. Kwa shukurani, waliomkimbia Kristo hiyo siku waliweza kutubu, lakini kwa wengine hiyo siku ilikuwa mwanzo wa uangamizi; na inaweza semwa kuwa Kristo aliwaangamiza kupitia kutafuta kuwaokoa.

Kwa ufahamu huu tunaweza soma mafungu kadhaa ya maandiko na kuelewa vyema kile yanamaanisha wakati watu walishikwa na hofu machoni pa Mungu.

> Nitatuma utisho wangu utangulie mbele yako, nami **nitawafadhaisha** [H2000] watu wote utakaowafikilia, nami nitawafanya hao adui zako wote wakuonyeshe maungo yao. (28) Nami nitapeleka mavu mbele yako, watakaomfukuza Mhivi, na Mkanaani, na Mhiti, watoke mbele yako. Kutoka 23:27-28

Neno la Kiebrania ambalo tafsiri ya King James inafasiri kama *kufadhaisha* linamaana hizi tofauti:

> H2000 – Hamam: kuhamisha kwa kelele, kuchanganya, kupiga kelele, kunyunya, kuvunja, kula, kuponda, angamiza, kufadhaisha, kusumbua

Hofu ambayo Mungu angeweka kwa Mataifa haya mengi ingekuwa sawa jinsi Yesu alifanya alipolitakasa hekalu mara ya pili. Mengi ya mataifa haya yaliyozunguka Israeli yalikuwa yamejaza vikombe vyao vya maovo, na walikuwa katika sehemu ya uamuzi wa mwisho. Hofu ambayo Mungu aliweka ndani yao ilikuwa hukumu yake kwa dhambi zao. Roho wa Mungu aliwakaribia katika hukumu. La kuhuzunisha, walikataa na hili liliwanyunya, kuwasumbua na kuwachanganya. Kukataa kwa Wayahudi kuipokea rehema ya Yesu kuliwaacha na hatimaye kuharibiwa na Waroma. Kukataa kutubu dhambi kwa mataifa haya yaliyowazunguka kuliyaacha yameanikwa kwa upanga wa Israeli. Tutachunguza upanga wa Israeli katika sura ifuatayo lakini sasa tunaona kuwa hofu ya Mungu iliyokuja juu ya mataifa haya ilikuwa Roho wa Mungu akitafuta kuwahukumu kwa dhambi zao ili kuwafanya kutubu kama juhudi ya mwisho ya kuwaokoa. Kuwafikia ili kuwaokoa kulipelekea katika mioyo yao kuwa migumu, na kwa hivyo wakachagua mauti badala ya uzima. Hukumu ya dhambi ilikuwa kama mavu nafsini mwao. Mataifa haya yalirusha mateke dhidi ya chomo cha dhamiri na wakakimbia uso wa Mungu na kwenda mikononi mwa shetani, mharibifu, na wakaangamia.

> Ikawa katika zamu ya alfajiri, Bwana akalichungulia jeshi la Wamisri katika ile nguzo ya moto na ya wingu, **akalifadhaisha** [H2000] jeshi la Wamisri. (25) Akayaondoa magurudumu ya magari yao, hata yakaenda kwa uzito; na Wamisri wakasema, Na tukimbie mbele ya Israeli; kwa kuwa Bwana anawapigania, kinyume cha Wamisri. Exodus 14:24-25

Katika bahari ya shamu, Mungu aliwasumbua Wamisri. Ni neno sawa na linalotajwa kuwa Mungu atawafadhaisha watu wote katika Kutoka 23:27.

Wamisiri walipendwa na Mungu sana kama alivyowapenda Waisraeli. Wakati Mungu alijenga nguzo ya moto kuwazuia kuwashambulia Waisraeli wangeona katika hili onyo, warudi nyumbani. Waliogopeshwa na hili, lakini walikataa kutubu. Walipowafukuza Waisraeli Mungu alituma malaika wake kuyaondoa magurudumu ya magari yao ili kupunguza mwendo wake na kuwazuia kwenda mbele. Kwa usumbufu wao walikataa kutii, wakaendelea hata kwenye kina cha maji na wakazama maji yaliporejea pamoja. Hakuna

thibitisho kuwa Mungu aliwasukuma majini ili kuwaua. Alifanya kila kiwezekanacho ili kuwazuia kufanya tendo hili.

> Na siku tulizokuwa tukienda kutoka Kadesh-barnea hata tulipovuka kijito cha Zeredi, zilikuwa ni miaka thelathini na minane; maana, hata walipokwisha kuangamizwa watu wa vita kutoka kati ya marago, kizazi chao chote, kama walivyoapiwa na Bwana. (15) Tena mkono wa Bwana ulikuwa juu yao ili **kuwaangamiza**[H2000], kuwatoa kati ya marago, hata walipokoma. Kumbukumbu 2:14-15

Waisraeli waliagizwa waende wakaichukue nchi ya Kanani, lakini waliyaogopa majitu katika inchi hiyo na wakakataa kumwamini Mungu. Wakati Mungu basi aliwaambia hawataingia Nchi ya ahadi kwa sababu ya kutokuamini kwao na kuwa wangekufia jangwani, waliasi tena na wakaamua kwenda kupigana. Baada ya kupigwa na adui zao walianza kumlaumu Musa kwa kila kitu na wakataka kumuua.

Watu walisema kila wakati kuwa Mungu alitaka kuwaua katika jangwa na kama walivyo hukumu ndivyo walivyo walipokea. Mungu aliruhusu mambo haya yatendeke kwa imani kuwa wangeona makosa yao na kutubu na kuomba msamaha. Kwa miaka 40 Mungu alituma Roho wake ili kuwasihi kwamba wajinyenyekeze na watubu dhambi zao. Iwapo wangetubu haingejalisha kama wangekufa jangwani; wangeweza kupata uzima wa milele.

> Kwa hiyo kwa kuwa inabaki kuwa wazi kwa ajili ya wengine kuingia, nao wale wa kwanza waliopokea Injili walishindwa kuingia kwa sababu ya kutokutii: Waebrania 4:6

Ni jinsi gani inahuzunisha kuwa Waisraeli hao wote walikataa kuingia katika pumziko lililo ndani ya Kristo na kujua kuwa dhambi zao zilisamehewa. Badala yake waliifanya mioyo Migumu dhidi ya kusihi kwa Roho, walikufa jangwani, na wakaukosa uzima wa milele. Hivyo ni Mungu aliwaangamiza? Alifanya ndani kama vile jua huufanya udongo kuwa mgumu. Kuendelea kwake kuwasihi kuliifanya mioyo yao kuwa migumu kwa kuendelea kukataa. Na kwa hivyo waliangamizwa.

Mkombozi anapokujia kupitia kwa kukutia hatiani kwa kina  kwa sababu ya dhambi, usigeuke kwa hofu na kuufanya moyo wako kuwa mgumu. Amini kuwa Baba yako usamehe bure na hutakasa dhambi na ufurahie amani na

uhuru wa msamaha. Furahia amani ya mbingu ndani ya hakalu la nafsi yako na ufurahie kuwa yuko tayari kulitakasa kwa ajili ya utukufu wake na kwa utukufu wake.

Katika siku hizi za mwisho ujumbe unatujia ulimwenguni ukitwagiza "Mcheni Mungu na kumtukuza." Ufunuo 14:7. Tunaporuhusu Roho wa Mungu kututia hatiani kwa makosa yetu na kutopinga wito wake, tutabarikiwa na tuanze kuelewa hekima, kwa kuwa tunaambiwa:

> Kumcha Bwana ni mwanzo wa hekima; Na kumjua Mtakatifu ni ufahamu. Methali 9:10

# 11. Hasira ya Bwana

Wakati wa juma moja kabla ya Kristo kusulubiwa msalabani alikuwa amempanda punda akizungukwa na umati wa watu.

> Umati mkubwa wa watu wakatandika nguo zao barabarani na wengine wakakata matawi kutoka kwenye miti wakayatandika barabarani. (9) Ule umati wa watu uliomtangulia na ule uliomfuata ukapiga kelele ukisema,"Hosana Mwana wa Daudi!" "Amebarikiwa Yeye ajaye kwa Jina la Bwana!" "Hosana juu mbinguni!" Mathayo 21:8-9

Kwa wanafunzi ilionekana kuwa matarajio yao ya muda mrefu yalikuwa yanakuja kupita: Hatimaye Mkuu wao alikuwa akitambuliwa na umati uliokuwa ukimwabudu. Lakini sawa ndani ya shughuli hizi za kumtukuza tunasoma:

> Alipokaribia Yerusalemu na kuuona mji, aliulilia, (42)akisema, "Laiti ungalijua hata wewe leo yale ambayo yangeleta amani, lakini sasa yamefichika machoni pako. Luka 19:41-42

Yesu alipoutazama mji na kuwaza yote ambayo taifa hilo lilikuwa limetenda katika kuasi dhidi ya Baba yake, na yale yatakayowatendekea chini ya muda wa siku arobaini kwanzia siku hiyo, alianza kulia. Hili halikuwa chozi la upole machoni; ilikuwa kutoa makali, huzuni isiyolaumika iliopasuka ndani na kulia

kwa uchungu. Moja yapo ya neno ambalo Bwana alitumia kuelezea tabia ya Mungu ni *Uvumilivu.*

> Bwana akapita mbele yake, akatangaza, Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, [H639 aph] mwingi wa rehema na kweli; Kutoka 34:6

Neno hili lina maana ifuatayo:

> Vizuri pua au shimo la pua; hivyo uso, na mara kwa mara mtu; pia (**kupumua kwa haraka kutokana na shauku**) ire: - hasira (-sirika), + kabla, uso, + uvumilivu, kipaji, + [refu-] **kuteseka**, pua, **shimo la pua**, pua, X stahili, ghadhabu.

> Lakini Hana humpa [H639 aph] sehemu mara mbili; maana alimpenda Hana, ingawa Bwana alikuwa amemfunga tumbo. 1 Samweli 1:5

Haileti maana yoyote kusema kuwa Hana alipewa sehemu ya huzuni kwa sababu alimpenda Hana. Kama jinsi *Gesenius Hebrew-Chaldee Lexicon* anavyoieleza:

> Pengine na huzuni mawazoni; kwani maneno ambayo yanamaanisha hasira yanaweza kutumiwa kwa huzuni

Machozi yaliyomchoma Yesu yalikuwa tokeo la moyo wake mkuu wa upendo kwa wana wake. Je, hili lilihusisha hasira? Ndio, hasira kwa kile dhambi ilikuwa imefanya kwa wanawe wapendwa na inaonyeshwa kwa kina huzuni cha machozi yachomayo. upendo wake mkuu wa moyoni.

> Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana. (9) Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu. Isaya 55:8-9

Tunaposoma kuhusu hasira ya bwana katika Bibilia tunauhakika kuwa tunaielewa kwa usahihi? Mara nyingine tena tunaangalia kwa maisha ya Yesu kuona jinsi anavyoonyesha hasira.

> “Ole wenu walimu wa sheria na Mafarisayo, enyi wanafiki! Mnakula katika nyumba za wajane, nanyi kwa kujifanya kuwa wema, mnasali sala ndefu. Kwa hiyo adhabu yenu itakuwa kubwa zaidi.” (15) “Ole wenu walimu wa sheria na Mafarisayo, wanafiki! Ninyi

> mnasafiri baharini na nchi kavu ili kumfanya mtu mmoja ageuke na kuwafuata ninyi, lakini baada ya kumpata, mnamfanya mwana wa jehanamu mara mbili kuliko ninyi! (16) "Ole wenu, viongozi vipofu! Ninyi mwasema, 'Mtu akiapa kwa hekalu, kiapo hicho si kitu, lakini mtu akiapa kwa dhahabu ya hekalu, amefungwa kwa kiapo chake.' (17) Ninyi vipofu wapumbavu! Ni kipi kilicho kikuu zaidi, ile dhahabu au lile hekalu ambalo ndilo linaloifanya hiyo dhahabu kuwa takatifu? Mathayo 23:14-17

Yesu hakika anasikika mwenye hasira katika fungu hili. Ole ambayo Yesu anatangaza inaendelea kwa mafungu kadhaa na kisha tunasoma jambo muhimu sana.

> "Ee Yerusalemu, mnaowaua manabii na kuwapiga mawe wale waliotumwa kwenu! Mara ngapi nimetamani kuwakusanya watoto wako, kama vile kuku akusanyavyo vifaranga vyake chini ya mbawa zake, lakini hukutaka! Mathayo 23:37

Yesu aliwapenda hawa masikini, waliogeuzwa viongozi wa wayahudi. Alitaka kuwakusanya chini ya ulinzi wake. Anazungumza kwa lugha ya upole ya kuku awakusanyae vifaranga wake. Ni sura ya kuguza mno ya upendo wa Mkombozi. Hasira yake ni onyesho la huzuni za ndani ya moyo alizokuwa ameweka wazi kwa kilio muda mchache kabla ya hili. Katika lugha ya Mathayo 23 tunaona ubainifu wa hasira ya Mungu.

Iwapo kuna fursa ambayo ingeidhinishwa kuita moto kutoka mbinguni ni sasa. Viongozi hawa walikuwa wakisababisha kupotea kwa taifa lote la Wayahudi. Walikuwa wakisimama kwenye njia za watu na kugeuza mafundisho safi ya Maandiko. Hakika hapa pangekuwa mahali pa kuwaua ndiposa ukweli uweze kuwafikia raia. Yesu hakuinua upanga wowote wala kuita moto ushuke kutoka mbinguni lakini aliyasema maneno haya:

> Tazama nyumba yako imeachwa tupu na ukiwa. Mathayo 23:38

Hapa pana hatima ya hasira ya Mungu. Mwana wa Mungu anatangaza kuwa ulinzi wa taifa umeondolewa. Na baada ya hatua hii ndipo shetani anaweza kuchukua uongozi kikamilifu wa viongozi wa Kiyahudi ambao muda mfupi baada ya kufaulu katika mipango yao ya uangamizi wa kumuua Yesu. Tunagundua kwa makini kuwa Yesu alipotangaza kwamba nyumba ya Israeli imeachwa ukiwa aliandaa njia kwa kifo chake mwenyewe, sio kifo cha wale

waliompinga, wakati Roho ya uzuizi ya Mungu iliwaacha makuhani na watawala hakukua na chochote cha kuwazuia kumuua Yesu. Shetani sasa angeweza kuchukua uongozi, na kwa kipindi cha miaka arobaini angeweza kuharibu mji ambao zaidi ya milioni ya Wayahudi waliweza kuuwawa na Warumi.

Hapa kuna ufafanuzi wa hasira ya Mungu ukielezewa kwa njia nyingine:

> Akawapelekea ukali wa hasira yake, Ghadhabu, na uchungu, na taabu, Kundi la malaika waletao mabaya. Zaburi 78:49 (NIV)

Mharibifu ni nani?

> Msinung'unike kama baadhi yao walivyofanya, wakaangamizwa na mharabu. 1 Wakorintho 10:10 (NIV)

Neno malaika wa uharibifu kwa Kiyunani humaanisha *Nyoka mwenye sumu.*

> Walikuwa na malaika kutoka kwenye hilo shimo lisilo na mwisho kama mfalme wao, ambaye jina lake kwa Kiebrania ni Abadonib na kwa Kiyunani ni Apolioni. Ufunuo 9:11

Mharibifu ni shetani. Wakati watu wanasisitiza kumkataa Kristo na kuweka wazi kuwa hawataki lolote kuhusiana naye, Kwa kilio cha uchungu Kristo huhuzunika kwa wanawe waliopotea na kuwaacha wawe na Bwana wa uchaguzi wao. Wakati haya yanapotendeka ua la ulinzi lililowekewa kila mtu huvunjika.

> Ndipo Shetani akamjibu Bwana, na kusema, Je! Huyo Ayubu yuamcha Bwana bure? (10) **Wewe hukumzingira kwa ukigo pande zote**, pamoja na nyumba yake, na vitu vyote alivyo navyo? Kazi za mikono yake umezibarikia, nayo mali yake imeongezeka katika nchi. Ayubu 1:9-10

> Malaika wa Bwana hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa. Zaburi 34:7

> Mwenye kuchimba shimo atatumbukia ndani yake; Na yeye abomoaye boma, nyoka atamwuma. Muhubiri 10:8

Ni mambo yapi hupelekea kwa ua la ulinzi kuweza kuvunjika?

Haya, enenda sasa, andika neno hili katika kibao mbele ya macho yao, lichore katika kitabu ili liwe kwa ajili ya majira yatakayokuja, kwa ushuhuda hata milele. (9) Kwa maana watu hawa ni**[1]** watu waasi, **[2]** watoto wasemao uongo, **[3]** watoto **wasiotaka kuisikia sheria ya Bwana;** (10) [4] wawaambiao waonaji, Msione; na manabii, **Msitoe unabii wa mambo ya haki, tuambieni maneno laini, hubirini maneno yadanganyayo;** (11) tokeni katika njia, geukeni mtoke katika mapito; mkomesheni Mtakatifu wa Israeli mbele yetu. (12) Basi kwa ajili ya hayo Mtakatifu wa Israeli[5] asema hivi, Kwa sababu **mwalidharau neno hili**, na kutumainia jeuri na ukaidi, na kuyategemea hayo; (13) basi, **uovu** huu utakuwa kwenu kama mahali **palipobomoka, palipo tayari kuanguka patokezapo katika ukuta mrefu, ambapo kuvunjika kwake huja ghafula kwa mara moja.** (14) Naye atapavunja kama chombo cha mfinyanzi kivunjwavyo, akikivunja-vunja asiache kukivunja, hata hakipatikani katika vipande vyake kigae kitoshacho kutwaa moto jikoni, au kuteka maji kisimani. Isaya 30:8-14

Fitina ya manabii wake imo ndani yake, kama simba angurumaye akirarua mawindo; **[1] wamekula roho za watu; hutwaa kwa nguvu hazina** na vitu vya thamani; **wameongeza hesabu ya wajane** wake ndani yake. (26) **[2]** Makuhani wake **wameihalifu sheria yangu**, **[3] wametia unajisi vitu vyangu vitakatifu;** hawakuweka tofauti ya vitu vitakatifu na vitu vya kutumiwa sikuzote; wala hawakuwafundisha watu kupambanua vitu vichafu na vitu vilivyo safi, nao **wamefumba macho yao, wasiziangalie sabato zangu, [4]** nami nimetiwa unajisi kati yao. (27) **[5]** Wakuu wake kati yake wamekuwa kama mbwa-mwitu wakirarua mawindo; ili kumwaga damu, na kuharibu roho za watu, **wapate faida kwa njia isiyo halali**. (28) Na**[6]** manabii wake wamewapakia chokaa isiyokorogwa vema, wakiona ubatili, na **kuwatabiria maneno ya uongo**, wakisema, Bwana MUNGU asema hivi; iwapo Bwana hakusema neno. (29) **[7]** Watu wa nchi **wametumia udhalimu, wamenyang'anya kwa nguvu; naam, wamewatenda jeuri maskini na wahitaji,** nao wamewaonea wageni bila haki. (30) **Nami nikatafuta mtu miongoni mwao, atakayelitengeneza boma, na kusimama mbele zangu mahali palipobomoka, kwa ajili ya nchi, nisije nikaiharibu,** lakini sikuona mtu. (31) **Kwa sababu hiyo nimemwaga ghadhabu yangu juu yao; nimewateketeza kwa moto wa hasira yangu;**

nami *nimeileta njia yao wenyewe juu ya vichwa vyao, asema Bwana MUNGU.* Ezekieli 22:25-31

Hizi ndizo hoja muhimu zinazojenga mwanya ndani ya ukuta:

1. Wamekula roho za watu; hutwaa kwa nguvu hazina
2. Wameihalifu sheria yangu
3. Wametia unajisi vitu vyangu vitakatifu; hawakuweka tofauti ya vitu vitakatifu na vitu vya kutumiwa sikuzote
4. Wamefumba macho yao, wasiziangalie sabato zangu
5. Wakuu wake wapata faida kwa njia isiyo halali
6. Kuwatabiria maneno ya uongo
7. Wametumia udhalimu, wamenyang'anya kwa nguvu; naam, wamewatenda jeuri maskini na wahitaji

Wakati wana wa Mungu wanavunja amri za Mungu na kukataa kutubu na kuendelea kutenda maovu, mwishowe Mungu anawekwa katika hali ambayo hawezi endelea kuwalinda. Hili humfanya kuhuzunika kwa ajabu. Hataki kuwaacha wana wake lakini shetani huwashtaki mbele za Mungu na kutaka haki ya kuwachukua. Huzuni na uchungu ni hasira ya Mungu. Orodha inayoelezewa katika Ezekieli 22:25-31 ina malalamiko sawa na yale yanayotajwa katika Mathayo 23. Katika wakati wa Ezekieli ua uliweza kutolewa na Waisraeli akashikwa mateka na Wababeli. Katika wakati wa Kristo ua uliondolewa , na Warumi wakaja na kuharibu Yerusalemi.

## Hoja saba muhimu zinazoonyesha kilicholeta uvunjaji

| Ezekieli 22:25-31 | Mathayo 23 |
|---|---|
| **1.** Wamekula roho za watu; hutwaa kwa nguvu hazina | Matt 23:25 “Ole wenu, walimu wa sheria na Mafarisayo, ninyi wanafiki! Kwa maana mnasafisha nje ya kikombe na kisahani, lakini ndani mmejaa unyang’anyi na kutokuwa na kiasi |
| 2. Wamehalifu sheria ya Mungu. | Matt 23:23 Ole wenu walimu wa sheria na Mafarisayo, ninyi wanafiki! Kwa maana mnatoa zaka ya mnanaa, bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu zaidi ya sheria, yaani, haki, huruma na uaminifu. Haya imewapasa kuyafanya bila kusahau hayo mengine. |
| 3. Wametia unajisi vitu vyangu | Matt 23:16-20 “Ole wenu, viongozi vipofu! Ninyi mwasema, ‘Mtu akiapa kwa hekalu, kiapo hicho si kitu, |

| | |
|---|---|
| vitakatifu; hawakuweka tofauti ya vitu vitakatifu na vitu vya kutumiwa sikuzote | lakini mtu akiapa kwa dhahabu ya hekalu, amefungwa kwa kiapo chake.' (17) **Ninyi vipofu wapumbavu! Ni kipi kilicho kikuu zaidi, ile dhahabu au lile hekalu ambalo ndilo linaloifanya hiyo dhahabu kuwa takatifu?** (19) Ninyi vipofu! Ni kipi kikuu zaidi, ile sadaka, au ile madhabahu ambayo ndiyo inayoifanya hiyo sadaka kuwa takatifu? 20 Kwa hiyo, mtu aapaye kwa madhabahu, huapa kwa hiyo madhabahu na vitu vyote vilivyo juu yake. |
| 4. Wamefumba macho yao, wasiziangalie sabato zangu | Matt 23:4 Wao **hufunga mizigo mikubwa na kuiweka mabegani mwa watu,** lakini wao wenyewe hawako radhi hata kuinua kidole ili kuisogeza. |
| 5. Wakuu wake wapata faida kwa njia isiyo halali | Matt 23:16 Ole wenu, viongozi vipofu! Ninyi mwasema, 'Mtu akiapa kwa hekalu, kiapo hicho si kitu, **lakini mtu akiapa kwa dhahabu ya hekalu, amefungwa kwa kiapo chake.'** |
| 6. Manabii Kuwatabiria maneno ya uongo | Matt 23:28 Vivyo hivyo, kwa nje ninyi mnaonekana kwa watu kuwa wenye haki, lakini kwa ndani **mmejaa unafiki na uovu**. |
| 7. Naam, wamewatenda jeuri maskini na wahitaji | Matt 23:14 "Ole wenu walimu wa sheria na Mafarisayo, enyi wanafiki! **Mnakula katika nyumba za wajane**, nanyi kwa kujifanya kuwa wema, mnasali sala ndefu. Kwa hiyo adhabu yenu itakuwa kubwa zaidi.'' |

Wacha tuangazie baadhi ya mifano ambayo kwayo watu huvunja ua hili la ulinzi.

> Hata walipofika kwa uga ya Nakoni, Uza akalinyoshea mkono sanduku la Mungu, akalikamata kwa maana wale ng'ombe walikunguwaa. (7) Ndipo hasira ya Bwana ikawaka juu ya Uza; naye Mungu akampiga huko kwa kosa lake; hata akafa pale pale penye sanduku la Mungu. (8) Daudi akaona uchungu kwa kuwa Bwana amemfurikia Uza; akapaita mahali pale Peres-uza hata leo. 2 Samweli 6:6-8

Maneno hasira ya Bwana ikawaka juu ya Uza yanatukaribisha katika kuhukumu tabia ya Mungu. Kama tulivyoainisha awali, maneno *hasira ya*

*bwana ikawaka yanaweza tafsiriwa kama kusononeka na kuhuzunika*. Uza alitenda kwa namna aliyojua sio sawa. Alikuwa amejiweka katika pahali ambapo hangeweza kulindwa. Roho wa bwana alihuzunika kwa Uza. Bwana hakutaka kumuacha, lakini uasi wake ulimuweka pahali ambapo lazima Bwana angeruhusu uvunjaji wa ulinzi. Andiko linasema kwamba Bwana akafanya uvunjaji juu ya Uza. Ilimsababishia Bwana uchungu mwingi kuweza kurudi nyuma juu ya Uza, Lakini Uza alikuwa amechagua njia ya uasi na Bwana lazima angeheshimu uchaguzi wake. Sio Bwana aliyemwangamiza Uza kwa mkono wake mwenyewe. Uasi wa Uza ulisababisha uvunjaji wa ulinzi.

Moja wapo ya viashiria vya kutoridhika moyoni mwa Uza kinapatikana katia aya ya awali.

> Wakaliweka sanduku la Mungu juu ya gari jipya, wakalitoa katika nyumba ya Abinadabu, iliyoko kilimani; nao Uza na Ahio wana wa Abinadabu wakaliendesha lile gari jipya. (4) Wakalitoa katika nyumba ya Abinadabu iliyoko kilimani, pamoja na sanduku la Bwana; na huyo Ahio akatangulia mbele ya sanduku. 2 Samweli 6:3-4

Uza anaorodheshwa mbele ya wana wawili wa Abinadabu lakini Ahio nduguye mchanga anatajwa kama anaye ongoza sanduku badala ya nduguye mkubwa. Kwani Uza alijazwa na uadui wa undugu? Kwani kulikuwepo chuki moyoni mwake kwa ndugu yake? Jambo la msingi lililosababisha ua kuvunjwa lilikuwa kuweka sanduku juu ya gari lililokuwa na ng'ombe. Musa alikuwa ameashiria kuwa sanduku lazima libebwe na makuhani.

> Na wakati huo Bwana aliitenga kabila ya Lawi ili walichukue lile sanduku la agano la Bwana, wasimame mbele ya Bwana kwa kumtumikia, na kuwabarikia watu kwa jina lake, hata hivi leo. Kumbukumbu 10:8

> Wakawaamuru watu wote wakisema, Mtakapoliona sanduku la agano la Bwana, Mungu wenu, na makuhani Walawi wakilichukua, ndipo mtakapoondoka hapa mlipo na kulifuata. Yoshua 3:3

Jambo la msingi la uvunjaji halikuwa linatosha kuondoa ua kwa mtu yeyote ila Uza ivo basi kuna uwezekana palikuwa na jambo moyoni mwa Uza lililosababisha ulinzi kuondolewa.

Basi ni jinsi gani unasoma? Je unasoma tabia ya Mungu kama hasira ichomayo iliyosababisha kuangamizwa kwa Uza hadi chini ama unamuona Baba mpole ambaye baadaye hujisalimisha mwenyewe kwa uchaguzi wa Uza kufuata njia ya uasi. Kila mmoja wetu lazima achague jinsi ya kusoma hili. Baba yetu aliye mbinguni ameruhusu tofauti ya maana ili kuwa kioo nafsini mwetu ili tuweze kuamua sisi wenyewe kuwa na tabia gani tunaona katika fungu hili. Je tunaona tabia kama yetu? Je tunaona mtu mwenye hasira nyingi ambaye huwapiga hadi kuwaua wale wafanyao kosa au tunaona Baba mwenye uchungu ambaye alilazimishwa kukubali uamuzi wa Uza ili kukumbatia roho wa shetani na kupeana kwa Bwana wake wa haki – mharibifu?

> Nami nitaleta upanga juu yenu, utakaopatiliza kisasi cha hilo agano; nanyi mtakutanishwa ndani ya miji yenu; nami nitaleta tauni kati yenu; nanyi mtatiwa mkononi mwa adui. Walawi 26:25

Katika sehemu nyingi za maandiko tunasoma kuhusu hasira ya Bwana kuwa Inawaka na upanga, njaa, na magonjwa ya kuambikiziana kuwaangukia watu. Kama fungu ambalo tumesoma linavyotwambia, watu wanaokolewa kutoka mikononi mwa adui. Hasira iwakayo ni huzuni ya uchungu ambao Baba yetu huvumilia wakati wanawe wapotovu wanaendelea kuasi ambayo baadaye husababisha kuvunjika kwa sheria zilizotengenezwa kwa ulinzi wao. Tutaisikiza sauti ya Baba yetu leo kwa makini?

> Msifanye sanamu yo yote, wala msijisimamishie sanamu ya kuchonga, wala mnara, wala msiweke jiwe lo lote lililochorwa katika nchi yenu ili kulisujudia; kwa kuwa mimi ndimi Bwana, Mungu wenu. (2) Zishikeni Sabato zangu, na kupastahi patakatifu pangu; mimi ndimi Bwana. (3) Kama mkienda katika amri zangu, na kuyashika maagizo yangu, na kuyafanya; (4) ndipo nitazinyesha mvua zenu kwa nyakati zake, na nchi itazaa maongeo yake, na miti ya mashambani itazaa matunda yake. (5) Tena kupura nafaka kwenu kutaendelea hata wakati wa kuvuna zabibu, na kuvuna zabibu kutaendelea hata wakati wa kupanda mbegu; nanyi mtakula chakula chenu na kushiba, na kuketi katika nchi yenu salama. (6) Nami nitawapa amani katika nchi, tena mtalala wala hapana atakayewatia hofu; nami nitawakomesha wanyama wabaya katika nchi yenu, wala hautapita upanga katika nchi yenu. Walawi 26:1-6

Iwapo tutatii Sheria za Mungu kwa furaha na kuchagua kuamini kwamba Baba yetu anataka kutubariki basi tutafurahia ulinzi wa malaika wa Bwana.

> Aketiye mahali pa siri pake Aliye juu Atakaa katika uvuli wake Mwenyezi. (2) Nitasema, Bwana ndiye kimbilio langu na ngome yangu, Mungu wangu nitakayemtumaini. (3) Maana Yeye atakuokoa na mtego wa mwindaji, Na katika tauni iharibuyo. (4) Kwa manyoya yake atakufunika, Chini ya mbawa zake utapata kimbilio; Uaminifu wake ni ngao na kigao. Zaburi 91:1-4

Hebu na tusisababishe Baba yetu na Bwana Yesu kuhuzunika na kuwa na machungu kwa kutotii kwetu. Anahamu ya kutulinda na kututunza. Iwapo tutaasi na kuchagua roho wa adui, mwoshowe adui lazima ataruhusiwa kuyatawala na kuongoza maisha yetu. Sio haki kwa mtu kuendelea kulindwa na mtu ambaye hataki kuwa naye.

Kuharibiwa kwa Yerusalemu ni utabiri wa mwisho wa ulimwengu. Kama vile taifa la Wayahudi walivyomkataa mwana wa Mungu miaka elfu mbili iliyopita, ndivyo leo Mwana wa Mungu anavyodharauliwa na kukataliwa na wanadamu. Bwana wa sabato alitemewa mate kwa kukataliwa kwa siku yake ya kuabudu. Uasherati na tama zimejaa kiasi kwamba hatimaye kwa kilio cha uchungu atasema kwa ulimwengu, "nyumba yako imebaki ukiwa." Kisha pepo za ugomvi ambazo ni malaika walioanguka wataachiliwa kabisa kuharibu dunia. Hebu na tuweze kujishikilia kwa Mkombozi wetu na tuweze kuamini ndani ya neema yake ili tuwe sehemu ya ile hesabu ya wale wazishikao sheria za Mungu na kuwa na imani ya Yesu Kristo.

## 12. Kuweka Upanga Pahali pake

Katika utulivu wa usiku juu ya mizeituni, Mkombozi wetu mpendwa alikuwa akiomba mbele ya Baba yake.

> "Baba yangu, kama inawezekana, kikombe hiki na kiniepuke, lakini si kama nitakavyo mimi bali kama utakavyo Wewe." Mathayo 26:39

Uzito wote wa uovu wa mwanadamu ulikuwa juu ya Mwana wa Adamu. Hivyo pambano lake lilikuwa kuu kiasi ya kwamba jasho la damu lilimtiririka. Utukufu wa Baba katika usafi wake wote uteketezao ulikabiliana na giza la dhambi ambalo Mwana wa Adamu alikuwa amechukua juu yake. Alitetemeka kama jani akijua jinsi ilivyomachukizo kwa Babaye dhambi alizozibeba. Kwa neno la nabii ilisemekana:

> **Amka, Ee upanga, juu ya mchungaji wangu**, na juu ya mtu aliye mwenzangu, asema Bwana wa majeshi; mpige mchungaji, nao kondoo watatawanyika; nami nitaugeuza mkono wangu juu ya wadogo. Zekaria 13:7

Upanga katika kipindi hiki ulikuwa upanga wa roho. Kama Kristo alivyoushikilia Upanga huo kwa ajili yetu alitoa uhai wake kwa nguvu. Mtu anapotiririkwa na jasho la damu yuko katika hatua ya kifo. Mkono utiao nguvu wa Babaye pekee ndio ulimpa uwezo wa kutoka kwenye bustani na kukabiliana na upanga wa Rumi ulioinuliwa kwa mikono ya viongozi wa

kiyahudi Wakati walinzi wa hekalu walikuja pamoja na Yuda kumshika Yesu, Petro aliinuka katika roho ya Yuda Maccabees[2] na za baba zake wa mbele zake ambao walikuwa wameinua upanga kwa ulinzi wa vitu walivyoweka hazina. Yesu alikuwa amemwambia Petro hakuja kuangamiza wanadamu bali kuwaokoa, ila kwa Petro Yesu aliyekufa alimaanisha mwisho wa matumaini yake yote. Jambo la kuhuzunisha ni kwamba upanga alioinua ulikuwa kwa tamaa zake mwenyewe kuliko ilivyokuwa hamu yake kwake Kristo.

> Simoni Petro aliyekuwa na upanga akaufuta na kumkata sikio la kuume mtumishi wa Kuhani Mkuu. Jina la mtumishi huyo aliitwa Malko. Yohana 18:10

Yesu alipomponya Malko, alimtenga na matumizi ya kutumia upanga halisi kujikinga yeye mwenyewe na ukweli. Kisha akasema:

> Ndipo Yesu akamwambia, "Rudisha upanga wako mahali pake, kwa maana wote watumiao upanga watakufa kwa upanga. (53)Je, unadhani siwezi kumwomba Baba yangu naye mara moja akaniletea zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika?(54)Lakini je, maandiko yatatimiaje yale yasemayo kwamba ni lazima itokee hivi?" Mathayo 26:52-54

Maneno ya Yesu yanamaana zote ya, kiroho na mtazamo wa mwili. Wakati mwanadamu anaposhikilia neno la Mungu, neno hilo litaweza kuweka katika hali ya kifo maisha yake ya kale na kuweza kufufuliwa upya kimaisha ndani ya Yesu Kristo. Wakati huo huo inamaanisha wale ambao waliinua upanga halisi watakufa kwa upanga. Yesu anatuachia funzo muhimu sana kwamba tunapaswa kuamini katika maombi na ulinzi wa malaika wa Baba yetu wala sio kwa upanga kutuokoa. Wacha ujumbe wa Mkombozi uwe mfano wazi kwetu. Yesu hakumpiga, kumjeruhi au kumpiga yeyote. Mkombozi wetu alituachia mfano huu ili tuufuate.

> Kwa kuwa ninyi mliitwa kwa ajili ya hayo, kwa sababu Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akiwaachia kielelezo, ili mzifuate nyayo zake. (22) "Yeye hakutenda dhambi, wala udanganyifu haukuonekana

[2] Yuda Maccabeus alikuwa kuhani Myahudi na mwana wa kuhani Mattathias. Aliongoza Maccabean katika kuasi Utawala wa Seleucid (167–160 BCE).

> kinywani mwake. (23) Yeye alipotukanwa, hakurudisha matukano, alipoteswa, hakutishia, bali alijikabidhi kwa Yeye ahukumuye kwa haki. 1 Petro 2:21-23

Changamoto kuu ambayo lazima tutaelezea kwa mwanga wa Yesu ni jinsi tunaweza angazia hadithi zote za Agano la kale zilizojawa na ukatili wa Isaraeli kuwakatakata na kuwaua adui zao kwa upanga? Waisraeli walipotoka Misri Mungu aliwaambia jinsi angekabiliana na mataifa yaliyowazunguza.

> Nitatuma utisho wangu utangulie mbele yako, nami nitawafadhaisha watu wote utakaowafikilia, nami nitawafanya hao adui zako wote wakuonyeshe maungo yao. (28) **Nami nitapeleka mavu mbele yako, watakaomfukuza Mhivi, na Mkanaani, na Mhiti**, watoke mbele yako. (29) Sitawafukuza mbele yako katika mwaka mmoja; nchi isiwe ukiwa, na wanyama wa bara wakaongezeka kukusumbua. (30) Nitawafukuza kidogo kidogo mbele yako, hata utakapoongezeka wewe, na kuirithi hiyo nchi. Kutoka 23:27-30

Kama waisraeli wangesalia waaminifu kwa Mungu inchi ya Kanani ingetakaswa jinsi Yesu alivyotakasa hekalu. Roho wa Mungu angetia hatiani dhambi za mataifa haya, Kisha katika usumbufu wao, pengine wangekimbia au wangeungama, kutubu na kuungana na Waisraeli au kujifunza kufuata Waisraeli wa Mungu. Tunatia mkazo sehemu ambayo fungu linasema mataifa wataokolewa wala sio kuchinjwa hadi kifo.

Kama alitaka wake kuwaua adui zao angemhimiza Musa kufanya zaidi ya kile alichofanya alipomuua Mmisri. Lakini badala yake alimtuma Musa jagwani kuwachunga kondoo kwa miaka arobaini. Tayari Musa alikuwa na mafunzo yote ya generali mkuu kama mjukuu wa Farao. Mbona Mungu akaruhusu huyu generali mwenye ujuzi mkubwa kwenda jangwani kuwachunga kondoo? Ilikuwa kumfunza Musa jinsi ya kuwahudumia watu. Mafunzo yapo kwa wale wanoahitaji kujifunza. Mungu hakukusudia kuchukua nchi ya Kanani kwa vita.

Katika kuwaokoa waisraeli kutoka Misri alikusudia wamjue na wajifunze kumuamini. Wakiishi katika inchi ya Misri, Waisraeli walikuwa

wemezungukwa na roho ya dhuluma. Katika mfano wa watoto wa Waebrania kutupwa mtoni na hali ngumu ya utumwa ya Misri wengi walishawishika na dhana kuwa Mungu alikuwa mjeuri ambaye angeweza

kuwageukia wakati wowote na kuwaua. Tunaona uoga huu ukidhihirika tangia mwanzo:

> Wakamwambia Musa, Je! Kwa sababu hapakuwa na makaburi katika Misri umetutoa huko ili tufe jangwani? Mbona umetutendea haya, kututoa katika nchi ya Misri? Kutoka 14:11

Uwoga huu unaweza rejelewa katika bustani ya Edeni shetani alipowafanya Adamu na Hawa kuamini kuwa wakati Mungu alisema kuwa hakika wangekufa ilimaaninisha kuwa ni yeye angekuja kuwaua.

> Akasema, Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha. Mwanzo 3:10

Kwa kumshtumu Musa Waisraeli walificha hofu ya Mungu waliyemjua. Lakini ilikuwa wazi na dhahiri kuwa Musa hakuwatoa watu Misri kwa nguvu zake mwenyewe. Shetani alikuwa akiwajaribu ili kufikiria kuwa Mungu alitaka kuwaua katika jangwa. Jaribio hili lingewezekana tu kutokana na kuelewa tabia ya Mungu isivyo. Hofu hii iliendelea kukua kwa Waisraeli.

> Wana wa Israeli wakawaambia, **Laiti tungalikufa kwa mkono wa Bwana katika nchi ya Misri,** hapo tulipoketi karibu na zile sufuria za nyama, tulipokula vyakula hata kushiba; kwani mmetutoa huko na kututia katika bara hii, ili kutuua kwa njaa kusanyiko hili lote. Kutoka 16:3

Waisraeli walionyesha hofu yao kwa Mungu na wakasema wazi afadhali wangekufa kwa mikono ya Mungu katika inchi ya Misri kuliko kuvumilia hali yao ya sasa. Ni wazi hawakumwamini Mungu, na akili zao zilipofushwa na shetani kwa kuona tabia ya kweli ya Mungu.

Katika sura inayofuata ya Kutoka Waisraeli wanaweka wazi hata zaidi mawazo yao potovu juu ya Mungu:

> Watu wakawa na kiu huko; nao wakamnung'unikia Musa, wakasema, Mbona umetupandisha kutoka Misri, kutuua sisi na watoto wetu na wanyama wetu kwa kiu? (4) Musa akamlilia Bwana, akisema, Niwatendee nini watu hawa? Bado kidogo nao watanipiga kwa mawe. Kutoka 17:3-4

Wanaendelea kunung’unika na kumshtumu Musa na, kwa hivyo, Mungu kutaka kuwaua. Ibada ya sanamu kwa mtazamo wa Mungu katili inaanza

kufasiri kwa vitisho vya kumuua Musa. Kwa kushikilia wazo hili la uongo la Mungu katili wanabadilishwa katika hiyo sura na wanapanga vitendo vya ukatili dhidi ya mtu ambaye Mungu alitumia kuwaokoa kutoka Misri.

Manung'uniko, malalamishi na kutomwamini Mungu daima, kunamweka katika nafasi ambayo ana uwezo mchache wa kuwalinda. Wanamchagua shetani kama Bwana wao, na shetani anadai fursa ya kuwaangamiza. Tunaona uhusiano kati ya malalamishi juu ya maji na ushambulizi wa Waamaleki ifuatavyo:

> Akapaita mahali pale jina lake Masa, na Meriba; kwa sababu ya mateto ya wana wa Israeli, na kwa sababu walimjaribu Bwana, wakisema, Je! Bwana yu kati yetu au sivyo? (8) Wakati huo Waamaleki wakatokea, wakapigana na Israeli huko Refidimu. Kutoka 17:7-8

Mateto ya Wana wa Israeli yalimfungulia shetani mlango wa kuwashawishi Waamaleki kuwashambulia. Hili halingetendeka kama Waisraeli wangemwamini Mungu. Waamaleki wangeogopa sana kuwaguza. Hakuna ushahidi wa kuonyesha kuwa Waisraeli walitubu juu ya dhambi zao dhidi ya Mungu. Walikuwa na mtazamo wa uongo kuwa Mungu ni mjeuri na anayekusudia kuwaua. Hapana ushahidi wa shukurani za kupokea maji. Hakuna kuomba radhi kwa Musa au neno lolote la kumshukuru kwa kuwaombea maji. Hakuna chochote kimerekodiwa kuonyesha hili. Waisraeli walikuwa wametishia kumuua Musa. Tunaweza fikiria kiasi ambacho hili lingemuumiza Musa? Angebaki katika ulimwengu mtulivu wa jagwa la nyumbani kwao akiiangalia familia yake na kuchunga kondoo wake. Pia angehisi msingi wa kutokuwa na shukurani waliokuwa wakimuonyesha Mungu. Ingekuwa ni jaribio la hakika kwa Musa. Kisha katika mawazo yake anapokea habari kuwa Waamaleki wanawashambulia na kuchukua wanyonge. Kinachotendeka baadaye ni muhimu. Ni uamuzi unaofanywa chini ya shinikizo na hali ya kuvunja moyo.

> Musa akamwambia Yoshua, Tuchagulie watu, ukatoke upigane na Waamaleki; kesho nitasimama juu ya kilele kile, na ile fimbo ya Mungu nitakuwa nayo mkononi mwangu. Kutoka 17:9

Haisemi, "Na Mungu akamwamuru Musa." Haisemi kuwa Mungu akaenda patakatifu na kumsihi Mungu. Inasema kuwa Musa akamwambia Yoshua utoke ukapigane. Nnapofikiria taswira ya Musa akimwendea Yoshua kila

kitu kinaenda polepole, na mawazo yangu yanageuka katika wakati ambao mtu katika ukoo wa Musa aliinua upanga dhidi ya wale walioitukana familia yake.

> Ikawa siku ya tatu, walipokuwa wakiumwa sana, wana wawili wa Yakobo, Simeoni na Lawi, nduguze Dina, wakatwaa kila mtu upanga wake, wakaujia mji kwa ujasiri, wakawaua waume wote. (26) Wakawaua Hamori, na Shekemu mwanawe, kwa makali ya upanga, wakamtwaa Dina katika nyumba ya Shekemu, wakatoka. (27) Wana wa Yakobo wakawajilia hao waliouawa, wakauteka nyara mji kwa sababu wamemharibu umbu lao. (28) Wakachukua kondoo zao, na ng'ombe zao, na punda zao, na vitu vilivyokuwamo mjini, navyo vilivyokuwako kondeni. (29) Wakatwaa na mali zao zote, na watoto wao wote, na wake zao, na vyote vilivyokuwamo nyumbani mwao wakavichukua mateka. Mwanzo 34:25-29

Kweli, Yakobo angeomboleza kuwa ukoo wake ungenuka machoni mwa Wakanani na Waamori. Wana wa Yakobo walikuwa wameuchukua upanga na basi upanga ungewafuata katika kizazi chao. Je, tunashuhudia athari za watoto wa Lawi wakielezea hadithi ya baba yao aliyeinuka kwa niaba ya umbu lao kuwaua Hamori? Kwani baadhi ya watoto wa Lawi wangejivunia kile baba yao alitenda kwa kumlinda dada yao? Je, shetani hangewaonyesha kuwa Lawi alihesabiwa haki kwa vitendo vyake kama njia ya kujikinga? Je, hii hadithi ingekuwa rahisi kusimulia kuliko kutaja kuwa baba yenu alikuwa muuaji na alipaswa kubeba aibu hadi kwa kizazi kingine? Yote ya historia hii sasa yanatembea kwenye nyao za Musa kuelekea kwa Yoshua.

Miaka arobaini katika jangwa ilikuwa imemwacha Musa kutoka kwenye jaribio la kuwalinda watu wake kwa uamuzi wake mwenyewe? Musa alikuwa amejua kuwa Waamaleki walikuwa wamewaua baadhi ya wanyonge katika kambi? Kabla ya kifo chake Musa alikumbuka:

> Kumbuka aliyokufanya Amaleki katika njia mlipokuwa mkitoka Misri; (18) jinsi alivyokukuta katika njia, akapiga katika watu wako walioachwa nyuma, wote waliokuwa wanyonge nyuma yako, ulipokuwa umechoka na kuzimia; wala asimche Mungu. (19) Basi itakuwa, hapo atakapokwisha kukupumzisha Bwana, Mungu wako, katika adui zako wote walio kando-kando, katika nchi akupayo Bwana, Mungu wako, iwe urithi uimiliki, ndipo uufute ukumbuko wa Amaleki chini ya mbingu; usisahau. Kumb 25:17-19

Haya yote yalikuja pamoja jinsi shetani alivyopanga ili kufanya Israeli kuvunda machoni pa ulimwengu? Aliweza kuongoza Israeli kubeba upanga tena, tabia ya Mungu imefasiriwa visivyo kwa muda mrefu? Udhihirisho wa matendo haya haukuwa wa mungu ambaye Israeli walifikiria? Kama mungu huyu waliyemfikiria hangeweza kuwapa maji wakayalihitajika basi angewezaji hata kwa kiasi kidogo kufikiria kuhusu kufa kwao mikononi mwa Waamaleki?

Katika hadithi ya Kora, Dathani na Abiramu na watoto wa kifalme 250 tunaona jinsi hofu hii ya Mungu aliyetaka kuwaua jagwani unawaongoza kutafuta uongozi mwengine kuliko Musa na Haruni. Kisha, walipofika kwenye mipaka ya Kanani, majasusi kumi walipeana taarifa za uongo juu ya nchi kwa sababu hawakuweza kuamini kuwa Mungu aliwapenda na alikuwa anawaazia mema tu. Walipuuza ulinzi wake na utunzaji wake wote na wakaangazia chochote hata kidogo hasi, pasipokuamini kuwa Mungu alikuwa na hekima na nia safi ya kutumia majaribu kuwatakasa. Shetani angewajaribu kwa urahisi kwa mambo hayo kwa sababu, walimwamini Mungu ambaye alitaka kuwaua na angebadilisha hali yake wakati wowote. Kila wakati ambao shetani aliruhusiwa kuvunja ua la ulinzi na kuwajeruhi Waisraeli angewaambia kuwa Mungu alikuwa anawaadhibu kwa mikono yake mwenyewe. Ni jinsi gani ilimhuzunishi Mungu kuona watu wake wakiamini kwa hiari uongo kama huo kumhusu.

> Kisha wana wa Israeli wote wakamnung'unikia Musa na Haruni; mkutano wote wakawaambia, Ingekuwa heri kama tungalikufa katika nchi ya Misri, au, ingekuwa heri kama tungalikufa katika jangwa hili. (3) **Mbona Bwana anatuleta mpaka nchi hii ili tuanguke kwa upanga? Wake zetu na watoto wetu watakuwa mateka**; je! Si afadhali turudi Misri? Hesabu 14:2-3

> kwa sababu watu hawa wote, ambao wameuona utukufu wangu na ishara zangu, nilizozitenda huko Misri, na huko jangwani, **pamoja na haya wamenijaribu mara hizi kumi, wala hawakuisikiza sauti yangu;** (23) hakika yangu hawataiona hiyo nchi niliyowaapia baba zao, wala katika hao wote walionidharau hapana atakayeiona; Hesabu 14:22-23

Israeli walipoambiwa hawangeiridhi inchi kwa sababu ya dhambi zao, waliasi tena na wakaamua kupanda juu na wakapigane, lakini Mungu hakuwa amewaamuru wakapigane. Kisha baada ya miaka arobaini kupita na kizazi chote kimekufa, walifika tena mpakani.

> Dhambi za mababa zao bado zilikuwa vinywani mwa wanao.**Watu wakamnung'unikia Mungu, na Musa, Mbona mmetupandisha huku kutoka nchi ya Misri, ili tufe jangwani?** Maana hapana chakula, wala hapana maji, na roho zetu zinakinai chakula hiki dhaifu. Hesabu 21:5

Shetani alikuwa akifanya kazi juu ya Musa wakati huu wote akimuhimiza afe moyo juu ya hawa masikini wadhalili. Mungu alikuwa amemjaribu Musa katika hatua hii kwa ajili yake, na kwa shukurani Musa alikuwa amemjibu Roho wa Kristo na kumuomba Mungu kuwasamehe jambo ambalo alilifanya kwa neema. Lakini, sasa kwa kuona kuwa Israeli wamekuwa wabaya hata kuliko mwanzo, alianguka majaribuni.

> Musa na Haruni wakawakusanya kusanyiko mbele ya mwamba, akawaambia, Sikieni sasa, enyi waasi; je! Tuwatokezee maji katika mwamba huu? (11) Musa akainua mkono wake akaupiga ule mwamba kwa fimbo yake mara mbili; maji yakatoka mengi, mkutano wakanywa na wanyama wao pia. Hesabu 20:10-11

Kuanguka kwa Musa majaribuni kulimpa shetani uwezo mkubwa wa kuingia katia mawazo ya Waisraeli. Musa alikuwa amewaombea na kuingia kati yao na shetani kwa njia nyingi sana. Lakini hatua hii ilimpa shetani fursa. Shetani alifurahia kuweza kuyachukua maisha ya Haruni kwa sababu ya anguko hili.

> Haruni atakusanywa awe pamoja na watu wake; kwa kuwa hataingia katika nchi niliyowapa wana wa Israeli, kwa sababu mliasi kinyume cha neno langu hapo penye maji ya Meriba. Hesabu 20:24

Kwa uwezo mkubwa wa kuzifikia akili za Waisraeli, Shetani aliwawezesha kufanya maafikiano na Mungu – Mungu Ambaye walifikiria alipenda kuwaua watu. Walikuwa wamevamiwa na kabila lingine kwa sababu ya dhambi zao, na sasa katika kukata tamaa kwao, waliapa:

> Na Mkanaani, mfalme wa Aradi, aliyeketi upande wa Negebu, alisikia habari ya kuwa Israeli alikuja kwa njia ya Atharimu; basi akapigana na Israeli, na watu kadha wa kadha miongoni mwao akawateka mateka. ( 2) **Basi Israeli akaweka nadhiri kwa Bwana akasema, Kama wewe utawatia watu hawa mikononi mwangu kweli ndipo mimi nitaiharibu miji yao kabisa.** (3) **Bwana akasikiza sauti ya Israeli,** akawatia Wakanaani mikononi mwao;

> nao wakawaharibu wao na miji yao kabisa; na jina la mahali hapo likaitwa Horma. Hesabu 21:1-3

Mungu hakuwaagiza Waisraeli kuwaangamizi adui zao; mtazamo wao wa uongo kuhusu Mungu uliwafanya kuamini kuwa Mungu alihitaji wafanye kiapo cha kiu ya damu kama hicho. Hili lingepokea idhini yake, na angewasaidia. Inasema kwamba Mungu akisikia sauti yao. Mbona Mungu akisikiza sauti yao? Si hili lingefanya wakite mizizi katika wazo kuwa Mungu alitaka wawaue adui zao? Jibu linapatikana katika mfano wa vipaji:

> "Kisha akaja yule mtumishi mwingine akasema, 'Bwana, hii hapa fedha yako. Niliitunza vizuri kwenye kitambaa. (21)Nilikuogopa, kwa sababu wewe ni mtu mgumu. Unachukua ambapo hukuweka kitu na unavuna mahali ambapo hukupanda kitu.'(22)"Bwana wake akamjibu, **'Nitakuhukumu kwa maneno yako mwenyewe, wewe mtumishi mwovu!** Kama ulifahamu kwamba mimi ni mtu mgumu, nichukuaye mahali ambapo sikuweka kitu na kuvuna mahali ambapo sikupanda, (23)kwa nini basi hukuweka fedha zangu kwa watoa riba ili nitakaporudi, nichukue iliyo yangu na riba yake?' Luka 19:20-23

Mtumishi mzembe alimfikiria Bwana wake kuwa mtu mkali. Kulingana na imani hii alipokea hukumu. Kama andiko linavyosema:

> So speak ye, and so do, as they that shall be judged by the law of Hivyo semeni na kutenda kama watu watakaohukumiwa kwa sheria ile iletayo uhuru. (13)Kwa kuwa hukumu itakuwa haina huruma kwa mtu ye yote asiyekuwa na huruma. Huruma huishinda hukumu. Yakobo 2:12-13

Mungu aliruhusu mtu ambaye alikuwa na mtazamo wa uongo kumhusu kuhukumiwa kulingana na mawazo yake mwenyewe. Mungu hufanyaje hili?

> Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi. Kwa kuwa kile apandacho mtu ndicho atakachovuna. Wagalatia 6:7

> Mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe; mwenye kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao, na wana wa wana wao pia, hata kizazi cha tatu na cha nne. Kutoka 34:7

Waisraeli walipoapa kwa Mungu kumuua mfalme wa Kanani walitawaliwa na roho wa shetani. Walikuwa wameua na kunung'nika dhidi ya Mungu na kuasi dhidi yake katika kila fursa. Mungu aliwaonya na kuwahimiza wafuate amri zake.

> Na sasa, Ee Israeli, zisikilizeni amri na hukumu niwafundishazo, ili mzitende; mpate kuishi na kuingia na kuimiliki nchi awapayo Bwana, Mungu wa baba zenu. Kumbukumbu 4:1

> Amri hii ninayokuamuru leo mtaishika kuitenda, mpate kuishi na kuongezeka, na kuingia katika nchi ile ambayo Bwana aliwaapia baba zenu; nanyi mtaimiliki. Kumbukumbu 8:1

Lakini Israeli walikataa kumtii Mungu, na shetani aliwezeshwa kudhibiti hamu yao ya kuhukumu bila huruma. Mungu aliwapa kile walihitaji hata ingawa haikuwa mpango wake. Pia aliwapa watu wa mataifa kile walichoogopa; kwa vile hawakuwa wakilindwa tena. Shetani alitumia Waisraeli kuwaua Wakanani. Kwa kufanya hivi angewaongoza mamilioni kwa kifo chao kwa kuelewa visivyo tabia ya Mungu, yaani yule auae na kuchinja watu.

Tunapata mtazamo wa mpango wa Mungu wa kukabiliana na adui wa Waisraeli bila Silaha katika mafungu kama haya:

> Nanyi mliuvuka Yordani, mkafika Yeriko; nao watu wa Yeriko wakapigana nanyi, Mwamori, na Mperizi, na Mkanaani, na Mhiti, na Mgirgashi, na Mhivi, na Myebusi; nami nikawatia mikononi mwenu. (12) Nikatuma mavu mbele yenu, waliowafukuza mbele yenu hao wafalme wawili wa Waamori**, si kwa upanga wako, wala kwa upinde wako.** Yoshua 24:11-12

> Akasema, Sikieni, Yuda wote, nanyi mkaao Yerusalemu, na wewe mfalme Yehoshafati; Bwana awaambia hivi, Msiogope, wala msifadhaike kwa ajili ya jeshi kubwa hili; kwani vita si yenu bali ni ya Mungu. (16) Kesho shukeni juu yao; tazameni, wanakwea kwa kupandia Sisi; nanyi mtawapata penye mwisho wa bonde, mbele ya jangwa la Yerueli. (17) Hamtahitaji kupigana vita, jipangeni, simameni, mkauone wokovu wa Bwana ulio pamoja nanyi, enyi Yuda na Yerusalemu; msiogope, wala msifadhaike; kesho tokeni juu yao; kwa kuwa Bwana yu pamoja nanyi. (18) Yehoshafati akainama kichwa, kifulifuli; wakaanguka mbele za Bwana Yuda wote na

> wakaao Yerusalemu, wakimsujudia Bwana. (19) Na Walawi, wa wana wa Wakohathi na wa wana wa Wakorahi, wakasimama ili wamsifu Bwana, Mungu wa Israeli, kwa sauti kuu sana. (20) Wakaamka asubuhi na mapema, wakaenda nje katika jangwa la Tekoa; nao walipokuwa wakitoka, Yehoshafati akasimama, akasema, Nisikieni, enyi Yuda nanyi wenyeji wa Yerusalemu; mwaminini Bwana, Mungu wenu, ndivyo mtakavyothibitika; waaminini manabii wake, ndivyo mtakavyofanikiwa. (21)**Naye alipokwisha kufanya shauri na watu, akawaweka wale watakaomwimbia Bwana, na kumsifu katika uzuri wa utakatifu, wakitoka mbele ya jeshi, na kusema, Mshukuruni Bwana; kwa maana fadhili zake ni za milele.** (22) Nao walipoanza kuimba na kusifu, Bwana akaweka waviziao juu ya wana wa Amoni, na Moabu, na wa mlima Seiri, waliokuja juu ya Yuda; nao wakapigwa. (23) Kwani wana wa Amoni na wa Moabu waliwaondokea wenyeji wa mlima Seiri kuwaulia mbali na kuwaharibu; nao walipokwisha kuwakomesha hao wakaao Seiri, wakajitia kuharibu kila mtu mwenziwe. 2 Mambo ya Nyakati 20:15-23

Waisraeli waliruhusiwa kuichukua nchi ya Kanani kwa Vita, lakini haukuwa mpango asili wa Mungu. Kwa kuwa daima Israeli waliogopa kuwa Mungu alijaribu kuwaua na walishuku utuzanji wake wa upendo, shetani aliwezeshwa kuwaingiza katika kuapa kwa Mungu kuwachinja Wakanani na mataifa mengine. Waisraeli waliwezeshwa kuwa washindi katika vita, lakini shetani alishinda vita dhidi ya tabia ya Mungu. Waisraeli walishindwa katika ushindi wao na kushikwa mateka katika mtazamo wa uongo wa Mungu.

Katika siku hizi za mwisho tunapewa fursa ya kuona tabia ya Mungu kama ilivyo kweli. Machoni pa Yesu kristo tunaweza anza kufunua mapenzi ya kweli ya Baba yetu wa mbinguni. Ni watu wangapi ambao Yesu aliua kwa upanga? Ni wangapi alichoma kwa moto? Ni watoto wangapi alitundika kwa mkuki? Hakuna kabisa! Kwa wale ambao hukaribisha mawazo kuwa Mungu alikuja kuangamiza maisha ya wanadamu kumbuka maneno ya Yesu:

> Yesu akawageukia, akawakanya.[Akasema, Hamjui ni roho ya namna gani mliyo nayo] (56) kwa maana Mwana wa Adamu hakuja kuziangamiza roho za watu, bali kuziokoa. Wakaondoka wakaenda kijiji kingine. Luka 9:55-56

Upanga ambao Yesu hutumia ni Neno lake litokalo kinywani mwake. Upanga wake ni neno lake.

> Katika mkono wake wa kuume alishikilia nyota saba na kinywani mwake ulitoka upanga wenye makali kuwili. Uso wake kama jua kali linalong'aa kwa nguvu zake zote. Ufunuo 1:16.

> Kwa maana Neno la Mungu li hai tena lina nguvu tena lina makali kuliko upanga uwao wote wenye makali kuwili, tena linachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, viungo na mafuta yaliyo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. Waebrania 4:12

> Akawaambia, "Lakini sasa, aliye na mfuko na auchukue na aliye na mkoba vivyo hivyo. Naye asiye na upanga, auze joho lake anunue mmoja. Luka 22:36

> … na mchukue upanga wa Roho, ambao ni Neno la Mungu. Waefeso 6:17

Wafuasi wa Yesu watafuata mfano wake. Yesu hakutumia upanga halisi. Basi ni jinsi gani tunaelezea fungu hili?

> Wanafunzi Wake wakamwambia, "Bwana, tazama hapa kuna panga mbili." Akawajibu, "Inatosha." Luka 22:38

Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi mafungu mawili awali "Naye asiye na upanga, auze joho lake anunue mmoja." Wanafunzi walipotoa mapanga mawili halisi hawakuwa wameuza joho na kuyanunua. Ujumbe wa Yesu ulikuwa kwa mtu binafsi. Kila mtu alikuwa auze joho lake anunue upanga. Vipi kuhusu wanafunzi wengine na amri la kuuza joho lako? Joho ambalo Yesu alitaka wanafunzi wauze ni nini?

> Basi, Yoshua alikuwa amevaa nguo chafu sana, naye alikuwa akisimama mbele ya malaika. (4) Naye huyo akajibu, akawaambia wale waliosimama mbele yake, akisema, **Mvueni nguo hizi zenye uchafu**. Kisha akamwambia yeye, Tazama, nimekuondolea uovu wako, nami nitakuvika mavazi ya thamani nyingi. Zekaria 3:3-4

Yesu alimwambia Pilato kuwa ufalme wake haukuwa wa ulimwengu huu.

> Yesu akajibu, "Ufalme Wangu si wa ulimwengu huu. **Ufalme Wangu ungekuwa wa ulimwengu huu wafuasi Wangu**

> **wangenipigania** ili nisitiwe mikononi mwa Wayahudi. Lakini kama ilivyo Ufalme Wangu hautoki hapa ulimwenguni." Yohana 18:36

Yesu alimwambia Pilato kuwa wafuasi wake hawangepigana kwa namna ya ulimwengu. Wanafunzi walihitaji kuitakasa mioyo yao ili kutumia kwa halali neno la kweli. 2 Timotheo 2:15. Pia tunagundua kuwa wanafunzi walipomwonyesha Yesu yale mapanga mawili alisema " haijatosha." Kama alihisi kuwa mapanga mawili yametosha angesema "yametosha" kwa kuwa walikuwa na zaidi ya upanga mmoja. Kama kwa sababu yoyote Yesu alikuwa akisema kuwa mapanga mawili yametosha, swali ni yametosha kwa nini? Wangetembea na mapanga mawili kila wakati ili daima wawe nayo? Mapanga haya yalitosha kujilinda dhidi ya Warumi na walinzi wa hekalu? Wazo hili halileti maana hata kidogo. Yesu aliposema "imetosha" katika umoja alimaanisha imetosha kwa mazungumzo ya namna hiyo. Kuyatoa mapanga hayo mawili kulidhihirisha joho hasa walilohitaji kuuza ili wawe na upanga wa kweli wa neno la Mungu ili kuhubiri injili ya amani. Hivi ndivyo aliwambia wanafunzi wake kujibu kwa waliowakosea:

> "Mmesikia kwamba ilinenwa, 'Jicho kwa jicho na jino kwa jino.' (39) Lakini mimi nawaambia, **msishindane na mtu mwovu. Lakini kama mtu akikupiga kwenye shavu la kuume, mgeuzie na la pili pia,** (40) Kama mtu akitaka kukushtaki na kuchukua shati lako, mwachie achukue na koti pia. (41) Kama mtu akikulazimisha kwenda kilometa moja, nenda naye kilometa mbili. (42) Mpe yeye akuombaye, wala usimgeuzie kisogo yeye atakaye kukukopa." Upendo Kwa Adui (43)"Mmesikia kwamba ilinenwa, 'Mpende jirani yako na umchukie adui yako.' (44) **Lakini mimi ninawaambia : Wapendeni adui zenu na waombeeni wanaowatesa ninyi,** (45) ili mpate kuwa watoto wa Baba yenu aliye mbinguni. Kwa maana Yeye huwaangazia jua lake watu waovu na watu wema, naye huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki. Mathayo 5:38-45

Je, Shetani atakushinda katika ushindi wa Waisareli juu ya Kanani kwa upanga, ama utaona Baba yetu mwingi wa rehema akiwacha watu kupokea matakwa yao na kufuata mwendo wao hadi mwisho. Chagua hivi leo utakayemtumikia; Mimi na nyumba yangu nitamtumikia Mungu mwenye rehema daima ambaye hawezi kwa vyovyote maovu bali kuruhusu ngano na magugu kukua pamoja ili kwamba moyo wa kila mtu udhihirishwe.

Inawezakanaje kutimiza vitu hivi kwa upanga au bunduki mkononi mwako kujilinda? Sio wakati wa kuweka upanga mahali pake? Wacha ushikwe na kutu, na tumwamini Baba yetu kuwatuma malaika wake kwa utunzaji wetu. Ushindi wa Waisraeli juu ya Kanani ulifanywa kwa upanga kwa sababu wengi wao hawakumwamini Mungu kuwaaondoa Wakanani kupitia kwa uwoga wa Mungu. Malalamiko yao yote, manung'uniko na uwoga kuwa Mungu alitaka kuwaua jangwani ilimaanisha badala ya kuwa nuru kwa mataifa, dhambi za mataifa yaliyowazunguka waisraeli ziliadhibiwa kwa dhambi za Waisraeli. Kama amri inavyosema:

> Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, Kutoka 20:5

Wengi wa Waisraeli walimchukia Mungu kwa sasbabu walihofu kuwa angewaua jangwani. Dhambi za mababa zao wa awali ziliendelezwa, na kwa hivyo historia ya waisraeli imelowekwa katika damu. Usiruhusu ushindi wa Waisraeli kwa upanga ushinde uelewa wako wa tabia ya Mungu kama inavyodhihirishwa katika Yesu. Usiruhusu kundi la utumwa wa manung'uniko, malalamiko kukuamulia jinsi Mungu alivyo. Tuzitunze amri zote za Mungu ikiwemo ile inayosema' "usiue.

# 13. Taji la Miiba

Kujaribiwa na kuuawa kwa Kristo kunakabiliana na unyonge wa asili ya mwanadamu. Wanaume na wanawake waliohusika katika udhalilishaji, kumchapa na hata kumuua Kristo walikuwa udhihirisho wa roho ya mwanadamu ambaye amedharau na kukataa Roho wa Kristo tangia anguko la mwanadamu. Kamba zilizomfunga Kristo na mijeredi aliyochapwa, mbao na misumari ya msalaba ambao alisulubishwa, vyote vilikuwa ni vitu alivyoviumba. Tunasoma:

> Vitu vyote viliumbwa kwa Yeye, wala pasipo Yeye hakuna cho chote kilichoumbwa ambacho kimeumbwa. Yohana 1:3

Taji la miiba alilovikwa kichwani mwake lilikuwa lenye maana sana na lilikuwa na ukweli wa kina wa kiroho. Adamu alipoanguka dhambini miiba iliyoota ilikuwa udhihirisho wa laana iliyoletwa na dhambi.

> Akamwambia Adamu, Kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza, nikisema, Usiyale; **ardhi imelaaniwa kwa ajili yako;** kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako; (18) **michongoma na miiba** itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni; Mwanzo 3:17-18

Mbona laana ikaanguka ardhini? Kulikuwa na uhusiano upi kati ya Mwanadamu na dunia?

> Bwana **Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi**, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai. Mwanzo 2:7

> Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; **wakatawale** samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, **na nchi yote pia**, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. Mwanzo 1:26

Mungu alimfanya mtu kutoka duniani na akamfanya mtawala wa dunia. Ukweli huu unadhihirisha kuwa kuna uhusiano wa karibu kati ya mtu na dunia. Mambo yanayofanywa na mtu yanaathari ya moja kwa moja kwa dunia. Laana iliyomwangukia Adamu mara moja iliakisiwa katika miiba na michongoma iliyoitoa. Ardhi ililaaniwa kwa ajili ya mwanadamu, ili aweze kutambua katika msukosuko wa maumbile kielelezo cha kiwango cha uovu uliopo katika jamii ya mwanadamu, na kwa hivyo itatumika kama onyo la hatari.

> Mtasikia habari za vita na matetesi ya vita,angalieni msitishike, kwa maana haya hayana budi kutukia, lakini ule mwisho bado. (7) Taifa litainuka dhidi ya taifa na ufalme dhidi ya ufalme. Kutakuwa na njaa na matetemeko ya ardhi sehemu mbalimbali. Mathayo 24:6-7

Kuna kisababishi cha uhusiano kati ya vita na migogoro ya watu, na misukosuko na vita katika maumbile. Migogoro na utovu wa maadili katika jamii inaongezea basi maafa katika maumbile yanaongezeka; hivo basi, maumbile ni kipimo cha kiwango cha uasi katika mwanadamu. Wakati upepo mwanana wa maumbile, uliyoundwa kumpoza na kumfariji mwanadamu, unageuka kuwa tufani; au mvua iliyoundwa kuleta uhai inafanya mito kuvunja kinga na kuleta maafa na uharibifu, basi tunaona thibitisho la uasi huo unaopatikana katika mioyo ya wanadamu ukiwekwa wazi katika majanga ya maumbile.

Kisababishi cha uhusiano kati ya mwanadamu na maumbile humaanisha kuwa kadri uasi wa jamii ya mwanadamu unaongezeka ndivyo uasi wa upepo, moto na mafuriko unaongezeka. Watu wanapozivunja amri za Mungu kwa bidii kubwa, ndivyo dunia itavunja sheria za maumbile na kuonesha kwa wanadamu uasi wao wenyewe. Roho wa uasi anapoinuka katika wanadamu dhidi ya Kristo na wanatafuta kumuua aliye na utawala juu yao, ndivyo maumbile yatainuka juu yao kwa uasi dhidi ya mwanadamu na kutafuta kumuua Kama wanadamu wanavyovamia dunia na kula wengine kwa ndimi

zao na mapanga yao, ndivyo wanyama wa mwituni wataivamia dunia na kuwala kwa namna hiyo hiyo. Kama mtu apandavyo ndivyo atakavyovuna. Kwa upande mwingine, dunia haitapigana na mtu aliye na amani na Mungu, wala sio katika uasi dhidi yake.

> Tazama, yu heri mtu yule Mungu amwadhibuye; Kwa hiyo usidharau kurudiwa na huyo Mwenyezi. (18) Kwani yeye huumiza, lakini tena huuguza; Yeye hutia jeraha, na mikono yake huponya. (19) Yeye atakuokoa na mateso sita; Naam, hata katika saba hapana uovu utakaokugusa. (20) Wakati wa njaa atakukomboa na mauti; Na vitani atakukomboa na nguvu za upanga. (21) Utafichwa na mapigo ya ulimi; Wala usiogope maangamizo yatakapokuja. (22) Wewe utayacheka maangamizo na njaa; Wala hutawaogopa wanyama wakali wa nchi. (23) Kwani utakuwa na mapatano na mawe ya bara; Nao wanyama wa bara watakuwa na amani kwako. (24) Nawe utajua ya kwamba hema yako ina salama; Na zizi lako utaliaua, wala usikose kitu. Ayubu 5:17-24

Yesu alipokuwa akininginia msalabani, jua lilikataa kuangaza, dunia ilitetemeka na komeo za umeme zilianguka kutoka mbinguni. Maumbile yalikuwa katika huruma pamoja na Mwanzilishi wake, Mwana wa Mungu. Wakati huo huo, akiwa amezibeba dhambi za ulimwengu na taji la miiba, maumbile yanaonekana ya kitafuta kumuua.

> Ndipo nchi iliyotikisika na kutetemeka, Misingi ya milima ikasukasuka; Ikatikisika kwa sababu alikuwa na ghadhabu. (8) Kukapanda moshi kutoka puani mwake, Moto ukatoka kinywani mwake ukala, Makaa yakawashwa nao. (13) Bwana alipiga radi mbinguni, Yeye Aliye juu akaitoa sauti yake, Mvua ya mawe na makaa ya moto. (14) Akaipiga mishale yake akawatawanya, Naam, umeme mwingi sana, akawatapanya. (15) Ndipo ilipoonekana mikondo ya maji, Misingi ya ulimwengu ikafichuliwa, Ee Bwana, kwa kukemea kwako, Kwa mvumo wa pumzi ya puani mwako. Zaburi 18:7-8,13-15.

Msukosuko wa maumbile katika kifo cha Kristo msalabani unatupa kidokezo cha namna maumbile huonesha uasi wa mwanadamu. Unyoofu wa Yesu ulifanya maumbile kuwa katika huruma pamoja naye; Lakini, kama mbeba wa dhambi zetu, maumbile yalimchoma kwa taji la miiba yake. Komeo za umeme kutoka mbinguni zilionekana kuashiria kutofurahia kwa mbingu

yenyewe. Katika uhusiano huu kati ya mtu na maumbile tunaweza gundua sababu ya mafuriko. Biblia inasema kuhusu wale walioishi kabla ya mafuriko:

> Ikawa wanadamu walipoanza kuzidi usoni pa nchi na wana wa kike walizaliwa kwao, (2) **wana wa Mungu waliwaona hao binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri; wakajitwalia wake wo wote waliowachagua.** (3) Bwana akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele, kwa kuwa yeye naye ni nyama; basi siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini. (4) Nao Wanefili walikuwako duniani siku zile;tena ,baada ya hayo ,wana wa Mungu walipoingia kwa binti za binadamu,wakazaa nao wana;hao ndiyo waliokuwa watu hodari zamani ,watu wenye sifa. (5) **Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu sikuzote.** (6) Bwana akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani, akahuzunika moyo. Mwanzo 6:1-6

Bibilia inasema kuwa mawazo ya akili za wanadamu ilikuwa dhambi wakati wote. Wanadamu walijawa na tamaa za mwili na kiu ya uongozi alitenda uovu wa kila aina unaoweza kuwazika. Uovu usiozuilika wa mwanadamu ulikuwa na athari kubwa na kubwa zaidi duniani. Uasi wa wanadamu dhidi ya sheria ya Mungu ulikuwa unaingizwa moja kwa moja katika mashine ya maumbile.

Kwa huruma Mungu aliionya dunia kupitia kwa Nuhu kwa gharika inakuja juu ya dunia. Kama vile mtu alikuwa amejiharibu kimaadili, ndivyo uharibifu ungewekwa wazi duniani.

> Dunia **ikaharibika** [H7843] mbele za Mungu, dunia ikajaa dhuluma. (12) Mungu akaiona dunia, na tazama, **imeharibika;** [H7843] maana kila mwenye mwili amejiharibia njia yake duniani. (13) Mungu akamwambia Nuhu, Mwisho wa kila mwenye mwili umekuja mbele zangu; kwa sababu wameijaza dunia dhuluma, basi nitawaharibu pamoja na dunia. Mwanzo 6:11-13

Mungu alipotazama duniani aliona kuwa wanadamu wamejiharibu kabisa. Jina sawa la Kiibrania la kuharibika katika Mwanzo6:11 linatumika katika Mwanzo 6:13 kama kuharibika. Katika fungu hili tunapewachangamoto tena kuuliza tunasomaje kifungu hiki. Sasa, mmoja anaweza hitimisha kuwa Mungu aliamua kuwaangamiza wote isipokuwa wanane katika wenyeji wa dunia kwa sababu ya uovu wao, na kwa hivyo kumaliza uovo. Kinyume chake

unaweza ona kuwa Mungu alijua uharibifu wa mwanadamu hatimaye ungeoneshwa duniani na na uharibifu huu Ungeharibu ulimwengu. Wanadamu walipozidi sana na kuasi dhidi ya Mungu, ndivyo ulimwengu ulianza kuzidisha mipaka yake na kuasi dhidi ya wanadamu.

Bibilia inasema kwamba Mungu aliona kuwa dunia ilijaa ukatili. Wakristo wengi wanaamini kuwa Mungu aatajibu ukatili wa mwanadamu kwa kuwa katili pia, na kuwaua wote katika gharika ya kikatili. Ni huzuni jinsi gani kuamini kuwa Mungu anaweza kuwa katili kama wanadamu ili kuangamiza ukatili wao. Ni ukatili kiasi gani unapatikana katika Mwana wa Mungu ambaye ni kielelezo cha sura ya Baba yake?

> Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; Na pamoja na matajiri katika kufa kwake; **Ingawa hakutenda jeuri**, Wala hapakuwa na hila kinywani mwake Isaya 53:9

Vurugu inatoka wapi?

> Kwa wingi wa uchuuzi wako watu walikujaza udhalimu ndani yako, nawe umetenda dhambi; kwa sababu hiyo nimekutoa kwa nguvu katika mlima wa Mungu, kama kitu kilicho najisi; nami nimekuangamiza, Ewe kerubi ufunikaye, utoke katika mawe hayo ya moto. Ezekieli 28:16

Andiko linasema uovu utamwua asiye haki. Zaburi 34:21. Sheria ya maumbile haihitaji kuwa katika vurugu na wanadamu. Maandiko yanatupa ishara jinsi sheria hizi zilianzilishwa hapo mwanzo.

> Ni nani aliyepanda mbinguni na kushuka chini? Ni nani aliyekamata upepo kwa makonzi yake? **Ni nani aliyeyafunga maji ndani ya nguo yake? Ni nani aliyefanya imara ncha zote za nchi?** Jina lake ni nani? Na ni nani jina la mwanawe, kama wajua? Methali 30:4

> Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya nchi? Haya! Sema, kama ukiwa na ufahamu. (5) Ni nani aliyeamrisha vipimo vyake, kama ukijua? Au ni nani aliyenyosha kamba juu yake? (6) Misingi yake ilikazwa juu ya kitu gani? Au ni nani aliyeliweka jiwe lake la pembeni, (7) Hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, Na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha? (8) Au ni nani aliyeifunga bahari kwa milango, Hapo ilipofurika kana kwamba imetoka tumboni. **(9) Nilipolifanya wingu kuwa vazi lake, Na giza zito**

**kuwa nguo ya kuifungia, (10) Nikaiagiza amri yangu; Nikaiwekea makomeo na milango, (11) Nikasema, Utafika mpaka hapa, lakini hutapita, Na hapa mawimbi yako yanyetayo yatazuiliwa?** Ayubu 38:4-11

Je! Umeziingia ghala za theluji, Au umeziona ghala za mvua ya mawe, (23) **Nilizoziweka akiba kwa wakati wa misiba, Kwa siku ya mapigano na vita?** (24) Je! Nuru hutengwa kwa njia gani, Au upepo wa mashariki hutawanywaje juu ya nchi? (25) **Ni nani aliyepasua mfereji kwa maji ya gharika, Au njia kwa umeme wa radi;** (26) Kunyesha mvua juu ya nchi isiyo na watu; Juu ya jangwa asiyokaa mwanadamu; (27) Kuishibisha nchi iliyo kame na ukiwa, Na kuyameza majani yaliyo mororo? Ayubu 38:22-27

**Sauti ya Bwana i juu ya maji; Mungu wa utukufu alipiga radi; Bwana yu juu ya maji mengi.** (4) Sauti ya Bwana ina nguvu; Sauti ya Bwana ina adhama; (5) Sauti ya Bwana yaivunja mierezi; Naam, Bwana aivunja-vunja mierezi ya Lebanoni; (6) Airusha-rusha kama ndama wa ng'ombe; Lebanoni na Sirioni kama mwana-nyati. (7) **Sauti ya Bwana yaipasua miali ya moto;** (8)Sauti ya Bwana yalitetemesha jangwa; Bwana alitetemesha jangwa la Kadeshi. (9) Sauti ya Bwana yawazalisha ayala, Na kuifichua misitu; Na ndani ya hekalu lake Wanasema wote, Utukufu. (10) Bwana aliketi juu ya Gharika; Naam, Bwana ameketi hali ya mfalme milele. (11) **Bwana atawapa watu wake nguvu; Bwana atawabariki watu wake kwa amani.** Zaburi 29:3-11

Sauti ya Bwana juu ya mambo ya maumbile inazungumza kuhusu sheria zilizowekwa katika maumbile. Sheria hizi zilizoundwa kumbariki na kumsaidia mwanadamu na zingeonesha utiifu wake,roho wa utiifu kwa Mungu ziligeuzwa kuwa silaha dhidi ya mwanadamu kwa kumwangamizi. Kwa njia hiyo hiyo amabayo wanadamu huchukua mzabibu safi na kuutumia kutengeneza kileo ambacho hupelekea kifo na uharibifu, hivyo watu wenye mawazo maovu huchafua dunia na kugeuza maumbile kuwa silaha ya uharibifu dhidi yao wenyewe. Ibada ya sanamu, makufuru, mauaji, wizi, tamaa, na dhambi zote ambazo zimezungumziwa katika Amri Kumi, amri, na hukumu italeta laana juu ya dunia.

Kupitia kwa Musa Waisraeli walionywa kuwa wangeguswa na maadali yao ya kupotosha

> Nanyi msifanye matendo kama yale ya nchi ya Misri mliyokaa; wala msifanye matendo kama yale ya nchi ya Kanaani, nitakayowapeleka; wala msiende katika amri zao hao. Walawi 18:3

Mungu aliwaonya Israeli wasijihusishe na uzinzi, uasherati, kulawiti, ushoga, na mengine ya tamaa za mwili za kupotosha. Iwapo wangetenga dhambi hizi, hakika nchi ingeitikia.

> Msijitie unajisi katika mambo hayo hata mojawapo; kwa maana hizo taifa nitakazozitoa mbele zenu zimekuwa najisi kwa mambo hayo yote; (25) na hiyo nchi imekuwa najisi; kwa ajili ya hayo naipatiliza uovu wake juu yake, **na hiyo nchi yatapika wenyeji wake na kuwatoa.** Walawi 18:24-25

Hamu ya ngono ya kupotosha ya wanadamu inaathari juu ya dunia. Kufichuliwa kwa muda mrefu kwa maovu hayo kwa dunia, huifanya dunia kugonjeka kikatili, na itawatapika wenyeji wa dunia watendao vitendo hivi.

> Dunia inaomboleza, inazimia; ulimwengu unadhoofika, unazimia; watu wakuu wa dunia wanadhoofika. (5) Tena dunia imetiwa unajisi kwa watu wanaoikaa; kwa maana wameziasi sheria, wameibadili amri, wamelivunja agano la milele. (6) **Ndiyo sababu laana imeila dunia hii, na hao wanaoikaa wameonekana kuwa na hatia, ndiyo sababu watu wanaoikaa dunia wameteketea, watu waliosalia wakawa wachache tu.** Isaya 24:4-6

Fungu hili linaonyesha wazi njia ya uharibifu na jinsi uasi wa sheria ya Mungu huifanya dunia kuwa najisi na kuitikia. Nabii Isaya ananakili kuwa uasi wa watu husababisha laana kuila dunia na kuwateketeza wenyeji wake. Uharibifu wa awali wa dunia kwa maji katika gharika na uharibifu wa usoni wa dunia kwa moto unahusishwa na tama za watu kwa njia ifuatayo:

> **Kwanza kabisa ni lazima mfahamu ya kwamba siku za mwisho watakuja watu wenye dhihaka wakidhihaki na kuzifuata tamaa zao mbaya.** (4) na kusema, "Iko wapi ile ahadi ya kuja Kwake? Tangu baba zetu walipokufa, kila kitu kinaendelea kama kilivyokuwa tangu mwanzo wa kuumbwa." (5) Wao kwa makusudi hupuza ukweli huu, ya kwamba kwa neno la Mungu mbingu zilikuwepo tangu zamani nayo dunia ilifanyizwa kutoka ndani ya maji na kwa hayo maji, (6) **ulimwengu wa wakati ule uligharikishwa na kuangamia.** (7) Lakini **kwa neno lilo hilo**

> **mbingu za sasa na dunia, zimewekwa akiba kwa ajili ya moto, zikihifadhiwa hadi siku ile ya hukumu na ya kuangamizwa kwa watu wasiomcha Mungu.** 2 Petro 3:3-7

Gharika ilisababishwa na tamaa na mawazo ya uovo ya watu. Mchakato sawa utatendeka wakati ulimwengu unaliwa na moto. Kama watu walivyoteketezwa katika tamaa zao kwa wengine katika siku za Sodoma, ndivyo mji ulivyoteketezwa kwa moto hivyo watu wachache walibaki. Kwa kweli ni watu watatu walioepuka mji huo mpotovu.

Kuharibiwa kwa Sodoma ni onyo kwetu kwa kile kitakacho tendeka katika mwisho wa wakati.

> Vivyo hivyo, Sodoma na Gomora na pia ile miji iliyokuwa kando-kando, ambayo kwa jinsi moja na hao, **walijifurahisha kwa uasherati na kufuata tamaa za mwili zisizo za asili**, waliwekwa wawe mfano kwa kuadhibiwa katika moto wa milele. Yuda 1:7

Sodoma na Gomora walijifurahisha kwa uasherati na kufuata tamaa za miili yao. Paulo anaelezea uovu wa watu wa Sodoma kama watu wa mji waliotaka kuwadhulumu kimapenzi wageni waliokuja katika nyumba ya Loti.

> Vivyo hivyo wanaume pia wakiacha matumizi ya asili ya wanawake **wakawakiana tamaa wao kwa wao.** Wanaume wakafanyiana matendo ya aibu na wanaume wengine nao wakapata katika maisha yao adhabu iliyowastahili kwa ajili ya upotovu wao. Warumi 1:27

Tamaa iwakayo ya watu wa Sodoma, ambayo ilikuwa ukiukaji wa sheria ya Mungu, ilisababisha dunia na maumbile kuitikia katika njia ya kupaparikana kutapika wenyeji hivyo basi watu wachache walibaki. Mungu aliuongoza moyo wa Ibrahimu kuomba kwa ajili ya mji wa Sodoma ili kwa kiasi aweze kuihifadhi nchi na wenyeji kutoka kwa matokeo ya kuepukika ya matokeo ya tamaa iwakayo. Kristo alibeba uzito wa tamaa zao kwa kushikilia nguvu za maumbile wakati aliwapa watu wa Sodomo muda wa kutubu. Jambo sawia lilikuwa limefanyika wakati wa gharika, Kabla ya gharika, Mungu alishikilia nguvu za maumbile kadri alivyoweza ili kuwapa watu muda wa kuamua kutubu na waokolewe.

Katika kukawia kuja, uumbaji wote hugumia na kuwa na utungu chini ya uzito wa dhambi za mwanadamu, na hili huturejesha nyuma kwenye uhalisia wa msalaba na taji la miiba.

> … Kristo ni nguvu na hekima ya Mungu. 1 Kor. 1:24

Ni kupitia kwa nguvu hii Kristo huushikilia ulimwengu.

> Mwana ni mng'ao wa utukufu wa Mungu na mfano halisi wa nafsi Yake, **akivihifadhi vitu vyote kwa neno Lake lenye uweza**. Waebrania 1:3

> Kwa Yeye vitu vyote vilivyoko mbinguni na juu ya nchi viliumbwa, vile vitu vinavyoonekana na vile visivyoonekana, kama ni **viti vya enzi au falme, au wenye mamlaka au watawala, vitu vyote viliumbwa na Yeye na kwa ajili Yake.** Wakolosai 1:16

Kwa kuwa Yesu hutekeleza vitu vyote kwa nguvu zake, roho ya uasi katika mwanadamu ambayo huathiri ulimwengu huu ulioumbwa ni kama uendelezo wa taji la miiba kwake, kumchoma kila siku anapofanya yote ili kuzuia madhara ya mwanadamu mwenye asili mbovu kutoiharibu na kuiangamiza dunia. Katika muktadha huu tunagundua kuwa ni kuteseka kwa Kristo kwa niaba ya mwanadamu kunakozuia pepo nne za ugomvi.

> Baada ya haya nikaona malaika wanne wakiwa wamesimama katika pembe nne za dunia, **wakizuia hizo pepo nne za dunia**, ili kwamba pasiwe na upepo utakaovuma juu ya nchi au juu ya bahari au juu ya mti wo wote. Ufunuo 7:1

Sababu pekee ambayo malaika anaweza zuia pepo hizi ni kuwa Yesu huchukua nguvu zote za uovu wa mwanadamu juu yake, na hivyo kuchelewesha matokeo ya uasi juu ya maumbile na dunia. Jamii inapoasi kabisa dhidi ya Roho wa Kristo hakuna anayesalia kusimama katika nafasi na kufyonza roho wa uasi wa mwanadamu ili kuzuia ugomvi kujiweka wazi katika maumbile.

Ulimwengu kama tujuavyo umechafuliwa kabisa na uovo. Mtandao umejazwa na video za mapenzi, na watu wanapatikana kila mahali wakitazama senema zilizojaa uasherati na ukatili. Idadi ya uhalifu, vita, na ukatili unaotawala vichwa vya habari zetu unadokeza kwa vyote kukosekana kwa utulivu ambao unapaswa kufasiriwa kwa mambo halisi ya maumbile yaliyowekwa chini ya utawala wetu hapo mwanzo.

Katika wakati huu wa sasa ulimwengu ungekuwa unawatapika wenyeji wake. Sababu ambayo hauwatapiki ni kuwa Mwana kondoo wa Mungu ***bado***

amevaa taji la miiba; ***bado*** amedharauliwa na kukataliwa; na ***bado*** anachomwa na maneno makali na mawazo maovu ya wanadamu.

Lakini hufyonza mengi ya haya awezavyo ili kwamba aweze kuwa na muda wa kugundua mambo haya na kutubu.

Wakati ujao ukitembea kwenye msitu au kando ya mto mtulivu au ziwa, jua kwa kweli utulivu unaoshuhudia ni kwa sababu Mkombozi wetu mpendwa anabeba uzito wa uasi wa mwanadamu. Katika kubeba uzito huu huzuia madhara ya uasi kadri awezavyo kulipuka katika tetemeko, tufani, mafuriko, na majanga. Ukweli kuwa majanga yanaongezeka humaanisha kuwa uovu katika mwanadamu unaongezeka. Wakati ambao karibu Kristo anakataliwa na kila mtu pepo nne zitaachiliwa juu ya dunia na kasha maumbile yataonesha ghadhabu ya mwanadamu.

Hii ndio sababu mbona Bibilia husema:

> Ndipo Bwana akanyesha juu ya Sodoma na juu ya Gomora kiberiti na moto toka mbinguni kwa Bwana. Mwanzo 19:24

Nguvu ambazo hushikilia mambo ya maumbile hutoka kwa Kristo kwa sababu hutekeleza maumbile yote. Nguvu zilizowekwa kwenye maumbile hufuata sheria iliyowekwa na Baba yetu aliye mbinguni. Sheria hizi ziliundwa kuonesha amani na maelewano ambayo ungekuwepo mioyoni mwa wanadamu wanapokuwa na ushirika na muumbaji wao. Dunia ingejazwa na misitu mizuri iliyojaa matunda, karanga na mbegu za ajabu, na rangi ya maisha ingedhihirishwa kila mahali katika uzuri wa utakatifu. Sheria hizi hizi zinageuzwa kifo na uharibifu watu wanapoishi katika uasi, na nguvu inayosababisha vitu hivi ni nguvu ya Kristo inayodumu katika sheria zisizobadilika. Hili linaelezea mfano wa fimbo iliyogeuzwa kuwa nyoka, lakini tutaangazia hili katika sura nyingine.

Gharika kuu ya dunia na moto ulioiyangukia Sodoma hayakuwa matendo ya kiholela ya Mungu katika kulipiza kisasi kwa uovu wa wanadamu.Matukio haya yalizuiliwa na Kristo kwa muda kadri alivyoweza ili kwapa watu fursa ya kutubu na kuona hatari yake. Japo sheria hizi ziliwekwa na kupeanwa kwa kubarikiwa kwa mwanadamu, Kristo amewekwa katika nafasi ya kubeba matokeo hasi ya upande mwingine wa kutenda wa sheria hizi. Saa ile Ambayo Kristo alikufa miaka 200 iliyopita mara moja tunagundua athari juu ya dunia:

> Basi yule jemadari na wale waliokuwa pamoja naye wakimlinda Yesu **walipoona lile tetemeko** na yale yote yaliyokuwa yametukia, wakaogopa wakasema, “Hakika huyu alikuwa ni Mwana wa Mungu!” Mathayo 27:54

Wakati mnyama wa pili wa Ufunuo 13 atawafanya watu wote kumwabudu mnyama wa kwanza na kuwafanya wote kuipokea chapa katika vipaji vya uso wao au katika mikono yao, Kristo atasulubiwa kupitia kwa kukataa amri zake. Pepo nne zitaachiliwa juu ya dunia, na roho ya uasi ya mwanadamu itakuwa kama makaa yachomao katika moyo wa dunia, na dunia itainuka katika roho ya ukatili na kujiharibu yenyewe pamoja na wenyeji wake. Wale tu ambao wamejifunza pahali pa siri pa aliye juu sana palipo na wanaishi chini ya kivuli cha Mwenyezi, kupitia kwa kuzitunza amri za Mungu kwa imani ya Yesu, watakingwa katika mambo ya ajabu. Ijapo watu elfu waanguka ubavuni pako, na kumi elfu mkono wako wa kuume, hata hivyop hautakukaribia wewe ( zaburi 91:7) kwa sababu wako katika amani na Munguna, kwa hivyo, pia pamoja na dunia.

Yesu angelala kwa amani katika merikebu iliyozungukwa na mawimbi kwa sababu dunia haikuwa vitani naye. Katika karne nyingi kumekuwa na wakati mwingi ambao upepo na mawimbi yamekuwa tayari kuwabeba wafuasi wake, lakini anainuka na kusema kwa mambo haya “amani iwe tuli.” Na kusihi  upige mbio pamoja na malaika kutoka mji wa Sodoma na  uingie katika safina ya usalama. Sasa ndio wakati wa kutubu na kuomba Roho wa Kristo ili tuweze kuacha kuwa na mioyo ya uasi dhidi ya Mungu, ambayo huifanya dunia kuasi dhidi yetu.

Asante Bwana Yesu kwa kuvalia taji la miiba kwa miaka hii yote, na kushikilia pepo za ugomvi – pepo ambazo huchochea nafsi za watu katika uasi na uovu na lazima hatimaye watavuna walichopanda duniani. Tugeuke kutoka kwenye njia zetu za uovu, uache kuvunja ua lako la milele na ujifunze kuzitunza sheria zako,amri, na hukumu ili kwamba amani itawale tena duniani.

# 14. Nguvu za Mauti

> Baada ya kuionja hiyo siki, Yesu akasema, "Imekwisha." Akainamisha kichwa chake, **akakata roho.** Yohana 19:30 (NKJV)
>
> Yesu akapaza sauti Yake akasema, "Baba, mikononi mwako naikabidhi roho Yangu." **Baada ya kusema haya, akakata roho.** Luka 23:46 (NKJV)
>
> Lakini Mungu anaudhihirisha upendo Wake kwetu kwamba: Tulipokuwa tungali wenye dhambi, **Kristo alikufa kwa ajili yetu.** Warumi 5:8

Yesu alipoinamisha kichwa chake na akafa, ulimwengu, ikiwemo waliokuwa duniani na walioshuhudia matukio yaliyopelekea kifo chake, walitazama onyesho kubwa sana la upendo wa Mungu kwa jamii ya wanadamu. Licha ya kukejeliwa, kutemewa mate, kupigwa na kuchapwa viboko Yesu hakujilipizia. Alisema "Baba wasamehe kwa kuwa hawajui walitendalo." Yesu alipokuwa akifa kwa uchungu, aliwaza juu ya mamake wa ulimwenguni na akamwagiza Yohana amtunze. Alimsamehe mwizi aliyetubu na kumuahidi uzima wa milele. Baada ya kushuhudia mambo haya askari wa Kirumi waliungama:

> "Hakika mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu!" Marko 15:39

Upendo wa ajabu, mtulivu na mvumilivu wa namna hiyo! Mkombozi wetu alivumilia kwa utulivu ukatili, ujeuri na vurugu zilizowekwa wazi kwa chuki ya

mwanadamu aliyeongozwa na mapepo. Shetani alikuwa amechochea chuki ya viongozi wa Wayahudi, makuhani na halaiki. Kwa vitendo vyao tunaona tabia ya shetani. Ukatili, chuki, udanganyifu, unyama na katili hadi mwisho, shetani alikuwa amedhihirishwa kikamilifu kuwa yeye ni nani. Katika hadithi ya msalaba tunaona kikamilifu udhihirisho wa tabia ya Mungu katika Kristo, na tabia ya shetani katika wanadamu. Kwa kujitoa mwenyewe kufa, Bwana wetu Yesu Kristo alimshinda yeye ambaye alimchukia tangia mwanzo wa pambano. Kwa kunena kuhusu shetani, Yesu aliwwaambia Mafarisayo:

> Ninyi ni watoto wa baba yenu Ibilisi, nanyi mnataka kutimiza matakwa ya baba yenu. **Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo,** wala hakushikana na kweli maana hamna kweli ndani yake. Asemapo uongo husema yaliyo yake mwenyewe **kwa maana yeye ni mwongo na baba wa huo uongo.** Yohana 8:44

Kupitia kukamatwa kwa Yesu usiku, na kinyago cha kujaribiwa kwake na washahidi wa kutatanisha waliosimama kumshtaki Kristo, tunaona udanganyifu, roho ya uongo ya shetani. Katika kumkejeli na kumpiga tunaona ukatili wake na unyama. Katika kumsulubisha tunaona kukithiri kwa ukatili wake. Kupitia kwa kifo Yesu alimshinda shetani. Kama maandiko yanavyotwambia:

> Basi kwa kuwa watoto wana nyama na damu, Yeye pia alishiriki katika ubinadamu wao, **ili kwa kifo chake, apate kumwangamiza huyo mwenye nguvu za mauti**, yaani, Shetani, Waebrania 2:14

Bibilia inatufundisha kuwa shetani anazonguvu za mauti. Hili linazua swali muhimu katika kuelewa tabia ya Mungu. Inawezekanaje shetani awe na nguvu za mauti ilihali ni Mungu aliyewaambia Adamu na Hawa:

> Walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika. Mwanzo. 2:17

Kwani, Mungu alitishia kuwaua Adamu na Hawa iwapo watakula tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya? Bibilia inaweka wazi kile kinachoua wadhambi.

> Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti… Romans 6:23

> Uovu utamwua asiye haki, Nao wamchukiao mwenye haki watahukumiwa. Zaburi 34:21

> Bali anikosaye hujidhuru nafsi yake mwenyewe, Na wao wanichukiao hupenda mauti. Methali 8:36

Mauti ni tokeo la dhambi. Ni hatia ya kutenda kwa ubinafsi, ukatili na namna ya kuchukia dhidi ya Baba yetu wa upendo aliye mbinguni ambaye atawaua wenye dhambi. Bibilia inatwambia kuwa Yesu hana uzima tu, bali yeye ni uzima.

> Yesu akawaambia, "**Mimi ndimi** njia na kweli na **uzima**. Mtu hawezi kuja kwa Baba isipokuwa kwa kupitia Kwangu. John 14:6

> Yesu akamwambia, "**Mimi ndiye huo ufufuo na uzima**. Yeye aniaminiye Mimi, hata akifa atakuwa anaishi Yohana 11:25

> Tunawajulisha lile lilokuwako tangu mwanzo, lile tulilosikia,ambalo tumeliona kwa macho yetu, ambalo tumelitazama na kuligusa kwa mikono yetu, kuhusu Neno la Uzima, (2) **Uzima huo ulidhihirishwa**, nasi tumeuona na kuushuhudia, nasi **twawatangazieni uzima wa milele**, ambao ulikuwa pamoja na Baba, nao ukadhihirishwa kwetu. 1 yohana 1:1-2

Tunahitaji tuwe makini sana kwa maneno ya Yesu. Hana *uzima tu*, bali yeye *ni* uzima. Iwapo Yesu ni uzima hawezi kuwa na uhusiano na mauti. Kama Yesu ni uzima basi haiwezekani *asababishe* mauti. Wacha tuzingatie kwa makini jinsi Yesu anaeleza hili:

> Mwivi huja ili aibe, kuua na kuangamiza. **Mimi nimekuja ili wapate uzima** kisha wawe nao tele. Yohana 10:10

Mwivi ndiye auwae, bali Yesu ndiye apeanae uzima. Kama Yesu alisababisha kifo kwa wale walioasi sheria za Baba yake, basi Kristo anaguvu zote, za uzima na mauti. Kwa hili tunamaanisha kuwa uzima na mauti huendelea kutoka kwake. Lakini hili ni pingamizi kabisa, na ndio maana Bibilia inatwambia kuwa shetani ana nguvu za mauti. Shetani hangekuwa na nguvu za mauti kama Kristo alitumia nguvu zake kuwaua watu. Hili lingemaanisha kuwa Kristo angekuwa na nguvu za mauti. Lakini Bibilia inasema wazi kuwa shetani anazo nguvu za mauti. Mauti pia yanalinganishwa na giza moja kwa moja:

> Kabla sijaenda huko ambako sitarudi kutoka huko tena, Ni hiyo nchi ya giza, giza tupu; Ayubu 10:21

> Waliokaa katika giza na uvuli wa mauti, Wamefungwa katika taabu na chuma, Zaburi 107:10

Kinyume chake, tunasoma kuhusu Kristo:

> Ndani Yake ndimo ulimokuwa uzima na huo uzima ulikuwa nuru ya watu. Yohana 1:4

Tunaambiwa ndani ya Kristo mlikuwamo uzima. Haisemi uzima na mauti. Uzima huu ulio na Kristo ni nuru ya watu. Hivyo nuru na uzima zimefungwa pamoja, na ndivyo ilivyo giza na mauti. Ujumbe ambao Yesu alikuja kuutangaza ulimwenguni ni huu:

> Huu ndio ujumbe tuliosikia kutoka Kwake na kuwatangazia ninyi, kwamba **Mungu ni nuru na ndani yake hamna giza lo lote**. 1 Yohana 1:5

Hakuna giza kwa Mungu kumaanisha hakuna mauti katika yeye, na hilo linatuongoza kimaantiki kuhitimisha kuwa Mungu sio mwanzilishi wa kifo; wala yeye hana nguvu za mauti. Kile anachoweza kukifanya ni kuwapa watu uhuru wa kujiangamiza wenyewe iwapo watachagua. Bibilia inaita mauti adui, Kumaanisha yanatoka *kwa* adui.

> Adui wa mwisho atakayeangamizwa ni mauti. 1 Wakorintho 15:26

Kifo ni adui na ndio maana Kristo tayari amebatilisha mauti.

> Ambaye alituokoa na kutuita katika mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu mema bali kwa sababu ya kusudi Lake mwenyewe na neema Yake. Neema hii tulipewa katika Kristo Yesu kabla ya kuwako kwa ulimwengu. (10) Lakini sasa imefunuliwa kwa kudhihirishwa Kwake Mwokozi wetu, Kristo Yesu, **ambaye amebatilisha mauti** na kuleta uzima na kutokufa kwa njia ya Injili. 2 Timotheo 1:9-10

Katika Kristo hakuna kifo ndio maana Yesu alimwambia Martha:

> Na ye yote aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele. Je, unasadiki haya?" Yohana 11:26

Inawezekanaje mtu anayeamini ndani ya Yesu asikufe? Watu hufa kila wakati. Zingatia jinsi Yesu alivyokirejelea kifo:

> Baada ya kusema haya, Yesu akawaambia, "**Rafiki yetu Lazaro amelala**, lakini nakwenda kumwamsha." Yohana 11:11

> Akawaambia, "Ondokeni! **Kwa maana binti huyu hakufa, bali amelala**." Wakamcheka kwa dhihaka. Mathayo 9:24

Kuna mtu mmoja tu katika historia ambaye amekufa kulingana na kijelizi hiki.

> Lakini twamwona Yesu, aliyefanywa chini kidogo kuliko malaika, sasa akiwa amevikwa taji ya utukufu na heshima kwa sababu alistahimili mauti, ili kwamba kwa neema ya Mungu apate **kuonja mauti kwa ajili ya kila mtu**. Waebrania 2:9

Kama kila mtu aliye kaburini sasa hivi ameonja mauti yeye mwenyewe, kungekuwa na kusudi gani la Yesu kuonja mauti kwa kila mtu isipokuwa alikufa yale mauti ya mwisho ya kutenganisha ambayo waovu watayashuhudia wakati wa mwisho wa miaka 1000?

Yesu ndiye mtu tu ambaye kweli alikufa. Wengine ambao waliishi wanalala makaburini. Kila mmoja atafufuliwa apate uzima wa milele au kwenye mauti ya pili, au mara ya pili kifo kitokeacho katika historia ya ulimwengu. Yesu alipolia " mikononi mwaka naiweka Roho yangu." Hali akizibeba thambi za ulimwengu mzima, alivunja nguvu za mauti. Alibatilisha kabisa haja ya mtu yeyote kufa. Hivyo kwa wakati huu wa sasa Bibilia inatwambia kuwa tayari mauti yamebatilishwa. Sababu pekee ambayo watu watakufa katika mwisho wa wakati ni kuwa wamekataa kukubali uzima ambao unapatikana ndani ya Kristo. Hauwezi batilisha mauti kasha baadaye usababishe mauti. Hili haliwezekani kabisa.

Katika wakati ambao waovu hatimaye wameangamizwa Bibilia inasema:

> Kisha Mauti na Kuzimu zikatupwa katika ziwa la moto. Hii ndio Mauti ya pili, yaani, hilo ziwa la moto. Ufunuo 20:14

Mara nyingi inaonyeshwa kuwa ziwa la moto ni kuzimu, lakini Bibilia inatwambia kuwa kuzimu kunatupwa katika ziwa la moto pamoja na mauti. Ziwa la moto ni nini? Ni sawa kabisa na mateso ambayo Kristo Yesu aliyapitia msalabani. Mungu wetu ni moto ulao. Waebrania 12:29. Usafi wa tabia yake

na kufia nafsi kwa upendo wake kunapodhihirishwa kwa wadhambi huwaonyesha hatia ya ajabu ya ubinafsi wao. Nuru huchoma katika giza na kwa sababu waovu hukataa kukubali rehema, kama Kaini wote hulia " Dhambi zangu ni nyingi haziwezi chukulika" na wanavunjwa na hatia yao wenyewe. Hivyo basi maovu huwaua waovu na na mshahara wa dhambi ni mauti. Zaburi 34:21, Warumi 6:23.

Kama Mungu na Mwanawe wanauwa watu basi wako na mauti katika Roho wao. Kama hili lingekuwa kweli basi mauti hayangeangamizwa na hayangezingatiwa kama adui. Pia tunahitaji kuainisha kuwa Kristo hana uzima wa milele tu, Yeye ni uzima wa milele. Hauwezi kuwa uzima wa milele na uwe na tabia ya mauti wakati mmoja, haiwezekani tu!

> Je, chemchemi yaweza kutoa katika tundu moja maji matamu na maji ya chumvi? Yakobo 3:11

Tunaangazia hoja nyingine muhimu juu ya swali hili.

> Nasi sote, tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji tunaakisi utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo. **Nasi tunabadilishwa ili tufanane naye,** toka utukufu hadi utukufu mkuu zaidi, utokao kwa Bwana, ambaye ndiye Roho. 2 Wakorintho 3:18

Tunapotazama utukufu au tabia ya Mungu tutabadilishwa katika sura sawa. Kwa vile Mungu na Mwanawe ni uzima, kuwatazama na kuwajua humaanisha tutakuwa na uzima

> Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma. Yohana 17:3

Hili humaanisha iwapo tutasoma hadithi za Agano la Kale za Bibilia kuamini kuwa Mungu huwaua watu, basi kwa kutazama hili kama tabia ya Mungu, itakuwa sehemu ya tabia yetu. Sasa fikiria hili kwa mtaamo mwingine. Bibilia inatwambia:

> Kwao, Mungu amechagua kujulisha miongoni mwa watu Mataifa utukufu wa utajiri wa siri hii, ambayo ni **Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu.** Wakolosai 1:27

> Nimesulibiwa pamoja na Kristo, wala si mimi tena ninayeishi bali **Kristo ndiye aishiye ndani yangu**. Uhai nilio nao sasa katika

> mwili, ninaishi kwa imani ya Mwana wa Mungu, aliyenipenda na kujitoa kwa ajili yangu. Wagalatia 2:20

Kama Kristo anaishi ndani yako katika Roho yake na unaamini kuwa Kristo huwaua watu kama sehemu ya tabia yake, basi utakuwa na roho ya muuaji ndani yako. Lakini kwa sababu Yesu ni uzima wa milele haiwezekani kuwa na Kristo na roho wa muuaji wakiishi ndani yako kwa wakati mmoja.

Hii ni moja ya sababu mbona watu hufa; ni kwa sababu wanamwabudu Mungu ambaye huwaua watu. Iwapo utaamini kuwa mkono wa Mungu umebadilika katika mauti ya mamia ya maelfu ya watu na atawauwa mabilioni ya watu katika siku za usoni basi nuru ya tabia ya Mungu humezwa na mauti, na mauti hueleweka kuwa yanatawala juu ya kiti cha enzi cha ulimwengu. Kama utamwabudu Mungu kama huyu na unatazama Mungu kama huyu siku baada ya siku, ibada ya jinsi hii itakuuwa. Mbona? Kwa kutazama tunabadilishwa na kuwa na sura sawa. 2 Wakorintho 3:18.

Njia pekee ya Mungu kuangamiza mauti ilikuwa kudhihirisha kwa watu kilichokuwa mioyoni mwao kwa Mwana wa Mungu. Yesu alipokuja duniani chuki asili iliyokuwepo ndani ya watu wote kwa Kristo ilidhihirishwa. Kwenye msalaba tunaona jinsi shetani anaweza kuiingiza mioyo ya watu kwa ukatili na mauaji kwa urahisi. Kupitia kwa kifo cha msalaba Kristo alidhihirisha tabia ya shetani na kuupa ulimwengu fursa ya kuona jinsi uovu wa jamii ya mwanadamu ulivyo kwa kweli. Tunapoutazama kwenye msalaba tunakabiliwa na ubinadamu, na kupitia kwa Roho wa Kristo tunapewa uwezo wa kupokea Kujikana nafsi, upendo, roho ya upole.

> Jifungeni nira yangu, mjifunze kutoka kwangu, kwa maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Mathayo 11:29

Yesu ni mpole na mnyenyekevu. Yesu anawapenda adui zake. Yesu huwaombea wale wanaomchukia, na humwagiza Baba awasamehe wale wanaomtesa. Hii ni Roho ya kupeana uzima. Huu ni uzima milele.

Lakini vipi kuhusu mafungu katika Bibilia ambayo huonekana kutuambia kuwa Mungu huwauwa watu? Tukumbuke kusoma agano la kale kwa kuongozwa na nuru ya maisha ya Kristo. Kusoma Bibilia nje ya maisha ya Kristo kwa kweli kutaleta mauti. Sababu ya hili, kama tulivyoainisha, ni iwapo utamwabudu Mungu auwae watu basi unamwabudu Mungu wa mauti, na

kwa kutazama hili utakufa. Huu ndio mfano unaopatikana katika amri kwa Waisraeli wasipande juu ya Mlima Sinai.

> Nawe utawawekea mipaka watu hawa pande zote, ukisema, Jihadharini, msipande mlima huu, wala msiuguse, hata mapambizo yake; kila mtu atakayeugusa mlima huu, bila shaka atauawa. (13) Mkono wa mtu awaye yote usimguse mtu huyo, **ila hakika yake atapigwa kwa mawe, au kupigwa kwa mkuki;** kwamba ni mnyama au kwamba ni mwanadamu, hataishi. Hapo panda itakapotoa sauti kwa kufuliza ndipo watakapoukaribia mlima. Kutoka 19:12-13

Ni kupitia kwa mjumbe tu ndio wangeweza kuzungumza na Mungu. Musa aliwakilisha Kristo kama mpatanishi wetu. Musa angepanda mlimani bila kufa kwa sababu aliielewa tabia ya Mungu. Alipoteremka kutoka mlimani uso wake uling'aa kwa utukufu wa Mungu au tabia. Iwapo tutasoma Agano la Kale bila kuwa na maisha ya Kristo kama mpatanishi basi tutazidiwa au "kujazwa" na mawazo ya uongo kuhusu Mungu na hilo hatimaye litatuua.

> Fahamu sasa ya kuwa Mimi, naam, Mimi ndiye, Wala hapana Mungu mwingine ila Mimi; Naua Mimi, nahuisha Mimi, Nimejeruhi, tena naponya; Wala hapana awezaye kuokoa katika mkono wangu, Kumbukumbu 32:39

Bila kuangazia maisha ya Kristo tutasoma hili kama:

> Naua baadhi ya watu na wengi nahuisha.

Tukijua kuwa Yesu hakuua yeyote alipokuwa duniani tunahimizwa kuendelea kuchunguza ili kuelewa hili lina maana gani. Kwanza tunagundua jinsi kuua na kuhuisha zimeunganishwa pamoja:

> Naua mimi, nahuisha mimi;

Neno kuua limeunganishwa na neno kuhuisha moja kwa moja. Basi tendo la kuua linafuatwa na kuhuisha. Kidokezo kingine kinapatikana katika sehemu ya fungu inayofuata:

> Naua mimi, nahuisha mimi;
> Nimejeruhi, tena naponya:

Hili ni umbo la kawaida katika maandishi ya Kiebrania. Unaitwa usambamba. Sehemu ya kwanza na sehemu ya pili zinaonyesha wazo sawa lakini kwa njia tofauti ili kupeana sura wazi ya maana ya kile kinachozungumziwa. Kanuni ya kujeruhi na kuponya inahusishwa na kazi ya injili moja kwa moja. Ili kuzaliwa upya lazima tufie maisha yetu ya kale. Ili kuponywa lazima tujeruhiwe na sheria ambayo hudhihirisha dhambi zetu kwetu. Hakuwezi kuwa na kufufuliwa katika upya wa maisha bila kufia maisha ya kale. Paulo anatuonyesha maana ya Kumbukumbu 32:39. Anaposema:

> … kwa kuwa andiko huua bali Roho hutia uzima. 2 Wakorinth 3:6

Mungu huua utu wa zamani kupitia kwa sheria lakini humfanya mtu mpya kuwa hai kupitia kwa Roho. Hivyo ujumbe huu wa Musa katika Kumbukumbu 32:39 unarejelea injili ya kazi ya Roho wa Mungu kutuokoa ili kwamba hakuna yeyote awezaye kututoa mikononi mwake.

Iwapo tutatafuta katika Bibilia mifano mingine ya mahali mpangilio huu wa maneno ya Kiebrania yanatokea tunapata mahali pengine ambapo panaelezea kirai hiki " Naua mimi, nahuisha mimi."

> Bwana huua, naye hufanya kuwa hai; Hushusha hata kuzimu, tena huleta juu. 1 Samweli 2:6

Sehemu ya kwanza ya fungu ina elezewa mara ya pili, lakini kwa njia nyingine ya kuelezea maana. Matumizi ya koloni katika tafsiri ya "king James" pia inatwambia kuwa kile ambacho kinatokea baada ya koloni ni maeleze ya yale ambayo tayari yamekwisha tolewa.

Bwana huua, naye hufanya kuwa hai: Hushusha hata kuzimu, tena huleta juu.

Basi neno hili linarejelea nguvu za kufufuka za Kristo ambaye ni ufufuo na uzima na sio mwanzilishi wa mauti. Fungu hili ni ombi la furaha la Hanna aliposhinda. Anaendelea:

> Bwana hufukarisha mtu, naye hutajirisha; Hushusha chini, tena huinua juu. (8) Humwinua mnyonge kutoka mavumbini, Humpandisha mhitaji kutoka jaani, Ili awaketishe pamoja na wakuu, Wakakirithi kiti cha enzi cha utukufu; Kwa maana nguzo za dunia zina Bwana, Naye ameuweka ulimwengu juu yake. 1 Samweli 2:7-8

Kila wakati muktadha wa kitendo cha kwanza unafuatwa na kitendo cha pili. Hanna alikuwa amedunishwa kwa sababu hakuwa na uwezo wa kupata mtoto akiwa bado anachekwa na mke mwingine aliyekuwa anapata watoto. Hali hii iliua tabia yake ya kale, lakini kwa vile aliamini ndani ya Bwana na mtoto wa ahadi akazaliwa, alifanywa hai tena. Alikuwa masikini wa kiroho, lakini sasa alikuwa tajiri. Ayubu pia anazungumzia hili.

> Mtu **akif**a, je! Atakuwa **hai** tena? Mimi ningengoja siku zote za vita vyangu, Hata kufunguliwa kwangu kunifikilie. Ayubu 14:14

Ayubu anazungumza kuhusu ufufuo akitumia maneno hayo mawili ya kiebrania yanayopatikana katika Kumbukumbu 32:39. Naamani anapokuja kwa mfalme wa Israeli kuomba uponyaji, mfalme alitumia usemi huu kutoka Kumbukumbu 32:39.

> Ikawa, mfalme wa Israeli alipousoma waraka, alirarua mavazi yake, akasema, Je! Mimi ni Mungu, niue na kuhuisha, hata mtu huyu akanipelekea mtu nimponye ukoma wake? Fahamuni, basi, nakusihini, mwone ya kuwa mtu huyu anataka kugombana nami. 2 Wafalme 5:7

Naami alikuwa chini ya kifo kwa sababu ya ukoma wake. Mfalme wa Israeli alishangaa katika athari, “Je mtu huyu anafikiria naweza wafufua watu katika mauti?!”

Hivyo tunapotumia kanuni ya kusoma Agano la Kale kupitia kwa mwanga wa maisha ya Yesu na kutumia sheria za Miller za kutafuta katika Bibilia mahali ambapo kirai sawa kinatumika, basi Bibilia itatudhihirishia kile inamaanisha. Musa alipoandika “huua mimi, nahuisha mimi” Kristo alikuwa anamwambia Musa kuwa yeye ni ufufuo na uzima! Ufunuo wa injili sawa unapatikana katika Agano Jipya. Tunapojua ukweli huu, hakuna chochote kinaweza tuondoa mikononi mwa Baba yetu aliye mbinguni. Hii ndio namna unasoma kifungu hiki, ama bado unasoma hili kama Mungu anakwambia, Naua baadhi ya watu na wengine naokoa. Unasomaje?

> Angalia, nimekuwekea leo mbele yako uzima na mema, na mauti na mabaya; Kumbukumbu 30:15

Ni jinsi gani inavyopendeza kujua Yesu ni uzima wa milele. Ni jambo la kupendeza jinsi gani kujua kuwa Mungu ni uzima wa milele. Ni mpaji wa uzima na mhuishaji, na kama tujuavyo yeye ni sura halisi ya Baba. Hakuna

giza wala mauti katika Baba. Yesu anadhihirisha hili kwetu akiwa duniani kwa sababu hakuua yeyote na alitunza amri zote za Baba yake. Basi unamwabudu nani?

Kama Mungu unayemtumikia ana roho ya mauti ndani yake basi sio Mungu wa Yesu Kristo kama anavyo funuliwa katika injili. Ndani ya shetani kuna mauti na maovu, na ndani ya Kristo ni uzima na mema. Chagua hivi leo ni nani utakayemtumikia.

> Mtu ye yote aliyeniona Mimi, amemwona Baba. Yohana 14:9

Basi unamwabudu nani? Ni juu yako kabisa.

## 15. Amri za Baba Yangu

Kitabu cha Zaburi hutunenea kuhusu upendo wa Kristo kwa Amri za Baba yake. Kabla ya Mkombozi kuja ulimwenguni alisema:

> Ndipo niliposema, Tazama nimekuja, (Katika gombo la chuo nimeandikiwa,) (8) Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu. Zaburi 40:7-8

Mwana wa Mungu anatuonyesha kwa njia ya kiungu juu ya sheria za Baba yake. Upendo wake kwa amri na mfano wake wa kila siku akiwa hapa ulimwenguni vyote vinatuonyesha jinsi sheria inavyoonekana katika rangi yake mahiri. Zaidi ya hili, maisha ya Yesu sio onyesho la sheria za Baba yake tu, mbali ni maisha yale ambayo huishi ndani ya mioyo ya wale wanaomtumikia.

> Sheria ya mwenye akili ni chemchemi ya uzima, Ili kuepukana na tanzi za mauti. Methali 13:14

Yesu ni hekima ya Mungu (1 Wakorintho 1:24) na mwanzo wa hekima ni heshima ya ndani na upendo wake kwa Baba na amri zake.

> Kumcha Bwana ni mwanzo wa hekima; Na kumjua Mtakatifu ni ufahamu. Methali 9:10

> Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe uzishike *amri* zake, Maana kwa jumla ndiyo *impasayo mtu*. Mhubiri12:13

Njia pekee ya kumwogopa au kumheshimu Mungu na kuzitunza amri zake ni kuwa na roho ya Mwana wa Mungu ndani yetu. Yeye ndiye chemchemi ya wale wote wanaozitunza amri za Baba. Wale wote walio na imani ya Kristo wanapokea uwezo wa kuzitunza amri kupitia kwa roho. Hapana uwezekano wa kuitunza sheria ya Mungu pasipokuwa na roho ya Kristo.

> Lakini sasa, haki itokayo kwa Mungu imedhihirishwa pasipo sheria, ambayo Torati na Manabii wanaishuhudia. (22) Haki hii itokayo kwa Mungu hupatikana kwa Yesu Kristo kwa wote wamwaminio. Kwa maana hapo hakuna tofauti, Warumi 3:21-22

Paulo anatwambia kwamba kuhesabiwa haki kumewekwa wazi kwa yesu kristo na tumepewa bure pasi na kuwa na haja kwetu kumridhisha Mungu kupitia kwa jitihada zetu. Tumepewa kila kitu kwa njia ya imani.

> Lakini tunajua ya kwamba mtu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria bali kwa njia ya imani katika Yesu Kristo. **Nasi tumemwamini Kristo Yesu ili tupate kuhesabiwa haki kwa njia ya imani katika Kristo, wala si kwa matendo ya sheria.** Wagalatia 2:16

Tunapokubali kwamba hakika yesu ni mwana wa Mungu na kuliamini jina lake, basi tunapokea imani yake kwa Baba na kutunza kwake kwote kwa sheria. Ni zawadi ya kupendeza jinsi gani tunapokea kwa Kristo! Uwezo wa kuitunza sheria unapatikana bure kupitia kwa karama ya Roho.

> Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, (23) upole, kiasi. Katika mambo **kama haya hakuna sheria.** Wagalatia 5:22-23

Kupitia kwa mwongozo wa roho ya Kristo tunasoma Zaburi jinsi Mwana wa Mungu alinena kuhusu sheria za Mungu.

> Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki; Wala hakusimama katika njia ya wakosaji; Wala hakuketi barazani pa wenye mizaha. (2) **Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, Na sheria yake huitafakari mchana na usiku.** (3) **Naye atakuwa kama mti uliopandwa Kandokando ya vijito vya maji**,

> Uzaao matunda yake kwa majira yake, Wala jani lake halinyauki; Na kila alitendalo litafanikiwa. Zaburi 1:1-3

Kupitia kwa roho ya Kristo, sheria ni chemichemi yenye nguvu ya maji ya uzima. Huu ndio mfano unaoonyeshwa kupitia kwa maji yaliyobubujika kutoka kwa mwamba uliogongwa.

> Tazama, nitasimama mbele yako huko, juu ya lile jabali katika Horebu; nawe utalipiga jabali, na maji yatatoka, watu wapate kunywa. Musa akafanya hivyo mbele ya wazee wa Israeli. Kutoka 17:6

Horebu ni mahali sawa na Mlima Sinai. Basi maji yalikuwa yakitiririka kutoka mahali sawa na pale ambapo sheria ilitolewa. Hivyo basi kwa Kristo sheria sio agano lililokufa bali ukweli unaoishi. Tunapompokea kristo basi tunapokea hisia ifuatayo kwa karama ya roho yake.

> Sheria yako naipenda mno ajabu, Ndiyo kutafakari kwangu mchana kutwa. Zaburi 119:97

Ujumbe huu ni kutoka kwa sura ndefu zaidi ya Bibilia, Sura ambayo inahusu jinsi sheria ni ya kupendeza. Mwana wa Mungu anaipenda sheria kwa sababu anampenda Baba yake. Unapolinganisha maelezo kuhusu sheria na sifa na tabia za Mungu unapata kwamba zote ni sawa kabisa.

| **Tabia/sifa za Mungu** | | **Sheria ya Mungu** | |
|---|---|---|---|
| 1. Roho | Yohana 4:24 | 1. Kiroho | Warumi 7:14 |
| 2. Upendo | 1 Yohana 4:8 | 2. Pendo | Matt. 22:37-40 |
| 3. Mkweli | Yohana 14:6 | 3. Kweli | Zaburi 119:142 |
| 4. Mwadilifu | 1 kor. 1:30 | 4. Adilifu | Zaburi 119:144,172 |
| 5. Mtakatifu | Isa. 6:3 | 5. Takatifu | Zaburi 7:12 |
| 6. Mkamilifu | Matt 5:48 | 6. Kamilifu | Zaburi 19:7 |
| 7. Mwema | Luka 18:19 | 7. Njema | Warumi 7:12 |
| 8. Mwenye haki | Kumb. 32:4 | 8. Haki | Warumi 7:12 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 9. Msafi | 1 John 3:3 | 9. Safi | Zaburi 19:8 |
| 10. Habadiliki | Yakobo 1:17 | 10. Haibadiliki | Matt. 5:18 |
| 11. Huishi milele | Zab. 90:2 | 11. Huishi milele | Zaburi 111:7,8 |
| 12. Ni njia | Yohana 14:6 | 12. Ni njia | Malaki 2:7-9 |
| 13. Mkuu | Zab. 48:1 | 13. Kuu | Hosea 8:12 |
| 14. Hutakasa | Matt. 8:3 | 14. Imetakaswa | Ezekieli 22:26 |

Tukizijuchunguzu amri tunagundua ya kwamba zote zinahusu kuhifadhi uhusiano; Uhusiano wetu na Mungu na uhusiano wetu na watu wengine.

| **Tabia/sifa za Mungu** | |
|---|---|
| 1. Nilikutoa katika nchi ya utumwa. Usiwe na miungu mingine ila mimi | Mkombozi, Mungu pekee, *mahusiano* |
| 2. Usijifanyie sanamu ya kuchongwa | Hauwezi kuwa na uhusiano na mbao, Au wazo la uongo |
| 3. Usilitaje jina la Mungu bure | uadilifu, uwazi, *mahusiano* |
| 4. Ikumbuke Sabato kwa kuwa siku sita Mungu alizifanya mbingu na nchi | Muumbaji, mwanzilishi wa maisha, *mahusiano* |
| 5. Waheshimu Baba na mama yako | Familia/*kuangazia mahusiano*, malezi |
| 6. Usiue | Uhai ni thamani, *uhusiano ni wa milele,* Mimi ndiye mwanzo wa maisha |
| 7. Usizini | Uhusiano halali wa karibu ni wa milele |
| 8. Usiibe | Kiroho/*mahusiano,* pasi kutazamia mali |
| 9. Usishuhudie uongo | Uadilifu, uwazi, *mahusiano* |
| 10. Usitamani mali ya mtu mwingine | Muumbaji, mwanzilishi wa maisha, *mahusiano* |

1. Amri ya kwanza inatwambia kwamba Mungu aliwatoa wana wa Israeli kutoka kwenye nchi ya utumwa ya Misri, hili linatwambia kwamba Mungu ni mkombozi. Anaponiagiza nisiwe na miungu mingine ila yeye, inanifahamisha kwamba anataka awe na urafiki wa karibu nami.

2. Amri ya pili inaniambia kwamba Mungu anataka uhusiano wa moyo-kwa-moyo. Ibada ya sanamu sio ibada ya moyo-kwa-moyo. Wala ibada ya sanamu sio ibada ya kiroho, kumaanisha kuunganika kwa roho na roho, akili na akili. Miungu ni upingamizi; ni kuanganika na kitu kisichokuwa na uhai na/au wazo ambalo si la kweli.
3. Amri ya tatu inanifahamisha kwamba Mungu yuko wazi katika *mahusiano* yake. Tunapoingia katika uhusiano naye, hataki tujifanye katika *uhusiano* na basi kuonekana kuwa hauna maana au ni bure.
4. Amri ya nne ni ya kipekee zaidi kwa sababu,inatwambia kwamba mungu ndiye chemchemi ya uzima, na kwamba aliumba kila kituAmri hii athari kubwa katika mtazamo wetu kwake na kwa kiwango kikubwa huathiri namna yetu kwake. Ni muhimu kutambua kwamba amri juu ya sabato inamaneno mengi kuliko ya amri yoyote ile.
5. Amri ya tano ni ya kipekee kwa sababu inanielezea jinsi maisha ya Mungu yanavyotiririka kupitia njia za ulimwengu. Amri hii inatupa ahadi ya maisha marefu tukiwaheshimu wazazi wetu. Inaonyesha hasa kwamba wazazi wetu hudhihirisha kitu cha kipekee sana kwetu kuhusu Mungu na basi kwa kuwaheshimu, tunamheshimu Mungu.
6. Amri ya sita inatuonyesha kwamba Mungu huyaona maisha kama kitu cha thamani. hutwambia kwamba Mungu anataka *mahusiano* yaishi milele.
7. Amri ya saba inatwambia kwamba mahusiano mengine ni hatari na kwa Mungu, ni kuonyesha amri ya kwanza usiwe na miungu mingine. Ni ya ukumbusho kwamba mungu ndiye mwanzilishi wa maisha yetu.
8. Amri ya nane inatufahamisha kwamba Mungu atatutimizia mahitaji yetu, na kwamba atatulinda. Pia inatufahamisha kuwa Mungu havutiwi na mali, ila *mahusiano* yetu.
9. Amri ya tisa inaakisi amri ya tatu. Mungu anataka uwazi na uadilifu katika *mahusiano*. Shahidi wa uongo huharibu utambulisho wa mmoja au hata pande zote na huharibu mawasiliano.
10. Amri ya kumi kwa kumzingatia Mungu, hutukumbusha kwamba yeye ndiye chechemi ya uzima. Hatutapungukiwa na chochote tukiamini hivyo. Pia hutwambia tena kuhusu *uhusiano wa kiroho na* akili za Mungu. Amri ya 5-9 zote zinaweza onekana na kuonyeshwa, lakini amri hizi ni jambo la moyoni. Haziwezi kuonekana. Hivyo basi amri hizi ni muhimu katika kuelewa jinsi ufalme wa mungu ulivyo. Hivyo kwa kifupi amri kumi zinatwambia kuwa Mungu ni:

1. Ni Chemchemi ya uzima
2. Ndiye muumbaji
3. Ni Mkombozi wetu
4. Anataka *mahusiano* ya moyo-kwa-moyo
5. Anatujali kama baba na anatupa mahitaji yetu ya kila siku.

Kwenye waraka wake wa kwanza, Yohana anatwambia kuwa Mungu ni upendo, na sheria kama kiakisi cha tabia zake pia ni upendo:

> Mtu ye yote asemaye kuwa, "Ninamjua" lakini hazishiki amri Zake, ni mwongo, wala ndani ya mtu huyo hamna kweli. (5) Lakini kama mtu ye yote analitii Neno Lake, upendo wa Mungu umekamilika ndani yake kweli kweli .Katika hili twajua kuwa tumo ndani yake. 1 Yohana 2:4-5

Yesu aliionyesha kwa njia hii:

> "Kama vile Baba alivyonipenda Mimi, hivyo ndivyo Mimi nilivyowapenda ninyi. Basi kaeni katika pendo Langu. (10)**Mkizishika amri Zangu mtakaa katika pendo Langu, kama Mimi nilivyozishika amri za Baba Yangu na kukaa katika pendo Lake.** (11) Nimewaambia mambo haya ili furaha Yangu iwe ndani yenu na furaha yenu iwe kamili. (12) **Amri Yangu ndiyo hii: Mpendane kama Mimi nilivyowapenda ninyi.** Yohana 15:9-12

Yesu:

- Hana miungu mingine kando na Baba kwa sababu anampenda Baba yake.
- Haabudu miungu mingine wala kujitengenezea mifano kwa sababu anampenda Baba yake.
- Halitaji jina lake wala tabia yake bure kwa sababu anaakisi tabia ya Baba kikamilifu.
- Hufarahia kushiriki katika sabato na Baba yake.
- Anamheshimu Baba yake.
- Haui kwa sababu yeye ni ufufuo na uzima.
  Hazini kwa sababu haiingi katika uhusiano ambao sio halali kwake.
- Haibi kwa sababu anaamini katika urithi aliopewa na baba yake.

- Hadanganyi kwa sababu udanganyifu huaribu uadilifu wa mahusiano.
- Hatamani kwa sababu anakaa katika masharti ya Baba yake.

Watu wengi hawatakuwa na swali juu ya amri tisa ya hizi kumi. Shida ya wengi iko katika amri ya sita – usiue. Tutafanya nini na hadithi kama Yoshua kukutana na amiri wa jeshi la Bwana?

> Ikawa hapo Yoshua alipokuwa karibu na mji wa Yeriko, akavua macho yake na kuangalia, na tazama, mtu mume akasimama kumkabili mbele yake, naye alikuwa na upanga wazi mkononi mwake; Yoshua akamwendea, na kumwambia, Je! Wewe u upande wetu, au upande wa adui zetu? (14) Akasema, La, lakini nimekuja sasa, nili amiri wa jeshi la Bwana. Yoshua akapomoka kiusouso hata nchi, naye akasujudu, akamwuliza, Bwana wangu aniambia nini mimi mtumishi wake? Yoshua 5:13-14

Yoshua alipokuwa akiwaua wakazi wa Kanani kwa wengi inaonekana kana kwamba vitendo hivi vilihimizwa na kuongozwa na Mwana wa Mungu ambaye Yoshua aliinamia na kumwabudu. Hadithi kama ya kuangamizwa kwa jeshi la Waashuri huwekwa mbele kama thibitisho kwamba kweli Mwana wa Mungu huua watu ili kuweza kuhifadhi wateule wake.

> Ikawa usiku uo huo malaika wa Bwana alitoka, akakiingia kituo cha Waashuri, akawapiga watu mia na themanini na tano elfu. Na watu walipoondoka asubuhi na mapema, kumbe! Hao walikuwa maiti wote pia. 2 Wafalme 19:35

Ukweli uliopo mbele yetu ni kwamba Yesu alipokuja ulimwenguni na kuishi kati yetu hakuua mtu yeyote. Tulianza mafunzo na wazo kuwa maisha ya Yesu Kristo hapa ulimwenguni yamejaa ufunuo wa Baba. Kama Yesu alivyo mwambia Philipo:

> Yesu akamjibu, "Filipo, nimekaa nanyi muda huu wote hata usinijue? Mtu ye yote aliyeniona Mimi, amemwona Baba. Sasa wawezaje kusema, 'Tuonyeshe Baba?' Yohana 14:9

Yesu alimwambia Philipo kwamba alikuwa akionyesha tabia zote za Baba yake kwa wanafunzi wake:

> **"Nimewajulisha Jina Lako wale ulionipa kutoka katika ulimwengu.** Walikuwa Wako, ukanipa Mimi, nao wamelitii Neno Lako. Yohana 17:6

Katika maandiko jina humaanisha tabia na Yesu anaonyeshwa kuwa alionyesha tabia hizi kwa wanafunzi – wale aliopewa kutoka ulimwenguni;

> **Nimekutukuza Wewe duniani** kwa kuitimiza ile kazi uliyonipa niifanye. Yohana 17:4

Yesu ni mng'ao wa utukufu wa Baba (Waebrania 1:3) na utukufu wake au tabia ameionesha duniani. Hilo linamaanisha kuwa maisha ya Yesu duniani ni kielelezo kamili cha Amri Kumi ambazo ni nakala ya tabia za Mungu. Hakuua yeyote alipokuwa duniani na hili linajumuishwa katika fungu lake kuwa amezihifadhi amri za Baba yake. Hili ni dhibitisho wazi kuwa Mungu haui watu. Imeandikwa katika sheria zake na kuonyeshwa na Mwanawe alipokuwa duniani.

Moja ya maana nyingi ya ukweli huu ni kuwa kwa kweli inatuhitaji tuwapende adui zetu. Iwapo kutakuwa na watu ambao wanachukuliwa na Mungu kuwa waovu kiasi cha lazima awaue, basi hili huwapa watu fursa ya kuhukumu hao wenyewe watu ambao wanawaona wanastahili kifo. Hili hukatiza mzunguko kabisa wa hitaji la kupenda adui zetu. Badala yake, tunaweza wahukumu tu kama watu waovu ambao Mungu ataangamiza, au ikihitajika kuwa "watumishi" wake kutenda kama wakala wa Mungu kufanya maangamizi. Kwa hivyo, imani kuwa Mungu huua watu ni utaratibu sawa ambao hutumiwa na wanadamu kuepuka hitaji la kuwapenda adui zao. Yesu anapoelezea sheria ya Mungu anatuagiza kumpenda Mungu na kuwapenda watu wote.

> Wakati huo mtaalam mmoja wa sheria alisimama ili kumjaribu Yesu, akamwuliza, "Mwalimu, nifanye nini ili nipate kurithi uzima wa milele?" (26) Yesu akamjibu, "Imeandikwaje katika Torati? Kwani unasoma nini humo?" (27) Akajibu, " 'Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa nguvu zako zote na kwa akili zako zote, tena mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe.'" (28) Yesu akamwambia, "Umejibu vema. Fanya hivyo nawe utaishi." (29) Lakini yule mtaalam wa sheria akitaka kuonyesha kuwa mwenye haki, akamwuliza Yesu, "Jirani yangu ni nani?" Luka 10:25-29

wakati mwanasheria aliwekwa chini ya hukumu ya kupenda jirani zake wote ikiwemo wala aliowachukia kwa wakati huo, alifanya kile ambacho watu wengi hutenda na hilo ni kujaribu kueleza maana ya maneno muhimu. Neno

alilotaka kuelezea ni *jirani*. Kwa njia sawa, watu wengi ili kuepuka kuhukumiwa na Amri ya sita hujaribu kuelezea neno *Ua*. Hata hivyo Yesu anatuelezea maana ya neno kwa maisha yake duniani, bado kuna salia na majaribio ya kugeuza dhamira ya sheria yake. Yafuatayo yanaonesha ufahamu wa kawaida:

> Kuna maneno mawili tofauti ya Kiebrania (ratsakh, mut) na maneno mawili ya Kigiriki (phoneuo, apokteino) ya "mauaji" na "kuua." Moja humaanisha "kuweka katika kifo," na hilo lingine humaanisha "kuua." **La mwisho ndilo ambalo limekataliwa na Amri Kumi sio la kwanza**. Kwa kweli, ratsakh lina maelezo mapana kuliko neno la kiingereza "mauaji." Ratsakh pia huhusisha kifo kwa sababu ya kutozingatia au kupuuza **lakini halitumiwi kamwe unapoelezea mauaji wakati wa vita. Ndio maana tafsiri nyingi za kisasa zinatoa amri ya sita "usiue."** Hata hivyo, suala kuu sana linaweza ibuka kwa kutegemea tafsiri ambayo mtu anaisoma. Tafsiri ambayo inapatikana kote ya King James inatoa fungu kama "Usiue" na hivyo kuweka wazi milango ya kulielewa fungu hilo visivyo. **kama maana iliyokusudiwa ya "usiue" ilikuwa hiyo tu—hakuna kuua—itatoa umwagaji wa damu uliotendwa na Waisraeli kuliopitishwa na Mungu ukiukaji wa Amri za Mungu mwenyewe** (Kumbukumbu 20). Lakini Mungu hazivunji Amri zake mwenyewe, **hivyo , kwa uwazi, fungu haliagizi kusitisha kabisa kwa kuchukua maisha ya mtu mwingine.** https://www.gotquestions.org/you-shall-not-murder.html

Uzingatifu wa makini wa maandiko unadhihirisha kuwa hoja hii ni ya uongo. Kwanza, katika kila maelezo mwandishi anakubali kuwa *ratsach* ambalo ni neno ambalo limetafsiriwa "ua" katika tafsiri ya King James, halimaanishi tu mauji bali pia mauaji ya bahati mbaya ambayo tunayaita ukatili. Haya sio mauaji.

> Lakini ikiwa alimsukuma ghafula pasipo kumchukia; au akamtupia kitu cho chote pasipo kumvizia, (23) au kwa jiwe liwalo lote, ambalo kwa kupigwa kwalo humkini mtu kufa, asipomwona, akamtupia hata akafa, naye hakuwa adui yake, wala hakumtakia madhara; (24) ndipo mkutano utaamua kati ya huyo aliyempiga mtu na huyo atakayetwaa kisasi cha damu, kama hukumu hizi zilivyo; (25) nao mkutano utamwokoa yule aliyemwua [H7523 Ratsach] mtu

> na mkono wa mwenye kutwaa kisasi cha damu; tena mkutano utamrejeza katika mji wake wa makimbilio, aliokuwa anaukimbilia; naye atakaa humo hata kifo chake kuhani mkuu, aliyepakwa mafuta kwa mafuta matakatifu. Hesabu 35:22-25

> Ili kwamba amwuaye [Ratsach H7523] mtu apate kukimbilia huko, amwuaye jirani yake pasipo kujua, wala hakumchukia tangu hapo; ili apate kuishi akimbiliapo mmojawapo miji hiyo; Kumbukumbu 4:42

Pili, hakuwagiza kuwa wale watu wanaotenda *ratsach* pia wafanyiwe vivyo hivyo.

> Mtu awaye yote atakayemwua[ratsach H7523] mtu, huyo mwuaji atauawa [ratsach H7523] kwa vinywa vya mashahidi; lakini shahidi mmoja hatashuhudia juu ya mtu hata akafa. Hesabu 35:30

Inawezekanaje kuwa Mungu angeamuru vitu ambavyo Amri Kumi zinakataa? Kwa kifupi, Mungu angeagiza mauaji ya aina yoyote katika maandiko kwa sababu Mungu anatafuta kuzuia hukumu ya kifo ili atoe rehema; sio kuwaua watu. Tunaangazia hoja hii katika sura ya 9 – ***Sheria kama Kioo.***

Tatu, neno *muth* [H4191] katika maandiko linatumika kuelezea mauaji. Sauli alitaka kumua Daudi bila haki:

> Kisha Sauli akasema na mwanawe Yonathani, tena na watumishi wake wote, kwamba wamwue[muth H4191] Daudi. 2 Lakini huyo Yonathani, mwana wake Sauli, alikuwa akipendezwa sana na Daudi. Basi Yonathani akamwambia Daudi, akasema, Sauli, baba yangu, anatafuta kukuua; basi, nakusihi, ujiangalie sana asubuhi, ukae mahali pa siri na kujificha; 1 Samweli 19:1-2

Sauli anaagiza mauji yasiyo ya haki ya makuhani:

> Kisha mfalme akawaambia askari walinzi waliosimama karibu naye Geukeni, mkawaue hao makuhani wa Bwana, kwa sababu mkono wao u pamoja na Daudi, na kwa sababu walijua ya kuwa amekimbia, wasiniarifu. Lakini watumishi wa mfalme walikataa kunyosha mkono na kuwaangukia makuhani wa Bwana. (18) Basi mfalme akamwambia Doegi, Geuka wewe, ukawaangukia hao makuhani. Basi Doegi, Mwedomi, akageuka, akawaangukia makuhani,

akaua[muth H4191] siku ile watu themanini na watano wenye kuvaa naivera ya kitani. 1 Samweli 22:17-18

## Mauaji ya Isboshethi:

Basi walipoingia katika ile nyumba, alipokuwa amelala kitandani mwake, katika chumba chake cha kulala, wakampiga, wakamwua,[muth H4191]wakamkata kichwa, wakachukua kichwa chake, wakaenda zao kwa njia ya Araba usiku kucha. 2 Samweli 4:7

## Absalomu anaagiza mauji yasiyo ya haki ya ndugu yake wa kambo Amnoni:

Kisha Absalomu akawaamuru watumishi wake, akasema, Angalieni basi, moyo wake Amnoni utakapofurahiwa kwa mvinyo; nami nitakapowaambia, Mpigeni Amnoni, ndipo mwueni, [muth H4191] msiogope; si mimi niliyewaamuru? Iweni hodari, iweni na ujasiri. 2 Samweli 13:28

## Athalia anawaua wana wote wa kiume wa mfalme isipokuwa Yoashi:

Ila Yehosheba, binti wa mfalme Yehoramu, umbu lake Ahazia ,akamtwaa Yoashi mwana wa Ahazia ,akamwiba miongoni mwa hao wana wa mfalme waliouawa[muth H4191] ,yeye na mlezi wake ,na kuwatia katika chumba cha kulala;wakamficha usoni pa Athalia,basi kwa hiyo hakuuawa. 2 Wafalme 11:2

## Angazia tafsiri katika New King James:

Ila Yehosheba, binti wa mfalme Yehoramu, umbu lake Ahazia ,akamtwaa Yoashi mwana wa Ahazia ,akamwiba miongoni mwa hao wana wa mfalme waliouawa ,yeye na mlezi wake ,na kuwatia katika chumba cha kulala;wakamficha usoni pa Athalia,basi kwa hiyo hakuuawa. 2 Wafalme 11:2 (NKJV)

## Mauaji mengine kwa kutumia neno muth na tafsiri katika NIV:

Na Peka mwana wa Remalia, jemadari wake, akamfanyia fitina, akampiga huko Samaria, katika ngome ya nyumba ya mfalme, pamoja na Argobu na Arie; na pamoja naye walikuwako watu

> hamsini wa Wagileadi. Akamwua, [muth H4191] akatawala mahali pake. 2 Wafalme 15:25 (NIV)

Kama *muth* inatumika to kuua mtu kwa haki kwa uamuzi wa mahakama basi inawezekana kwa waovu kwa hivyo kuagizwa kumwangamiza mtu?

> Mtu asiye haki humvizia mwenye haki, Na kutafuta jinsi ya kumfisha. [muth H4191] Zaburi 37:32

> Kwa kuwa hakukumbuka kutenda fadhili, Bali alimfukuza mnyonge na mhitaji, Hata akamfisha[muth H4191] mtu aliyevunjika moyo, (17) Naye alipenda kulaani, nako kukampata. Hakupendezwa na kubariki, kukawa mbali naye, Zaburi 109:16-17

Kwa hivyo neno *muth* kwa kweli linaweza tumiwa kumaanisha mauaji na neno *rastsach* linaweza tumiwa kumaanisha kifo cha ajali. Hili linadhibitisha madai kuwa *muth* kwa kiasi ni kwa mauaji ya haki na *ratsach* ni kwa mauaji tu.

Hatimaye, pasi na kuzingatia jinsi hili linavyoelezwa mauaji na mauaji ya mahakama yote huhusisha nguvu zisizoweza kuepukika. Je matumizi ya nguvu ni sehemu ya Ufalme wa Mungu? Yesu alielezea wazi katika mahubiri juu ya mlima na kupitia kwa matendo yake katika maisha yake yote kuwa yeye hatumii nguvu zisizoweza kuepukika.

> Lakini kama mtu akikupiga kwenye shavu la kuume, mgeuzie na la pili pia,. Mathayo 5:39

Ni jibu lipi linaweza peanwa kwa mtu anayesema kwa Bwana, 'nilifuata mfano wako katika agano la kale, nilipomwangamizi mtenda maovu huyu" huyo mtu akiambiwa kuwa, "ulifuata mfano mbaya, sehemu hiyo ya maandiko sio ya kufuatwa nawe" huoni inafanya mambo kuwa magumu zaidi? Ni wakati wa kuweka kando majadiliano kuhusu kifo na kuamini ukweli kwamba usiue inamaanisha kuwa usiondoe uhai.
Maisha ya yesu ulimwenguni yanatufunulia fasiri sahihi ya amri "usiue" Yesu hakuua mtu yeyote.

Amri kumi ni sheria ya upendo na upendo haujishurutishi ili kujikinga. Amri zenyewe zinatwambia jinsi wenye dhambi, wanaadhibiwa.

> … Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, Kutoka 20:5

Waovu hakika watakufa; wataadhibiwa kwa matendo yao wenyewe. Kama tulivyoonyesha hapo mbeleni hili litatendeka kwa kumruhusu shetani kuyatawala maisha yao hadi kiwango cha kuwaangamiza, ama kwa ulimwengu wenyewe kuonyesha kwa wanadamu uasi na kuwaangamiza.

Jinsi gani inavyopendeza kujua kwamba Baba yetu aliye mbinguni ni mwenye haki kama Yesu alipokuwa ulimwenguni! Furaha iliyoje kufahamu kwamba Yesu ametuonyesha ufafanuzi kamili wa amri kumi kwa vitendo vya kweli, ikiwemo maana ya kufuata sheria "usiue." Yesu hakuua yeyote na huu ndio mfano pekee unaowezekana kwetu kujifunza kupenda adui zetu kwa kweli kama alivyotufunza.

## 16. Tajiri na Lazaro Kwenye Kioo

Fumbo la tajiri na Lazaro ni ushahidi wa hakika kwa Wakristo wengi kwamba Mungu atawatesa na kuwachoma wenye dhambi kuzimuni. Hiyo lugha inaonekana kama ni dhahiri na Yesu mwenyewe akinena katika msemo.

> Wakati ukafika yule maskini akafa, nao malaika wakamchukua akae pamoja na Abrahamu. Yule tajiri naye akafa na akazikwa. (23) Kule kuzimu alipokuwa akiteseka, alitazama juu, akamwona Abrahamu kwa mbali, naye Lazaro alikuwa karibu yake. (24) Hivyo yule tajiri akamwita, 'Baba Abrahamu, nihurumie naumtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake ndani ya maji aupoze ulimi wangu, **kwa sababu nina maumivu makuu kwenye moto huu.**' (25) "Lakini Abrahamu akamjibu, 'Mwanangu, kumbuka kwamba wakati wa uhai wako ulipata mambo mazuri, lakini Lazaro alipata mambo mabaya. Lakini sasa anafarijiwa hapa na weweuko katika maumivu makuu. Luka 16:22-25

Hadithi hii ikiongezewa mafungu mengine kwenye maandiko, mwisho kabisa inaonekana kana kwamba bila kuponyoka Mungu kwa kweli atawachoma na kuwatesa watu kuzimuni sawasawa na kiwango cha dhambi zao.

> Msiwaogope wale wauao mwili lakini hawawezi kuua roho afadhali mwogopeni yeye awezaye kuiangamiza roho na mwili katika jehanam. Mathayo 10:28

> Ikiwa mkonowako au mguu wako unakusababisha utende dhambi, ukate na uutupe mbali. Ni afadhali kwako kuingia katika uzima ukiwa huna mkono mmoja au mguu mmoja, kuliko kuwa na mikono miwili au miguu miwili na kutupwa katika moto wa milele. Mathayo 18:8
>
> "Kisha atawaambia wale walio upande Wake wa kushoto, 'Ondokeni kwangu, ninyi mliolaaniwa, nendeni kwenye moto wa milele alioandaliwa kwa ajili ya ibilisi na malaika zake. Mathayo 25:41
>
> Yeye naye,atakunywa mvinyo wa hasira kali ya Mungu ambayo imemiminwa katika kikombe cha ghadhabu yake pasipo kuchanganywa na maji. Naye atateswa kwa moto uwakao na kiberiti mbele ya malaika watakatifu na mbele za Mwana-Kondoo. (11) Nao Moshi wa mateso yao hupanda juu milele na milele. Hakuna mapumziko, mchana wala usiku, kwa wale wamwabuduo huyo mnyama na sanamu yake, au kwa ye yote anayepokea chapa ya jina lake." Ufunuo 14:10-11

Msikilizaji wa neno la Mungu atayasoma mafungu haya na adhani kwamba Mungu atawaadhibu wenye dhambi kwa maumivu makali yasioelezeka kila kukicha. Mtu ambaye amesoma vitabu vya Injili kwa makini na ametafakari maisha ya Yesu ataachwa na maswala mengi ambayo yatamfanya achunguze Biblia kwa undani imueleze mafungu haya.

Wale ambao wana hasira moyoni kwa yoyote au wangelipenda kumuumiza mtu yeyote wataridhika na haya mafungu machache yaliyo juu ilikuhesabia haki roho zao za kulipiza kisasi, kwa kuwa inaonekana Mungu hulipiza kisasi maadui wake. Fauka ya hayo,wale ambao wanaojihukumu kwa ukali huhisi kusadikishwa kwamba wanastahili kufaa kwa ajili ya dhambi zao ,wao pia huridhishwa na haya mafungu.Walakini, yatupasa kwenda ndani kuliko hivi. Badala ya kukubali kwa moyo msamaha kamili wa dhambi zao na upendo wa Mungu, haya mafungu yaonyesha kwa nnje sauti ya unyenyekevu kudhibitisha imani yao ya ndani kuwa Mungu ni mdhalimu tena mkali. Wanapeana miili yao ichomwe lakini hawana upendo.

Moja wapo ya baadhi ya sababu muhimu zinazowafanya watu wengi kuyasoma mafungu haya kama Mungu akilipiza kisasi na kuwaadhibu maadui wake ni mwelekeo wakibinadamu wa kuwasukumia wengine

makosa. Huu uzoefu ulianza na Adamu wakati alipomlaumu Hawa kwa kumfanya ale tunda. Ni njia isiyo ya adili ya kuwawekea wengine makosa kwa minajili ya kumletea mtu au jamii amani na mapatano wakati watu wamo hatarini. Kuhani mkuu Kayafa alimfanyia Kristo hivi.

> Hamjui kwamba ni afadhali mtu mmoja afe kwa ajili ya watu,kuliko taifa lote liangamie?" Yohana 11:50

Viongozi wa kidini wa Israeli walikuwa hatarini. Dhambi zao zilikuwa zinawekwa wazi na walitaka kugeuza mawazo ya watu kwa matendo ya Kristo ya "haramu"; kwa hivyo wakamweka kana kwamba anampinga Musa, na ni mwenye dhambi aliyestahili kufa. Kwa mioyo ya wivu ya mafarisayo, Kristo alifanya kafara ya dhihaka, si kwa kulingana na injili lakini kwa kumtumia Pilato kigeugeu kumfanya Kristo asukumiwe makosa yao. Walijaribu kuinyamazisha sauti ya dhamira si kwa sababu ya kujitoa lakini kwa kujitahidi kumtoa shahidi aliyehai ambaye aliyekuwa akiwasumbua. Tabia zao za hasira na chuki zilizoelekezwa kwa Kristo zilitakaswa kibinafsi kwa kuzirusha kwa Mungu na kuonyesha kwamba Kristo alipigwa na Mungu na Kuteswa.

Wakati Wakristo wanapoinuka kwa haki inayoonekana kama hasira, kutangazia ulimwengu kwamba Mungu anaenda kufuta uaasi wa wenye dhambi kwa sauti za ushindi za labda "hasira takatifu" kuna ukweli kabisa naona haina budi hiyo namna ya kafara ya kibinafsi itakuwa sawa na ile ya Kayafa. Inayopatika kwa haki ya kibinafsi kwa kupitia kuridhika binafsi kwa kuwaona wengine kuwa wenye thamani kuliko wengine na huteswa na kufanywa wafe.

Kwa kulingana na vile Kristo alivyotendewa, hii kafara ya viongozi wa kiyahudi Ilielekezewa mtu mwema. Ilikuwa sawa na ule mfano wa Kaini na Habili. Habili aliisumbua dhamira ya Kaini na hukumu yake kwa Kaini iliyomfanya Kaini ajihisi mwenye dhambi. Ili apate kafara ya kibinafsi Kaini alimtoa nduguye kafara na kumfanya afe.Kwa mfano wa Kristo viongozi wa Kiyahudi waliinyamazisha sauti ya Yule ambaye aliyeisumbua dhamira yao, na tena kuwauwa wevi wawili ambao waliowaona walikuwa na thamani ya chini kuwaliko.

Wakristo wengi huenda wakapata upatanisho wa uongo kwa kuridhika kujua majangili, wevi na wenye dhambi wote watachomwa kuzimuni na wao

wakienda kwa furaha mbinguni. Pia wanaweza kutumia hii elimu ya mwili kunyamazisha sauti ya dhamira ya maisha ya haki ya mwamini mwengine. Wazo la upatanisho linatatanishwa kati ya Kristo  kwa kweli kuchukua dhambi zao na wale wanaonekana waovu kupokea adhabu ambayo tunayoiona wanastahili. Huu moto geni wa hii injili unaweza kwa juu juu kutuliza dhamira inayosumbuliwa kwa sababu ya dhambi zake.

Tukiirudia  hadithi yetu, kidokezo cha kwanza tunastahili kusema ni kwamba ukisoma maandiko kamili tunaonyeshwa kwamba watu hawana dhamira wakifa.

> kwa sababu walio hai wanajua ya kwamba watakufa; lakini wafu hawajui neno lo lote, wala hawana ijara tena; maana kumbukumbu lao limesahauliwa. Muhubiri 9:5

> Sio wafu wamsifuo Bwana, Wala wo wote washukao kwenye kimya; Zaburi 115:17

> Kama vile maji kupwa katika bahari, Na mto kupunguka na kukatika; (12) Ni vivyo mwanadamu hulala chini, **asiinuke; Hata wakati wa mbingu kutokuwako tena, hawataamka,** Ayubu 14:11-12

> Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi. Ndipo mbingu zitatoweka kwa kishindo kikuu na vitu vya asili vitateketezwa kwa moto, nayo dunia na kila kitu kilichomo ndani yake kitaunguzwa. 2 Petro 3:10

> Kwa maana, angalieni, siku ile inakuja, inawaka kama tanuru; na watu wote wenye kiburi, nao wote watendao uovu, watakuwa makapi; na siku ile inayokuja **itawateketeza,** asema Bwana wa majeshi; hata haitawaachia shina wala tawi. (2) Lakini kwenu ninyi mnaolicha jina langu, jua la haki litawazukia, lenye kuponya katika mbawa zake; nanyi mtatoka nje, na kucheza-cheza kama ndama wa mazizini. (3) Nanyi mtawakanyaga waovu**; maana watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu; katika siku ile niifanyayo, asema Bwana wa majeshi**. Malaki 4:1-3

> Kwa maana kama vile mlivyokunywa juu ya mlima wangu mtakatifu, ndivyo mataifa yote watakavyokunywa daima; **naam, watakunywa na kubabaika, nao watakuwa kana kwamba hawakuwa kamwe**. Obadia 1:16

> “Ndugu zangu Waisraeli, nataka niwaambie kwa uhakika kwamba baba yetu Daudi alikufa na kuzikwa, nalo kaburi lake lipo hapa mpaka leo. (34) Kwa kuwa Daudi hakupaa kwenda mbinguni, lakini anasema,“ ‘BWANA alimwambia Bwana wangu: Kaa wewe upande wangu wa kuume, (35) mpaka nitakapowafanya adui zako kuwa chini ya miguu yako.’ ” Matendo 2:29,34-35

> Atafuta kila chozi, kutoka katika macho yao. Mauti haitakuwepo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu, kwa maana mambo ya kwanza yamekwisha kupita.” Ufunuo 21:4

Biblia inafundisha ya kuwa watu hawaendi mbinguni au kuzimu wakifariki. Wanabaki kaburini mpaka mbingu zitatoweka. 2 Petro 3:10 inatuambia wakati wa kurudi kwa Kristo. Je inakuwaje kwamba Yesu anafundisha hadithi ambayo inaenda kinyume na Biblia? Vile inavyoonekana hadithi hii ilikukua inajulikana na Wayahudi kwa sababu walishawishiwa na Wayunani karne nyingi kitambo.

> Alan F. Johnson na Robert E. Webber wanafafanua “Inawezekana vyema kutazama hadithi hii si kama ufunuo wa mambo ya ndani ya maisha baada ya kifo, bali kutupatia mtazamo tofauti wa mawazo ya kawaida yaliyo shikwa kuhusu maisha.” Edward William Fudge, *Moto unao Maliza*, ukurasa 149.

> “Hadithi hii inabeba mangwi ya wazi ya hadithi za kale zilizo fahamika, kwa Yesu napeana upya mtazamo wa ajabu uliogeuka” N.T Wright, *Yesu na Ushindi wa Mungu*, ukurasa 255.

Hili ni chimbuko fahamivu la kuelewa. Yesu hutumia hadithi za kawaida zilizoaminiwa na wasikilizaji, ili kuwafundisha ukweli muhimu.

> Geldenhuys atamatisha kwamba Yesu “alilinganisha fumbu hili si kwa minajili ya kuridhisha udadisi juu ya maisha baada yaa mauti bali kutilimkazo dhahiri umuhimu wa maisha upande huu wa kaburi” Edward William Fudge, *Moto Unao Teketeza*, ukurasa 149.

Tukijadili sura ya 9, Kristo hutumia kioo kumrudishia nyuma mtu fikira zake mwenyewe. Hufanya hivi kwa sehemu ndogo kuzungumza na watu kwa njia wanazoweza kufahamu, walakini pia kujaribu kilicho mioyoni mwao. Mtu ambaye ni mtiifu kwa neno la Mungu na anaongozwa na Roho ataweza kutambua maana ya kiroho maneno ya Yesu pia mawazo ya mtu aliye kimwili inaonekana yatadhibitishwa. Yesu akamwambia Nikodemo;

Nikodemo akamwuliza, "Mambo haya yanawezekanaje?" (10) Yesu akamwambia, "Wewe ni mwalimu mashuhuri wa Waisraeli, nawe huelewi mambo haya? (11) Amin, amin, ninakwambia, sisi tunazungumza lile tunalolijua na tunashuhudia lile tulililoliona. Lakini ninyi watu hamkubali ushuhuda wetu. (12) Nimewaambia mambo ya duniani, nanyi hamkuniamini, mtaniaminije basi nitakapowaambia mambo ya mbinguni? Yohana 3:9-12

Kioo ambacho Yesu anachokitumia katika kitabu cha Yohana kinazidi kukuwa kigumu kuelewa hadi mtu akubali kwamba mawazo yake ni mabaya au atembee amwache Yesu.

| Nakala ya Biblia | Fasiri |
|---|---|
| Yohana 2:19-21 Yesu akawajibu, "Libomoeni hili hekalu,nami nitalijenga tena kwa siku tatu!''(20)Wale Wayahudi wakamjibu, "Hekalu hili lilijengwa kwa muda wa miaka arobaini na sita,nawe wasema utalijenga kwa siku tatu?'' (21) Lakini Yeye, 'hekalu' alilozungumzia ni mwili Wake. (22) Baada ya kufufuka kutoka kwa wafu,wanafunzi Wake wakakumbuka yale aliyokuwa amesema. Ndipo wakayaamini Maandiko na yale maneno Yesu aliyokuwa amesema. | Yesu anazungumzia mwili wake, hekalu hai,lakini wao wanaelewa hekalu linalo onekana kwa macho mjini. |
| Yohana 3:3-4 Yesu akamjibu, "Amin, amin nakuambia,mtu hawezi kuuona Ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili.''(4)Nikodemo akauliza, "Awezeje mtu kuzaliwa wakati akiwa mzee?" ''Hakika hawezi kuingia mara ya pili kwenye tumbo la mama yake ili azaliwe!" | Yesu anazungumzia kuzaliwa wa kiroho na Nikodemo alikuwa akifiria Yesu anamanisha kuzaliwa kimwili |

| | |
|---|---|
| Yohana 4:13-15 Yesu akamjibu, "Kila mtu anayekunywa maji ya kisima hiki, ataona kiu tena. (14)Lakini ye yote anywaye maji nitakayompa, hataona kiu kamwe. Maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji yakibubujika uzima wa milele.'' (15)Yule mwanamke akamwambia, "Bwana,tafadhali nipe maji hayo ili nisipate kiu tena na wala nisije tena hapa kuteka maji!'' | Yesu anazungumzia maji ya kiroho na mwanamke anafikiria Yesu anazungumzia maji ya kawaida |
| Yohana 5:17-18 Yesu akawajibu, "Baba yangu anafanya kazi yake daima hata siku hii ya leo, nami pia ninafanya kazi.'' (18) Maneno haya yaliwaudhi sana viongozi wa Wayahudi. Wakajaribu kila njia wapate jinsi ya kumwua, kwani si kwamba alivunja Sabato tu, bali alikuwa akimwita Mungu Baba Yake, hivyo kujifanya sawa na Mungu. | Yesu anazungumzia kazi ya kiroho na Wayahudi wanafikiria Yesu anamanisha kazi ya kawaida,waliamua kushika maelezo ya kimakosa ambayo yaliwafanya wamkatae na kutaka kumua Yesu. |
| Yohana 6:51-52,60,66 Mimi ni mkate wa uzima ule uliotoka mbinguni. Mtu ye yote akiula mkate huu, ataishi milele. Mkate huu ni mwili wangu, ambao nitautoa kwa ajili ya uzima wa ulimwengu.'' (52)Ndipo Wayahudi wakaanza kuhojiana vikali wao kwa wao wakisema, "Mtu huyu awezaje kutupatia mwili wake tuule?'' (60)Wengi wa wafuasi Wake waliposikia jambo hili wakasema, "Mafundisho haya ni magumu. Ni nani awezaye kuyapokea?'' (66)Tangu wakati huo wafuasi Wake wengi wakarejea nyuma wakaacha kumfuata. | Yesu anazungumzi mkate wa kiroho na kinywaji lakini watu wengi wakageuka na kumkana Yesu kwa ajili ya kuelewa kwao maneno aliyo waambia. |

Njia hii katika kitabu cha Yohana yafunua ongezeko katika utumiaji wa kioo inayoendesha huduma ya Yesu. Tunaona lugha ya Yesu katika Yohana sura ya sita inayosisitiza kula mwili wake na kunywa damu yake. Yesu alifafanua mifano aliyokuwa akitumia katika Yohana 6:35. Alikuwa akiwaalika waje kwake na wale maneno yake yaliyowashibisha njaa ya chakula cha kiroho;

kumuamini kwamba alitumwa na Mungu kumaliza kiu yao ya faraja ya kiroho na kukubaliwa na Mungu. Kukataa kwa watu kumsikiza aliyoyanena ndiyo yaliwafanya wamkatae. Hii njia inafunua kile kilichokua ndani ya mioyo yao isiyobadilika. Inaonyesha yakuwa walikusudia kutomuelewa ili kuthibitisha kumkana na kupindua sababu zote zilizoonyesha kwamba yeye ni Masihi wa kweli.

Kwa kulingana na kioo ambacho Yesu anakitumia katika hadithi ya tajiri na Lazaro, inaenda kwa undani kuliko kuelewa vitu vya asili  au kiroho. Yesu anatumia mawazo ambayo watu waliamini ili kuwafundisha kitu muhimu. Wayahudi walianza kutaka kwa nguvu kujua ishara ya mamlaka yake. Walikaza mioyo yao kumpinga. Umuhimu wa mambo vile yalivyokuwa yalimuhitaji Yesu kuwaelezea uzima na mauti yaliyowakumba.

Alinena nao kupitia hadithi waliyoifahamu. Kwa hivyo iliwarudia fikira zao wenyewe. Hii ilihitajika kwa sababu ya mioyo yao migumu. Wale wanayo isoma imani ya kwamba waalifu wanastahili kuteswa watathibitisha chuki yao kwa wengine. Wengine wanajiuliza swali hili mbona Yesu alifanya hivyo? Mbona anasema vitu ambavyo haviweza kueleweka vyema?

Kazi ya kwanza ya injili ni kudhibitishia hatia ya kosa. Dhibitisho hili la dhambi huwa linafunua dhambi ndani ya mioyo yetu. Luka 8:17, Mariko 4:22, Luka 12:2. Hii ndiyo maana ya kioo cha Mungu cha sheria.Kwamba sote tumetenda dhambi, hatukubali, kunyamazisha, kuelewa kamili umuhimu. Ufunuo wa dhambi mioyoni mwa watu  inahitaji kwa kweli hekima ya Mungu.

> Naye atakapokuja, atauthibitishia ulimwengu kuhusu dhambi, haki na hukumu. Yohana 16:8

> Heri walio maskini wa roho; Maana ufalme wa mbinguni ni wao. (4) Heri wenye huzuni; Maana hao watafarijika. Mathayo 5:3-4

> Basi tunajua ya kwamba cho chote sheria inachosema, inawaambia wale walio chini ya sheria ili kila kinywa kinyamazishwe na ulimwengu wote uwajibike kwa Mungu. Warumi 3:19

Tunakumbuka hadithi ya mwanamke mgeni kutoka Kanani ambaye alimuomba Yesu amponye binti yake. Kunyamaza kwake kwa mara ya kwanza ilikuwa kama kioo cha kuleta nia mbaya za wanafunzi wake kwa

wageni. Kioo cha Mungu hurudisha mawazo na makusudi yetu. Kristo kama neno la Mungu la tuzungumzia njia ambayo inapambanua kutafakari na shauku zetu.

> Kwa maana Neno la Mungu li hai tena lina nguvu tena lina makali kuliko upanga uwao wote wenye makali kuwili, tena linachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, viungo na mafuta yaliyo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. Waebrania 4:12

Wakati watu wanatumia maneno mengine ya Yesu kudhibitisha kwamba Mungu hutesa na kuchoma watu, kwa kweli inafunua vile wanavyo waza kumhusu Yeye. Wakati maneno mengine yanapoletwa kuonyesha ya kuwa Kristo si mkali na hauwi watu na anadai kuwa sawa na Babake, hivyo basi tunawekwa pahali ambapo tunastahili kufanya uchaguzi.

Wakati ambapo yule mwanamke mgeni alimuomba Yesu amponye binti yake alimsikiza akisema, "si vizuri kuchukua chakula cha watoto na kuwapatia mbwa,"Ilimbidi afanye uamuzi unaofaa. Je angelichukua aliyoyanena kumkana au angelichukua aliyojifundisha kuhusu tabia yake kushikilia imani akiwa na matumaini kwamba atamsaidia? Hii ni kazi ya uungu katika injili kutuleta mpaka wakati tunapo kata shauri juu ya tabia ya Baba yetu.

Tunda la kujifunza kutoka kwa maandiko na kutembea na Yesu si sauti zinazototofautiana kwa mwanafunzi wa kweli na myenyekevu ambaye anayeshikilia imani ili apate jawabu hata kama fundisho la kanuni la kiasili la karne nyingi linaonekana kwamba linamzingira kwa hofu. Nikisoma hadithi ya tajiri motoni na Yesu akisema kwamba Mungu anauwezo wa kuharibu mwili na roho kuzimuni. Ninafanya uamuzi wa kufanya utafiti na kulinganisha haya na mafungu mengine kama vile mpende adui yako, na usiue. Tumesimulia sehemu ya kifo cha waovu hapo awali kwa hivyo hivi sasa wacha tulete mafungu yanayozungumza kuhusu Mungu na moto.

> Malaika wa **Bwana akamtokea, katika mwali wa moto uliotoka katikati ya kijiti**; akatazama, na kumbe! Kile kijiti kiliwaka moto, nacho kijiti hakikuteketea. Kutoka 3:2

> Na kuonekana **kwake ule utukufu wa Bwana** kulikuwa kama moto uteketezao, juu ya mlima machoni pa wana wa Israeli. Kutoka 24:17

Tazama, **jina la Bwana linakuja kutoka mbali sana**, linawaka kwa hasira yake, kwa moshi mwingi sana unaopaa juu; midomo yake imejaa ghadhabu, **na ulimi wake ni moto ulao;** Isaya 30:27

Wenye dhambi walio katika Sayuni wanaogopa; tetemeko limewashika wasiomcha Mungu; **Ni nani kwetu sisi awezaye kukaa na moto ulao**; ni nani kwetu sisi awezaye kukaa na moto uteketezao milele? (15) **Ni yeye aendaye kwa haki, anenaye maneno ya adili**; ni yeye anayedharau faida ipatikanayo kwa dhuluma; akung'utaye mikono yake asipokee rushwa; azibaye masikio yake asisikie habari za damu; afumbaye macho yake asitazame uovu. Isaiah 33:14-15

kwa kuwa "**Mungu wetu ni moto ulao**." Waebrania 12:29

Ghafula sauti kama mvumo mkubwa wa upepo uliotoka mbinguni, ukaijaza nyumba yote walimokuwa wameketi. (3)Zikatokea **ndimi kama za moto zilizogawanyika na kukaa juu ya kila mmoja wao**. (4)**Wote wakajazwa na Roho Mtakatifu**, wakaanza kunena kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia. Matendo 2:2-4

Badala yake:"adui yako akiwa na njaa, mpe chakula, akiwa na kiu, mnyweshe.Maana ukifanya hivyo, **utampalia makaa ya moto yanayowaka kichwani pake**. Warumi 12:20

Siku ya Pentekoste mitume walivishwa moto wa Roho wa Mungu. Waliwaka kwa moto lakini hawakuteketezwa kama vile kijiti kilichowaka wakati wa Musa. Swali lililoulizwa katika Isaya 33:14 ni: Ni nani kwetu sisi awezaye kukaa na moto ulao? Ni wenye haki ndio watakao chomeka milele katika miyale ya moto wa upendo wa Mungu. Wakati ambapo upendo wa Mungu utafunuliwa wakati wa mwisho, wakati waovu wote watakapoona kwa kweli kile ambacho Mungu amewatendea na juhudi zake zote za kuwaokowa, hatia na aiibu ya kumkana itakuwa makaa ya moto kwenye vichwa vyao. Uovu wao ndio utakaowavyoga – si mkono wa Mungu.Moto ni upendo bila ubinafsi, na huo upendo unapofunuliwa unaleta kwa mara moja mtu kujilaumu na uchungu wa ndani. Je, sababu ya Mungu kuwa na uwezo wa kuangamiza mwili na roho kuzimuni ni sababu Yeye ni upendo, mwenye rehema na anajali?

Msiwaogope wale wauao mwili lakini hawawezi kuua roho afadhali mwogopeni yeye awezaye kuiangamiza roho na mwili katika

> jehanam (29) Je, shomoro wawili hawauzwi kwa senti mbili tu? Lakini hakuna hata mmoja wao atakayeanguka pasipo Baba yenu kujua.. (30) Hata nywele za vichwa vyenu zote zimehesabiwa. (31) Hivyo msiogope, kwa maana ninyi ni wa thamani kubwa zaidi kuliko shomoro wengi. Mathayo 10:28-31

Mstari wa 28 ukilinganisha na 29-31 yaonekana kwamba haijaambatana. Mwanzo Yesu anasema tumchee Yeye aliye na uwezo wa kuangamiza mwili na roho kuzimuni na tena anatuambia kuhusu vile Baba anatujali na tusiogope. Kama Mungu ndiye anayewatesa watu kuzimuni kutumia moto wa kawaida unaoyeyusha ngozi basi kwa nini katika mstari wa 31 anasema "msiogope" bila ukinzani?

Yesu anatumia mstari wa 28 kusema mawazo ya wanadamu kwa kioo. Anarudishia mawazo yetu ya asili kuhusu Mungu. Kwa mtu anayesoma ambaye amejawa na dhambi na uovu, anastahili kuogopa anapoona tofauti kati ya tabia yake na ya Mungu na vile amemtesa Kristo kwa ubinafsi wake.

> Basi ile tamaa akiisha kuchukua mimba, huzaa dhambi, ile dhambi ikikomaa, huzaa mauti. Yakobo 1:15

> Uovu utamwua asiye haki, Nao wamchukiao mwenye haki watahukumiwa. Zaburi 34:21

Dhambi inaleta mauti – si Mungu. Ni kwa kupitia fahamu kali vile Baba yetu wa mbinguni anatujali kwa undani, vile anavyo jali ndege wa angani, na anajuwa idadi ya nywele vichwani vyetu, na vile anavyo tufikiria kwa njia ya upendo saa zote, ndivyo tutakavyo haribiwa kabisa. Hiyo fahamu kamili ndiyo itakayoleta hatia mbaya kwa mwenye dhambi na atashindwa na kumalizwa. Ni kwa njia hii mathayo 10:28 na mathayo10: 29-31 inaleta maana zikilinganishwa.

Wazo hili wakati mwengine linaonyeshwa kwamba kwa sababbu Mungu hufunua tabia ya, na anajua kwamba mwenye dhambi atakufa ni kana kwamba yeye anawajibika kuhusu vifo vyao. Jambo la hakika kuwa Yeye hujifunua linamfanya kuwa muuaji.Hii inaleta maana kwa tabibu ambaye ameombwa kuzima chombo cha kuponea uhai kwa mgonjwa ambaye mwishowe atakufa kuchukuliwa kama muaji au anawajibika kwa vifo. Ili wanadamu kuwa na ushirika na Mungu, halisi milele, Mungu lazima ajifunue kweli Yeye ni nani. Tunakumbuka pia waovu wakati wa mwisho

wanauzunguka mji wa Yerusalemu Mpya wakitamani kuuteka nyara, inamaanisha wakiukaribia huo mji ndani ya mioyo yao wana uuaji, wivu na uizi.

> Nao walitembea (Shetani na waovu) katika eneo lote la dunia, wakaizunguka kambi ya watakatifu na ule mji uliopendwa. Lakini moto( wa upendo bila ubinafsi kama siku ya Pentekoste) ukashuka kutoka mbinguni na kuwateketeza. Ufunuo 20:9

Wakati ubinafsi anapokaribia kutokuwa na ubinafsi, hatia ya kupondwa kwa ubinafsi inafanya kifo cha muovu kiweni cha hakika. Wakati tunaposoma Biblia, kioo kiko mbele zetu, Kinaturudishia vile tunavyo fikiria kisha tunafanya uamuzi wa milele.

> Kwake ajitakasaye utajionyesha kuwa mtakatifu; Na kwa mpotovu utajionyesha kuwa mkaidi. Zaburi 18:26.

Wakati malaika alimwita Ibrahimu na kumzuia asitoe uhai wa mwanawe Isaka kama kafara, Ibrahimu kwa ghafla alikuwa na uamuzi wa kubadili picha ya Mungu aliyokuwa nayo. Amri ya kumchinja mtoto wake ilikuwa mawazo yake yaliyo rudishwa na ilionekana kwa hakika kwamba mwana wake alistahili afe. Sisi sote tumewahi kufika mahali hapo pa uamuzi. Naomba tusikie sauti *usimchinje mwana wako* na kufahamu Mungu si mwanzilishi wa kifo. “Kafara na sadaka za dhambi hukuzitaka.” Zaburi 40:6.

Je nini hasa ilikuwa madhumuni ya Yesu kutoa hadithi hiyo? Inapatikana katika wazo lake la mwisho.

> “Abrahamu akamwambia, ‘Kama wasipowasikiliza Musa na manabii, hawataweza kushawishiwa hata kama atafufuka mtu kutoka kwa wafu.’ ” Luka 16:31

Kristo aliwatilia moyoni umuhimu wa maamuzi tunayo ya fanya upande huu wa kaburi, na tunastahili kuyatilia maanani maandiko ya Musa na manabi katika hayo maamuzi.

## 17. Malaika Wanao Piga Sana

Malaika wa Mungu walikuwa na sehemu muhimu katika maisha ya Yesu duniani. Malaika Gabrieli alimtangazia Maria heshima yake ya kumzaa Masihi. Malaika waliimba wa kikaribisha kuzaliwa kwake. Katika wakati fahamivu kabla ya kuangikwa malaika alikuja akamtia Yesu nguvu kwa kazi yake. Luka 22:43. Malaika alitumwa na Baba kumuita Yesu atoke kaburini na waliwatangazia wafuasi wake waliovunjwa moyo kwamba Yesu amefufuka kutoka kwa wafu. Malaika walichukuwa nafasi muhimu katika kazi ya Yesu na kazi zao zote zilikuwa zinahusu tabia ya Kristo kwani tunasoma:

> Nathanaeli akamwambia, "Mwalimu, Wewe ni Mwana wa Mungu! Wewe ni Mfalme wa Israeli!" (50) Yesu akamwambia, "Unaamini kwa kuwa nilikuambia nilikuona ulipokuwa bado uko chini ya mtini? Basi utaona mambo makuu zaidi kuliko hilo." (51) Ndipo akawaambia, "Amin, amin nawaambia, ninyi mtaona mbingu ikifunguka na malaika wa Mungu wakipanda na kushuka juu ya Mwana wa Adamu." Yohana 1:49-51

Kazi ya malaika inafanywa kwa kupitia msingi wa tabia ya Kristo na kazi ya Kristo kwa sababu kazi yote wanayoifanya ikokatika msingi wa mwana wa Adamu. Biblia inasema;

> Je, malaika wote si roho watumikao waliotumwa kuwahudumia wale watakaorithi wokovu? Waebrania 1:14

Malaika wa Mungu wanapenda kumtumikia Baba yetu na Bwana Yesu. Wanapenda kumtumikia kwa kutulinda na kututia moyo.

> Malaika wa Bwana hufanya kituo, Akiwazungukia wamchao na kuwaokoa. Zaburi 34:7

Wamejazwa na Roho wa Mungu na wanaimba nyimbo za sifa za Mungu na Mwana wake.

> Nami nikatazama, nikasikia sauti za malaika wengi wakiwa wamekizunguka kile kiti cha enzi, pamoja na wale viumbe wenye uhai wanne na wale wazee ishirini na wanne, idadi yao ilikuwa kumi elfu mara kumi elfu na maelfu ya maelfu. (12) Nao wakiimba kwa sauti kuu, wakisema: "Anastahili Mwana-Kondoo, Yeye aliyechinjwa, kupokea uweza na utajiri na hekima na nguvu na heshima na utukufu na sifa!" Ufunuo 5:11-12

Malaika hupenda kabisa injili na mpango wa wokovu.

> Mitume walidhihirishiwa kwamba walikuwa hawajihudumii wao wenyewe, bali walihudumu kwa ajili yenu katika mambo hayo ambayo sasa yamehubiriwa kwenu na wale waliowahubiri ninyi Injili kwa Roho Mtakatifu aliyetumwa kutoka mbinguni. Mambo ambayo hata malaika wanatamani kuyafahamu. 1 Petero 1:12

Wanafurahia kuleta amani duniani na nia nzuri kwetu.

> Ghafula pakawa na jeshi kubwa la mbinguni pamoja na huyo malaika wakimsifu Mungu wakisema, (14) "Atukuzwe Mungu juu mbinguni na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia." Luka 2:13-14

Wako bora kwa uwezo na wanamtii Mungu kikamilifu na kuzi tunza amri zake zote.

> Mhimidini Bwana, enyi malaika zake, Ninyi mlio hodari, mtendao neno lake, Mkiisikiliza sauti ya neno lake. Zaburi 103:20

Baba yetu anawaamrisha malaika wake watakatifu kutulinda kutokana na Shetani na malaika wake waharibifu vile tumegundua katika sura ya kumi na moja kulingana na hasira ya Bwana. Kama vile malaika watakatifu wa mejazwa na Roho wa Kristo, wanazitii amri za Baba. Ijapokuwa malaika watakatifu hawaui watu, wanatumia uwezo wao kuzuia nguvu za giza na

kuenda na kuangamiza vitu vyenye vizivyo na uhai. Kuna mafungu ya maandiko ambayo yanatushauri kinyume, na haya ndio tunaenda kuangazia katika huu ukurasa. Ukitafuta maneno malaika na piga kwa maandiko utapata hadithi nne za Biblia zilizotajwa;

1. Hesabu 22. Balaamu na punda. Balaamu alimpiga punda ambaye aliyemuona malaika.
2. 2 Samweli 24. Daudi anawahesabu wa Israeli na 70,000 waliuawa na malaika wa Bwana.
3. 2 Wafalme 19:35 na Isaya 37:36. Jeshi la Waashuri wanaume 185,000 waliuawa na malaika wa Bwana.
4. Matendo 12:24.Malaika wa Bwana alimuua Herode kwa dhambi zake.

Katika hadithi ya kwanza, malaika hakumpiga yeyote bali Balaamu alimpiga punda wake baada ya kusimama kwa kumuogopa malaika. Malaika alisimama mbele ya Balaamu na upanga.

> Na yule punda akamwona malaika wa Bwana amesimama njiani, na upanga wake mkononi mwake amekwisha kuufuta; punda akageuka upande ili kuiacha njia, akaingia shambani. Balaamu akampiga punda ili kumrejeza njiani. Hesabu 22:23

Hali ya kuogofya ya malaika na upanga mkononi inashauri kwamba alikuwa tayari kumfanyia Balaamu mabaya na mawazo haya yanaonekana kudhibitishwa na hadithi zingine katika orodha yetu.

Katika hadithi inayofuata, Daudi anatafuta kuhesabu jeshi lake kwa sababu ya Kiburi iliorodhesha Israeli kati mataifa na matokeo yalikuwa vifo vya wanaisraeli 70,000.

> Tena hasira ya Bwana ikawaka juu ya Israeli, akamtia Daudi nia juu yao, akisema, Nenda, ukawahesabu Israeli na Yuda. 2 Samweli 24:1

> Basi Bwana akawaletea Israeli tauni tangu asubuhi hata wakati ulioamriwa; nao wakafa watu toka Dani mpaka Beer-sheba sabini elfu. (16) Lakini huyo malaika aliponyosha mkono wake kuelekea Yerusalemu ili auharibu, Bwana akaghairi katika mabaya, akamwambia huyo malaika mwenye kuwaharibu watu, Yatosha, sasa ulegeze mkono wako. Naye yule malaika wa Bwana alikuwako

> karibu na kiwanja cha kupuria cha Arauna, Myebusi. 2 Samweli 24:15-16

Kusoma hadithi kwa mara ya kwanza kwa tuarifu kitu kinachoogofya. Kwa kiburi, mfalme anawahesabu watu kisha Mungu anaonekana kana kwamba anamtuma malaika kuwaua watu 70,000 na anatubu kuhusu uovu uliofanywa na anaona huruma ya kuwa watu wengine zaidi. Jambo la kushangaza ni kwamba 2 Samweli 24:1 kwa hakika inaonekana ikisema Mungu mwenyewe alimfanya Daudi kuwahesabu Wanaisraeli ikidokeza kwamba Mungu anawajibika kwa kile kilichotokea baadaye. Kwa mtu yoyote ambaye anaamini "Mungu ni upendo" swali la kuulizwa ni "hadithi hii duniani inahusu nini? Utakumbuka katika ukurasa wa kenda tuliona vile sheria inafanya kazi kama kioo kwa roho zetu na hizi hadithi kuhusu malaika wanaoua unatoa jaribio kamili kuona kama maandiko yanapo somwa kwa kulingana na tabia ya Yesu au kurusha tabia yetu ya kibinadamu kwa Mungu.

Ijapokuwa hadithi inayofuata kuhusu maangamizo ya jeshi la Waashuri inahusu vifo vya watu wengi, inaonekana rahisi kuishi nayo kwa sababu watu hawa walitaka kuwauwa watu wa Mungu na walikuwa watu wakatili duniani. Waashuri waliwatoa watu ngozi wakiwa hai na kuwachoma kwa miiba. Mwenendo huo wa kinyama kwa wafuasi wa Mungu unaweza kutuliza maswali mengi kuhusu malaika wa Bwana kutumia nguvu zinazo dhuru sana.

> Ikawa usiku uo huo malaika wa Bwana alitoka, akakiingia kituo cha Waashuri, akawapiga watu mia na themanini na tano elfu. Na watu walipoondoka asubuhi na mapema, kumbe! Hao walikuwa maiti wote pia. 2 Wafalme 19:35

Dhana ya usomaji wazi wa matamshi haya unatushauri kwa nguvu sana malaika wa Bwana waliwaua majeshi 185,000 ya waashuri. Inaonekana kuwa na hoja kamili kwamba wakati ambapo uovu unaotia hofu unaotaka kuwauwa watu wa Mungu basi majeshi wanastahili kuuliwa kwa ajili ya mipango yao ya kikatili. Hadithi yetu ya mwisho katika orodha yetu ni Herode. Yeye anaoneka kama mtu aliyefaa kuuawa kwa sababu ya matendo yake yote aliyoyafanya.

> Katika siku iliyochaguliwa Herode Agripa akavaa mavazi yake ya kifalme, akaketi kwenye kiti chake cha enzi na kuwahutubia watu. (22) Watu waliokuwa wamekusanyika wakapiga kelele, wakisema, "Hii si sauti ya mwanadamu, bali ni ya Mungu." (23) Ghafula, kwa

> kuwa Herode Agripa hakumpa Mungu utukufu, malaika akampiga, akaliwa na chango akafa. Matendo 12:21-23

Herode alimuua Yakobo nduguye Yohana kisha alipanga kumuua Petro. Inaonekana wazi kwamba ni malaika mzuri ndiye aliyempiga Herode. Ni wazi pia ilikuwa adhabu ya kulipiza kisasa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kulipiza kisasi ni malipo au upatilizo kwa matendo yaliyo fanywa. Inaweza kuwa jaribio kubwa kabisa kutamatisha upelelezi wetu hapa na kufanya uamuzi wa mwisho kwamba Mungu kwa hakika anawatuma malaika wake wazuri kuwauwa watu waovu. Ijapokuwa hadithi ya kwanza ina mashaka, lakini hizo zengine mbili kuhusu Waashuri na Herode zinaonekana dhahiri na kufanyia maneno wazo hili lisilo fikiriwa kwa watu wengi.

Katika hiki kitabu tumeweka wazi wazo ambalo kwa kupitia kwa kioo cha miwani ya maisha ya Kristo, mtazamo wetu wa hadithi za Biblia zinastahili kuafikiwa. Kama mtu hachukuwi wazo hili, bila shaka atatia kikomo kwa upekuzi wake hapa na mwisho aamue malaika wa haki wa Mungu huua watu.

Katika sura ya pili ya kitabu hiki tulitaja kanuni ya William Miller kwamba tuchukuwe kila kitu maandiko yanayo nena kuhusu kitu kinachonenwa kufikia uamuzi wa mwisho. Inatutia moyo kusoma kwa undani kuleta mapatano kwa maandiko wakati kunaoneka kwamba kuna ukinzani. Ni vyema kujuwa kwamba hakuja nakiliwa kuwa malaika waliua watu wakati wa huduma ya Yesu duniani. Je, hii ina mapatano kwa jinsi gani katika hadithi ya malaika wanaoua? Wacha tuanze na hadithi ya Daudi kuwahesabu Wanaisraeli. Je tunaelewaje fungu linalo fuata? Je Mungu alimfanya Daudi vipi ili awahesabu wanaisraeli.

> Tena hasira ya Bwana ikawaka juu ya Israeli, akamtia Daudi nia juu yao, akisema, Nenda, ukawahesabu Israeli na Yuda. 2 Samweli 24:1

Je tukilinganisha hii na hiyo hiyo hadithi mahali pengine, tunasoma hivi:

> Tena shetani akasimama juu ya Israeli, akamshawishi Daudi kuwahesabu Israeli. 1 Mambo ya Nyakati 21:1

Kama tutasoma 2 Samuel 24:1 *pekee* kisha tutake kusomwa wazi kwa hili fungu basi tutasema kwamba Mungu mwenyewe ndiye aliyemuongoza Daudi

ndiyo wanaisraeli 70,000 wauliwe. Je haya hayatualiki kuuliza vile wazo hili lina ambatana je na Mungu anayedai ni upendo?

Katika upelelezi ili kujibu swali hilo, tunatambua 1 Mambo Ya Nyakati 21:1 inadhihirisha kwamba shetani aliruhusiwa kumjaribu Daudi kuwahesabu wanaisraeli. Tunaalikwa kupatanisha hoja hizo mbili. Je tunatoa uamuzi wa mwisho kwamba Mungu na Shetani wanashirikiana kufanya kazi pamoja ilikuleta maangamizo ya wanaisraeli? Kwa mara nyengine tena tunaalikwa kuchimba ndani zaidi ilikupata ufumbuzi. Njia hii inajaribu mioyo ya watu kuona kwamba kama kweli wanaamini Mungu ni upendo, hakimu wa kutopenda, au sultani mkorofi. Wale ambao wanaona neema machoni mwa Bwana wataendelea kusoma mpaka wapatanishe hizo hoja, wengine wanaamini ukinzani na wanasema kwamba Mungu ni upendo ijapokuwa anafanya haya mambo.

Hapo awali katika historia ya Israeli, ombi lilitolewa kuweko mfalme kama mataifa mengine. Israeli alitaka kuwa kama wengine.

> wakamwambia, Angalia, wewe umekuwa mzee, na wanao hawaendi katika njia zako; basi, tufanyie mfalme atuamue, mfano wa mataifa yote. 1 Samweli 8:5

Ombi hili lilionyesha shauku ya ukuu wakitaifa. Walakini ombi hili kwa kweli lilikuwa kumkana Mungu.

> Bwana akamwambia Samweli, Isikilize sauti ya watu hawa katika kila neno watakalokuambia; kwa maana hawakukukataa wewe, bali wamenikataa mimi, ili nisiwe mfalme juu yao. 1 Samweli 8:7

Chimbuko hili lote la kifalme lilikuwa kukana uongozi wa Mungu. Ijapokuwa Sauli alianza vyema kama mfalme wa Israeli, unyonge wa tabia yake hivi karibuni ulionekana na hakuweza kuendeleza fahari ya kifalme ya Israeli mbali sana. Kwengineko Daudi aliwashinda maadui wa Israeli na chini ya uongozi wake taifa lilinawiri na kuwa kuu. Shetani alimjaribu Daudi kulinganisha ustawi wakati wake na ule uliopita na akaanza kumsifu mno. Mungu alituma ujumbe kwa Daudi kwa kupitia amri jeshi, Yoabu, lakini shetani alifanikiwa kumdanganya Daudi awahesabu wanaisraeli.

> Naye Yoabu akamwambia mfalme, Bwana, Mungu wako, na awaongeze watu, hesabu yao ikiwa yo yote, mara mia, tena macho

> ya bwana wangu mfalme na yawaone; ila kwa nini neno hili limempendeza bwana wangu mfalme? 2 Samweli 24:3

Bwana aliruhusu hili litendeke na hakuyazuia majaribu ya Shetani kwa Daudi. Kuanguka kulileta maradhi ya kuambukiza juu ya Israeli.

> Basi Bwana akawaletea [H5414] Israeli tauni tangu asubuhi hata wakati ulioamriwa; nao wakafa watu toka Dani mpaka Beer-sheba sabini elfu.2 Samweli 24:15

Neno la kiebrania kuleta kwa kweli ni *nathan* ambalo inamaanisha kumpa na saa zengine kukata tamaa. Nataka utazame kwa makini fungu linalofuata ukilinganisha na tauni na ahadi ya Mungu.

> Nami nitaleta upanga juu yenu, utakaopatiliza kisasi cha hilo agano; nanyi mtakutanishwa ndani ya miji yenu; nami nitaleta tauni kati yenu; nanyi mtatiwa[H5414] mkononi mwa adui. Walawi 26:25

Hapa *nathan* inatafsiriwa mtatiwa. Chunguza kwa makini sehemu ya mwisho wa fungu hili. Neno na limepewa na laweza kusomwa kwa urahisi:

> nami nitaleta tauni kati yenu; nanyi mtatiwa[H5414] mkononi mwa adui.

Hii inamaanisha tauni ikija ni kwa sababu wametiwa mikononi mwa adui.

> Aketiye mahali pa siri pake Aliye juu Atakaa katika uvuli wake Mwenyezi. (2) Nitasema, Bwana ndiye kimbilio langu na ngome yangu, Mungu wangu nitakayemtumaini. (3) **Maana Yeye atakuokoa na mtego wa mwindaji, Na katika tauni iharibuyo.** Zaburi 91:1-3

Ni Shetani ambaye anawaangamiza hawa watu. Hiari nyingine ni Mungu alimruhusu Shetani kumjaribu Daudi na Israeli na akawaongoza kwa dhambi na Mungu akageuka na kuwaponda watu 70,000. Nia hii haiambatani. Shetani aliamka na akaweza kumjaribu Daudi kwa sababu Daudi hakuwa akifanya kulingana na mapenzi ya Mungu. Wakati Daudi alishindwa na haya majaribu ilimpatia shetani nafasi kubwa kwa Israeli. Shetani alichukuwa manufaa ya hali vile ilivyo kuwa akaleta tauni kati yao. Lakini hii haifafanui malaika aliowapiga wanaisraeli.

> Lakini huyo malaika aliponyosha [H7971 mtuma, funguka] mkono wake kuelekea Yerusalemu ili auharibu, Bwana akaghairi katika mabaya, akamwambia huyo malaika mwenye kuwaharibu [H7483 tupa mavulio, legeza] watu, Yatosha, sasa ulegeze mkono wako. Naye yule malaika wa Bwana alikuwako karibu na kiwanja cha kupuria cha Arauna, Myebusi. (17) Daudi, alipomwoma malaika aliyewapiga watu, akanena na Bwana, akasema, Tazama, ni mimi niliyekosa, ni mimi niliyepotoka; lakini kondoo hawa, wamefanya nini? Mkono wako na uwe juu yangu, na juu ya nyumba ya baba yangu. 2 Samweli 24:16-17

Shetani ndiye mjumbe aliyeleta tauni lakini huu upanga ambao malaika wa Bwana aliounyosha juu ya Yerusalemu ni nini? Ni upanga gani ambao Mwana wa Mungu hutumia?

> Katika mkono wake wa kuume alishikilia nyota saba na kinywani mwake ulitoka upanga wenye makali kuwili. Uso wake kama jua kali linalong'aa kwa nguvu zake zote. (17) Nilipomwona, nilianguka miguuni pake kama aliyekufa. Ndipo akaweka mkono wake wa kuume juu yangu na kusema, "Usiogope, Mimi ni wa Kwanza na wa Mwisho. Ufunuo 1:16-17

Tunaona jinsi mtume Yohana alivyoshituka alipoona uso wa Mwana wa Mungu na upanga uliotoka kinywani mwake. Upanga ulikuwa nini?

> Kwa maana Neno la Mungu li hai tena lina nguvu tena lina makali kuliko upanga uwao wote wenye makali kuwili, tena linachoma hatakuzigawanya nafsi na roho, viungo na mafuta yaliyo ndani yake, tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. Waebrania 4:12

Kwa wale watu 70,000 ambao walikumbana na hasira ya mharabu, Roho wa Mungu aliwajia kuwadhibitishia hatia ya dhambi kwa undani ili waje tobani. Kazi ya kusadikisha dhambi kwa undani ni kazi ya haraka kwa sababu kama wangelikata kumsikiza Roho wa Mungu wangelikuwa hawana kinga na wangelikumbana na Shetani mharibifu. Kama wale watu wakati wa kulitakasa hekalu walikimbia mbali na Yeye. Kwa wale 70,000 walikimbia mbali na Yesu wakaenda mikononi mwa Shetani iliyowangoja kuwapokea ambaye aliyewakata na tauni. Wangelitubu dhambi zao na wamuombe Mungu msamaha lakini walikimbia mbali na uwepo Wake na kukatokea mauti.

Hii njia inafanana hakika vile Mungu alisema atawafanyia Wakanaani.

> Nitatuma utisho wangu utangulie mbele yako, nami nitawafadhaisha watu wote utakaowafikilia, nami nitawafanya hao adui zako wote wakuonyeshe maungo yao. (28) Nami nitapeleka mavu mbele yako, watakaomfukuza Mhivi, na Mkanaani, na Mhiti, watoke mbele yako. Kutoka 23:27-28

Kutuma utisho ni kusadikisha dhambi ambayo inayoleta hofu kwa mwenye dhambi. Mavu ni kuchomwa kwa hatia ya dhamiri inayoteswa na dhambi. Kuchomwa kunawafanya wakimbie kutoka uwepo wa Mungu na kuingia mikononi mwa adui. Kama wangelitubu na kuwa kama watoto wadogo wangeliokolewa. Sikila mtu alitoka hekaluni lakini wote walikumbwa na upanga.

Kwa hivyo tunaona kwa hadithi ya kuwahesabu Israeli katika jaribio la mwisho kuwafikia wale waliokuwa wakianguka mikononi mwa Shetani, Roho wa Mungu aliwajia na akatamani atakase roho zao kutoka dhambini iliwaokolewe lakini walikataa. Yesu aliyasema maneno ya kuhuzunisha "Nyumba yako imeachwa ukiwa." Neno upanga kwa kiebrania kwa kweli linamaanisha ukosefu, na roho ilimkana Yesu kabisa, Yeye alilazimishwa kuwaacha mikononi mwa Shetani kwa sababu walimkata aingie.

Hebu fikiria, Shetani pia hutawala mioyo ya watu. Kristo alikuwa akitafuta nafasi ya mwisho iliawafikie. Shetani aliamua asiache mateka wake na wakati ambapo moyo wa mwanadamu umekataa Kristo aingie, Shetani hutafuta kuwaifadhi pasipo hofu kwa kuchukua uhai wao badala ya kujihatarisha wanapotubu dhambi zao. Hatujui habari hii halisi kwa kinaganaga lakini njia si ngumu kufuata.

Shtaka la tolewa "Unafanya haya mafungu ya maandiko yawe ya kiroho." Biblia inatumia neno upanga na tunastahili kuchukulia ili neno vile lilowazi. Kwanza, ilikuwa tauni ambayo iliyowaua watu. Hawakufari kwa sababu ya upanga wa kiasili. Pili tunastahili kuleta vitu vyote ambavyo tunaweza kuleta pamoja ndipo tufikie uamuzi wa mwisho. Tazama kwa makini sheria ya 11 ya William Miller hapa sasa.

> Ilikujuwa kama neno limetumiwa kama fumbo. Kama linatoa maana inayofahamika vile hilo neno liko.Na halifunji sheria rahisi ya

> maumbile.Kwa hivyo linastahili kueleweka vile lilivyo au sivyo, fumbo.

Watu walivyo angamia kotokana na tauni, upanga ambao uliokuwako mikononi mwa malaika ulikuwa na kazi nyengine. Biblia inatuambia mahali pengine upanga ambao Kristo hutumia, upanga ni neno la Mungu. Tumeonyesha vile malaika aligonga watu na upanga lakini waliangamia kwa tauni. Je malaika wa Bwana aliwapigaje? Upanga ulikuwa neno likiwadhibitishia watu hatia ya makosa.Walikata kufia ubinafsi kwa kupitia huu upanga na Roho wa Mungu akawaacha na Mharabu akachukua uhai wao. Na je nini kilicho wafanya majeshi 185,000 ya Waashuri?

> Ikawa usiku uo huo malaika wa Bwana alitoka, akakiingia kituo cha Waashuri, akawapiga watu mia na themanini na tano elfu. Na watu walipoondoka asubuhi na mapema, kumbe! Hao walikuwa maiti wote pia. 2 Wafalme 19:35

Tazama kwa makini kwamba inasema malaika wa Bwana aliwapiga na wakapatikana asubuhi kuwa wamefariki. Haisemi, malaika wa Bwana aliwapiga kwa silaha kwa nguvu wakafa mara moja. Tukiangalia agano jipya tunaona kitu kinacho shangaza.

> Ghafula pakawa na tetemeko kubwa la ardhi, kwa sababu malaika wa Bwana alishuka kutoka mbinguni akaenda penye kaburi akalivingirisha lile jiwe na kulikalia. (3) Sura ya huyo malaika ilikuwa kama umeme na mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji.(4) Wale walinzi wa kaburi walimwogopa sana, wakatetemeka hata wakawa kama wafu. Matthayo 28:2-4

Kumwangalia malaika kuliwafanya watetemeke na wawe kama watu waliofariki. Tukio hili liliwatendekea watu wenye haki kama vile Danieli na Yohana.

> Nami, Danielii, nikaona maono haya peke yangu; maana wale watu waliokuwa pamoja nami hawakuyaona maono haya; lakini tetemeko kuu liliwashika, hata wakakimbia ili kujificha. (8) Basi nikaachwa peke yangu, nikaona maono haya makubwa, wala hazikubaki nguvu ndani yangu; maana uzuri wangu uligeuzwa ndani yangu kuwa uharibifu, wala sikusaziwa nguvu. Danieli 10:7-8

> Nilipomwona, nilianguka miguuni pake kama aliyekufa. Ndipo akaweka mkono wake wa kuume juu yangu na kusema, "Usiogope, Mimi ni wa Kwanza na wa Mwisho. Ufunuo 1:1

Katika kesi ya Yohana, ni Yesu ndiye aliyemwona katika njozi. Utakatifu na hali ya haki ya malaika inaweka wazi hali ya dhambi ya wanadamu kama vile Yesu na Baba.

Katika sura ya 10 tuliona ni nini kinachotendeka tukifika pahali Mungu yuko:

> **Nami nitawakaribieni ili kuhukumu**; nami nitakuwa shahidi mwepesi juu ya wachawi, na juu ya wazinzi, na juu yao waapao kwa uongo; na juu yao wamwoneao mwenye kuajiriwa, kwa ajili ya mshahara wake, wamwoneao mjane na yatima, na kumpotosha mgeni asipate haki yake, wala hawaniogopi mimi, asema Bwana wa majeshi. Malaki 3:5

Fikira zetu za kiasili wakati tunaposoma hili fungu ya nafikiria kwamba Mungu anaenda kuangamiza na kuwamaliza waasi katika hasira yake. Tena neno la Mungu linatumika kama kioo. Fungu linasema "Nami nitawakaribieni ili kuhukumu" Baba yetu anatakakutukaribia na kuhojiana nasi kuhusu dhambi zetu. Kumkaribia Yeye asiye na ubinafsi na ana upendo kunatuacha bila hiari bali kutubu au kukimbia kutoka kwa mwangaza. Ni vigumu kukaa tu katika uwepo wa Mungu. Wale ambao wanaozishikilia dhambi zao wanakimbilia kile wanacho fikiria ni uhai wao, lakini wanaonyesha kwamba wanapenda mauti na wanakimbia kutoka kwa uhai.

Hali ya malaika ni takatifu ambapo wakijidhihirisha, uwepo wao unafanya hofu ndani ya mioyo ya wanadamu na kufanya mioyo yao inyooke na wasiweze kutembea. Tunaendelea kusoma hadithi ya Danieli katika sura ya 10, tunaona Danieli ilibidi atiwe nguvu ili astahimili malaika mtakatifu.

> Walakini naliisikia sauti ya maneno yake; nami niliposikia sauti ya maneno yake, ndipo nikashikwa na usingizi mzito, na uso wangu umeielekea nchi. (10) **Na tazama, mkono ukanigusa, ukaniweka juu ya magoti yangu, na vitanga vya mikono yangu.** (11) Akaniambia, Ee Danielii, mtu upendwaye sana, yafahamu maneno nikuambiayo, ukasimame kiwima-wima; maana kwako nimetumwa sasa. Na aliponiambia neno hili, **nalisimama nikitetemeka**.(12) Ndipo akaniambia, **Usiogope, Danieli**; kwa maana tangu siku ile ya kwanza ulipotia moyo wako ufahamu, na kujinyenyekeza mbele

> za Mungu wako, maneno yako yalisikiwa; nami nimekuja kwa ajili ya maneno yako….(15) Na alipokwisha kusema nami maneno hayo, nikauelekeza uso wangu chini, nikawa bubu. (16) Na kumbe, mmoja mfano wa wanadamu akanigusa midomo yangu; ndipo nikafumbua kinywa changu, nikanena, nikamwambia yeye aliyesimama karibu nami, Ee Bwana wangu, kwa sababu ya maono haya huzuni zangu zimenipata tena; hata sikusaziwa nguvu. (17) Maana, mtumishi wa Bwana wangu huyu atawezaje kusema na Bwana wangu huyu? Kwa maana kwangu mimi, mara hazikusalia nguvu ndani yangu, wala pumzi haikusalia ndani yangu. (18) Kisha mmoja mfano wa mwanadamu akanigusa tena, akanitia nguvu. (19) Akasema, Ee mtu upendwaye sana, usiogope; amani na iwe kwako, uwe na nguvu, naam, uwe na nguvu. Aliposema nami nikapata nguvu, nikasema, Ee Bwana wangu, na aseme Bwana wangu; kwa maana umenitia nguvu. Danieli 10:9-12,15-19

Ilibidi malaika amuondolee Danieli mashaka, kwamba alipendwa sana mara mbili kwa hivyo hakustahili kuogopa. Hakuna dhambi iliyonakiliwa katika maisha ya Danieli na hivyo ndivyo mtu mzuri alivyo akiwa karibu na malaika mwenye haki. Malaika hakumtakia mabaya na alimdhibitishia upendo wa Mungu na Danieli alitetemeka na kutapatapa na uoga mpaka akaishiwa na nguvu na hii ilikuwa baada wiki nyingi za kuomba na kufunga. Kama haya mambo ya maisha yalimfanyikia mtu mwenye haki, je ni nini kitakacho mfanyikia muovu? Kama Danieli angekuwa karibu na malaika kwa muda mrefu bila kutiwa nguvu, kuna uwezekano angekufa ijapokuwa nia ya malaika kwa Danieli ilikuwa upendo.

Swali ambalo linastahili kuulizwa ni nini kilichosababisha Danieli kuogopa kabisa na kumfanya apoteze nguvu? Ilikuwa hali yake ya dhambi kukaribiana na hali takatifu ya malaika wa Mungu. Utakatifu na upendo bila ubinafsi ni moto unaoteketeza kwa binadamu mwenye dhimbi.

> Na kuonekana kwake ule utukufu wa Bwana kulikuwa kama moto uteketezao, juu ya mlima machoni pa wana wa Israeli. Kutoka 24:17

Je majeshi ya Wanawaashuri walikufa kwa ajili ya uoga walipo muona malaika? Kuna uwezekano. Je majeshi hawakuwezakujongea uwepo wa malaika uliowaacha kama wamezimia kwa sababu ya uoga kisha Shetani akachukua uhai wao kwa hasira katika hali yao ya unyonge? Hatujaambiwa. Tunaarifiwa ya kwamba jeshi lilikutana na malaika na asubuhi walifariki.

Ukisoma hii hadithi katika kioo cha miwani ya tabia ya Yesu utajuwa kwamba ilikuwa si nia ya malaika kuwauwa. Wakati Yesu alilitakasa hekalu, watu walikimbia kwa uoga lakini yoyote angeligeuka atubu na kumuomba Mungu msamaha kwa sababu ya maovu yao. Katika uwepo wa malaika,jeshi lilikuwa na fursa fupi ya kugundua uovu wa ndani. Malaika labda aliwakumba na dhambi zao na kuwatia moyo wa tubu mipango yao na waokolewe lakini walikataa akawaacha mikononi mwa Shetani. Hatuwezi kusema hivi kwa uhakika lakini twajua malaika wa Mungu wa mejazwa na tabia ya Yesu na Yesu hajamuua yoyote.

Tunajuwa wakati wa kurudi kwa Yesu kwa mara ya pili, waasi wataangamizwa na utukufu (mwangaza) wa kuja kwa Kristo.Hii inamaanisha ufunuo wa tabia ya Kristo unaleta mateso makali kwa mdhambi. Mateso yanakuja kwa sababu mdhambi amekataa kutubu. Mioyo yao inashindwa kwa ajili ya hofu. Maelezo ya njia hii yamenakiliwa katika kitabu cha pili cha Esdrasi katika Apokarifa.

> Lakini niliona alituma kutoka kinywani mweke kama ilivyokuwa mshindo wa ghafla wa moto, na kutoka mdomoni pumzi ya moto, na kutoka katika ulimi wake alitoa miyale ya moto na tufani (11) Nazote zilichanganyika pamoja, mshindo wa ghafla wa moto, pumzi ya moto, miyale ya moto na tufani, na zilianguka kwa vishindo kwa watu waliojitayarisha kupigana,na kila mmoja akateketezwa, hadi kwa halaiki ya watu isiyohesabika,hakuna kilicho onekana,bali vumbi na harufu ya moshi: Nilivyo ona niliogopa. 2 Esdrasi 13:10-11
>
> Nionyesha sasa hata sasa fasiri ya hii ndoto. 2 Esdrasi 13:15
>
> Na halaiki ya watu isiyohesabika watakusanywa pamoja, kama vile ulivyo Waona, wanaotaka kuja na kumshinda vitani. (35) Lakini atasimama juu ya Mlima Sayuni. (36) Na Sayuni itakuja na itaonyeshwa watu wote,iliyoandaliwa na kujengwa,kama vile uliona mlima kuchongwa bila mkono (37) Na huyu Mwanangu atakemea ugunduzi wa uovu wa hayo mataifa,ambayo kwa uovu wa maisha yao ya naporomoka kwa tufani; (38) Na ataweka wazi mbele yao mawazo yao ya uovu,na kuteswa wataanza kuteseka ni kama moto:na atawaangamiza bila kazi kwa sheria ambayo kama mimi. 2 Esdrasi 13:34-38

Kupigwa kwa Waashuri na malaika wa Bwana inaonyesha kwamba hili ni neno la Mungu linalowasadikisha hawa watu dhambi zao. Ilianguka kama tufani kuu juu yao na kukataa kwao kutubu kulisababisha uchungu.

> Watu wakaunguzwa na hilo joto kali, lakini wakalaani Jina la Mungu, aliyekuwa na uwezo juu ya mapigo haya, wala hawakutubu na kumtukuza M ungu. (10) Malaika wa tano akamimina bakuli lake kwenye kiti cha enzi cha yule mnyama, nao ufalme wake ukagubikwa na giza. Watu wakatafuna ndimi zao kwa ajili ya maumivu (11) wakamlaani Mungu wa mbinguni kwa sababu ya maumivu na majeraha yao, wala hawakutubu kwa ajili ya matendo yao maovu. Ufunuo 16:9-11

"Waliangamizwa bila kazi kwa sheria ambayo ni" nakala ya tabia ya Mungu.Je huu si huo moto ambao uliowateketeza wanawa Haruni wawili Nadabu na Abihu wakati walipoleta moto geni hekaluni? Hata moto kutoka kwa Bwana uliwateketeza wa kabebwa na nguo zao.

> Kisha moto ukatoka hapo mbele za Bwana, nao ukawala, nao wakafa mbele za Bwana. (3) Ndipo Musa akamwambia Haruni, Jambo hili ni hilo Bwana alilolinena, akisema, Nitatakaswa mimi katika hao wanikaribiao, nami nitatukuzwa mbele ya watu hao wote. Haruni akanyamaza kimya. (4) Musa akawaita Mishaeli na Elisafani, wana wa Uzieli mjombaye Haruni, na kuwaambia, Njoni karibu, mwachukue hawa ndugu zenu, mkawaondoe hapa mbele ya maskani, mwende nao nje ya marago. (5) **Basi wakaja karibu, na kuwachukua, hali wamevaa nguo zao, wakawachukua nje ya marago**; kama Musa alivyosema.Walawi 10:2-5

Tena njia nyengine ambayo inatutambulisha kwamba hili pigo ni kusadikishwa kwa dhambi kwa neno ni kwa njia neno hili limetumika;

> Lakini halafu, **moyo wake Daudi ukamchoma** [H5221], kwa sababu amekata upindo wa vazi lake Sauli. 1 Samweli 24:5

> **Ndipo moyo wake Daudi ukamchoma**[H5221], baada ya kuwahesabu hao watu. Naye Daudi akamwambia Bwana, Nimekosa sana kwa haya niliyoyafanya; lakini sasa, Ee Bwana, nakusihi uuondolee mbali uovu wa mtumishi wako; kwani nimefanya upumbavu kabisa. 2 Samuel 24:10

Neno hili ni sawa kama 2 Wafalme 19:35

> Nimepata leo miaka themanini; nami je! Naweza kupambanua mema na mabaya? Mimi mtumwa wako, je! Naweza kuonja nilacho au ninywacho? Naweza kusikia tena sauti ya waimbaji waume na wake? Kwa nini basi mtumwa wako amlemee bado bwana wangu mfalme? 2 Wafalme 19:35

Hadithi yetu ya mwisho katika orodha yetu ni kifo cha herode.

> Ghafula, kwa kuwa Herode Agripa hakumpa Mungu utukufu, malaika akampiga, akaliwa na chango akafa. Matendo 12:23

Kutoka kwa mifano ya hapo awali, hii hadithi ni rahisi kuelezea. Herod alivunja sheria na akavunja ahadi ya milele. Neno la Mungu lilimsadikisha tabia zake za dhambi iliaje tobani. Kusadikishwa kulimsababishia maumivu makuu rohoni hata hivyo alikataa kutubu. Huku kukataa kwake kulimpatia Shetani mwanya wa kumuua kwa ugonjwa. Herode alipewa adui kwa sababu aliivunja ahadi.

> Nami nitaleta upanga juu yenu, utakaopatiliza kisasi cha hilo agano; nanyi mtakutanishwa ndani ya miji yenu; nami nitaleta tauni kati yenu; nanyi mtatiwa mkononi mwa adui. Mambo ya Walawi 26:25

Kristo alimletea Herode upanga wa neno lake.Herode alikataa kutubu na kwa hivyo "alitiwa mkononi mwa adui" ambaye alimletea tauni. Je kuna tofauti gani kati ya pigo Herode aliona ukilinganisha na la Petero? Petero akitembea kwa nguvu za Pentekosti alikuwa na dhamira safi, Herode hakuwa nayo. Petero alitiwa korokoroni kwa sababu ya kuhubiri kwa jina la Yesu na alikuwaakingoja kunyongwa. Wakati malaika alimuamsha Petero hakuwa na uoga kwa kuwepo kwa malaika. Herode aliona kitu tofauti kabisa. Kwake ilikuwa mshindo wa ngurumo.

> Baba, litukuze Jina Lako. "Ndipo ikaja sauti kutoka mbinguni, "Nimelitukuza, nami nitalitukuza tena." (29) Ule umati wa watu uliokuwa mahali pale uliisikia nao ukasema, "Hiyo ni sauti ya radi", wengine wakasema, "Malaika ameongea naye." Yohana 12:28-29

Pigo hilo ambalo lingekuwa sauti ndogo tulivu ilikuwa kama mshindo wa ngurumo kwa Herode na aliogopa mpaka kifo. Malaika hawana muelekeo wa kuwauwa watu; wanafahamu kwamba uovu wa wanadamu ukifunuliwa na utakatifu wa umetosha kuwauwa bila nia yoyote upande wao. Malaika

wanapita katikati ya watu wakiwaziba watu kila saa kutoka kwa uwepo wa kamili kuwalinda. Rehema zao kwetu za shangaza!

Je, tunaona malaika ambao wanaogonga wakisababisha kifo kama neno la Mungu likiwasadikisha watu dhambi zao. Mateso ya dhambi za mtu binafsi ndio zinazo sababisha maumivu makali ya akili. Kuwepo kwa tauni inaonyesha kwamba Roho wa Mungu amekwisha tolewa na mharabu anafanya kazi yake kwa kuwa Mungu huacha kuwalinda wale wanaokataa kutubu. Ni dhambi ambayo inaadhibu dhambi. Malaika wa Mungu wa mejazwa na Roho ya Yesu. Wanatunza amri za Mungu na hawatikisi mkononi upanga wa kawaida. Wana nguvu kutoka kwa neno la Mungu na wamejawa na haki ya Yesu. Usafi, upendo na utakatifu wao ni tisho kwa uovu wa wadhambi na utakatifu wao unaleta hofu kwa mioyo ya wasiohaki. Utakatifu wao ndio nguvu yao pia wana mamlaka za kuzuia nguvu za yule muovu. Kwa hivyo malaika watakatifu wana nguvu nyingi mno. Wakiamriwa walegeze mikono yao na waache kazi yao ya kulinda, wanaacha nguvu za hasira kamili za Shetani kuachiliwa. Ijapokuwa hawapendi kufanya hivyo, huwa wanafanya hivyo waki amrishwa. Hili la tendeka kama mtu anapopuuza onyo la Mungu na anaendelea kuvunja amri za Mungu. Baada ya miaka mingi ya Kustahimili mwishowe Roho wa Mungu kwa huruma humuacha mwenye dhambi awe na Bwana aliyemchagu Je tuna heri kuwa na ulinzi na muongozo wao. Wakati mwingine wanajidhihirisha kwa watu kuwazuia watu kwa matendo yao maovu, lakini wanadamu wamekata kauli kufuata njia yao ya dhambi na afadhali wafe kwa uoga badala ya kutubu na kuokoka. Huo ndio uovu wa moyo wa binadamu. Hatuna kitu cha kuogopa kwa malaika wa Mungu, hakuna vile wanaweza kugeuka kotoka kuwa walinzi wetu na kuwa wauwaji wetu. Kila siku wanapanda na kushuka kutoka kwa Mwana wa Adamu ambaye hakumuuwa yeyote.

## 18. Kauli Wazi

Kabla ya kuendelea kutowa mifano mingine kwa Biblia kuhusu kana kwamba Mungu anaonekana kuuwa watu, tunahitaji kujikumbusha na kutumia mafunzo tulioona na kuanzisha hapo awali.

Ni rahisi sana kuchukuwa sehemu tofauti za Biblia na kuziweka pamoja na kujenga hoja ambayo inayoharibu ukweli kwamba Mungu kweli ni upendo, mpole na mkarimu.Nimeambiwa mara nyingi unasema kwamba "Unasema kwamba Mungu hauwi watu lakini Biblia inasema wazi kwamba anafanya hivyo" Nitaorodhesha mafungu ambayo yanayo tumika kudhibitisha hivi. Ukiziweka kwa pamoja inaonekana kuonyesha kesi iliyo thabiti kwa watu wengi.

> Bwana akasema, Nitamfutilia mbali mwanadamu niliyemwumba usoni pa nchi; mwanadamu na mnyama, na kitambaacho na ndege wa angani; kwa maana naghairi ya kwamba nimewafanya. Mwanzo 6:7

> Ndipo Bwana akanyesha juu ya Sodoma na juu ya Gomora kiberiti na moto toka mbinguni kwa Bwana. Mwanzo 19:24

> Naye Eri, mzaliwa wa kwanza wa Yuda, alikuwa mbaya machoni pa Bwana; na Bwana akamwua. Mwanzo 38:7

Neno hili alilolifanya likawa baya machoni pa Bwana, basi akamwua yeye naye. Mwanzo 38:10

basi ilikuwa hapo Farao alipojifanya kuwa mgumu ili asitupe ruhusa kuondoka, Bwana akawapiga wazaliwa wa kwanza wote waliokuwa katika nchi ya Misri, wa binadamu na wa mnyama; kwa ajili ya hayo namtolea Bwana wote wafunguao tumbo, wakiwa waume; lakini wazaliwa wa kwanza wote wa wana wangu nawakomboa.Kutoka 13:15

Bwana akamwambia Musa, Nyosha mkono wako juu ya bahari, ili maji yarudi tena juu ya Wamisri, juu ya magari yao, na juu ya farasi zao. (27) Musa akaunyosha mkono wake juu ya bahari, na kulipopambazuka, bahari ikarudi kwa nguvu zake; Wamisri wakakimbia mbele yake; na Bwana akawakukutia mbali hao Wamisri kati ya bahari. (28) Yale maji yakarudi yakafunikiza magari na wapanda farasi, hata jeshi lote la Farao lililoingia katika bahari nyuma yao; hakusalia hata mtu mmoja.Kutoka 14:26-28

Tena Bwana akamwambia Musa, Mimi nimewaona watu hawa, na tazama, ni watu wenye shingo ngumu 10 basi sasa niache, ili hasira zangu ziwake juu yao, niwaangamize, nami nitakufanya wewe uwe taifa kuu. Kutoka 32:9-10

Akawaambia, Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi, Kila mtu na ajifunge upanga wake pajani mwake, akapite huko na huko toka mlango hata mlango kati ya marago, mkamchinje kila mtu ndugu yake, na kila mtu mwenziwe na kila mtu jirani yake. (28) Na hao wana wa Lawi wakafanya kama vile alivyosema Musa, wakaanguka siku ile kama watu elfu tatu. Kutoka 32:27-28

Na Nadabu na Abihu, wana wa Haruni, wakatwaa kila mtu chetezo chake, wakatia moto ndani yake, wakatia na uvumba, nao wakatoa moto wa kigeni mbele ya Bwana, ambao yeye hakuwaagiza. (2) Kisha moto ukatoka hapo mbele za Bwana, nao ukawala, nao wakafa mbele za Bwana. Walawi 10:1-2

Kisha hao watu walikuwa kama wanung'unikao, wakinena maovu masikioni mwa Bwana; Bwana aliposikia hayo, hasira zake zikawaka; na moto wa Bwana ukawaka kati yao, ukateketeza katika mipaka ya mwisho wa marago. Hesabu 11:1

Kisha Bwana akamwambia Musa, Watwae wakuu wote wa hao watu, ukamtungikie Bwana watu hao mbele ya jua, ili kwamba hizo hasira kali za Bwana ziwaondokee Israeli. Hesabu 25:4

Nao wakapigana na Midiani kama Bwana alivyomwagiza Musa; nao wakamwua kila mume. Hesabu 31:7

wakati Bwana, Mungu wako, atakapowatoa mbele yako, nawe utawapiga; wakati huo ndipo uwaondoe kabisa; usifanye agano nao, wala kuwahurumia; wala usioane nao; Kumbukumbu la Torati 7:2

Fahamu sasa ya kuwa Mimi, naam, Mimi ndiye, Wala hapana Mungu mwingine ila Mimi; Naua Mimi, nahuisha Mimi, Nimejeruhi, tena naponya; Wala hapana awezaye kuokoa katika mkono wangu, Kumbukumbu la Torati 32:39

Bwana naye akawatapanya mbele ya Israeli, naye Israeli akawaua uuaji ulio mkuu hapo Gibeoni, akawafukuza waikimbilie hiyo njia ya kukwelea kwenda Beth-horoni, na kuwapiga hata kufikilia Azeka, tena hata kufikilia Makeda. (11) Kisha ikawa, hapo walipokuwa wakimbia mbele ya Israeli, hapo walipokuwa katika kutelemkia Beth-horoni, ndipo Bwana alipowatupia mawe makubwa kutoka mbinguni juu yao hata kufikilia Azeka, nao wakafa; hao waliokufa kwa kuuawa na hayo mawe ya barafu walikuwa ni wengi kuliko hao waliouawa na wana wa Israeli kwa upanga. Yoshua 10:10-11

Bwana wa majeshi asema hivi, Nimeyatia moyoni mwangu mambo hayo Amaleki waliyowatenda Israeli, jinsi walivyowapinga njiani, hapo walipopanda kutoka Misri. (3) Basi sasa enda ukawapige Amaleki, na kuviharibu kabisa vitu vyote walivyo navyo, wala msiwaachilie; bali waueni, mwanamume na mwanamke, mtoto naye anyonyaye, ng'ombe na kondoo, ngamia na punda. 1 Samweli 15:2-3

Tunaweza kuorodhesha mafungu mengi zaidi kama haya. Zipo hadithi nyingi katika agano la kale ambazo zinazosomeka wazi lakini hata ukizijumlisha hizo hadithi huuwezi kulinganisha machinjo kwa wingi ya watu ya nayosimuliwa katika agano jipya.

Hiyo miaka 1,000 itakapotimia, Shetani atafunguliwa kutoka kifungoni mwake, (8) naye atatoka ili kuyadanganya mataifa yaliyopo katika pembe nne za dunia, yaani, Gogu na Magogu apate kuwakusanya tayari kwa vita. Idadi yao ni kama mchanga ulioko

> Pwani. (9) Nao walitembea katika eneo lote la dunia, wakaizunguka kambi ya watakatifu na ule mji uliopendwa. Lakini moto ukashuka kutoka mbinguni na kuwateketeza.(10) Naye Ibilisi aliyewadanganya akatupwa katikaziwa la moto na kiberiti alipo yule mnyama na yule nabii wa uongo. Nao wakateswa huko mchana na usiku, milele na milele. Ufunuo 20:7-10

Inasema kwamba waovu watakuwa kama mchanga ulioko pwani? Je ni punje ngapi za mchanga zilizoko ufuoni mwa bahari? Tunaweza kushauri tarakimu iliyohifadhiwa 100 mamilioni milioni ya watu ambao wanaonekana wote wakipiga mayowe na kuzoma wakiwa katika maumivu mabaya kushinda yote. Hii linafanya hadithi za Agano la Kale kuwa kama hekaya za chuo cha watoto kwa mlinganisho.

Wakristo wengi, katika kwa ushindi wa ajabu, husoma maandishi haya na kutangaza ya kwamba inathibitisha ya kuwa Mungu wanaye "muabudu" anapasisha maumivi makuu kwa mamilion milioni na mamilioni milioni ya watu ambao walimwasi Yeye kwa kuwachoma wakiwa hai kwa kipimo kizuri.

Inakubalika kwamba mafungu ambayo yanazungumza, inaonekana kana kwamba Mungu anaamrisha kukatwakatwa kwa watoto wadogo mpaka wafe, kwa hila yana achiliwa isipokuwa kwa wale watu sugu na wagumu ambao kwa njia nyengine wanaweza kulinda tabia yake ya uuaji kama ni tabia ya uungu.

Kile wanachodhania kama ni ushahidi wa ushindi kweli unakuwa ni dhibitisho la kushindwa kabisa.

Ni nani anayefiria vizuri anaweza kuwaza kuishi milele karibu, na pia kupiga magoti akiabudu kiumbe kikatili mno, na akiendelea kujiaminisha asihisi hofu bila tumaini kwamba siku moja wewe pia utauwawa.

Kama kusoma vizuri hizi hadithi zinamaanisha Mungu anatuma mashuka ya moto kutoka kwake kuelekezwa waasi, na wateule wote wakitazama matukio kama sinema kutoka kwa kuta za Sayuni wakisikia unyende na ukelele kwa sababu ya maumivu ya waliolaaniwa milele, kusema kweli,je watakatifu watafurahi kama wapendwa wao waliokata ukweli wakiteketezwa (iwe kwa masaa machache au milele) bila huruma yoyote. Je kuna kutosheka kitakatifu kwamba Mungu unaye muabudu hawauwi tu jamii yako wakaidi bali huwatesa na kuwauwa polepole katika hofu kuu isiyoeleweka?Najuwa

huenda wengine watasema Mungu atawafuta machozi kutoka machoni mwao na afute ya kale kutoka akilini mwao.

> Atafuta kila chozi, kutoka katika macho yao. Mauti haitakuwepo tena, wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu, kwa maana mambo ya kwanza yamekwisha kupita." Ufunuo 21:4

Je hiki ni kipeo cha furaha ya milele kinachotamaniwa, au ni kuharibu sababu na yeye aliyemkatili na mkali mno?

Kuna kitu ambacho cha fadhaisha kabisa katika hii picha kwa yoyote anayefiria na amewahi kuona furaha ya upendo wa ndoa, au amemmbeba mtoto mikononi mwake au kulala karibu sana na upendo wa mzazi, au wale wameweza kuwatunza wanyama wao kama vile farasi,mbwa au paka.

Matumizi ya maandiko haya ni kwa njia ambayo inaambatana na maadai kuwa Bibilia inastahili kuchukuliwa vile inavyo soma na ukubali wazi masimulizi kama thibitsho kuwa Mungu anawauwa waovu.

Ni kweli kabisa Bibilia lazima ichukuliwe vile inavyosoma na kuchukuwa Bibilia vile inavyosoma ina maanisha kuchukuwa Bibilia yote na si sehemu zingine za Bibilia ambazo zinafaa ubishi tunaoufanya.

Kama tulivyojifunza katika sura ya pili, lazima tuchukuwe mafungu yote juu ya hiyo mada na kuyaweka pamoja. Wale ambao wanaofika tamati kwamba Mungu anawauwa watu hawasomi Bibilia yote. Ukisoma Bibilia yote utawekwa mahali ambapo vitu havi ingiani. Hebu fikiria haya:

| Mpole, Mvumilivu na Upendo, | Mlipiza kisasi, Mwenye Chuki, Muangamizi. |
|---|---|
| Mathayo 26:52 Ndipo Yesu akamwambia, "Rudisha upanga wako mahali pake, kwa maana **wote watumiao upanga watakufa kwa upanga.** | Kumbu 32:40-41 Maana, nainua mkono wangu mbinguni, Na kusema, Kama Mimi niishivyo milele, (41) Nikiunoa **upanga wangu wa umeme, Mkono wangu ukishika hukumu, Nitawatoza kisasi adui zangu,** Nitawalipa wanaonichukia. |
| Luka 9:56 Kwa kuwa Mwana wa Mungu hakuja kuangamiza maisha ya watu bali kuwaokoa.<br>Isa 11:9 Hawatadhuru wala | Mwanzo 6:7 Bwana akasema, Nitamfutilia mbali mwanadamu niliyemwumba usoni pa nchi; mwanadamu na mnyama, na kitambaacho na ndege wa angani; kwa |

| | |
|---|---|
| hawataharibu katika mlima wangu wote mtakatifu; maana dunia itajawa na kumjua Bwana, kama vile maji yanavyoifunika bahari. | maana naghairi ya kwamba nimewafanya. |
| Math5:44 Lakini mimi ninawaambia : Wapendeni adui zenu na waombeeni wanaowatesa ninyi, | Zaburi 18:40 Naam, adui zangu umewafanya wanipe visogo, Nao walionichukia nimewakatilia mbali.<br>Zaburi 143:12 Kwa fadhili zako utawakatilia mbali adui zangu; Na kuwaangamiza wote wanitesao nafsi, Kwa maana mimi ni mtumishi wako. |
| Kutoka 20:13 Usiue.<br>2Wakorintho 4:18 Nasi sote, tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji **tunaakisi utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo. Nasi tunabadilishwa ili tufanane naye,** toka utukufu hadi utukufu mkuu zaidi, utokao kwa Bwana, ambaye ndiye Roho. | Mwanzo 38:7 Naye Eri, mzaliwa wa kwanza wa Yuda, alikuwa mbaya machoni pa Bwana; na Bwana akamwua.<br>Muhubiri 3:3Wakati wa kurarua, na wakati wa kushona; Wakati wa kunyamaza, na wakati wa kunena; |
| 1Yohana 4:8 Yeye asiyependa hamjui Mungu, kwa sababu Mungu ni upendo. | Mal 1:2-3 Nimewapenda ninyi, asema Bwana. Lakini ninyi mwasema, Umetupendaje? Je! Esau siye ndugu yake Yakobo? Asema Bwana; ila nimempenda Yakobo ; (3) **bali Esau nimemchukia** na kuifanya milima yake kuwa ukiwa, na urithi wake nimewapa mbweha wa nyikani. |
| Zaburi 100:5 Kwa kuwa Bwana ndiye mwema; Rehema zake ni za milele; Na uaminifu wake vizazi na vizazi.<br>1 Mambo ya Nyakati 16:34 Mshukuruni Bwana kwa kuwa ni mwema; Kwa maana fadhili zake ni za milele. | Isa 9:17 Kwa sababu hiyo Bwana hatawafurahia vijana wao, wala hatawahurumia yatima zao wala wajane wao; maana kila mtu ni mnajisi, dhalimu, na kila ulimi hunena upumbavu. Pamoja na hayo yote hasira yake haikugeukia mbali, lakini mkono wake umenyoshwa hata sasa. |
| Isa 27:4 Hasira sinayo ndani yangu; Kama mibigili na miiba ingekuwa mbele zangu, Ningepanga vita juu yake, Ningeiteketeza yote pamoja | Ayubu 20:23 Hapo atakapo kulijaza tumbo lake, Mungu atamtupia ukali wa ghadhabu zake, Na kuunyesha juu yake akiwa anakula. |

Ukisoma Biblia kwa makini inaonekana kwamba hitilafu inaanza kujitokeza. Katika sehemu ya ukinzani ni lazima ufanye uchaguzi wa kupuuza sehemu ambazo haziambatani na yale ambayo unayo ya fahamu au unyenyekee kwa kupiga magoti mbele ya Mungu na kumuomba akufunze jinsi ya kusoma Biblia na kupatanisha ukinzani.

Swali ni kwa nini Mungu aliandika Bibilia kwa njia hii? Mbona haingeandikwa kwa njia rahisi kuliko vile ilivyo. Mtu ambaye hajabadilika yeye kwa asili huwa ni mwenye kiburi. Na pia ana asili ya uhasama kwa Mungu ijapokuwa hajui kuhusu hivyo.

> Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui na Mungu, kwa maana haiitii sheria ya Mungu,wala haiwezi kuitii. Warumi 8:7

Uadui wake wa asili utamfanya kusoma Bibilia kwa njia ambayo inaamfunua Mungu kuwa mkatili na mdhulumu. Mtu kama huyo anaweza kuoneka kwamba anampenda na kumtukuza Mungu walakini uadui wake wa asili haukubali kushinda huu ukinzani; bali utachaguwa kosoma mufungu yote ambayo ya na mfunua Mungu kama muuaji halafu anasema kwa sauti ya unyenyekevu  lazima tukubali vile Bibilia inasema.

Lakini mtu kama huyo kwa kweli hakubaliani na yote Bibilia inasema. Mtu huyu anakubali yale ambayo anataka kukubali na anapuuza sehemu ambazo zinaonyesha Mungu kwa Mwangaza tofauti. Kwa hii njia tunagunduwa ukweli kwamba:

> "….Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema." Yakobo 4:6

Je hii inafanya kazi vipi?

> Kwa maana kama mtu ni msikiaji tu wa Neno wala hatendi kile linachosema, yeye ni kama mtu ajitazamaye uso wake kwenye kioo Yakobo 1:23

> Kwa maana kwa jinsi ile unavyowahukumu wengine, ndivyo utakavyohukumiwa na kwa kipimo kile utakachotoa ndicho utakachopokea. Mathayo 7:2

> Kwa hiyo huna udhuru wo wote, wewe mtu uwaye yote, utoaye hukumu kwa mwingine, kwa maana katika jambo lo lote

> unalowahukumu wengine, unajihukumu wewe mwenyewe kwa sababu wewe unayehukumu. Warumi 2:1

Mtu akisoma Bibilia na akipuuza mafungu ambayo yanamzungumzia kabisa Mungu wa upendo na achague yale ambayo yaonekana kana kwamba yanamzungumzia Mungu anayeuwa watu,anafunua tabia yake. Huyo mtu kama Shetani anabandika tabia yake kwa Mungu na anafunua uhasama kwa Mungu.

> Ndivyo ulivyofanya, nami nikanyamaza; Ukadhani ya kuwa Mimi ni kama wewe. Walakini nitakukemea; Nitayapanga hayo mbele ya macho yako. Zaburi 50:21

Mungu amevuvia Bibilia iandikwe kwa njia ambayo inafunua tabia ya Mwanadamu. Asili ya mwanadamu ya makufuru huwainapenda kumfanya Mungu kwa mfano wake. Inaelekeza asili na hukumu ya Mungu kwa hivyo Bibilia kwa uangalifu imebuniwa kufanya kioo kwa roho za wanadamu.

Mtu ambaye hajabadilika akisoma Bibilia anaona picha tofauti ya Mungu Tabia ya Kristo inafunuliwa kwa wanadamu duniani inabadilisha mfano ndani ya kioo cha Bibilia na magamba ya nyoka yanaanguka kutoka machoni pake na anaona kile kwa kweli ni chenye thamani ambacho cha furahisha moyo. Mtu wa asili anasoma sehemu ya maandiko ambayo inakubaliana na mawazo yake na anapuuza sehemu zengine, ama anaona ukinzani wa juujuu na kisha anaikataa kabisa Bibilia.

Mtu wa kiroho anasoma maandiko yote na kisha ananyenyekezwa na ukinzani unaoonekana. Yeye hukubali unyonge wake wa kutofahamu kabisa neno la Mungu na anaomba uzaidizi kuelewa. Wakati anapofunzwa Bibilia inaanza kumfunulia tabia nzuri ya Mungu. Inahitaji maombi sana na unyenyekeve kuweka vipande pamoja vile Mungu ange tarajia. Haya ndiyo yamekuwa maono yangu na maono ya wengine. Nimemsihi Bwana nikisoma sehemu ambazo haziambatani na fikira zangu. Ninapiga magoti na kuomba Baba nisaidie na unionyeshe ukweli. Ni furaha wakati ukweli unapofunuliwa baada ya jitihada za maombi.

Tukiangalia hadithi zifuatazo, hatuta chukuwa tu fungu moja au mafungu mawili ilitufanye uamuzi wa mwisho lakini lazima tukusanye mafungu yote kuhusu mada hii na kuyaleta pamoja ili yaambatane.

Tutakumbuka chimbuko la kioo, Katika sura ya 9 tulijifunza kwa kupitia hadithi ya mwanamke ambaye alimwuliza Yesu amponye bintiye na Yesu kwa uangalifu alitunga lugha yake ilikuwa ruhusu wasikilizaji wake wa mrushie uamuzi wao kwake.

Mapendeleo ya kitaifa ya wanafunzi wake yalionekana kabisa kwa kupitia kioo ambacho Yesu alikituimia ili kuwasaidia kuona makosa yao wakati alisikia ombi la yule mke. Katika hadithi ya tajiri na Lazaro tulijifunza kwamba Yesu atatumia hadithi inayofahamika na mawazo ya wasikilizaji kufunza ukweli muhimu. Haya mawazo si Yake, lakini anayatumia ilikuwafundishe nasi pia tuelewe. Hili ni chimbuko muhimu kufahamu tukisoma maandiko. Yesu anaweza kutumia lugha na maneno ambayo si Yake na kama mtu hatafuti kuweka pamoja Bibilia yote haya mafungu yanaweza kutumika kudhibitisha mawazo ya uongo ya msomaji. Kwa mara nyengine tena kioo cha fanya kazi.

Wacha tufanye muhtasari ya baadhi ya chimbuko muhimu kabla hatuja endelea.

1. Tuchukuwe mafungu yote katika mada, usichaguwe tu yale unayoyataka.
2. Njoo kwa unyenyekevu kwa maandiko ukiomba hekima.
3. Soma Bibilia kwa kupitia maisha ya Yesu duniani.
4. Kila siku tilia maanani chimbuko la kioo. Bibilia inaweza kusimulia mawazo yaliyoshikwa na watu kupitisha ukweli wa Bibilia. Bibilia ina weza kunukuliwa kwa njia inaweza kusomeka kimaumbile au kiroho. Msomaji ataamua vile inavyosomwa.

## 19. Alijeruhiwa kwa Makosa Yetu

Ingelikuwa sehemu ya mchezo wa hofu kuu isiyoweza kufikiriwa. Watu na wanyama walikuwa wakikimbilia maisha yao kwa hofu nyingi.

> Katika mwaka wa mia sita wa maisha ya Nuhu, mwezi wa pili, siku ya kumi na saba ya mwezi, siku ile chemchemi zote za vilindi vikuu zilibubujika kwa nguvu, madirisha ya mbinguni yakafunguka. (12) Mvua ikanyesha juu ya nchi, siku arobaini mchana na usiku. Mwanzo 7:11-12

Hadithi ya gharika iliyoathiri ulimwengu wote inawasumbua wengi. Je ni kweli Mungu anaweza kuwafanya mamilioni ya watu kufa maji kwa sababu huruma zake zimemalizika na mkono wake wa upondaji wa hukumu hautawezwa kuzuiliwa? Je Mungu wa upendo anaweza kufanya hivyo kweli? Kwa wengi hili ni fumbo la ajabu.

Tukiangalia swali la hukumu ya Mungu, lazima tuangalia kifo msalabani mbele yetu kila siku kwa sababu msalaba unatufunulia vile hukumu ya Mungu inavyo fanya kazi. Kifo msalabani ndiyo ufunguo wa kuangalia hukumu zote ndani ya Bibilia. Yesu alibeba dhambi za watu wote, na uzito wa dhambi ulimponda na ukafinya maisha yake ikisaidiwa na fikira za uwaji wa wale waliomtafuta kummuwa. Ni dhambi ndiyo iliyomuua Kristo na ni

dhambi iuwayo watu wote. Shida ni kwamba watu wanafikiria ni ghadhabu ya Mungu iliyotaka kifo cha Kristo. Isaya alitabiri.

> Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa. (5) Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Isaya 53:3-4

Tukimuangalia Kristo ya kuwa amepigwa na Mungu msalabani basi hadithi zote katika Bibilia ambazo zinafunua hukumu juu ya wenye dhambi zitaonekana kana kwamba Mungu anawapiga. Hebu tuangalia hadithi ya gharika kwa makini.

Mtu kwa unyenyekevu anatembea katika duka la vyakula na anamjulisha mwenye duka kwamba kuna hatari inayoonekana katika biashara yake. “kuna hatari inayokuja kwa biashara yake na familia yake, ” anasema “hakuna kitu ambacho kinacho weza kuzuia hayo maangamizi ila uje kwa ulinzi wetu” anaendelea kusema “tumepeana safina ya usalama kwa wale ambao wanaotutambua sisi kama walinzi wa uhuru.” Huyo mtu anamjulisha kwamba amekuja kwa ajili ya utume wa neema wa kumuokowa mwenye duka kwa maangamizo fulani. Kwa kubali msaada na tegemeo la huyu mtu mwenye duka atanusurika maangamizo ya nayowajia wenye maduka yote ambao wamekataa huo ulinzi. Mtu huyu kwa unyenyekevu anaweka mikono yake mabegani mwa mwenye duka akimsihi tafakari kwa makini huu uzaidizi wa “neema.” Hatungependa madhara yoyote ya kujie na familia yako. Tutakuwa na huzuni kuhusu hayo madhara.” Kwa hivyo anamuhimiza akubali masharti ya neema ya ulinzi huo.

Kama huyu mtu anayetowa ulinzi akijitenga basi atajihusisha na kosa la uhalifu unaoitwa ulinzi wa ghasia. Kama tisho la maangamizi litafanywa na kundi ambalo huyu mtu analoliwakilisha basi hii itakuwa kosa la uhalifu linaloitwa upokonyaji. Ni njia ya kulazimisha dhamira ya mtu kwa kumtia hofu na tisho kwa kutumia shinikizo fulani.

Je, Kuna uwezekano yule ambaye anayetowa ujumbe wa kweli wa neema pia awe yule anayewakilisha wale wanaotishia maangamizo, kwa kuwa shinikiza wanaosikia ujumbe, na kuleta maangamizo kwa wale wanaokataa neema? Je

hadithi ya gharika kwa Bibilia kwa kweli ni upokonyaji? Je, Mungu wa Bibilia anatowa ulinzi kwa wale wanaotenda atakalo na anawauwa wale ambao wanaokataa kumuunga mkono?

> Mungu akamwambia Nuhu, Mwisho wa kila mwenye mwili umekuja mbele zangu; kwa sababu wameijaza dunia dhuluma, basi nitawaharibu pamoja na dunia. (14) Ujifanyie safina ya mti wa mvinje; fanya na vyumba ndani ya safina, ukaifunike ndani na nje kwa lami. Mwanzo 6:13-14

Bibilia inasema kwamba dunia ilijawa na dhuluma. Je, ni jambo la busara kwa dhuluma kuwaangamiza watu kwa sababu wana dhuluma? je, hii haita angalikuwa unafiki?

Tukiangalia neno kuu kuwaharibu kwa kiebrania linamaanisha:

> H7843: Mzizi wa zamani; ku *haribu* hiyo ni, (kusababisha) *maangamizi* (halisi au fumbo)
>
> : - gongagonga, kutupa, chafua (kitu), haribu, kupoteza, vunja, potea, mwaga, mharibifu, takataka.

Neno hilo hilo linatumika katika mafungu kabla ya fungu la kumi na tatu.

> Dunia ikaharibika [H7843] mbele za Mungu, dunia ikajaa dhuluma.(12)Mungu akaiona dunia, na tazama, imeharibika [H7843]; maana kila mwenye mwili amejiharibia[H7843] njia yake. Mwanzo 6:11-12

Kama tukitumia neno haribi, ambalo watafsiri walitumia kwa hilo neno la kebrania, Mwanzo 6:13 ,linasomeka hivi:

> Dunia *ikaharibika* [H7843] mbele za Mungu, dunia ikajaa dhuluma.(12)Mungu akaiona dunia, na tazama, *imeharibika* [H7843]; maana kila mwenye mwili *amejiharibia*[H7843] njia yake. Mwanzo 6:11-12

Sababu ambayo dunia ilionekana kuharibika ni kwa sababu mtu alichafua au kuharibu njia yake ya kufikiria; alikuwa amejawa na dhuluma. Wakati huu

dunia ilikuwa inaonyesha mawazo ya Shetani. Maandiko yanatuonyesha chanzo cha dhuluma:

> Kwa wingi wa uchuuzi wako watu walikujaza udhalimu ndani yako, nawe umetenda dhambi Ezekieli 28:16;

Hii ni kinyume sana na Kristo ambaye, maandiko yanasema, hatendi jeuri:

> Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; Na pamoja na matajiri katika kufa kwake; **Ingawa hakutenda jeuri**, Wala hapakuwa na hila kinywani mwake. Isaya 53:9

Akimzungumzia mwana wa mfalme, mwandishi wa zaburi anatangaza:

> Atawakomboa nafsi zao na kuonewa na udhalimu, Na damu yao ina thamani machoni pake. Zaburi 72:14

Kwa hivyo mwana wa Mungu hatendi udhalimu, na kwa wale anaowakomboa anawaokoa kwa kujihushisha na udhalimu na pia kufanyiwa ujeuri. Shetani amejawa na udhalimu na amejaza dunia na roho hii. Je, kidozi muhimu ni nini kilichomfanya Shetani kuwa na hii roho ya Udhalimu?

> Tena, Mungu amletapo mzaliwa Wake wa kwanza ulimwenguni, husema,"Malaika wote wa Mungu na wamsujudu" Waebrania 1:6

> Kwa mara nyingine, ibilisi akamchukua Yesu mpaka kwenye kilele cha mlima mrefu na kumwonyesha falme zote za dunia na fahari zake, (9) kisha akamwambia, "Nitakupa hivi vyote kama ukinisujudia na kuniabudu." Mathayo 4:8-9

Shetani alimwonea Kristo wivu. Alitaka kuabudiwa Kama vile Kristo alivyo abudiwa, lakini Shetani alikuwa kiumbe kilicho umbwa lakini Yesu alikuwa Mwana wa Mungu wa kiungu. Tofauti ilikuwa pasipo mwisho, lakini bado Shetani alitamani kupata nafasi ya Kristo. Hii ndiyo iliyopanda mbegu ya chuki moyoni mwa Shetani ikielekezewa Kristo. Chuki ya Shetani ilikuwa kubwa mno ikielekezewa Kristo hata akapanga kumuuwa Mwana wa Mungu kuanzia mwanzo. Kusulubishwa kwa Kristo kulifunua kwa ulimwengu malengo ya kweli ya Shetani kabla ya kuumbwa kwa hii dunia.

> Ninyi ni watoto wa baba yenu Ibilisi, nanyi mnataka kutimiza matakwa ya baba yenu. **Yeye alikuwa mwuaji tangu mwanzo**, wala hakushikana na kweli … Yohana 8:44

Mpango wa Shetani wa mauaji ndio ulitia moto roho yake ya udhalimu. Adamu na Hawa walipoanguka dhambini walikuwa kama asili ya Shetani. Kristo ambaye alikuwa ndani yao alichomwa na kupondwa kama meno yanayosaga mbegu. Ni roho ya Kristo ndani ya mwanadamu ambayo inampatia uhai. Yeye ndiye nuru ambayo imwangaziayo kila mtu anayekuja ulimwenguni, Yohana 1:9. Kama Kristo angelimuacha Adamu kabisa basi angefariki. Roho ya Kristo ndani ya Adamu ilipondwa lakini Kristo hakujitoa, ijapokuwa ilimletea maumivu makali kukaa. Katika mateso ya Kristo, mwamba, ulitowa maji ya kiroho yakumfanya Adamu aishi. Hii ndiyo maana Paulo anasema:

> Sikuzote twachukua katika mwili **kufa Kwake Yesu** ili kwamba uzima wa Yesu uweze kudhihirika katika miili yetu. 2 Wakorintho 4:10

> kisha wakaanguka, kwa kuwa kwa nafsi zao **wanamsulibisha Mwana wa Mungu mara ya pili na kumfedhehi hadharani.** Waebrania 6:6

Adamu na Hawa waliumbwa kwa mfano wa Mungu. Shetani alichukia huu mfano na alitaka kuuharibu. Kila tendo la udhalimu kwa watu likielekezwa kwa watu linafunua roho ya Shetani ambayo inapigana na Roho ya Kristo. Hili wazo kwa mara ya kwanza ni vigumu kuelewa lakini imefunuliwa wazi kwa maandiko. Baada ya kueleweka, linabadili vile tunavyo elewa udhalimu inavyoelezwa kwa Bibilia na nini kinacho endelea. Wazo la watu kuwauwa wenzao ni uwendawazimu kabisa mpaka uelewe Shetani anavyotafuta kumchoma Kristo kwa kupitia uwezo wake wakuwafanya wadhulumiane.

> "Naye Mfalme atawajibu, 'Amin, amin ninawaambia, kwa jinsi mlimvyotendea mmojawapo wa hawa ndugu Zangu walio wadogo, mlinitendea Mimi.' Mathayo 25:40

Kidokezi hiki ni muhimu kuelewa. Udhalimu wote umevuviwa na roho ambayo imetiwa moto na wivu na chuki kwa Mwana wa Mungu. Kwa hivyo udhalimu wote hata pia udhalimu wa kibinafsi na kutaka kujiua ni kuelekeza

chuki kwa Kristo hata kama sababu haifahamiki kwa mtu Kudhihirisha chuki kwa majirani na udhalimu juu ya jirani yetu na udhalimu kwa maadui wetu nasi imetiwa moto na chuki ya Shetani kwa Yesu. Huu ndio ulikuwa udhalimu wa kwanza na chuki.

Udhalimu wote unaoelezewa katika mwanzo sita ni dhihirisho la chuki ya Shetani kwake Kristo unayopitishwa kwa wanaume na wanawake. Kwa kuwa Kristo ni mwanzo wa uhai, mwisho wa hiyo chuki itakuwa ni kujiangamiza tu.

Roho hii ya udhalimu ndani ya mtu ilidhihirishwa kwa kifo cha kwanza mwana kondoo shambani. Kumuua huyu mnyama ilionyesha asili ya udhalimu ya Adamu. Kwa kupitia kwa hii kafara Mungu alikuwa anamfunulia Adamu mbegu iliyokuwa ndani yake. Hii mbegu ya udhalimu karibuni ililipuka ndani ya Kaini alivyomuuwa Habili.

Njia moja tu ambayo mtu angeendelea kuishi ilikuwa kwa kupitia kwa Kristo akiendelea kupeena uwezo wa uhai wa maisha yake kwa kizazi cha binadamu. Hii ndiyo maana Kristo alisulubiwa tangia msingi wa dunia. Ufunuo 13:8. Kristo alijeruhiwa kwa sababu ya dhambi zetu tangu mwanzo; alichubuliwa kwa sababu makosa yetu tangu mwanzo wa dhambi. Ili mwanadamu aishi, Kristo ilimlazimu aendelee kumbeba kila mtu hataingawa kuna chuki inayovuviwa na Shetani.

> **Katika mateso yao yote yeye aliteswa**, na malaika wa uso wake akawaokoa; kwa mapenzi yake, na huruma zake, aliwakomboa mwenyewe; **akawainua, akawachukua siku zote za kale.** Isaya 63:9

Haya mawazo yanabadilisha vile tunavyoelewa msalaba wa Kristo, kudhihirishwa kwa udhalimu na hata tabia ya Mungu. Wakati mtu anapigwa, kubakwa au kuuwawa ni dhihirisho la Shetani kuta kumchoma Kristo na kumchibuwa. Kila tendo la kujitimiza tamaa bila kujali ambayo inasababisha ugonjwa na kifo cha mtu binafsi au wengine ni pia dhihirisho la shauku kupita kiasi la Shetani kuta kusababisha uchungu mno kwa Kristo. Ni chuki ambayo ukatili wake usioelezeka.

Ukweli wa kutenda kwa msalaba unatambaa tangia mwanzo wa dhambi ulimwenguni hadi siku ya leo. Kila kiumbe ambacho kinafanya mapenzi ya Mungu kiko vitani na maisha yaliyoko ndani yake kwa kuwa uhai unatoka

Kristo. Hii ndiyo siri ya asili ya kujiangamiza. Ni vita vya Shetani dhidi ya Kristo. Kwa hivyo sasa kwa makini hebu tuchunguze kioo katika fungu lifuatalo.

> Ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni dhidi ya uasi wote na uovu wa wanadamu ambao huipinga kweli kwa uovu wao, (19)kwa maana yote yanayoweza kujulikana kumhusu Mungu ni dhahiri kwao, kwa sababu Mungu mwenyewe ameliweka wazi kwao. Warumi 1:18-19

Neno hasira kwa kiyunani linamaanisha tamaa na unakuja mzizi wa neno ambalo linamaanisha kufikia baadaye. Inaweza kutafsiriwa shauku, hamaki au hasira. Neno la juu ya laweza kumaanisha kwenda kwa. Tukitafsiri fungu hili na haya mawazo na pia kidokezo kimoja. Yesu aliseama mimi ni ukweli. Yohana 14:6, kwa hivyo kunyanyasa ukweli ni kumgandamiza Kristo.

> **Shauku** ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni **juu ya** wote na uovu wa wanadamu ambao huipinga **Kristo** kwa uovu wao, (19) kwa maana yote yanayoweza kujulikana kumhusu Mungu ni dhahiri kwao, kwa sababu Mungu mwenyewe ameliweka wazi kwao. Warumi 1:18-19 *tengenezwa*

Kila siku Mungu hutuma Roho wa Mwana wake ili akae ndani ya mioyo yetu. Wengine wanaizamisha sauti, wengine katika juhudi zao kumpinga wana watafuta wale ambao Roho yake inaishi ndani ya na wanawatesa. Katika kila mtu ulimwenguni katika hii sayari Kristo anadharauliwa na kukanwa. Leo ni mtu wa masikitiko na yuajuwa huzuni. Kila siku Kristo hujikana na anabeba msalaba wake,na anaachilia uhai wake. Kwa haya inaoneka shauku ya Mungu kwetu sisi. Anafikia kila siku na shauku shupavu na ingawa dunia inagandamiza sauti ya dhamira na inazamisha kusadikishwa.

Uovu wa wanadamu unawafanya wa elekeze roho zao hasira kwa Mungu. Kukataa kwa hasira kwa wanadamu upendo wa Mungu ndio inaelekezewa Mungu kuwa mjeuri. Tabia ya wanadamu inawekewa Yeye na Kristo inaonekana kama amepigwa na Mungu na kuteswa, lakini Kristo alipigwa kwa ajili ya dhambi zetu na si kwa sababu ya hasira ya Mungu. Na Mungu anasema nini kwa watu wake, kwa wale ambao wanaodai kumfuata?

> Lakini kuhusu Israeli anasema,"Mchana kutwa nimewanyoshea watu wakaidi na wasiotii mikono Yangu." Warumi 10:21

Ni kwa nuru ya msalaba ndiyo tunaweza kuanza kuelewa tisho si la gharika peke pia la moto wa Sodoma na Gomora, uharibifu wa Yerusalemu, na mwisho wa dunia. Chuki ya Shetani dhidi ya Kristo inadhihirika kwa nia yake ya kutaka kuwauwa wote kwa sababu kwa kila mtu Kristo amewapa uzima. Alikubali kutoa uhai wake kwa kila mtu iliwapatie uwezo wa kuishi. Kristo awezi kuishi pahali ambapo dhambi inapendwa lakini kupondwa kwa Roho Yake inatoa uwezo kwa nafsi kuishi hata kwa maji yaliyo tiririka ubavuni mwake alipokufa msalabani.

> Mwe na kiasi na kukesha, maana adui yenu Ibilisi, kama simba angurumaye huzungukazunguka akitafuta mtu ili apate kummeza.1 Petro 5:8

Katika ukurasa wa 13 tulizungumza kuhusu matokeo ambayo roho ya binadamu inayoleta duniani. Wakati wanadamu wanapomnyanyasa Kristo na wanapoonyesha chuki ya Shetani kwa Kristo kwa kuonyeshana ukatili, dunia inaanza kurudisha haya kwa kupitia sheria za kimaumbile. Wakati watu walikuwa wakizamisha sauti ya Kristo katika nafsi zao, maumbile yange jibu kwa kuzamisha nafsi za wanadamu. Wakati Bwana alipotazama uovu wa dunia Alidokeza kwamba kutakuwa na mwisho.

> Bwana akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele, kwa kuwa yeye naye ni nyama; basi siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini. Mwanzo 6:3

Kikomo kilikuwa mdaa ambao Roho wa Mungu atajitahidi kumuokowa mwanadamu. Roho wa Kristo alikuwa akiwasihii usiku na mchana watoto wake wapotovu. Aliwasihi na kuwafikia siku baada ya siku. Lakini twakumbuka vile watu walivyo fanya kwa jitihada ya Roho.

> Ghadhabu ya Mungu imedhihirishwa kutoka mbinguni dhidi ya uasi wote na uovu wa wanadamu ambao huipinga kweli kwa uovu wao, Warumi 1:18

Watu wa zamani sana walizamisha sauti ya dhamiri. Kila siku walikataa sauti iliyowasihi kwa upole, na waliendelea kwa kishondo kwa njia yao ya uovu.Huku kugandamiza kwa Roho ya Kristo ilikuwa ni kana kwamba

Inashikilia chini kwa juhudi za kumzamisha. Roho Yake ilisumbuliwa siku baada ya siku, Kristo alihisi kuhuzunishwa.

> Lakini wakaasi, wakamhuzunisha Roho yake Mtakatifu; kwa hiyo akawageukia, akawa adui, akapigana nao.Isaya 63:10

Watu waliokaribia kuharibiwa, kusihi kulikuwa kwa haraka na sauti yake ikawa kwao kama mlio wa adui. Ushuhuda wake kwao ulichukuliwa kwa kejeli na chuki.

> Na nafsi yangu imefadhaika sana; Na Wewe, Bwana, hata lini? (4) Bwana urudi, uniopoe nafsi yangu, Uniokoe kwa ajili ya fadhili zako (5) Maana mautini hapana kumbukumbu lako; Katika kuzimu ni nani atakayekushukuru? (6) Nimechoka kwa kuugua kwangu; Kila usiku nakieleza kitanda changu; Naliloweshа godoro langu kwa machozi yangu. (7) Jicho langu limeharibika kwa masumbufu, Na kuchakaa kwa sababu yao wanaoniudhi. (8) Ondokeni kwangu, ninyi nyote mtendao uovu; Kwa kuwa Bwana ameisikia sauti ya kilio changu.Zaburi 6:3-8

Mateso ya Kristo hayangeweza kufichwa. Kama wanadamu wangekataa kuukubali msalaba wa Kristo basi mawe yasiyo na uhai yangepiga makelele kushuhudia mateso ya Muumba wao. Kwa kuwa Kristo ndiye Muumba wa ulimwengu kwa hivyo maumbile yaitikia mateso Yake.

> Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote vimekuwa vikilia kwa uchungu kama utungu wa wakati wa mwanamke kuzaa hata sasa.
> Warumi 8:22

Zaburi nyingi zinadhihirisha vile Kristo alivyopata kuona kwa sababu huyo Roho wa Kristo alikuwa ndani ya mioyo ya wote walioandika maandiko pamoja na Zaburi.

> Kwa habari ya wokovu huu, wale manabii walosema kuhusu neema ambayo ingewajia ninyi, walitafuta kwa bidii na kwa uangalifu mkubwa, (11) wakijaribu kujua ni wakati upi na katika mazingira gani ambayo ndani yao Roho wa Kristo aliyokuwa akionyesha alipotabiri
>
> kuhusu mateso ya Kristo na utukufu ule ambao ungefuata.

> 1 Petro 1:10-11

Katika Zaburi 18 tumefunua mateso ya Kristo msalabani kwa kulingana na gharika.

> Kamba za mauti zilinizunguka, Mafuriko ya uovu yakanitia hofu. (5) Kamba za kuzimu zilinizunguka, Mitego ya mauti ikanikabili. Zaburi 18:4-5

Maelezo mengine katika Zaburi 18 inanena kwa lugha ya gharika bali zengine zinasema kuhusu moto unao teketeza ikidokezea visa vya Sodoma na Gomora na mwisho wa wenye dhambi. Wakati Kristo alijitahidi na wanadamu watoke kwa uovu wao, aliangamizwa na gharika kutokana na tabia yao ya uovu.

> Bwana akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani, akahuzunika moyo. Mwanzo 6:6

Watu wakale walikuwa wakimweka Kristo katika aibu ya wazi. Nafsi yake iliteswa na kuhuzunishwa na uovu wao na akalia katika msalaba wa watu wakale – Niko na kiu! Roho wa Mungu akawacha kumsihi mwanadamu. Baada ya kusukumwa nyuma kwa miaka zaidi ya mia, Baba mwishowe akakubali uamuzi wao.

> Je! Utaiandama njia ya zamani Waliyoikanyaga watu waovu? (16) Ambao walinyakuliwa kabla ya wakati wao, Msingi wao ulimwagika kama kijito cha maji; (17) Waliomwambia Mungu, Tuondokee; Tena, Huyo Mwenyezi aweza kutufanyia nini? (18) Naye ndiye aliyezijaza nyumba zao vitu vyema; Lakini mashauri ya waovu na yawe mbali nami. Ayubu 22:15-18

Baba alisukumwa na watu. Lakini Kristo lazima abaki na watu na ateseke nao katika maamuzi yao ama sivyo wangelikufa mara moja na Mungu angelaumiwa. Kwa hivyo ngurumo na radi zilipoanza kufiringika kwa watu wa kale,Kristo alikuwa nao. Aliteseka nao na kuwabeba mpaka mwisho. Yeye ni Immanueli – Mungu pamoja nasi. Gharika ni ufunuo wa msalaba ijapokuwa tunamchukuwa Yeye kama alipigwa na Mungu na kuteswa.

Vitu visivyo na uhai havingezuiliwa kuhubiri injili kwa matukio ya gharika. Tazama uhusiano katika kisa cha gharika na msalaba katika mafungu ya maneno haya:

## 1. Kuita / kulia

Kamba za mauti zilinizunguka, **Mafuriko ya uovu yakanitia hofu**. (5) Kamba za kuzimu zilinizunguka, Mitego ya mauti ikanikabili. (6) **Katika shida yangu nalimwita Bwana**, Na kumlalamikia Mungu wangu. Akaisikia sauti yangu hekaluni mwake, Kilio changu kikaingia masikioni mwake. Zaburi 18:4-6

Ilipofika saa tisa **Yesu akapaza sauti akalia, "Eloi, Eloi lama sabakthan**i?"Maana yake, "Mungu wangu, Mungu wangu,mbona umeniacha?" Mathayo 27:46

## 2. Dunia inatetemeka.

**Ndipo nchi iliyotikisika na kutetemeka,** Misingi ya milima ikasuka-suka; Ikatikisika kwa sababu alikuwa na ghadhabu. Zaburi 18:7

Wakati huo huo pazia la hekalu likachanika vipande viwili, kuanzia juu hadi chini. Dunia ikatetemeka na miamba ikapasuka.
Mathayo 27:51

## 3. Giza

Aliziinamisha mbingu akashuka, Kukawa na **giza kuu chini ya miguu yake.** [ utaponda viganja vya miguu yake]Zaburi 18:9

**Alifanya giza kuwa mahali pake pa kujificha,** Kuwa hema yake ya kumzunguka. Giza la maji na mawingu makuu ya mbinguni. Zaburi 18:11

Tangu saa sita hadi saa tisa **giza lilifunika nchi yote.** Mathayo 27:45

## 4. Mikondo ya Maji na Misingi kufunuliwa.

Ndipo ilipoonekana mikondo ya maji, Misingi ya ulimwengu ikafichuliwa, Ee Bwana, kwa kukemea kwako, Kwa mvumo wa pumzi ya puani mwako. Zaburi 18:15

Katika mwaka wa mia sita wa maisha ya Nuhu, mwezi wa pili, siku ya kumi na saba ya mwezi, siku ile chemchemi zote za **vilindi vikuu zilibubujika kwa nguvu**, madirisha ya mbinguni yakafunguka. Mwanzo 7:11

## 5. Uso ulifichwa na Hisia Zikaachwa

**Kwa kitambo kidogo nimekuacha**; lakini kwa rehema nyingi nitakukusanya. (8) **Kwa ghadhabu ifurikayo nalikuficha uso wangu dakika moja**; lakini kwa fadhili za milele nitakurehemu, asema Bwana, Mkombozi wako. (9) **Kwa maana jambo hili limekuwa kama maji ya Nuhu kwangu;** maana kama nilivyoapa ya kwamba maji ya Nuhu hayatapita juu ya dunia tena, kadhalika nimeapa ya kwamba sitakuonea hasira, wala kukukemea. Isaya 54:7-9

Tangu saa sita hadi saa tisa giza lilifunika nchi yote. 46Ilipofika saa tisa Yesu akapaza sauti akalia, "Eloi, Eloi lama sabakthani?"Maana yake, "**Mungu wangu, Mungu wangu,mbona umeniacha?**"
Mathayo 27:45-46

## 6. Wokovu.

Alipeleka kutoka juu akanishika, **Na kunitoa katika maji mengi.** Zaburi 18:16

Na Mungu akamkumbuka Nuhu, na kila kilicho hai, na wanyama wote waliokuwamo pamoja naye katika safina; Mungu akavumisha upepo juu ya nchi, maji yakapungua; (2) chemchemi za vilindi zikafungwa, pia na madirisha ya mbinguni, mvua kutoka mbinguni ikazuiliwa; (3) maji yakadumu kuondoka katika nchi; na mwisho wa siku mia na hamsini maji yakapunguka. Mwanzo 8:1-3

Maumbile yanashuhudia kile kilicho mtendekea Muumba wake. Kwa kuwa Kristo ndiye nuru imwangaziayo kila mtu anayekuja duniani, mateso yake yalidhihirika katika maisha ya wote ambao walio angamia katika gharika.

Kwa neno la Bwana mbingu zilifanyika, Na jeshi lake lote kwa pumzi ya kinywa chake. (7) Hukusanya maji ya bahari chungu chungu, Huviweka vilindi katika ghala. Zaburi 33:6-7

Ni kwa kupitia uwezo wa Kristo mbingu zilifanywa. Sauti yake inanena kwa viumbe vyote. Ni kwa neno la Kristo maji yalikusanywa pamoja na kuwekwa

katika ghala ardhini. Wakati watu wakale sana walimkana Kristo, sauti Yake ilinyamazishwa na uwezo ambao ulioweka maji katika ghala ukavunjika na vitu vya asili vya kimaumbile vilitiwa mkononi mwa kanuni za machafuko.

Si Shetani ambaye alisababisha kutoka kwa maji, bali kwa kuwachochea watu wampinge Kristo mpaka mwishowe kwa huzuni alikubali uamuzi wao; matokeo yalikuwa ya kwamba uumbaji haungeweza kusikia sauti ya upole ya Bwana wake ambaye alikuwa akiwaita kila saa "uwe kimya,tulia" Maji ya karudisha msukosuko wa Shetani na watu waovu. Shetani mwenywe alifanywa astahimili vita vya vitu vya kiasili vya maumbile kama vile ukubwa kupita kiasi wa msalaba wa Kristo unavyofunuliwa kwa maji ya gharika.Kutetemeka kwa vilindi vilidhihirisha moyo wa Kristo uliovunjika.Maji yaliyomwagika kutoka juu ilikuwa ni ushuhuda machozi Yake (Zaburi 119:136) ambayo alimwaga kwa wanawa Adamu walioanguka. Watu wakale sana walikataa kutambua mateso ya Kristo, lakini maumbile yalishuhudia mateso ya mwanzilisha wake na yakarudisha huzuni na kifo chake. Shetani ndiye aliyesababisha uharibifu huu kwa kuwasukuma watu wakale sana kumkana Kristo na Roho yake. Wakati kukataliwa kulipofika kilele, basi maumbile yakatoa ushuhuda wa huko kukataliwa na pia kurudisha kutia kazini kwa nguvu roho ya machafuko.

Tunakumbuka yakuwa hakuna mtu anayeweza kuishi ila Kristo kuwa nao, kwa hivyo Kristo aliwekwa wazi kwa ukatili na huzuni ya kila mtu aliyeangamia katika gharika. Katika mateso yao yote aliteswa. Alibeba na kuzichukua katika siku zote za maisha yao. Aliposhuhudia kila kifo cha wana wake wapotovu, alichomwa na huzuni nyingi. Katika kila nafsi iliyopumuwa kwa hofu, Kristo alihisi uchungu wao na alitaka kuwaokoa lakini hangefanya hivyo. Kama vile alivyo kuwa akifa msalabani bila matumaini, pia alihisi kukata tamaa kwao na kutokuwa na matumaini walivyofariki.

Ili kuziba msalaba wa Kristo, wakristo leo wanasema kwamba Mungu anawaadhibu waovu kwa hasira. Mshindo wa gharika unawekelewa Mungu kana kwamba ni Yeye ambaye aliyewauwa hao wenye dhambi. Ni kweli kwamba uwezo wa Mungu ulitumika kuvunja ardhi na kusababisha gharika kama vile nguvu za Mungu zilitumika katika majeshi ya kirumi ambao walimsulubisha Yesu msalabani. Je Mungu alimuangika Mwana Wake msalabani? Je ulikuwa ukali wake ambao ulimfanya afe? La hasha, mara elfu

moja hapana! Ilikuwa ni nguvu za Mungu mikononi mwa nyoka ilimponda Kristo kisiginoni.

70 AD wakati wanawake waliwala watoto wao na wengi walisulubishwa mpaka kulikosa nafasi ya kusimamisha misalaba mingine. Mambo kama hayo pia yanafafanuliwa katika Maombolezo.

> Heri wale waliouawa kwa upanga Kuliko wao waliouawa kwa njaa; Maana hao husinyaa, wakichomwa Kwa kukosa matunda ya mashamba. (10) Mikono ya wanawake wenye huruma Imewatokosa watoto wao wenyewe; Walikuwa ndio chakula chao Katika uharibifu wa binti ya watu wangu.(11) Bwana ameitimiza kani yake, Ameimimina hasira yake kali; Naye amewasha moto katika Sayuni Ulioiteketeza misingi yake. (12 )Wafalme wa dunia hawakusadiki, Wala wote wakaao duniani, Ya kwamba mtesi na adui wangeingia Katika malango ya Yerusalemu.(13) Ni kwa sababu ya dhambi za manabii wake Na maovu ya makuhani wake, Walioimwaga damu ya wenye haki Katikati yake. Maombolezo 4:9-13

Katika fungu la 11 imetajwa hasira ya Bwana na inaendelea kunena kuhusu ghadhabu yake, ambayo tunafahamu katika sura ya 11 inaweza kumaanisha huzuni. Fungu la 12 linatuonyesha mshutuko wa kweli wa mtesi na adui kuingia Yerusalemu. Fungu la 13 linanena kuhusu kuchinjwa kwa "wenye haki Katikati yake." Je, ni nani mwenye haki aliyechinjwa?

> Kwa kuwa Kristo naye aliteswa mara moja tu, mwenye haki kwa ajili ya wasio na haki, ili awalete ninyi kwa Mungu. Mwili wake ukauawa, lakini akafanywa hai katika Roho,1 Petro 3:18

Mji wa Yerusalemu ulikuwa mji wa amani na Kristo alikuwa kiongozi wake wa kiroho. Katika huzuni iliyokamilika na iliyokuwa kali sana uso wa Baba ulifichwa na dhambi za manabii na makuhani. Hii ilimfanaya Shetani mtesi kuingia mjini na Kristo mwenye haki akauawa katikati yake. Vivyo hivyo damu ya Kristo ilimwagika wakati watu wa Mungu wali chukuliwa na kuangamizwa wakati wa Yeremia na danieli. Pia hilo latendeka katika kila uharibifu wa watu wa Mungu; Kristo huteseka nao na anabeba msalaba.

Je unaweza kuona gharika katika miwani ya msalaba? Je wa mwuona Kristo akiteseka Sodoma? Je unaona uchungu wa Kristo katika vifo vya wafungua mimba Misri na uharibifu Yerusalemi? Je waona kalivari katika uharibifu

mkali wa kila mtu? Ni kwa kupitia msalaba wa Kristo unaweza kuona hukumu ya Bibilia kama ufunuo wa upendo wa Mungu wa ajabu. Wakati ambapo tunaweza kushika chanzo cha ukatili unaoonekana kwa wanadamu na maumbile kama ufunuo wa chuki ya Shetani kwa Kristo, ndipo tunaweza kutambua vyema vizuri siri ya mfano wa nyoka katika mti. Wakati nyoka anatambulika kulingana na msalaba, basi kuumwa kwa nyoka kwa kulingana na tabia ya Mungu kwa kweli kutapona.

## 20. Nyoka Aliyewekwa Wazi Kwa Msalaba

Shetani ndiye muanzilishi wa mateso, magonjwa, na kifo. Tuligundua yakuwa Kristo humpatia kila mtu uhai na Yuko karibu na kila mtu anayeishi duniani. Kila tendo la kikatili ambalo watu hujifanyia wao wenyewe au wengine linasababisha mateso makali kwa Kristo. Shetani kwa ujuzi ameficha tendo lake lakikatili dhidi ya Kristo katika uharibifu wa watu kwa kuwashawishi wanadamu kwamba Mungu ndiye mshari na kila utenzi wa fafanuzi hukumu katika Bibilia zinaelekezewa Yeye.

Katika mkutano wa usiku na Nikodemo, Yesu anamuelezea mojawapo ya ukweli wenye maana sana ambao haujawahi kutamkwa. Ni ufunuo wa msalaba maajabu sana na ijapokuwa ni ukweli ambao umefichika katika uliwengu mzima.

> Kama vile Mose alivyomwinua yule nyoka kule jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa juu. Yohana 3:14

Kisa ambacho Yesu alikuwa akirejelea kinapatikana katika Hesabu 21. Wana wa Israeli walikuwa wakinung'unika na kumlalamikia Mungu na Musa. Hiyo roho ya kulalamika ilisababisha kuvunjika kwa boma la ulinzi.

> Mwenye kuchimba shimo atatumbukia ndani yake; Na yeye abomoaye boma, nyoka atamwuma. Mhubiri 10:8

Kuvunjika kwa boma kuliruhusu hatari za jangwa ambazo Mungu aliwakinga nazo kudhihirika. Kwa upesi nyoka wenye sumu wakaanza kuuma watu, na kwa matokeo ya vifo kwa ajili ya sumu ya kali, walimlilia Musa kuwasaidia.

> Watu wakamnung'unikia Mungu, na Musa, Mbona mmetupandisha huku kutoka nchi ya Misri, ili tufe jangwani? Maana hapana chakula, wala hapana maji, na roho zetu zinakinai chakula hiki dhaifu.(6) Bwana akatuma nyoka za moto kati ya watu, wakawauma, watu wengi wakafa.(7) Watu wakamwendea Musa, wakasema, Tumefanya dhambi kwa sababu tumemnung'unikia Mungu, na wewe; utuombee kwa Bwana, atuondolee nyoka hawa. Basi Musa akawaombea watu (8) Bwana akamwambia Musa, Jifanyie nyoka ya shaba, ukaiweke juu ya mti, na itakuwa kila mtu aliyeumwa, aitazamapo ataishi.(9) Musa akafanya nyoka ya shaba, akaiweka juu ya mti, hata ikiwa nyoka amemwuma mtu, alipoitazama ile nyoka ya shaba, akaishi. Hesabu 21:5-9

Unaposoma hadithi hii tafadhali kumbuka kioo vile kinavyosema :

> Bwana akatuma nyoka za moto kati ya watu, wakawauma, watu wengi wakafa. Hesabu 21:6

Neno la kiebrania *kutuma* pia lina maanisha *kuachilia, kukata tamaa* au *kutupwa.* Wakati watu walipo mshtaki Mungu, alisukumwa nyuma katika kuwalinda kutokana na nyoka. Aliwalinda wakati huo wote lakini walimuacha Mungu alipingwa kuendelea kuwalinda. Bibilia inatuambia vile nyoka walivyokuja.

> Wala tusimjaribu Bwana, kama baadhi yao walivyofanya, wakafa kwa kuumwa na nyoka. (10) Msinung'unike kama baadhi yao walivyofanya, wakaangamizwa na mharabu. 1 Wakorintho 10:9-10

Neno la kiebrania la mharabu linamaanisha mharibifu au nyoka mwenye sumu kali katika fungu la 10 paulo anaunganisha neno nyoka katika fungu la 9 na neno mharabu katika fungu la 10. Shetani ndiye mharabu.

> Walikuwa na malaika kutoka kwenye hilo shimo lisilo na mwisho kama mfalme wao, ambaye jina lake kwa Kiebrania ni Abadoni**b** na kwa Kiyunani ni Apolioni—Mharabu. Ufunuo 9:11 (NLT)

Wakati watu watu walitengeneza tundu katika boma la ulinzi kwa kupitia uaasi wao, Shetani aliwezeshwa kuingia ndani na kwa upesi akaanza

kuwauwa watu. Nijambo la hakika watafsiri wa Bibilia walitumia neno kutumwa kuelezea kuachiliwa kwa nyoka inatupatia kioo kamili cha uungu kwa watu wanavyoisoma hadithi. Wazo la Mungu kutuma nyoka kuuwa watu ni kurudisha vile watu wanafikiria kuhusu Mungu. Wale ambao wameangalia maisha ya Yesu kama ni picha ya Baba kwa haraka watatafuta majibu ya kuelezea kisa kinacho tisha. Je Mungu anaweza kutuma nyoka hatari kuwauwa watu kwa sababu ya malalamishi? Hii ni tofauti na tabia ya Yesu. Utafiti wangu uliniongoza kwa 1 Wakorintho 10:9,10 ambayo inazungumzia hii hadithi na inapeana kidokezo kwamba waliuwawa na mharabu. Ufunuo 9:10 inatuambia mharabu ni malaika kutoka kwenye shimo lisilo na mwisho. Kisha ona neno kutumwa inamaana nyingi kwa hivyo hilo fungu linaletwa katika mapatano tukikubali kuchunguza.

Swali la kushangaza ni mbona Mungu katika hadithi amwambie Musa atengeneze sanamu ya nyoka na aweke mtini na awaambie watu watazame na wapone? Hili ni jambo geni sana. Nyoka katika Bibilia ni mfano wa Shetani.

> Lile joka kuu likatupwa chini, **yule nyoka wa zamani aitwaye Ibilisi au Shetani**, aupotoshaye ulimwenguni wote. Akatupwa chini duniani, yeye pamoja na malaika zake. Ufunuo 12:9

> Lakini nina hofu kuwa, kama vile Eva alivyodanganywa kwa ujanja wa yule nyoka, mawazo yenu yasije yakapotoshwa, mkauacha unyofu na usafi wa upendo wenu kwa Kristo. 2 Wakorintho 11:3

Iliwezekana je kwa kumtazama nyoka aliyeinuliwa juu ya mti angeleta uponyaji kwa mtu aliyeumwa? Ni ujumbe gani Mungu alikuwa anataka kuwafunza? Hii inatuleta nyuma hadi usiku Yesu alikuwa akinena na Nikodemo. Je Kristo alijilinganisha na nyoka?

> Kama vile Mose alivyomwinua yule nyoka kule jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa juu. Yohana 3:14

Yesu analinganisha kuinuliwa kwa nyoka na kuinuliwa kwake msalabani. Wakristo wengi huelewa njia ya kuponywa kwa kumtazama Yesu aliyekufa msalabani kwa ajili yao.

Wakati mwenye dhambi ambaye yuko chini ya laana ya dhambi anapomtazama Kristo na anaona kwamba Kristo alichukua laana yake,

inaleta busara kwa undani ya shukrani inayowezesha kubadili moyo na tabia. Hii inaleta uponyaji kotokana na laana ya dhambi iliyosababishwa na majaribu ya Shetani, ambayo ni kama kuumwa na nyoka kunako leta ugonjwa na kifo.

Kwa nini nyoka aliye inuliwa mtini anatumika kama mfano wa uponyaji? Je ingekuwa ni busara kutumia mfano wa mwana kondoo na kumuinua mtini? Kwa nini Kristo anatambulishwa na mfano wa Shetani?

> Mungu alimfanya Yeye asiyekuwa na dhambi kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kufanywa haki ya Mungu katika Yeye. 2 Wakorintho 5:21

Kusulubishwa kwa Kristo kulifunua tabia halisi ya Shetani. Msalaba wa Kristo unafunua vile mtu anavyo jiharibu na matokeo ya mwisho yatakayo watendekea wenye dhambi wasio tubu, na tena wakati huo huo inafichua tabia kamili ya Shetani kama muuaji mkatili. Ili wote wamuone Shetani akidhihirisha roho yake ya uovu, uwezo ambao ni wa Kristo alikubaliwa kutumiwa na Shetani kwa mbinu ya wanadamu ambao waliomtesa na kumuuwa Kristo. Ili Mungu aruhusu Mwana Wake akabidhiwe mateso ya kikatili na kifo inafunua upendo wa agape unaowashinda wanadamu kuelewa. Msalaba unaleta mwangazani matokeo ya mwisho ya huzuni ya dhambi ndani ya mwenye dhambi na tabia halisi ya Shetani.

Msalabani Yesu alilia "Mungu wangu Mungu wangu mbona umeniacha?" Hii ndiyo hali ya mwenye dhambi anaye hisi hatia ya uzito wa dhambi. Katika haya maumivu ya akili, Mwenye dhambi ambaye amesadikishwa dhambi zake atakuwa na busara sana ya uamuzi katika nafsi yake. Mwenye dhambi anahisi kwamba Mungu anampulizia moto, lakini ni hukumu ya kibinafsi katika nafsi na hatia katika uwepo wa upendo mtakatifu usiona ubinafsi uliofanya hali kuwa hivyo.

Hii ndio ugumu wa msalaba kufahamika. Unadhihirisha tabia ya kikatili ya Shetani na asili ya matokeo ya maisha ya dhambi na inahisi kana kwamba Mungu katika hasira kali ndiye anayelundika mateso kwa mwenye dhambi. Uso wa upendo wa Mungu umefichwa katika giza la hatia na yote yanayo hisiwa ni hofu ya kutisha ya aibu ya dhambi kupindukia. Tunaona pande mbili za asili ya msalaba katika maisha ya Kaini. Tafsiri ya Wycliffe inaonyesha sehemu hizi mbili.

> Kaini akamwambia Bwana, Adhabu yangu imenikulia kubwa, haichukuliki. (14) Tazama, umenifukuza leo katika uso wa ardhi, nitasitirika mbali na uso wako… Mwanzo 4:13-14 (Tafsiri ya Wycliffe).

Kaini anahisi Hukumu yake ya kibinafsi ambayo ni matokeo ya dhambi yake. Anahisi kwamba dhambi yake ni kubwa mpaka hawezi kusamehewa. Lakini pia usemi wa kumrudishia Mungu haya na kumfanya awajibike kwa sababu ya matokeo haya. Hizi ndizo sehemu mbili za hukumu na kwa hivyo ni sehemu mbili za msalaba.

1. Hatia na hukumu ya kibinafsi bila matumaini ya kusamehewa.
2. Kumrudishia Mungu lawama na kumfanya mshari katika hukumu.

Ni kwa kulingana na hili kwamba tunapoona matendo ya kikatili katika Bibilia, ni kwa kweli inafunua tabia ya Shetani lakini inaonekana kana kwamba Mungu anamimina ghadhabu kwa mwenye dhambi. Katika mtazamo wa mwenye dhambi, hukumu kila siku inahisi kuwa Mungu ni mkatili mshari.

> Na kuonekana kwake ule utukufu wa Bwana kulikuwa kama moto uteketezao, juu ya mlima machoni pa wana wa Israeli. Kutoka 24:17

Kama vile ilivyo angaziwa katika ukurasa wa hapo awali, ili Shetani adhihirishe ukatili wake, Kristo lazima ajikane na abebe msalaba wa mateso kwa kuwaona wana wake wakiteseka. Shida ni kwamba wanadamu wanadhania kwamba ni Mungu anayewaangamiza kwasababu dhamiri ya hatia inawasadikisha kwamba wanastahili kufa.

> Ingawa wanafahamu sheria ya haki ya Mungu kwamba watu wanaofanya mambo kama hayo wanastahili mauti, si kwamba wanaendelea kutenda hayo tu, bali pia wanakubaliana na wale wanaoyatenda. Warumi 1:32

Hata sasa wakati tunapomuona Kristo akiinuliwa katika hali sahihi ya msalaba, tunamuona nyoka akifunuliwa na tunatambua si Mungu anayeangamiza bali ni Shetani. Hii inaleta uponyaji katika moyo wa mwanadamu dhidi ya upinzani kwa Baba kufikiria ni Yeye anayefanya mauaji. Mfano wa akili nyingi sana na unachukua mda kukubalika kweli kweli, lakini ukweli unabaki kwamba wakati uonapo nyoka katika hukumu za kikatili

katika Bibilia unaweza kopona kwa upinzani kwa Mungu. Unaweza kupatanishwa kweli kweli na Yeye na uwoga wako kutupiliwa mbali.

> Katika upendo hakuna hofu. Lakini upendo ulio kamili huitupa nje hofu, kwa sababu hofu inahusika na adhabu. Kila mwenye hofu hakukamilika katika upendo. 1 Yohana 4:18

Kwa haya mafundisho akilini, tuko tayari kuangalia vile fimbo ilibadilishwa kuwa nyoka katika mapigo kumi.

> Bwana akamwambia, Ni nini hiyo uliyo nayo mkononi mwako? Akasema, Ni fimbo. (3) Akamwambia, Itupe chini; akaitupa chini, nayo ikawa nyoka; Musa akakimbia mbele yake (4) Bwana akamwambia Musa, Nyosha mkono wako, kamshike mkia; (akaunyosha mkono wake akamshika, naye akageuka kuwa fimbo mkononi mwake;) (5) ili kwamba wapate kusadiki ya kwamba Bwana, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, amekutokea. Kutoka 4:2-5

Ufito au fimbo ni ishara ya mamlaka. Katika lugha ya kifalme hii inaitwa fimbo. Kristo Mwana wa Mungu ana fimbo.

> Lakini kwa habari za Mwana asema,"Kiti chako cha enzi, Ee Mungu, kitadumu milele na milele, nayo haki itakuwa fimbo ya utawala ya Ufalme Wako. Waebrania 1:8

Kristo pia aliita hii fimbo.

> Namwona, lakini si sasa; Namtazama, lakini si karibu; Nyota itatokea katika Yakobo **Na fimbo ya enzi itainuka katika Israeli**; Nayo itazipiga-piga pembe za Moabu, Na kuwavunja-vunja wana wote wa ghasia. Hesabu 24:17

Kristo ni uwezo wa Mungu ( 1 Wakorintho 1:24) na ni mkono wa kulia wa Mungu (Waebrania 1:3). Anaitwa mkono wa kuume wa Mungu ama kile tungeweza kukiita " mtu wake wa mkono wa kuume"

> Bwana, mkono wako wa kuume umepata fahari ya uwezo, Bwana, mkono wako wa kuume wawaseta-seta adui. Kutoka 15:6

Mungu anamwambia Musa kwa atamuwakilisha Mungu na Aruni atakuwa msemaji wake. Kutoka 4:16. Wakati Musa alipoachilia fimbo na ikaanguka chini nguvu ambazo ziko kwa Kristo zilikuwa kama kama nyoka.Kristo ni

nguvu za Mungu. Wakati Mungu alipomwambia Shetani "Tazama, yote aliyo nayo yamo katika uwezo wako" (Ayubu 1:12)

Mungu alikuwa anatupa fimbo ya chini. Fimbo ni Kristo ambaye nguvu zake ndani ya wanadamu na uumbaji iliachiliwa Shetani ilikutumikia lengo la Shetani, kama vile Shetani aliwavuvia majeshi ya Kirumi kumlazimisha Kristo kuubeba msalaba hadi katika mlima wa kalvari.

Fikira za majeshi ya Kirumi yalitawaliwa na Shetani, ijapokuwa pumzi ambayo walitumia kuishi ni uhai unaomuangazia kila mtu ajaye duniani. Nguvu za Kristo ndani ya nafsi za wanadamu ilitumika na Shetani kumsulubisha msalabani. Hebu simama,na uyatafakari hayo kwa mda mchache. Mfano mmoja wa Askari wa Kirumi aliyebeba nyundo juu na kugonga msumari ndani ya mikono yenye dhamani kuu ya mwokozi yuko na ufunguo wa mapigo ya Misri na uwezo wote wa uharibifu unaodhihirika duniani. Hii ndiyo fimbo iliyoanguka chini:

> Akaenda mbele kidogo, akajitupa chini kifudifudi akaomba akisema, kama ikiwezekana saa hiyo ya mateso imwepuke. Marko 14:35

Wakati watu wanapoanguka chini kwa sababu ya nguvu za uharibifu, kuna fimbo ambayo inayo anguka chini na kuwa nyoka.

> Nao wakamleta yule mvulana. Yule pepo mchafu alipomwona Yesu, mara akamtia Yule mvulana kifafa, akaanguka, akagaagaa chini huku a kitokwa na povu kinywani. Marko 9:20

Kwa hivyo tunaweza kuona wakati wowote tunapoona watu wakiteseka tunaona:

> Katika mateso yao yote yeye aliteswa, na malaika wa uso wake akawaokoa; kwa mapenzi yake, na huruma zake, aliwakomboa mwenyewe; akawainua, akawachukua siku zote za kale. Isaya 63:9

Ukweli ni kwamba kama Mungu angeliweza kutumia nguvu za kimabavu angelimaliza uhai wa wale walio chagua kumfuata Shetani ilinguvu za Mungu ndani ya Kristo haingelitumika na Shetani kufanya uharibifu. Walakini, ili Kristo ampatie kila mtu uhuru wa uchaguzi, Kristo lazima aruhusu nguvu Zake ndani ya wanadamu zitumiwe na Shetani wakati watu wmeamua kumpinga Mungu na amri Zake. Je ni vipi Shetani hutumia hizi nguvu? Watu wote wasio tawaliwa na hutawaliwa na Shetani. Wakitawaliwa na yeye anawafanya watu

kujiangamiza wenye kwa wenyewe. Wakati fikira za wanadamu ziko chini ya utawala wa Shetan Uwezo wa uhai waliopatiwa na Kristo unatumika kutekeleza malengo ya Shetani. Kwa hivyo nguvu za Mungu zinabadilika kuwa nyoka wakati imetoka mikononi Mwake.

Wakati tunaposoma vitaa vikuu vya kihistoria, ambapo mamilioni ya watu wamenda mautini kwa njia ya kikatili, nguvu za Kristo zilizokabidhiwa wanadamu zinatumiwa na Shetani kufanya kazi yake ya uharibifu. Katika huu uharibifu wote Mungu anaonyesha upendo wake kwa kupeana Mwana Wake kufunua chimbuko la kikatili la Shetani. Je tuna weza shika maumivu ya Kristo kama pumzi anayowapulizia wanadamu ilivyotumika wakati wa Kirumi ? Jeshi la askari la vijana wakiume wakijazwa na pumzi ya Mwana wamesimama tayari kupigana wenyewe kwa wenyewe. Majeshi ya pande zote mbili wakijawa na uhai wa Kristo wanaongozwa na Shetani iliwapambane wenyewe wengine wanakatana kwa upanga, mikuki, visu na mishale. Kila kijana akipumua pumzi ya mwisho, Kristo Yuko hapo akihisi huzuni nyingi sana nafsi zi kifariki na tama ya damu ndani ya mioyo yao na mikononi mwao. Nguvu za Kristo zinabadilika kuwa nyoka wakati wanadamu wanapochagua kujitoa mikononi mwa Mungu. Lakini ili ufalme wa Shetani wakikatili ufunuliwe, Kristo lazima ajikane na akubali kuchomwa na huzuni kwa kuona uhai wake wa uzima unatumika kufanya vitu viuovu na vikatili. Katika kila tendo la kigaidi Kristo hudungwa kwa sababu lazima ajikane, abebe msalaba, na awaruhusu wanadamu wawe na uhuru wa kuchagua mwisho wa tamaa zao hao wenyewe.

Pima kwa uwangalifu kidokezi hiki, ni cha busara kuelewa ilikuona nguvu za uponyaji katika nyoka mtini. Kujikana kwa Kristo kwa kubali nguvu zake kutumika na Shetani inafunua tabia halisi ya Shetani. Wakati Kristo alikubali nguvu za kutumiwa na Shetani kumuuwa, ukatili halisi wa Shetani ulifunuliwa. Msalaba wa kweli unafungua mlango kwa watu kuona kwamba ugaidi au ukatili wote unatokana na chanzo ndani ya Shetani. Inamfungulia mwanadamu uwezo wa kuona kweli Mungu anapenda maadui Zake.Katika Kristo Mungu alikuwa akipatanisha ulimwengu na Yeye Mwenyewe na alionyesha upendo wake na tabia yake ya kutokuwa na ubinafsi. Walakini ili nyoka mwishowe aharibiwe, nguvu za Kristo lazima zirudishwe ziwe fimbo .

> Bwana akamwambia Musa, Nyosha mkono wako, kamshike mkia; (akaunyosha mkono wake akamshika, naye akageuka kuwa fimbo mkononi mwake;) Kutoka 4:4

Je mkia unasimamia nini?

> Mzee mwenye kuheshimiwa ndiye kichwa, na nabii afundishaye uongo ndiye mkia. Isaya 9:15

Mkia wa nyoka una uongo ambao anadanganya ulimwengu kuhusu tabia ya Mungu. Shetani ajulisha ulimwengu kwamba Mungu alimuua mwana wake katika hasira Yake ya kikatili.

> Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa. Isaya 53:4

Ili nguvu za nyoka zivunjwe, uongo ambao Shetani amesema kulingana na tabia ya Mungu lazima zifunuliwe. Wakati Kristo aliposema "Imekwisha" Swali ni, nini alilomaliza?

> Nimekutukuza Wewe duniani kwa kuitimiza ile kazi uliyonipa niifanye. Yohana 17:4

Wakati Kristo aliposema nimekuutukuza duniani anasema nimefunuwa tabia yako halisi duniani. Kutoka 33:18; Kutoka 34:5-7. Wakati Kristo alipolia" imekwisha " Alimshika Shetani kwa mkia: inamaanisha alifunua uongo ambao Shetani alikuwa akisema kuhusu tabia ya Baba Yake kama aliye mkatitli, na kuonyesha kwamba ni Shetani ambaye ndiye chanzo halisi cha mauuaji na uharibifu.

Ni kwa kupitia mwanga wa huu ukweli injili ilikuwa na nguvu kuhubiriwa duniani nzima katika mdaa mfupi wakati wa mitume.

> mradi tu kwamba mtaendelea kuwa waaminifu, mkiwa mmefanywa imara na thabiti katika imani, pasipo kuliacha tumaini lililoahidiwa na Injili ile mliyosikia, hii ndiyo ile Injili mliyoisikia na **ambayo imehubiriwa kwa kila kiumbe chini ya mbingu** na ambayo mimi Paulo, nimekuwa mtumwa wake. Wakolosai 1:23

Changa moto inabaki ni kwamba mtazamo wa msalaba kwa binadamu asili unaonekana kana kwamba Mungu anamuadhibu Kutosheleza hasira yake

kwetu. Hii imefanya kuwa rahisi kwa Shetani kuvumbua uongo mwingi kwa kupitia huyo mtu mdhambi kuficha nguvu kamili za msalaba. Hii imemfanya nyoka kuteremka chini kutoka pahali alipofichuliwa kwa kupitia msalaba na kwa mara nyingine tena kujificha katika giza na kuuma watu kutoka kwa kivuli na kuwashawishi kwamba Mungu ndiye mkatili anayewaadhibu. Wamisri walikuwa na fursa kuu ya kujifunza kuhusu Mungu wa kweli kwa kupitia Yusufu. Mungu alimpatia Yusufu hekima ya kuwabariki Wamisri kwa kuwaanda kutokana na njaa ambayo iliyokuja Misri na nchi zilizowazunguka.

> ikaanza kuja miaka ile saba ya njaa, kama vile Yusufu alivyosema. Kukawa na njaa katika nchi zote, bali katika nchi yote ya Misri palikuwa na chakula. Mwanzo 41:54

Farao alionywa katika ndoto ya miaka saba ya njaa iliyokuwa ikija. Maongozi ya Mungu yalimuweka Yusufu mahali ambapo angeweza kusaidia kutayarisha watu katika wakati mgumu kutokana na ukame uliotarajiwa. Mwanzo 41:25-36. Je, ni kwa nini ukame huo wakutisha ulikuwa ukiyazuru hayo mataifa?

> Msifanye sanamu yo yote, wala msijisimamishie sanamu ya kuchonga, wala mnara, wala msiweke jiwe lo lote lililochorwa katika nchi yenu ili kulisujudia; kwa kuwa mimi ndimi Bwana, Mungu wenu.(2 )Zishikeni (3) Kama mkienda katika amri zangu, na kuyashika maagizo yangu, na kuyafanya;(4) ndipo nitazinyesha mvua zenu kwa nyakati zake, na nchi itazaa maongeo yake, na miti ya mashambani itazaa matunda yake.Mambo ya Walawi 26:1-4

Tunakumbuka katika sura ya 13 kwamba Mungu alizifanya sheria za kimaumbile kumbariki mwanadamu.

> Kuna kisababishi cha uhusiano kati ya vita na migogoro ya watu, na misukosuko na vita katika maumbile. Migogoro na utovu wa maadili katika jamii inaongezea basi maafa katika maumbile yanaongezeka; hivo basi, maumbile ni kipimo cha kiwango cha uasi katika mwanadamu. Wakati upepo mwanana wa maumbile, uliyoundwa kumpoza na kumfariji mwanadamu, unageuka kuwa tufani; au mvua iliyoundwa kuleta uhai inafanya mito kuvunja kinga na kuleta maafa na uharibifu, basi tunaona thibitisha la uasi huo unaopatikana katika mioyo ya wanadamu ukiwekwa wazi katika majanga ya maumbile. *Agape,* Sura 13, ukurasa 121.

Wamisri waliabudu sanamu nyingi pamoja na mataifa yaliyowazingira. Hawakuitunza sabato wala kuheshimu hekalu la Bwana. Wakati Musa alienda kwa farao na akatoa ombi kwa niaba ya Bwana, farao kwa ufidhuli akauliza Bwana ni nani? Na madharau akasema, "Mimi si mjui." Hapa farao hakumkumbuka Yusufu. Misri ilifanywa kuwa tajiri kwa kupitia Yusufu. Kwa hivyo, hii ilikuwa kukataa kumtambua Mungu.

> Kwa maana **ingawa walimjua Mungu, hawakumtukuza Yeye kama ndiye Mungu wala hawakumshukuru**, bali fikira zao zimekuwa batili na mioyo yao ya ujinga ikatiwa giza. (**22)**Ingawa wakijidai kuwa wenye hekima, wakawa wajinga (**23)**na **kubadili utukufu wa Mungu aishiye milele kwa sanamu zilizofanywa zifanane na mwanadamu ambaye hufa, ndege, wanyama na viumbe vitambaavyo**. Warumi 1:21-23

Walikuwa hawatunzi sheria na hukumu kwa sababu tangu wakati wa Nimrodi mataifa yaliyokuwa ya kichipuka yalimdharau Mungu wa mbinguni na kuchagua kuasi na kufanya wapendavyo. Nchi ya misri na kanani zilijulikana kama nchi za Hamu.

> Israeli naye akaingia Misri, Yakobo akawa mgeni katika nchi ya Hamu. Zaburi 105:23

Hamu aliwapatia uzao wake urithi wa kutisha kwa jinaya potovu aliomfanyia baba yake Nuhu.

> Hamu, baba wa Kanaani, akauona uchi wa baba yake, akawaeleza ndugu zake wawili waliokuwa nje. (23) Shemu na Yafethi wakatwaa vazi, wakalitanda mabegani mwao wote wawili, wakaenda kinyumenyume, wakaufunika uchi wa baba yao; na nyuso zao zilielekea nyuma, wala hawakuuona uchi wa baba yao.( 24) Nuhu akalevuka katika ulevi wake, akajua mwana wake mdogo alivyomtendea. (25) Akasema,Na alaaniwe Kaanani;Atakuwa mtumwa kabisa kwa ndugu zake. Mwanzo 9:22-25

Bila shaka Nuhu alimjua mwana wake alimfanyia kitu wakati alipoamkaa inaonyesha kwamba hakumwangalia tu. Wakati Israeli alipotoka Misri aliwaambia wasifuate mienendo Wakanani na Wamisri.

> Nanyi msifanye matendo kama yale ya nchi ya Misri mliyokaa; wala msifanye matendo kama yale ya nchi ya Kanaani, nitakayowapeleka; wala msiende katika amri zao hao. Walawi 18:3

Je ni mambo gani ambayo Bwana aliwaamuru Israeli kutofanya ambayo haya mataifa yalikuwa yakifanya?

1. Zinaa ya maharimu. Walawi 18:6-18
2. Ngono wakati mwanamke ameingia mwezini. Walawi 18:19
2. Uzinifu. Walawi 18:20
3. Kutoa watoto kafara kwa sanamu. Walawi 18:21
4. Ushoga. Walawi 18:22
5. Kufanya ngono na wanyama. Walawi 18:24

Hizi dhambi zote ni urithi wa dhambi za wana wa Hamu. Hizi ni uvunjaji wa sheria za Mungu na zina mgongano mmbaya katika maumbile kwa sababu ni kinyume na maumbile

> Kwa hiyo, Mungu akawaacha wazifuate tamaa mbaya za mioyo yao katika uasherati, hata wakavunjiana heshima miili yao wao kwa wao. (25) Kwa sababu waliibadili kweli ya Mungu kuwa uongo, wakaabudu na kutumikia kiumbe badala ya Mwumba, ahimidiwaye milele! Amen. (26) Kwa sababu hii, Mungu aliwaacha wavunjiane heshima kwa kufuata tamaa zao za aibu. Hata wanawake wao wakabadili matumizi ya asili ya miili yao wakaitumia isivyokusudiwa. Warumi 1:24-26

Hizi dhambi pamoja na kula vyakula najisi, damu na vyingi vinavyopatikana Walawi, vina najisi dunia na kuifanya dhoofika.

> Dunia inaomboleza, inazimia; ulimwengu unadhoofika, unazimia; watu wakuu wa dunia wanadhoofika.(5) Tena dunia imetiwa unajisi kwa watu wanaoikaa; kwa maana wameziasi sheria, wameibadili amri, wamelivunja agano la milele.(6) Ndiyo sababu laana imeila dunia hii, na hao wanaoikaa wameonekana kuwa na hatia, ndiyo sababu watu wanaoikaa dunia wameteketea, watu waliosalia wakawa wachache tu. Isaya 24:4-6

Kanani na Misri walikuwa wakivunja amri za Mungu. Miaka saba ya njaa ilikuwa ni onyo kwa haya mataifa kwa machukizo waliyokuwa wakitenda yataathiri vibaya sana maumbile katika siku zijazo. Neema za Mungu

ziliruhusu Yusufu apelekwe Misri iliawafahamishe Mungu wa kweli ili Misri itubu machukizo yao na wahifadhiwe uharibifu ya kimaumbile. Kwa kulingana na machukizo ya uasherati, onyo limepewa haapa chini.

> na hiyo nchi imekuwa najisi; kwa ajili ya hayo naipatiliza uovu wake juu yake, na hiyo nchi yatapika wenyeji wake na kuwatoa. Walawi 18:25

Machukizo ya Misri na Kanani yalikuwa yanatayarisha nchi kutapika wakazi wake. Ukinzani wa wanadamu kwa Mungu utarudishiwa kwa wanadamu kwa kupitia maumbile.Shetani alikuwa akiwasukuma haya mataifa kwa hizi dhambi ilikuleta matokeo ya kikaidi kwa maumbile na kisha kumzingizia Mungu kwamba anafanya kwa hasira ilikuapata njia ya kuwaangamiza, lakini Bwana alitarajia kuokowa Misri na mataifa ya uasherati. Ilikuwa si tarajio lake kwa yoyote kuangamia lakini walikata kusikia ushauri wake.

Wakati tunayaangalia mapigo,ni lazima tuchunguze fungu ambalo ni la muhimu.

> Maana mimi ni Bwana, Mungu wako; Mtakatifu wa Israeli, mwokozi wako, nimetoa Misri kuwa ukombozi wako…Isaya 43:3

Bibilia inazungumzia mapigo kwa lugha ya msalaba. Fidia ililipwa ili Israeli awekwe huru. Kuna tabaka nyingi za mifano katika mapigo na hatuwezi kuangazia zote hapa. Tutaangalia ufunuo wa msalaba kwa kupitia mapigo yaliyo anguka Misri.

> Basi Musa na Haruni wakaingia kwa Farao, wakafanya vivyo kama Bwana alivyowaambia; Haruni akaibwaga fimbo yake chini mbele ya Farao, mbele ya watumishi wake, ikawa nyoka. Kutoka 7:10

Muujiza wa fimbo kugeuka nyoka inarudiwa mbele ya Farao. Hii inatowa funzo kwa Misri kwamba nguvu za nyoka siko karibu kuachiliwa.

> Akawapelekea ukali wa hasira yake, Ghadhabu, na uchungu, na taabu, **Kundi la malaika waletao mabaya.**Zaburi 78:49

Kwa kuelezea visa vya mapigo katika kitabu cha Zaburi kinazungumza kuhusu kuachiliwa kwa nguvu za malaika waletao mabaya.

> Aligeuza damu mito yao, Na vijito wasipate kunywa. (45) Aliwapelekea mainzi wakawala, Na vyura wakawaharibu.(46)

> Akawapa tunutu mazao yao, Na nzige kazi yao. (47) Aliiharibu mizabibu yao kwa mvua ya mawe, Na mikuyu yao kwa mawe ya barafu. (48) Akaacha ng'ombe zao wapigwe kwa mvua ya mawe, Na makundi yao kwa umeme.(49) Akawapelekea ukali wa hasira yake, Ghadhabu, na uchungu, na taabu, Kundi la malaika waletao mabaya. (50) Akiifanyizia njia hasira yake; Wala hakuziepusha roho zao na mauti, Bali aliiachia tauni uhai wao;(51) Akampiga kila mzaliwa wa kwanza wa Misri, Malimbuko ya nguvu katika hema za Hamu. Zaburi 78:44-51

Mapigo haya yote yanayotajwa hapa juu yanahusiana na kuachiliwa kwa malaika waletao mabaya au malaika waharibifu. Mungu aliwachilia wa ka kumbwa na tauni kwa sababu walikataa kumtambua Mungu na amri Zake. Kutajwa kwa tauni inaonyesha kuvunja agano la Mungu la milele.

> Nami nitaleta upanga juu yenu, **utakaopatiliza kisasi cha hilo agano;** nanyi mtakutanishwa ndani ya miji yenu; nami nitaleta tauni kati yenu; **nanyi mtatiwa mkononi mwa adui.** Walawi 26:25

Haiko wazi vile malaika wovu wanavyo husishwa au vile wanavyo fanywa watumie sheria za kimaumbile ambazo zilikuwa zikiwatapika wakazi. Walakini yalikuwa haya mambo mawili sheria za kimaumbile zikiunganishwa na kazi ya uharibifu wa malaika waovu walioleta uharibifu Misri. Hata hivyo kwa hii njia ya uharibifu Mungu pia anawafikia iliwatubu dhambi zao na waokolewe.Lazima ikumbukwe ya kwamba nguvu zote zilizoonyeshwa zinatoka kwa Kristo ambaye ni uwezo na hekima ya Mungu. Walakini Kristo lazima abebe msalaba wake wa mateso kwa kuruhusu haya matendo ya uharibifu ya tendeke.

Nguvu za Kristo ziliishi ndani ya nafsi za Wamisri. Mauaji ya mtu yoyote ilihusu kumtesa mtu wa Kristo. Je unaweza kufikiria Mwanamke wa kimisri akimshika mwana wake aliyefariki, akiinama juu ya mwili usio na uhai akilia kwa roho ya huzuni? Hapa Kristo pia ameteseka mateso yake huyo mama, hapa msalaba umeinuliwa na Kristo amesulubiwa tena. Mungu akimruhusu Shetani kuchukuwa nguvu za Mwana Wake, amemruhusu Shetani kugusa jicho Lake.

> Akiifanyizia njia *hasira* [H639 pua, uso] yake; Wala hakuziepusha roho zao na mauti, Bali aliiachia *tauni* [H1698 – haribu] uhai wao; Zaburi 78:50

Fungu hili linaelezea mapigo ya Misri. Inasema Mungu alitengeneza njia kwa uso wake. Mwana Wake mpendwa ndiye furaha ya maisha yake. Kwa kuwaruhusu wa Misri wafe mikononi mwa mharabu, aliruhusu uchungu na mateso ya Mwana Wake; na Baba Alisimama peke Yake gizani akiomboleza Mwana wake wakati wa mapigo ya Misri na mateso yote ambayo Mwana alipata.

Mapigo yalikuwa si bila utaratibu lakini yalielekeziwa miungu Wamisri waliotumikia. Wamisri kama vile waabudu wengine wa kipagani, ilikuwa ni lazima wawaridhishi miungu yao na wasiwakasirishe amasivyo wangeadhibiwa. Mapigo ya merudishiwa Wamisri kwa kioo cha uungu. Kuona kwao hatia kutokana na ibada zao za Sanamu za machukizo. kuuwa watoto, ukatili wa wakitumwa, ulafi wao waupotovu, na ngono zao za upotovu zilikuwa zinawarudia kwa hiki kioo. Mto Naili ulikuwa ukiabudiwa chini ya mungu Hapi, mungu wa uzaaji.

Amri ya kuwatupa watoto wakiebrania ndani ya mto miaka 80 hapo awali ilikuwa inawarudia kwa kioo cha matendo yao. Na wakati huo huo sheria za kimaumbile zilizobebwa na Kristo zilikuwa zinaanguka kwa uzito wa machukizo. Mwana wa Mungu alivyotazama Misri kwa siku za usoni, alilemewa na huzuni, na mto unatupatia mfano wa kile Kristo angekiona katika shamba la Gethsimani wakati jasho lake liligeuka damu na mwili wake ukaanza kuanguka. Ni uzito wa dhambi ambao ulikuwa ukileta uharibifu ndani ya Kristo na ni matendo ya unajisi wa kibinafsi ya Wamisri ambayo yalifanya Naili kuharibika na vyote vilivyomo ndani yake.

Matumizi ya fimbo ni muhimu.

> Musa na Haruni wakafanya hivyo, kama Bwana alivyowaambia; **naye akaiinua ile fimbo, na kuyapiga maji yaliyokuwa mtoni**, mbele ya Farao, mbele ya watumishi wake; na hayo maji yote yaliyokuwa katika mto yakageuzwa kuwa damu. Kutoka 7:20

Kutafuta matumizi ya fimbo kupiga mahali pengine katika maandiko ni muhimi.

> bali kwa haki atawahukumu maskini, naye atawaonya wanyenyekevu wa dunia kwa adili; **naye ataipiga dunia kwa fimbo ya kinywa chake**, na kwa pumzi ya midomo yake atawaua wabaya. Isaya 11:4

Fimbo ni mfano wa Neno la Mungu na pumzi ya kinywa Chake. Wakati Kristo alipoangikwa msalabani ni hatia ya dhambi katika uso wa amri zilizovunjwa ndiyo iliyofanya nafsi yake kuchomeka kama moto. Chimbuko hili la kupigwa lapatikana kwengineko ndani ya maandiko.

> Sasa utajikusanya vikosi vikosi, Ee binti wa vikosi; yeye amemhusuru; **watampiga mwamuzi wa Israeli** shavuni mwake kwa fimbo. Mika 5:1
>
> Amka, Ee upanga, juu ya mchungaji wangu, na juu ya mtu aliye mwenzangu, asema Bwana wa majeshi; **mpige mchungaji**, nao kondoo watatawanyika; nami nitaugeuza mkono wangu juu ya wadogo. Zekaria 13:7
>
> Tazama, nitasimama mbele yako huko, juu ya lile jabali katika Horebu; nawe **utalipiga jabali**, na maji yatatoka, watu wapate kunywa. Musa akafanya hivyo mbele ya wazee wa Israeli. Kutoka 17:6

Kristo ndiye mtawala wa maumbile yote. Uovu wa Wamisri ulinajisi dunia na kumfanya Kristo kuchomwa na taji ya miiba. Kupigwa kwa jabali ili maji yatoke ilikuwa inaonyesha jinsi Wamisri walikuwa wakimfanyia Kristo. Kristo ndiye chemichemi ya maji ya uhai na walikuwa wakimpiga na kumfanya ateseke. Mungu anawafunilia Wamisri madhara ambayo hali yao ilikuwa ikifanya. Hii ndiyo kazi ya sheria kumrudishia mwanadamu aliyeanguka hali yake ya dhambi. Walakini dunia nzima inaona Mungu kama anaharibu pahali panapo waletea Wamisri maji. Ukimwaangalia Kristo kama amepigwa na Mungu na mteswa. Wakati Kristo alichomwa kulitoka damu na maji na hili ndilo tunaona katika Naili.

Pigo la pili lilikuwa ni kioo kwa mungu mwengine wakike Hekweti.

> Hekweti (Mmisri ḥqt, also ḥqtyt "Heqtit") ni mungu Wakimisri wakike wa uzaaji na anajulikana na Hathori, anayesimamiwa na chura.kwa Wamisri, chura alikuwa ni mfano wa kale wa uzaaji,inayolinganishwa na mafuriko ya kila mwaka wa Naili...imependekezwa ya kwamba jina lake lina chanzo katika jina Hekate,mungu wa uchawi wa kiyunani. *Wikipedia*.

Uzaaji wa Misri uliharibiwa na machukizo ya Wamisri wenyewe. Dunia ilikuwa ikiwatapiaka na vyura walikuwa ni rudisho la haya matapishi. Mungu

aliruhusu ibada yao warudishiwe katika kioo. Walikuwa wakitembelewa na Kuogopa kwa miungu. Haya si matukio bila utaratibu bali maumbile yanarudisha mawazo ya wanadamu. Kama vile Yesu anavyo tuambia:

> Kwa maana kwa jinsi ile unavyowahukumu wengine, ndivyo utakavyohukumiwa na kwa kipimo kile utakachotoa ndicho utakachopokea. Mathayo 7:2

Hata hivyo, chura anaelezea chimbuko la uongo. Tulitambua hapo juu Hekweti alihusishwa na uchawi. Shetani alikuwa akiiga haya maono katika maumbile kwa kupitia makuhani wake.Vyura wanahusishwa na pepo wachafu zinazotenda miujiza.

> Kisha nikaona roho wachafu watatu waliofanana na vyura wakitoka katika kinywa cha lile joka na katika kinywa cha yule mnyama na katika kinywa cha yule nabii wa uongo. (14) **Hizo ndizo roho za pepo wachafu zitendazo miujiza. Nazo huwaendea wafalme** wa ulimwengu wote na kuwakusanya tayari kwa ajili ya vita katika siku ile kuu ya Mungu Mwenyezi. Ufunuo 16:13-14

> Huyu mnyama wa pili akafanya ishara kuu na za ajabu, hata kusababisha moto kushuka toka mbinguni kuja duniani watu wakiona waziwazi. (14) **Kwa sababu ya zile ishara alizokuwa amepewa uwezo wa kufanya kwa niaba ya yule mnyama wa kwanza, akawadanganya wakaao duniani.** Akawaamuru wasimamishe sanamu kwa heshima ya Yule mnyama aliyekuwa amejeruhiwa kwa upanga lakini akaishi. Ufunuo 13:13-14

Roho ya uongo katika udanganyifu wa miujiza ya nyoka, na mapigo mawili ya kwanza yaliyoigwa na makuhani ya lizuia roho ya toba kwa Wamisri, ambayo mwishowe ilitia muhuri kuangamia kwao. Kwa njia hiyo hiyo roho ya uongo ilikuwa wakati Kristo alihukumiwa kwa kumshuhudia uongo na kwa sababu hii kumhifadhi kwa maangamizi msalabani.

Pigo la tatu lilihusiana na mavumbi ya ardhi.Kulikuwa na miungu miwili ambayo ilihusika na mchanga. Horus, ambaye alikuwa bwana wa mchanga mweusi na Set ambaye alikuwa mungu wa mchanga mwekundu wa jangwa. Mchanga mweusi wenye rotuba ulitumiwa kupandia mimea. Chawa ambao walitoka kwa mchanga ilikuwa ni onyo kwamba kwamba mchanga ulikuwa ukiharibika na kuchakaa kama vazi.

> Inueni macho yenu mbinguni, mkaitazame nchi chini; maana mbingu zitatoweka kama moshi, na **nchi itachakaa kama vazi, nao wakaao ndani yake watakufa kadhalika**; bali wokovu wangu utakuwa wa milele, na haki yangu haitatanguka. Isaya 51:6

Neno la kiebrania nakadhalika kwa kweli ni chawa. Niufunuo wa  nchi kuchakaa. Laana ya machukizo ya watu yalifinya moyo wa Kristo. Kama vile inavyo sema kwa Zaburi:

> Heri BWANA asiyemhesabia upotovu, Ambaye rohoni mwake hamna hila. (3) **Niliponyamaza mifupa yangu ilichakaa Kwa kuugua kwangu mchana kutwa**. (4) Kwa maana mchana na usiku Mkono wako ulinilemea. Jasho langu likakauka hata nikawa Kama nchi kavu wakati wa kaskazi. Selah. Zaburi 32:2-4

Mwana wa Mungu alitulia, akiwapatia Wamisri uhuru wao, uzito alioubeba akijaribu kuhifadhi nchi kutokana na unajisi ulimfanya kuugua.

> Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote vimekuwa vikilia kwa uchungu kama utungu wa wakati wa mwanamke kuzaa hata sasa. Warumi 8:22

Kuugua huku na kulia kwa uchungu wa kuzaa vinaonyesha mateso ya Kristo katika shamba chini ya uzito wa dhambi. Kwa mtu wa kawaida hii ilikuwa hasira ya Horus iliyokuwa ikiwajia, lakini kwa mtu wa kiroho tunaona kuoza na kudhoofika kwa dunia chini ya upotovu Wamisri na matokeo ni mateso ya Kristo.

Pigo la nne lilikuwa aina ya maainzi, wadudu na inaweza kuwa mdudu mwenye mabawa anayetambaa wa jamii ya mende kama vile ilivyotafsiriwa katika Tafsri Ndogo Ya Wazi. Haya mapigo yanasema nchi iliharibika kabisa kwa pigo.

> Bwana akafanya; wakaja wingi wa mainzi kwa uzito sana, wakaingia nyumbani mwa Farao, na katika nyumba za watumishi wake, tena katika nchi yote ya Misri; nayo nchi iliharibiwa kwa ajili ya wale mainzi.Kutoka 8:24

Jina la kiebrania la ufisadi ndio neno kamili lilotumika kwa mharabu aliyetajwa pigo la mwisho aliye wauwa kifungua mimba huko Misri. Na pia ni neno hilo hilo linalotumika kuelezea dunia kabla ya gharika.

> Mungu akaiona dunia, na tazama, **imeharibika**; maana kila mwenye mwili amejiharibia njia yake duniani. Mwanzo 6:12

Hili pigo la nne lilionyesha unajisi uliosababishwa na Wamisri. Farao alimkana Mungu wa kweli wa mbinguni na akafanya vitu vya machukizo, kwa hivyo mbegu ambazo yeye pamoja babu zake walizo panda zilikuwa sasa zikionekana:

> Mpumbavu amesema moyoni, Hakuna Mungu; Wameharibu matendo yao na **kuyafanya chukizo**, Hakuna atendaye mema. Zaburi 14:1

> Hakuna hata mmoja mwenye ufahamu, hakuna hata mmoja amtafutaye Mungu.(12)Wote wamegeukia mbali, wote kwa pamoja hawafai, hakuna atendaye mema, naam, hata mmoja." (13)"Makoo yao ni makaburi wazi, Warumi 3:11-13

Bwana alikuwa akishikilia hizi pepo nne za vita na alikuwa akitaka kusema, "upepo tulia," kwa dunia lakini mwishowe dunia ikawatapika wakazi wake

Pigo la tano lilikuwa kwa mifugo, farasi, ngamia na punda. Wamisri hawakuwa na kinga dhidi ya mharabu. Kama Farao angelitubu basi kazi ya malaika ya uharibifu ingezuiliwa kwa kupitia maumbile lakini haikuwa hivyo. Ilibidi Bwana apeane mifugo kwa mharabu. Wamisri walikataa kuja kwa Bwana iliwaokolewa, kwa hivyo Shetani achukua utawala mwingi na mwingi wa Misri.

Tunafahamu ya kwamba Shetani aliruhusiwa, akamletea Ayubu majipu, na hivi ndivyo Shetani aliwafanyia wa Misri katika pigo la sita. Ni jinsi gani Kristo aliteseka akiwaona wana Wake wakiteseka kwa kupitia majipu, na je ni maumivu gani aliyoyapata kwa kumruhusu Shetani kufanya hivi vitu. Kwa hakika mapigo yalisonga kutoka kwa wanyama kwenda kwa majipu ya wanadamu inaonyesha kwamba Shetani alipata utawala mwingi wa hiyo hali kama vile alivyofanya kwa Ayubu.

> Bwana akamwuliza Shetani, Je! Umemwangalia huyo mtumishi wangu Ayubu? Kwa kuwa hapana mmoja aliye kama yeye duniani, mtu mkamilifu na mwelekevu, mwenye kumcha Mungu na kuepukana na uovu; naye hata sasa anashikamana na utimilifu wake, ujapokuwa ulinichochea juu yake, ili nimwangamize pasipokuwa na sababu.(4) Shetani akamjibu Bwana, na kusema, Ngozi kwa ngozi,

> naam, yote aliyo nayo mtu atayatoa kwa ajili ya uhai wake.(5) Lakini sasa nyosha mkono wako, uuguse mfupa wake na nyama yake, naye atakukufuru mbele za uso wako.(6) Bwana akamwambia Shetani, Tazama, yeye yumo mkononi mwako; lakini tunza tu uhai wake.(7) Basi Shetani akatoka mbele za uso wa Bwana, akampiga Ayubu na majipu mabaya tangu wayo wa mguu hata utosi wa kichwa. Ayubu 2:3-7

Majipu yaliyodhihirika kwa Wamisri yanaweza kuzungumzia mateso ya Kristo wakati alipoangikwa kwa msalaba Wake. Ilikuwa ni kuumiza mwili wa mwanadamu.

Mateso ya Wamisri yalikuwa mateso Yake na uchungu wao ulimdhuru sana, na hata hivyo aliendelea kumruhusu Shetani aonyeshe hiyo nguvu kwa sababu hawa watu walikata kuitikia wito kubadilika waokolewe. Kama Yesu alivyo waambia mafarisayo, "Mara ngapi nimetamani kuwakusanya watoto wako, kama vile kuku akusanyavyo vifaranga wake chini ya mbawa zake, lakini hukutaka!"

Kwanza ni samaki alikufa, kisha vyura, baadaye ng'ombe na sasa majipu kwa miili ya watu. Musa aliwaonya Wamisri kwa kila pigo iliwawe waangalifu kumfukuza mharabu. Wangeli mwacha huyu nyoka anayeuma na kumwangalia nyoka aliyeinuliwa mtini. Kwa kuinuliwa kwa Kristo kwa kupitia uchungu wa mapigo, nyoka aliwekwa hadharani kwa yule aliyekuwa-mharabu. Shetani anatafuta kujificha katika nguvu za Mungu na atume vyura kwetu na kutuambia ni Mungu anayefanya haya hivi vitu. Mwana wa Mungu aliteseka sana kwa kuona nguvu zake zinatumika duniani kuleta uharibifu kwa njia ya kikatili. Sheria zake za kimaumbile, ambazo zilibuniwa kubariki wale ambao wanampenda Bwana na kutunza amri zake, zilikuwa sasa zimebadilishwa kama silaha za uharibifu kwa wingi. Shetani na malaika wake walihusika kwa njia nyingi za kuongeza uharibifu kwa sababu Shetani alijuwa angeliwafanya wanadamu kufikiria kwamba ni Mungu ndiye anayefanya uharibifu.

> Musa akaunyosha mkono wake kuelekea mbinguni; na Bwana akaleta ngurumo na mvua ya mawe, na moto ukashuka juu ya nchi; Bwana akanyesha mvua ya mawe juu ya nchi yote ya Misri. Kutoka 9:23

Wakati Musa alipoinua fimbo kuelekea mbinguni, ilikuwa ni ishara ya Mwana wa Mungu kuinuliwa juu msalabani.Kristo nguvu za Mungu alikabidhiwa Shetani kumtumia kwa kulingana na kusudi lake. Mungu aliruhusu mwanya katika ulinzi wake na malaika walioasi ambao wanaopenda vifo wakarusha mvua yam awe nchini. Kumbuka vile Zaburi inavyonena:

> **Aliiharibu mizabibu yao kwa mvua ya mawe**, Na mikuyu yao kwa mawe ya barafu.48 Akaacha ng'ombe zao wapigwe kwa mvua ya mawe, Na makundi yao kwa umeme.49 Akawapelekea ukali wa hasira yake, Ghadhabu, na uchungu, na taabu, **Kundi la malaika waletao mabaya**. Zaburi 78:47-49

Mvua ya mawe imetajwa katika Zaburi 18 ambayo inazungumzia mateso ya Kristo msalabani.

> Toka mwangaza uliokuwa mbele zake Kukapita mawingu yake makuu. Mvua ya mawe na makaa ya moto. Zaburi 18:12

Tazama inasema kwamba "aliachilia" ng'ombe zao kwa mvua ya mawe na kiebrania "kuwatupia" inamaanisha kuachilia au kulegeza. Tunaona nguvu za Mungu zikipewa Shetani na tunatilia mkazo kidokezo kwamba hii inafanyika kwa kupitia mateso na maumivu ya Kristo. Wakati wowote Mungu anamruhusu Shetani kuharibu kwa nguvu zake, Mwana wake anainuliwa msalabani, lakini wakati huo huo Shetani anafunuliwa kama mharabu kwa wale wanao angalia kioo cha injili ya kweli. Wakati wa pigo la mvua ya mawe tunashuhudia yafuatayo:

> Kitani na shayiri zilipigwa; maana shayiri zilikuwa na masuke na kitani zilikuwa katika kutoa maua. Kutoka 9:31

Shayiri ilitumika kama sadaka ya tunda la kwanza. Kwa watu waliouawa kwa mvua ya mawe, matunda ya kwanza pia yaliharibiwa. Maandiko yanasema:

> Lakini kila mmoja kwa wakati wake: Kristo,tunda la kwanza la ufufuo, kisha, wale walio wake atakapokuja. 1 Wakorintho 15:23

Mvua ya mawe kuharibu shayiri ni mfano wa kugongwa gongwa kwa Kristo, tunda la kwanza. ("tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu" Isaya 53:4) Pigo linalo fuata lilihusu nzige na tunaambiwa pahali pigo la nzige linapo toka katika Ufunuo.

> Alipolifungua hilo shimo lisilo na mwisho, moshi ukapanda kutoka humo kama moshi wa tanuru kubwa sana. Jua na anga vikatiwa giza na ule moshi uliotoka katika hilo shimo lisilokuwa na mwisho. (3) **Ndipo katika ule moshi wakatoka nzige wakaenda juu ya nchi, nao wakapewa nguvu kama zile za nge wa duniani.** Ufunuo 9:2-3

Hii inatuelekeza kwa nguvu za uharibifu wa Shetani kwa kupitia uongo wake na hii ndiyo iliyotendeka katika pigo hili. Shetani angeguguna chini na kutoa kila chupukizi kijani kibichi cha tumaini la kushikamana na wokovu. Shetani alikuwa akimsukumia Kristo fikira za kuonyesha kwamba hiyo kazi yake yote ilikuwa ni ya bure na hakuna ambaye atakaye kuikubalia. Pia alipeana jaribu kali kwamba Baba Yake atamuacha.

> Wamenizua mikono na miguu. (17) Naweza kuihesabu mifupa yangu yote; Wao wananitazama na kunikodolea macho.(18) Wanagawanya nguo zangu, Na vazi langu wanalipigia kura. Zaburi 22:16-18

> Watu waliokuwa wakipita njiani wakamvurumishia matukano huku wakatikisa vichwa vyao(40)na kusema, "Wewe ambaye utalivunja hekalu na kulijenga kwa siku tatu, jiokoe mwenyewe basi! Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, shuka kutoka msalabani."(41)Vivyo hivyo, viongozi wa , makuhani, walimu wa sheria na wazee wakamdhihaki wakisema, (42) "Aliwaokoa wengine, lakini hawezi kujiokoa mwenyewe!. Yeye ni Mfalme wa Israeli! Ashuke sasa kutoka msalabani, tutamwamini. (43)Anamwamini Mungu, basi Mungu na amwokoe sasa kama anamtaka, kwa maana alisema, 'Mimi ni Mwana wa Mungu.' " (44) Hata wale wanyang'anyi waliosulibiwa pamoja naye wakamtukana vivyo hivyo. Mathayo 27:39-44

Pigo la kumi la giza lina warudishia Wamisri hasira ya mungu wa jua Ra, lakini kwa anayetafuta ukweli inazungumzia tisho la Kristo msalabani kwa kuwa alizingirwa na pepo mbaya. Hapa Shetani alijua kwamba angeweza kutekeleza uharibifu kamili wa Misri; hii nchi tukufu ambayo walijifunza mengi kwa Israeli hapo awali na Mungu aliibariki sana. Kile kicheko laghai kinacho tambulisha uso wa waovu kinatokea akijua Misri itaangamia milele. Katika maangamizi hayo inaonyesha mateso ya Kristo msalabani na maumivu

yake akiona kupotea kwa wana wa Misri wakiangamizwa na Shetani. Giza linazungumzia kwa kweli matukio ya msalaba.

> Siku kwa siku nilikuwa pamoja nanyi hekaluni lakini hamkunikamata. Lakini hii ni saa yenu, wakati giza linatawala!" Luka 22:53

> Tangu saa sita hadi saa tisa giza lilifunika nchi yote. Mathayo 27:45

Je saa tisa inauhusiano na pigo la tisa?Kwa njia yoyote haya masaa yalikuwa ya giza kwa Kristo na kwa wa Misri.Wote walipigwa na hofu kwa kile kilicho karibu kuwa angukia.Giza pia linazungumzia kufunikwa kabisa uso wa Baba.

> Huu ndio ujumbe tuliosikia kutoka Kwake na kuwatangazia ninyi, kwamba **Mungi ni nuru na ndani yake hamna giza lo l**ote. 1Yohana 1:5

Giza linaonyesha kwamba Shetani amechukuwa kamili utawala wa Misri. Kilichobaki ni kifo cha kifungua mimba ambalo ni pigo la mwisho, na hii ndiyo tamati ya kazi ya mharabu. Katika vifo vyao kinafunuliwa kifo cha Kristo.Kristo kwa kupenda angekubali kuwafilia! lakin walichagua mharabu na sasa lazima wa kutane naye.Na kwa wale ambao kwa rehema na kwa imani waliweka damu ya mwana kondoo katika juu ya milango yao, Shetani angeruhusiwa kuingia ndani ya nyumba.

> Kwa kuwa Bwana atapita ili awapige hao Wamisri; na hapo atakapoiona hiyo damu katika kizingiti cha juu, na katika ile miimo miwili, Bwana atapita juu ya mlango, **wala hatamwacha mwenye kuharibu aingie nyumbani mwenu kuwapiga ninyi.** Kutoka 12:23

Tena wacha tujikumbushe – mharabu ni nani?

> Walikuwa na malaika kutoka kwenye hilo shimo lisilo na mwisho kama mfalme wao, ambaye jina lake kwa Kiebrania ni Abadoni**b** na kwa Kiyunani ni Apolioni—Mharabu. Ufunuo 9:11 (NLT)

> Msinung'unike kama baadhi yao w alivyofanya, wakaangamizwa na mharabu.[ nyoka mwenye sumu.] 1 Wakorintho 10:10

Kwa kumlazimisha Mungu atoe ulinzi wake, malaika wanaoleta mabaya hawakuzuiliwa kufanya kazi yao kwa kulingana na kibali, na vifungua mimba

wa Wamisri wote wakafariki, ikionyesha mbele kifo cha Kristo. Katika mapigo kumi ya Misri msalaba wa Kristo uliinuliwa juu sana kuonyesha kwamba nguvu za Mungu ambazo zilitumika kuleta uharibifu kwa kupitia sheria za maumbile kwa mwiitikio wa uovu wa Misri kwa kuvunja boma na kumruhusu Shetani na malaika wake waingie kuharibu. Huu uharibifu ungefanyika kwa kupitia uchungu na mateso ya Kristo ambaye alichinjwa tangia msingi wa ulimwengu kwa kupitia matendo ya mharabu kwa wanadamu. Chuki ya Shetani kwa mfano wa Mungu inapatikana kwa mwanadamu inamfanya kuwa na karamu ya furaha kwa kufurahia kummuuwa wakati na mahali kunapo wezekana. Jinsi gani Shetani alishangilia kwa kuona kuharibika kwa Misri na mateso aliyosababisha kwa Kristo na Baba. Mkono wa kuume uligeuka wa ukoma na fimbo yake ikawa nyoka. Kama tunawezaona kwa kupitia tope la kunata la vyura, uongo wa Shetani unasimulia kuhusu haya mapigo, hapo tutaona Mungu akiteseka na Mwana wake, msalaba wa Kristo ukiinuliwa juu, na huko kuiinuliwa juu tunamwona nyoka vile alivyo – muuaji na muongo kwanzia mwanzo. Yohana 8:44. Msalaba unatufunuliya uovu wa Shetani na Mungu si mwepesi wa hasira kwa kumruhusu kutumia uhuru wake wa uchaguzi kwa hasara yake.

Uharibifu unaletwa na:

Nguvu za Mungu
→ Sheria za maumbile
→ Na uovu wa Misri
→ Unaleta mwanya kwa boma
→ Shetani na malaika waovu

Kufahamu kwetu kwamba mapigo yanaletwa na Mungu kutumia nguvu kumlazimisha Farao kuwaachilia Israeli waende inaonyesha vile moyo wa mwanadamu usugu na vile kuna uchache wa kuelewa tabia ya upendo wa Baba aliye mbinguni. Si mapenzi ya Mungu mtu yoyote apotee bali wote waje tobani wakubali kutunza sabbato, amri na sheria.

Tuache dhambi zetu,na twende kwa Kristo ilitusimsulubishe upya kwa matendo yetu ya dhambi lakini tusulubishwe ndani yake kila siku na tufufuliwe kwa maisha mapya kupitia nguvu za ufufuo wake. Je tunawezaona kwa mapigo, mahubiri ya msalaba wa Kristo na mateso yake makuu na kujua Shetani atafurahia uamuzi wake kuhusu Misri na kuwaangamiza? Je unaona picha ya upole ya Mungu kwamba alifanya kila awezalo kuwaokowa?

“Ni jinsi gani upendo wa Baba kwetu ni mkuu. Ni jinsi gani u mepita kipimo kwamba angepeana Mwana wake pekee kufanya rasilimali yake kuisha.” [3]

> Maana mawazo yangu si mawazo yenu, wala njia zenu si njia zangu; asema Bwana.9 Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu. Isaya 55:8-9

[3] Wimbo na Stuart Townend, Ni jinsi gani kina kirefu upendo wa Baba kwetu. 1990


# 21. Agano la Milele na Utumishi wa Kifo

Agano la kale limejawa na hadithi za vifo vya kikatili sana ambavyo vinaoneka kufanywa na wafuasi wa Mungu na pia au kutekelezwa mara moja na Mungu Mwenyewe. Hatuwezi kuwasomea watoto wetu  hizi hadithi kwa sababu ya uwoga wa kuwatia hofu. Agano la kale linaonekana kama la kuaibisha kwa Ukristo ambao unataka kuhubiri upendo na rehema za Mungu kupitia hadithi ya Yesu.

Njia moja ambayo Wakristo wamejaribu kuangazia ukatili ambao unaonekana kwamba unatoka kwa Mungu katika Agano La Kale ni kwa kuelewa Agano la Kale na Jipya. Wakristo wengi hufunza ya kwamba Ahadi ya Kale linahusiana na Agano la kale au wakati ambao kabla ya Kristo kuja duniani na kufa msalabani.Ilikuwa ni kipindi sheria ambapo ilikuwa lazima "uti na uishi," au kutoti na kufa. Pia kuna hisia kwamba watu wa Agano la Kale walikuwa watu wa zamani katika na wangeelewa lugha ya ukatili katika kusuluhisha mambo katika shida.

Kinyume na Agano jipya vile inavyoeleweka kama kipindi cha neema. Upendo wa Mungu sasa unafunuliwa kwa Kristo, na karama ya Roho mtakatifu ambayo ilikuja wakati iliwaruhusu wanadamu kufahamu injili. Wale wa Agano la kale wangeliota kuhusu ukweli wa siku za usoni za injili ambazo hawangeweza kuzifikia. Wasomi wa maandiko wengine wamefikiria haya kwamba Mungu anajaribu kufanya vitu kwa njia moja tu kuona haijafaulu na

halafu kujaribu njia moja ya upendo. Wengini wanaonyesha hiyo hali kama Mungu anafanya vile awezavyo mpaka wakati Masihi angefika. Hii inazua mjadala kwa nini ilimchukuwa muda mwingi kuja duniani? Wengine wanasema ingekuwa bora kumtuma kitambo ilikuleta njia ya upendo mapema.




Njia hii kwa Agano la Kale na Agano Jipya inatuonyesha kanunu mbili za wokovu zilizo na ukinzani. Agano la Kale laangazia sheria bali Agano Jipya linaonyesha rehema. Kuonyesha kwa kanuni mbili katika nyakati tofauti za historia ya ulimwengu inahakikisha kwamba hizo Ahadi zinaeleweka kwa njia ya kupingana. Lakini wakati kanuni hizo zikiwekwa katika utaratibu wa maisha ya mtu yanafunua njia nzuri ya uungu ya matengenezo.

Ijapokuwa somo hili linaonekana kama la kuchosha na haliambatani na tabia ya Mungu, lakini likieleweka litachangia sehemu muhimu kufunguwa ayaa zinazoonyesha Mungu kama ni mkatili na matendo Yake ya kinyama.

Hebu tuchukuwe mfano wa mtu ambaye ana mfupa unaokua vibaya. Baada ya kumtembelea daktari, daktari anamfahamisha kwamba lazima uvunjwe na uwekwetena vizuri iliuwe vizuri. Je, itakuwaje kama daktari amefanya sehemu ya kwanza? Je itakuwaje kama atavunja mfupa kisha auwache? daktari ataonekana kama hana ujuzi kabisa wa kazi yake. Hebu mwangalia mwengine ambaye anamtembelea daktari wa meno kwa sababu ya kuhisi uchungu mdomoni. Daktati wa meno anagundu jino lililooza sana. Kwa ruhusa ya mgonjwa aanze kutoboa jino ilikulijaza. Wakati mwingine mgonjwa anaweza kuhisi uchungu mwingi mno. Je iwapo daktari afanye sehemu moja ya kazi? Ikitoboa jino nakutowa sehemu iliyooza kisha amwache mgonjwa kwenda nyumbani bila kukinga sehemu iliyowachwa wazi, hilo jino bado litaleta uchungu. Na huyo daktari wa meno itaonekana kwamba anamadharau *kwa sababu ya kufanya sehemu moja ya matengenezo*.

Hebu tuone katika maandiko. Hebu angalia kwa makini tumizi la neno *na* likipigwa mstari. Hii inaonyesha matendo lile kabla na baada ya nayofanywa kwa utaratibu si moja au lengine.

> Fahamu sasa ya kuwa Mimi, naam, Mimi ndiye, Wala hapana Mungu mwingine ila Mimi; Naua **Mimi, nahuisha Mimi, Nimejeruhi, tena naponya**; Wala hapana awezaye kuokoa katika mkono wangu, Kumbukumbu la Torati 32:39
>
> Bwana huua, naye hufanya kuwa hai; Hushusha hata kuzimu,tena huleta juu. (7) Bwana hufukarisha mtu, naye hutajirisha; Hushusha chini, tena huinua juu. 1 Samweli 2:6-7
>
> Wakati wa kuua, **na** wakati wa kupoza; Wakati wa kubomoa, **na** wakati wa kujenga;(4) Wakati wa kulia, **na** wakati wa kucheka; Wakati wa kuomboleza, **na** wakati wa kucheza;(5) Wakati wa kutupa mawe, **na** wakati wa kukusanya mawe; Wakati wa kukumbatia, na wakati wa kutokumbatia; Mhubiri 3:3-5
>
> Yeye ndiye aliyetufanya sisi kuwa wahudumu wa Agano Jipya, si wa andiko bali wa Roho, sisi ni watumishi wenu kwa ajili ya Yesu.2 Wakorintho 3:6

Katika visa hivi Bibilia inafunua njia ya viwango viwili. Kwanza kuna kupima kujuwa ukubwa wa tatizo na ufunuo kiasi cha uchungu. Pili kuna tiba iliyotolewa na uponyaji. Hivi ndivyo ahadi inavyofanya kazi kwa kila maisha ya mtu. Fungu katika 2 Wakorintho 3:6 linafungamanisha njia ya mauaji na njia ambayo Roho anapeana uhai na neno la kiyunani *de* [G1161] ambalo laweza kutafsiriwa *na* Kamusi ya maneno makuu ya Nguvu inaelezea kwamba ni msingi wa kipande ambacho cha weza kuwa "inapinga au inaendeleza." Tendo la ahadi ya kwanza linapinga ahadi ya pili kwa sababu inafichua na kuvunja, bali la pili linaponya na kujenga. Inaendeleza kwa maana ahadi ya pili inafuata au inaendelea kutoka kwa ya kwanza. Hebu tuangalia hii njia kama vile Paulo anaelezea kwa maisha ya Ibrahimu.

> Kwa maana imeandikwa kwamba Abrahamu alikuwa na wana wawili, mmoja wa mwanamke mtumwa na wa pili wa mwanamke huru. (23) Lakini, mtoto wa mwanamke mtumwa alizaliwa kwa mapenzi ya mwili na yule mwingine wa mwanamke huru alizaliwa kutokana na ahadi ya Mungu. (24) Mambo haya yanaweza kuchukuliwa kama mfano. Kwa maana hao wanawake wawili ni

> mfano wa maagano mawili: Agano la kwanza, ni lile lililofanyika katika mlima wa Sinai, lizaalo watoto wa utumwa. Hili ndilo huyo Hajiri. (25) Basi Hajiri anawakilisha mlima Sinai ulioko Arabuni na unafanana na Yerusalemu ya sasa ambayo iko utumwani pamoja na watoto wake. (26) Lakini Yerusalemu wa juu ni huru, nayo ndiye mama yetu. Wagalatia 4:22-26 (NKJV)

Mungu aliahidi kumpa Ibrahimu mwana wa kiume. Shida ilkuwa ya kwamba Ibrahimu alikosa imani kwa Mungu.Hakujuwa alikuwa na shida kiasi gani mpaka yeye na bibi yake wakakosa kupata mtoto. Haya aliyokuwa akipitia ilikuwa kupima tatizo. Mungu aliruhusu kuchelewa kwa Sara kupata mtoto ilikutokuwa na imani kwa Ibrahimu na Sara kudhihirike. Hii sehemu ni muhimu iliuponyaji utendeke. Ukubwa wa tatizo lazima lidhihirike kamili iliuponyaji halisi utimike. Badala ya kumgoja Bwana, Ibrahimu aliitikia wito wa maoni ya Bibi yake kumchukuwa mjakazi wakeiliapate mtoto na yeye. Mwanzo 16:1-2.

Kwanza wakati Ishmaili alipozaliwa na Hagari, ilionekana kama suluhisho kamili, lakini mambo ya kaanza kwenda mrama. Kutokuwa na imani ilileta mbegu za ugomvi nyumbani kwake. Huu ugomvi umeendelea hadi sasa katika hisia kali za wayahudi na waislamu. Hadithi hii inaonyesha vile kutokuwa na imani kunavyo leta matokeo maovu. Bwana aliruhusu haya ya tendeke ilikudhihirisha kutokuwa na imani. Huzuni ni kwamba katika hii njia Sara na Ibrahimu walidokeza kwamba Bwana alifanya makosa kuchelewa kutimiza ahadi yake ya kuwapa mtoto

> Sarai akamwambia Abramu, Basi sasa, **Bwana amenifunga tumbo nisizae**, umwingilie mjakazi wangu labda nitapata uzao kwa yeye. Abramu akaisikiliza sauti ya Sarai. Mwanzo 16:2

> Mungu akamwambia Ibrahimu, Sarai mkeo, hutamwita jina lake Sarai, kwa kuwa jina lake litakuwa Sara. (16) Nami nitambariki, na tena nitakupa mwana kwake, naam, nitambariki, naye atakuwa mama wa mataifa, na wafalme wa kabila za watu watatoka kwake. (17) **Ndipo Ibrahimu akaanguka kifudifudi akacheka, akasema moyoni, Je! Mtu wa umri wa miaka mia, kwake atazaliwa mtoto?** Naye Sara mwenye umri wa miaka tisini atazaa? (18) **Ibrahimu akamwambia Mungu, Lau kwamba Ishmaeli angeishi mbele yako.** Mwanzo 17:15-18

Hivi visa vyote vilikuwa vikionyesha ukubwa wa tatizo la Ibrahimu na Sarah. Kutokuwa na imani kwao kulikuwa kunadhihirika polepole. Paulo anafunua kwamba kuunganika kwa Ibrahimu na wanawake wawili, Sarai na Hagai, inadhihirisha vile ahadi mbili zinafanya kazi. Ibrahimu aliwaowa wanawake wawili. Hagai akazaa mtoto wa kwanza lakini hii ilimletea Ibrahimu uchungu mwingi mpaka alilazimishwa kumfukuza Hagari na mtoto wake. Huu uchungu unaonyesha mateso aliyoyapata Ibrahimu kwa kutokuwa na imani. Ibrahimu aliweza kusonga kabisa katika maarifa ya ahadi mpya. Ilikuwa na sehemu mbili ambayo zilikuwa na kupishana katikati kwa sababu kulikuwa na kipindi ambacho wana hawa wawili walikuwa wakiishi katika nyumba moja. Katika jaribio la kumtoa mtoto wake Izaka Ibrahimu aliweza mwishowe kupita katika ahadi mpya. Imani yake kwa Bwana haiku yumba yumba. Ukamilifu wa imani yake ilimletea uponyaji ambao Mungu alikusudia tangu mwanzo.

Ili Mungu afanye hii kazi ya uponyaji, Ilimbidi Bwana aache muda upite kudhihirisha kutokuwa na imani iliamponye. Mungu aliacha mambo yatendeke ambayo yaliyokuwa fikira zake za kitambo na kumfufua katika uhakika wa haki kwa imani.

Katika sura mbili za hapo awali tulizungumzia jambo la busara la kioo. Kioo ni chombo kinachotumiwa na daktari wa meno kutuonyesha shida iliyoko mdomoni mwetu. Daktari anatumia uyoka kama chombo cha kutuonyesha shida mahali ambapo hatuwezi ona na macho ya kawaida. Sheria ya Mungu inakuwa kama chombo hicho kutuoyesha ukubwa wa ugonjwa wetu wa dhambi. Kioo hiki ni chombo ambacho kinatuongoza kwa Kristo tukikubali kupimwa.

> Hivyo, sheria ilikuwa kiongozi kutufikisha kwa Kristo, ili tupate tuhesabiwa haki kwa imani. Wagalatia 3:24

Dhambi ndiyo shida ambayo inaanza ndani ya dhamira ya mwili. Ili kutatuwa shida hii Baba yetu lazima atufinulie makosa kwa kufikiria kwetu. Hii kazi ina fanywa kupitia sheria. Shida nikwamba kwa watu wengi huu ufunuo wa kutuonyesha vile tulivyo wabaya unawafanya kumrudishia Mungu huu ufunuo.

> Basi iweni watendaji wa Neno wala msiwe wasikiaji tu, huku mkijidanganya nafsi zenu. (**23)** Kwa maana kama mtu ni msikiaji tu wa Neno wala hatendi kile linachosema, yeye **ni kama mtu ajitazamaye uso wake kwenye kioo** (**24)** na baada ya kujiona

alivyo, huenda zake na mara husahau jinsi alivyo. (**25)** Lakini yeye anayeangalia kwa bidii katika sheria kamilifu, ile iletayo uhuru, naye akaendelea kufanya hivyo bila kusahau alichosikia, bali akalitenda, atabarikiwa katika kile anachofanya. Yakobo 1:22-25

Inamaanisha nini kuwa msikiaji waneno? Mfano bora wa hili linapatikana katika kisa cha wana Israeli walipofika mlima wa Sinai. Mungu aliwaahidi kuwatendaea mengi lakini hawakusikia kwa makini. Badala ya kuamini ahadi ya Mungu, Wanaisraeli walimwambia Mungu watafanya kile Mungu alichosema atawafanyia.

> **Mmeona jinsi nilivyowatendea Wamisri, na jinsi nilivyowachukua ninyi juu ya mbawa za tai, nikawaleta ninyi kwangu mimi.** (5) Sasa basi ikiwa mtaitii sauti yangu kweli kweli, na kulishika agano langu, hapo ndipo mtakapokuwa tunu kwangu kuliko makabila yote ya watu; maana dunia yote pia ni mali yangu, (6) **nanyi mtakuwa kwangu ufalme wa makuhani, na taifa takatifu.** Hayo ndiyo maneno utakayowaambia wana wa Israeli. (7) Musa akaenda akawaita wazee wa watu, akawafunulia maneno hayo yote, Bwana aliyokuwa amemwagiza. (8) **Watu wote wakaitika pamoja wakisema, Hayo yote aliyoyasema Bwana tutayatenda.** Naye Musa akamwambia Bwana maneno ya hao watu. Kutoka 19:4-8

Mungu alisema atawapatia neema ya kumtii kwa roho na kweli. Utiifu ilimaanisha kuamini kwamba Mungu atafanya wafalme na makuhani wake. Utiifu ulikuwa unastahili kuelewa si kufanya kitu lakini kumuamini Mungu kwamba anawafanyia kitu. Kwa huzuni, wanaisraeli wakapindua ahadi kuwa kitu ambacho wangeli mtendea Mungu iliwapate sifa. Huu mtindo ndiyo Bibilia inaita agano la kale. Hiki kisa kinaonekana wazi kwa unyonge wa mtu kumsikiza Mungu na kuamini kile anacho sema.

> Kwa maana kama hapakuwa na kasorokatika lile agano la kwanza, pasingekuwa na haja ya kutafuta nafasi kwa ajili ya jingine. (8) Lakini Mungu aliona kosa kwa watu naye akasema: "Siku zinakuja, asema Bwana, itakapofanya agano jipya na nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda. (9) **Agano hili halitakuwa kama lile nililofanya na baba zao nilipowashika mkono ili kuwatoa katika nchi ya Misri, kwa kuwa hawakuendelea kuwa waaminifu katika agano Langu**, nami nikawaacha,Asema Bwana. **(**10)Baada ya siku zile, hili ndilo agano nitakalofanya na nyumba ya

> Israeli, asema Bwana, 'Nitaweka sheria zangu katika nia zao na kuziandika katika mioyo yao. Nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu Wangu. Waebrania 8:7-10

Bwana alijuwa wanaisraeli hawatamsikiza kwa makini bali watajaribu kufanya hao wenyewe kile alichowaahidi. Hii ndiyo sehemu ya kazi ya mwalimu kwa kumleta mtu kwa Kristo.

> Hivyo, sheria ilikuwa kiongozi kutufikisha kwa Kristo, ili tupate tuhesabiwa haki kwa imani. (25)Lakini sasa kwa kuwa ile Imani imekuja, hatusimamiwi tena na sheria. Wagalatia 3:24-25

Mungu alijua wanaisraeli hawangeweza kutimiza ahadi yao kwake lakini aliwaacha wajaribu kufanya hivyo ili wakishindwa walikuwa bado wanauchaguzi wa kuachana na uwezo wao, na wamtumainiye Yeye ili awamalizie alichowa.

Kama ilivyoonyeshwa kwa kisa cha Ibrahimu na Sara, shida ambayo tunayo kama wanadamu ni kwamba wakati Mungu anatufunulia uovu wetu mioyo yetu inamsukumia shida zetu kwake. Sara alisema kwamba Mungu alimzuia kupata mtoto. Alishauri kuwa ilikuwa ni makosa ya Mungu ndio maana mambo yalimuendea mrama. Wakati Bwana alimuuliza Adamu kama alikula tunda la mti, Adamu alimsukumia Mungu lawama.

> Akasema, Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! Umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale? (12) **Adamu akasema, Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala.** Mwanzo 3:11-12

Hii shida ya kumtupia Mungu makosa ambayo tunayo inatudhuru vile tu na soma na kufasiri Bibilia. Bibilia inatuonya kuhusu hali yetu ya kimwili na inafunua fikara na makusudio ya mioyo yetu kwamba sisi ni wabinafsi, waongo, waharibifu na wauaji.

> **Kama ilivyoandikwa:"Hakuna mwenye haki, hakuna hata mmoja**.(11)**Hakuna hata mmoja mwenye ufahamu, hakuna hata mmoja amtafutaye Mungu**. (12) Wote wamegeukia mbali,wote kwa pamoja hawafai,hakuna atendaye mema, naam, hata mmoja." (13) "Makoo yao ni makaburi wazi, **kwa ndimi zao hufanya udanganyifu**."Sumu ya nyoka iko midomoni mwao. (14) "Vinywa vyao vimejaa laana na uchungu." (15) **"Miguu yao ina**

> **haraka kumwaga damu,** (16) **maangamizi na taabu viko katika njia zao, (17)wala njia ya amani hawaijui."** (18) "Hakuna hofu ya Mungu machoni pao." Warumi 3:10-18

Ukweli wa asili yetu umekuwa tofauti na maisha ya Yesu. Upendo na huruma alizowaonyesha maadui zake na uvumilivu katika huduma Yake ya kutunza watu inahukumu ubinafsi wetu. Badala ya kutubu, moyo wa mwanadamu inamrudishia Mungu hizi tabia ilikusadikisha ubinafsi wetu. Kama ilivyonikuliwa katika Yakobo, mtu wa asili anasoma neno la Mungu na anaona asili ya uso wake.

> Kwa maana kama mtu ni msikiaji tu wa Neno wala hatendi kile linachosema, yeye ni **kama mtu ajitazamaye uso wake kwenye kioo** Yakobo 1:23

Bwana anafanya kama tabibu au daktari wa meno wakati anapotuonyesha ukubwa wa shida yetu, lakini hii haitoshi, kwa sababu hatuamini kwamba hii shida inaweza leta mauti, lakini tukiamini tunafikiri kwamba kuna njia nyengine nzuri kuliko anayotupatia, dawa ya kutoa maumivu katika kipindi cha maisha yetu kwa mfano ya tosha. Walakini hakuna kutambua ya kwamba dhambi haileti amani kwa kuwa "hakuna amani, asema Bwana kwa wabaya," si kwa mwili na si kwa aliyepagawa na pepo chafu, na Mungu lazima atuache tushuudie matokeo ya kuumwa kwa uovu wa matendo yetu ili sote tufahamu yakuwa – kwamba "kinachofanywa pasipo imani ni dhambi." Isaya 48:22, Warumi 14:23.

Kwa huzuni Yeye kwa mara nyingi humtazama mwanadamu akipitia mienendo ya agano la kale la wokovu kwa njia zake mwenyewe, anatusihi sisi tutambue ya kwamba tunaweza kusuluhisha hiyo shida kwa kumruhusu Kristo afanye kazi mioyoni mwetu. Lakini, bado tunakataa kukubali hayo matokeo ya uchungu ni kazi ya matendo ya mienendo asili ya miili yetu, ambayo yangelikuwa mabaya zaidi kama hayangelivurugwa kidogo na ulinzi wa utulivu wa Baba yetu mwenye upendo ambaye lengo lake ni kufanya hii adhabu iwekwa maanufa yetu. Walakini tunajaribiwa kumlaumu na kumshtaki kwamba anatabia ya ukatili katika mtazamo wetu wa ufisadi, kutudhulumu na kuacha uchungu utuangukie.Watu wamevumbua njia nyingi za ujanja zaidi za kumrudishia Mungu mienendo ya mibaya. Kama vile maandiko yanavyo sema:

> **Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote,** una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua? Yeremia 17:9

> Ndivyo ulivyofanya, nami nikanyamaza; **Ukadhani ya kuwa Mimi ni kama wewe**. Walakini nitakukemea; Nitayapanga hayo mbele ya macho yako. Zaburi 50:21

Kwa huzuni, tangu kuanguka kwa mwanadamu, asili ya mioyo yetu ni udanganyifu na mauwaji. Mwanadamu wa asili akisoma Bibilia anamrudishia Mungu huu uovu. Mungu akionekana kama ni mkatili na mdhalimu kwa msomaji, hii inafunua kabisa na kufanya mbegu zilizoko moyoni mwa msomaji kunawiri. Kama vile Paulo anavyo elezea:

> Lakini dhambi kwa kupata nafasi katika amri, hii ikazaa ndani yangu kila aina ya tamaa. Kwa maana pasipo sheria, dhambi imekufa. (9)Wakati fulani nilikuwa hai pasipo sheria, lakini amri ilipokuja, dhambi ikawa hai, nami nikafa. (10) Nikaona kwamba ile amri iliyokusudiwa kuleta uzima, ilileta mauti. (11) Kwa maana dhambi kwa kupata nafasi katika amri, ilinidanganya na kwa kupitia hiyo amri, ikaniua. (12) Hivyo basi, sheria yenyewe ni takatifu na amri ni takatifu na ya haki, tena ni njema. (13) Je, kile kilicho chema basi kilikuwa mauti kwangu? La, hasha! Lakini ili dhambi itambuliwe kuwa ni dhambi, ilileta mauti ndani yangu kupitia kile kilichokuwa chema, ili kwa njia ya amri dhambi izidi kuwa mbaya kupita kiasi. Warumi 7:8-13

Watu wanatumia hadithi za Agano la kale ambazo zaonekana kana kwamba za sema Mungu anawangamiza na kuuwa watu ilikudhibitisha asili yao ya mauwaji. Bibilia imeandikwa kwa makini kuwa huruhusu kufunua kilicho mioyoni mwao. Maisha ya Yesu duniani yanatuonyesha kwa uhakika vile Mungu alivyo. Yesu hakumuuwa yoyote, lakini badala ya kuangalia kioo cha upendo kamili wa Mungu, watu wamechagua kusoma agano la kale kama wasikiaji wa neno na wanaona nyuso zao kwa kile wanacho fikiria ni uso wa Mungu.

> Nasi sote, **tukiwa na nyuso zisizotiwa utaji tunaakisi utukufu wa Bwana, kama kwenye kioo**. Nasi tunabadilishwa ili tufanane naye, toka utukufu hadi utukufu mkuu zaidi, utokao kwa Bwana, ambaye ndiye Roho. 2 Wakorintho 3:18

Utukufu wa Bwana ni tabia kamili ya Baba ikifunuliwa katika maisha ya Yesu duniani.

> **Nimekutukuza Wewe duniani** kwa kuitimiza ile kazi uliyonipa niifanye. Yohana 17:4

Utukufu wa Mungu ni tabia yake vile anavyo tuambia sisi.

> Akasema, **Nakusihi unionyeshe utukufu wako**…(34:5)Bwana akashuka ndani ya lile wingu, akasimama pamoja naye huko, akalitangaza jina la Bwana. (6) **Bwana akapita mbele yake, akatangaza, Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli** Kutoka 33:18; 34:5-6

Ukisoma Bibilia kupitia kwa kioo cha utukufu, au tabia, ya Yesu unaona kitu tofauti kabisa katika Agano la Kale kuliko ukisoma katika kioo cha moyo wako wa asili. Je inawezekanaje kuona utukufu wa Kristo Bwana katika kioo?Yafaa tujione kwa kioo au si vyo? Je tunamuona Kristo vipi?

> Kwao, Mungu amechagua kujulisha miongoni mwa watu Mataifa utukufu wa utajiri wa siri hii, ambayo ni **Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu**. Wakolosai 1:27

Tukija kwa Agano Jipya, tunazaliwa upya na Kristo anaanza kufunuliwa mioyoni mwetu. Hii inaanza kubadilisha kile tunachoona kwa kiooTukimuona Kristo kwa kioo njia yetu yote ya kusoma Bibilia inabadilika. Vile tulivyosema katika ukurasa wa 18 kuhusu maneno ya wazi, tunaanza kunaona mara moja ukinzani unaoneka na juu juu ni vigumu kusuluhisha. Hii ni sababu ya kuhama kutoka kwa Agano la Kale kwenda kwa Agano Jipya. Macho yetu yanabadilika kwa njia tunavyosoma.

> Yesu akamshika mkono huyo kipofu akampeleka nje ya kijiji. Baada ya kuyatemea mate macho ya yule kipofu na kumwekea mikono, Yesu akamwuliza, "Unaona cho chote?" (24) Yule kipofu akaangalia, akasema, "Ninaona watu, wanaonekana kama miti inayotembea." (25) Yesu akamwekea tena mikono machoni. Kisha macho yake yakafunguka, kuona kwake kukarejea kuona kila kitu kwa udhahiri. (26) Yesu akamwaga aende nyumbani kwake, akimwambia, "Hata kijijini usiingie. " Mariko 8:23-25

Kwanza tunaona watu kama miti inayotembea, lakini Bwana akiweka mikono yake machoni kwetu tunaanza kuoana vitu vile Yeye anavyoviona na picha nzuri namna gani inayofunuliwa!

La muhimu kwa haya yote ni Ahadi ya kale ni muhimu kutusaidia kutafuta tiba ya kweli kwa Kristo. Ahadi ya kale kupitia sheria. Inatuonyesha vile sisi ni ilituweze kumkimbilia Kristo na atuponye katika Ahadi mpya. Hizi njia mbili huwa ziko pamoja na zinatendeka kwa maisha ya kila mtu ambaye anamjia Bwana. Njia hiyo hiyo leo kama wakati wa Adamu, Nuhu, Ibrahimu na Musa.

Kujaribu kutenganisha hizi njia mbili inaonyesha Mungu katika Agano la Kale kama anavunja mifupa na kutoboa meno bila dawa yoyote. Hii inamfanya Mungu kuwa mkali na mkatili. Ambayo ni mbaya zaidi ni injili ambayo watu hufunza leo ambayo inasema amini Yesu tu na usijali kuhusu mifupa yako iliyokombo na meno yanayooza. Hii injili ingempata Yesu anayejaza mashimo bila kusafisha nje sehemu zilizooza. Kutenganisha hizi njia mbili katika maisha ya mtu inamfanya Mungu kuonekana mkali katika Agano la Kale na mpole na mwenye mapatano katika Agano Jipya.

Waliojeruhiwa sana kwa kutofahamu hizi njia mbili vizuri ni wakati Mungu anaruhusu mambo yatendeke yanayofunua dhambi kwa wale anowataka kuwaokowa, kudhihirishwa kwa dhambi inaelekezewa Mungu vile Yeye anavyotaka.

> Zaidi ya hayo, **sheria ilikuja, ili uvunjaji wa sheria uongezeke**. Lakini dhambi ilipoongezeka,neema iliongezeka zaidi. Warumi 5:20

Wakati sheria inapoingia mioyoni mwetu na fikira zetu zinafanya dhambi kuongezeka kwa watu na kuonekana sana.Watu wanaalikwa kumgeukia Kristo na kupokea uponyaji.

> Naye atakapokuja, atauthibitishia ulimwengu kuhusu dhambi, haki na hukumu. Yohana 16:8

Mdhambi akitiwa hatiani ya dhambi basi anawezeshwa kwa imani kupokea haki Yake - haki ya Kristo inayomtayarisha mwenye dhambi kwa hukumu ya milele. Tumefikia sasa sehemu muhimu kufahamu katika hii njia. Mtu akiwa katika hali yake mawazo ya asili, ya onyesho la Mungu kwake linanena kwa kile kilicho moyoni mwa mtu. Mungu anatafuta kufunua mawazo na

makusudi ya moyo wa mwanadamu. Mungu kwa upendo anatamani kufichua vile vitu ambavyo mtu mwenyewe hajui vimo ndani yake.

> Basi sasa, umelaaniwa wewe katika ardhi, iliyofumbua kinywa chake ipokee damu ya ndugu yako kwa mkono wako; (12) utakapoilima ardhi haitakupa mazao yake; utakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani. Mwanzo 4:11-12

Katika mafungu haya  Mungu anamfunulia Kaini kilicho ndani yake.Kaini ameleta laana kwa dunia kupitia dhambi zake. Mauaji aliyo ya tenda ye meharibu utu wake bora na yakamuacha mtu aliyepondeka. Haya mambo haya janenwa kumharibu Kaini bali Kaini aone hali yake iliamrudie Mungu na kuomba kupokea msamaha. Je kaini anaitika vipi?

> Kaini akamwambia Bwana, **Adhabu yangu imenikulia kubwa, haichukuliki. 14 Tazama, umenifukuza leo katika uso wa ardhi, nitasitirika mbali na uso wako, nami nitakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani**; hata itakuwa kila anionaye ataniua. Mwanzo 4:13-14

Mara nyingine Mungu anaamrisha kilicho moyoni mwa mtu ili hizo fikira zifunue kilicho moyoni mwa mtu.

Badala ya kukubali kupimwa kwa hali yake halisi, Kaini alichagua kumrudishia Mungu lawama. Kaini alikata kutubu kwa kumuuwa nduguye na kwa hivyo hangepata amani. Hatia ya kumuuwa ndugu yake haingemwacha usiku na mchana na kumkimbiza katika fikira zake na kumfanya kuwa mtoro. Mara nyingine Mungu anamrisha kilicho moyoni mwa mtu ili hizo fikira zifunue kilicho moyoni mwa mtu.

Wakati Israeli ilitakakudadisi nchi, Mungu alitoa amri waende na wafanye hivyo. Matokeo ni 10 kati ya 12 wapelelezi walirudi na habari isiyo na imani.

> **Nanyi mkanikaribia kila mmoja wenu, mkasema, Na tupeleke watu mbele yetu, ili watupelelezee nchi** na kutuletea habari za njia itupasayo kuipandia, na za miji tutakayoifikia. (23) Neno hili likanipendeza sana; nikatwaa watu kumi na wawili, mtu mmoja wa kila kabila. Kumbukumbu La Torati 1:22-23

> Kisha Bwana akanena na Musa, akamwambia,(2) Tuma watu, ili waende wakaipeleleze nchi ya Kanaani, niwapayo wana wa Israeli; katika kabila ya baba zao mtamtuma mtu mmoja, kila mtu na awe mkuu kati yao. Hesabu 13:1-2

Sababu za kuwafanya watu wapeleleze ni kukosa imani kwa neno la Mungu. Mungu alitaka waone kukosa imani kwao kwa hivyo aliwarudishia mawazo yao na akatoa amri ambayo tayari waliokuwa nayo mioyoni mwao: kupeleleza nchi ilikujitayarisha kuchukua nchi kwa nguvu za mkono wao.

Tunarudia hapa kwamba Mungu anafanya na watu katika Agano la Kale au hali yao ya asili, amri anazozitoa ambazo zinapingana na maisha ya Yesu duniani inatoa sababu za kioo cha uungu kikifanya kazi. Hizo ni fikira za wanadamu ilikufanya dhambi iongezeke. Hizo si mawazo au mapenzi ya Mungu. Hii ndio sehemu ambayo wasomaji wa Bibilia wanachanganyikiwa na hatimaye kudanganywa.

Katika Agano la kale au hali ya ki asili, amri silizotolewa zinapingana na maisha ya Yesu duniani ambayo inatupatia sababu ya kuona kioo cha uungu kikifanya kazi.

Chukua kisa cha Balaamu. Mungu anamwambia Balaamu asiende kuwalaani Israeli. Mwanzo Balaamu anamtii Mungu na wakati watu wa Balaki wanarudi kumahidi heshima kubwa, anaanza kuyumbayumba na anawambia watu wangoje.

> Balaamu akaondoka asubuhi, akatandika punda wake, akaenda pamoja na wakuu wa Moabu. (22) Hasira ya Mungu ikawaka kwa sababu alikwenda; malaika wa Bwana akajiweka njiani, ili kumpinga. Basi alikuwa amepanda punda wake, na watumishi wake wawili walikuwa pamoja naye. Hesabu 22:20-21

Amri hii ilikuwa ni kurudishwa kwa tama ya Baalamu kwenda. Mungu alimjibu  na kumrudishia tama zake iliajione mwenyewe. Kama hauelewi njia ya Agano, mafungu yafuatayo hayatakuwa na maana kwako kabisa.

> Hasira ya Mungu ikawaka kwa sababu alikwenda; malaika wa Bwana akajiweka njiani, ili kumpinga. Basi alikuwa amepanda punda wake, na watumishi wake wawili walikuwa pamoja naye. Hesabu 22:22

Tunakumbuka neno la kiebrania *Hasira* inaweza kutafsiriwa kama *huzuni.* Mungu alihuzunishwa kwamba Balaamu alichagua kwenda na watu na akamtuma malaika wake kumkanya. Balaamu anaonekana anaelewa arudi nyumbani lakini neno moja linasaliti kilicho moyoni mwake – kama.

> Balaamu akamwambia malaika wa Bwana, Nimefanya dhambi; maana sikujua ya kuwa wewe umesimama njiani ili kunipinga; basi sasa, ikiwa umechukizwa, nitarudi tena. Hesabu 22:34

Balaamu alijua kwamba hii haikuwa mapenzi ya Mungu. Mkasa wote wa punda na malaika kilionyesha wazi kwamba alichokuwa akitenda ni makosa. Tena alikubali dhambi zake , lakini alisema, "KAMA unataka nirudi nyuma basi nitarudi" Mungu lazima anene naye kwa kioo.

> Malaika wa Bwana akamwambia Balaamu Enenda pamoja na watu hawa, lakini neno lile nitakalokuambia, ndilo utakalosema. Basi Balaamu akaenda pamoja na wakuu wa Balaki. Hesabu 22:35

Amri za Mungu kwa Baalamu kwenda ni marudio ya fikira zake kwa sababu Baalamu yuko katika Agano la kale. Mungu akiona wanadamu wanatia bidii kufuata njia nyingine, Hangependa kuwazuia kufanya kinyuna mapenzi yao.

> lakini hawakusikiliza, wala hawakutega masikio yao, bali walifanya shingo zao kuwa ngumu, ili wasisikilize wala wasipokee mafundisho.Yeremia 17:23.

Anawapatia uhuru wakufanya vile wanavyotaka. Hii inaruhusu mbegu ya dhambi kuwa ili dhambi iongezeke. Dhambi ikiongezeka fursa inakuja pia ya kutubu na kuchagua njia nzuri ili neema iongezeke zaidi.

Hebu tafakari tena mfano wa Israeli kuomba mfalme. Mungu aliwaonya kuhusu hili lakini walikuwa vinchwa ngumu. Kwa hivyo Mungu akawapa mfalme kulingana na tamaa zao. Ilikuwa si mapenzi ya Mungu kufanya hivi lakini katika kioo cha mapenzi yao aliwaruhusu kufanya kuwa na mfalme wakidunia.

Wakati wa Musa, Mungu alimwambia Israeli kwamba wakanani watafukuzwa pamoja na mavu.Hakukuwa na kutajwa kuuwawa au kuharibiwa. Lakini Israeli walifunua tamaa yao ya mauaji katika hesabu 21.

> Na Mkanaani, mfalme wa Aradi, aliyeketi upande wa Negebu, alisikia habari ya kuwa Israeli alikuja kwa njia ya Atharimu; basi akapigana na Israeli, na watu kadha wa kadha miongoni mwao akawateka mateka. (2) **Basi Israeli akaweka nadhiri kwa Bwana akasema, Kama wewe utawatia watu hawa mikononi mwangu kweli ndipo mimi nitaiharibu miji yao kabisa.**(3) Bwana akasikiza sauti ya Israeli, akawatia Wakanaani mikononi mwao; nao wakawaharibu wao na miji yao kabisa; na jina la mahali hapo likaitwa Horma. Hesabu 21:1-3

Mungu alirushusu tama za kuuwa mataifa megine, kwa hivyo Mungu katika siku za usoni

Bwana angeli warudishia tamaa zao za mauaji kila siku kwa amri katika kioo ya kuwachinja maadui zao na haya yalifurahisha masikio yao.

> Maana wakati utakuja watu watakapokataa kuyakubali mafundisho yenye uzima, badala yake, ili kutimiza tamaa zaowenyewe watajikusanyia idadi kubwa ya walimu wapate kuwaambia yale ambayo masikio yao yanayowasha yanatamani kuyasikia. 2 Timotheo 4:3

Kama hauelewi njia hizi mbili za agano utamwekelea tabia za mwanadamu kufunuliwa dhambi kama tabia ya Mungu mwenyewe!

Kama hauelewi njia hizi mbili za agano utamwekele tabia za mwanadamu kufunuliwa dhambi kama tabia ya  Mungu mwenyewe! Hii ndio imekuwa kasoro kubwa kwa wanadamu katika kusoma maandikokarne baada ya karne; kasoro ya kufichua tabia ya asili ya mwanadamu kumrudishia roho ya mauaji ya kulipiza kisasi kwa uso wa upendo wa Mungu.

Mtu yoyote ambaye anamkiri Kristo kama mwokozi wake lazima akubali kwamba wanahatia ya kifo cha Mwana wa Mungu. Huu ukweli unafunua wanadamu kwa kiasili wanamchukia Mungu na Mwana wake.

Ili kusadikisha hii roho ya chuki watu wanamrushia Mungu hii tabia ya kikatili, na kumtangaza kwamba Yeye ndiye muaji mkuu wa wanadamu, kuidhinisha roho ya mauaji waliyonayo kwa wale wangelichagua kuwadhihaki, na kwa siri au wazi wanakiri  tamaa ya kuona maadui yao wanateswa na kuuwawa kwa

moto wa jehanamu. Wakati huu, wito wa kumcha Mungu na kumtukuza unaanza. Katika kuelewa vizuri tabia ya Mungu tunatolewa kwa uwoga wa Baba anayelipiza kisasi, hadi kwa upendo ulio juu unaotowa heshima ya ndani  na toba kabisa ya kushtaki Mungu kwa uongo.

> Katika upendo hakuna hofu. Lakini upendo ulio kamili huitupa nje hofu, kwa sababu hofu inahusika na adhabu. Kila mwenye hofu hakukamilika katika upendo. 1 Yohana 4:18

Mwangaza unaanza kuinuka na utukufu wa Bwana unadhihirishwa. Wakati unaanza kuelewa kweli njia za ahadi katika mpango wa wokovu, mawingu ya giza yaliyotupwa na kupaka tabia ya Mungu ya tatawanyishwa katika mwangaza wa utukufu wa wokovu.

Kwa haya mambo ya busara tulioweka msingi, sasa tuna vifaa vya kuchunguza hadithi za kikatili katika Bibilia na kuona uvumilivu, hekima haki, neema na upendo wa Mungu.

## 22. Musa Mtu Mnyenyekevu Sana

> (Basi huyo mtu, huyo Musa, alikuwa mpole sana zaidi ya wanadamu wote waliokuwa juu ya uso wa nchi.) Hesabu 12:3

Alilelewa katika wakati wa ukaidi, utumwa, kafara ya binadamu, na vita, fungu hili limesimama kama mnara wa mwanga katika dunia ya giza. Musa alikuwa mtu mnyenyekevu sana na mpole. Alifunua upendo wa Kristo bila ubinafsi kwa njia ambayo watu wachache wameweza waliomtangulia au waliokuja nyuma yake.

Alipoangalia uovu wa watu aliyoitwa awaongoze kutoka Misri, na baada ya kustahimili mashtaka yao kwake pamoja na nia ya kutaka kumuuwa, walakini Musa bado aliwaombea. Ijapokuwa wasomaji wengi wangefikiria ya kwamba wangeliachwa waangamie – lakini Musa aliomba, "unifute, nakusihi, katika kitabu chako ulichoandika.."

> Musa akarejea kwa Bwana akasema, Aa! Watu hawa wametenda dhambi kuu wamejifanyia miungu ya dhahabu.(32)Walakini sasa, ikiwa utawasamehe dhambi yao -- na kama sivyo, unifute, nakusihi, katika kitabu chako ulichoandika. Kutoka 32:31-32

Ni rahisi kusoma aya hii na kusonga mbele haraka – lakini kutoa uhai wako kwa wale wasiokujali, au wanaokuchukia na pia wanajaribu kukuuwa? Viumbe vilivyoumbwa ambavyo vimenakiliwa kwamba nyuso zao zinang'aa

na utukufu wa Mungu ni malaika. Huyu mtu alikuwa jangwani miaka arubaini akichunga kondoo, akiwabeba wana kondoo mikononi mwake akiwaongoza kwa upole na kuwakinga kwa hatari.

Katika Sinai aliishi siku arubaini pekee katika uwepo wa Mungu akiwasiliana na Mwokozi wa wanadamu mwenye upendo, rehema na mpole. Musa alielewa mpango wa wokovu; aliomba kwa kweli kuona utukufu wa Mungu na kwake Mungu alimfunulia tabia yake: mwenye huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; Musa alivumilia sana uongo na matusi aliyoelekezewa. Aliomba mbele za Mungu kwa ajili ya maisha ya watu waliotaka cheo chake. Ndiyo maana kwamba Baba yetu alitaka sana kumfufua Musa kutoka kaburini na kumpeleka mbinguni iliwaendelee na huo ushirika mtamu, na pia kuwa nay eye kusaidia huduma ya Yesu kwa kazi ya wokovu.

Kwa haya yaliyosemwa, ukiongezea maneno ya busara katika ukurasa wa hapo awali, tunaelekea katika hadithi kali sana zilizohusiana na maisha ya Musa.

> ndipo Musa akasimama katika mlango wa marago, akasema, Mtu awaye yote aliye upande wa Bwana, na aje kwangu. Wana wa Lawi wote wakamkusanyikia (27) Akawaambia, Bwana, Mungu wa Israeli, asema hivi, Kila mtu na ajifunge upanga wake pajani mwake, akapite huko na huko toka mlango hata mlango kati ya marago, mkamchinje kila mtu ndugu yake, na kila mtu mwenziwe na kila mtu jirani yake.(28) **Na hao wana wa Lawi wakafanya kama vile alivyosema Musa, wakaanguka siku ile kama watu elfu tatu.** Kutoka 32:26-28

Katika fungu la nne baada ya haya Musa anakubali kutoa uhai wake wa milele kama dhambi za Israeli hazitasamehewa. Musa alijuwa upendo mkuu na rehema za Mungu, na pia katika fikira zake alijuwa dhambi inayohuzunisha ilifanywa na ilitendwa kwa madharau na uovu mbele zake Mungu. Je huu uovu ulikuwa nini? Ilikuwa ibaada ya ndama ya dhahabu, mmoja wa miungu ya Misri .

> Bwana akamwambia Musa, Haya! Shuka; kwa maana watu wako uliowatoa katika nchi ya Misri wamejiharibu nafsi zao,(8)wamepotoka upesi kuiacha ile njia niliyowaamuru, wamejifanyizia ndama ya kuyeyusha wakaiabudu na kuitolea

> dhabihu, wakasema, Hiyo ndiyo miungu yako, Ee Israeli, iliyokutoa katika nchi ya Misri. Kutoka 32:7-8

Ilikuwa ni siku arubaini hapo mbeleni ambapo Israeli yote iliahidi kumuabudu Mungu wa kweli wakiahidi kuwaaminifu Kwake. Katika kipindi cha wiki ambazo ni chini ya sita walikuwa wakicheza, kunywa, na kujihusisha na uasherati na kafara za karamu kwa miungu ya bure ya Misri.

Tunahitaji kutoka nje ya hadithi ilitupate mtazamo mpana wa mambo yalivyokuwa. Kabla ya mapigo Mungu aliwaahidi Waisraeli mambo saba ili kutimiza ahadi aliyoifanya na Ibrahimu, Izaka na Yakobo. Hizi ahadi zimenakiliwa katika Kutoka 6:6-8:

1. *Nami* nitawatoa ninyi mtoke chini ya mizigo ya Wamisri,na…
2. *Nami* nitawaokoa na utumwa wao,na…
3. *Nami* nitawakomboa kwa mkono ulionyoshwa, na kwa hukumu kubwa; na…
4. *Nami* nitawatwaeni kuwa watu wangu,
5. *Nami* nitakuwa Mungu kwenu; nanyi mtajua ya kuwa mimi ni YEHOVA, Mungu wenu, niwatoaye mtoke chini ya mizigo ya Wamisri, na…
6. *Nami* nitawaleta hata nchi ile ambayo naliinua mkono wangu, niwape Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo; na…
7. *Nami* nitawapa iwe urithi wenu; Mimi ni YEHOVA.

Huu ulikuwa mwaliko waje katika Agano la milele. Kile walichostahili kufanya ni kukubali na kuamini ahadi hizi. Je, walijibu vipi?

> Musa akawaambia wana wa Israeli maneno haya; lakini **hawakumsikiliza Musa kwa ajili ya uchungu wa moyo,** na kwa ajili ya utumwa mgumu**.** Kutoka 6:9

Walikataa kusikiza au kukubali ahadi. Kwa nini ukatae hii ahadi ya ajabu! Jibu liko katika maneno “kwa ajili ya uchungu wa moyo**,** na kwa ajili ya utumwa mgumu. ”Walimlaumu Mungu kwa hiyo hali ya ngumu na wakakata kumuamini. Lakini utumwa wao umesababishwa na wao wenyewe. Wengi wao waliacha kumuabudu Mungu wa kweli kama vile ilivyodhihirika katika ibada ya ndama wa dhahabu. Waliiacha sabato na ulinzi uliokuwa katika amri za Mungu. Hii ilikuwa makosa yao kabisa. Lakini badala ya kutubu dhambi zao na kwa shukrani kukubali ahadi, walichagua kumrudishia Mungu hatia

yao. Ni jinsi gani moyo wa mwanadamu ni uovu? Baada ya kuokolewa kwa miujiza katika karne hizo zote za utumwa, walisimama kwa madharau, wakikana kabisa kutubu na kukubali kuhusishwa kwao kwa hii mikasa.

Mungu kwa wingi Wake wa rehema na upendo alichagua kuwakomboa, ijapokuwa wengi wao walikataa kumsikia. Si mpaka waliposimama ng'ambo hiyo nyingine ya ufuo wa bahari ya Shamu, ndipo ilipowaingilia katika fikira zao zilizojawa na mawingu kwamba wako uhuru. Utumwa wa kimaumbile ulikuwa umechukuliwa, lakini pingu za fikira bado ziliwakaza kweli kweli. Manung'uniko na malalamiko yalianza.

> **Na mkutano mzima wa wana wa Israeli ukawanung'unikia Musa na Haruni, huko barani;**(3) wana wa Israeli wakawaambia, Laiti tungalikufa kwa mkono wa Bwana katika nchi ya Misri, hapo tulipoketi karibu na zile sufuria za nyama, tulipokula vyakula hata kushiba; kwani mmetutoa huko na kututia katika bara hii, ili kutuua kwa njaa kusanyiko hili lote. Kutoka 16:2-3

Ni muhimu kutambua hapa kwamba umati wote ulimnung'unikia Musa na Haruni. Wote kuanzia wa kwanza hadi wa mwisho walilalamika kuhusu maamuzi ambayo Musa na Haruni walikuwa wakifanya ijapokuwa waliona wingu mchana na nguzo ya moto usiku kama sababu ya hakika ya uongozi wa Mungu.

Hii roho ya kushtaki ya manung'uniko ni roho ya Shetani. Yeye ndiye mshtaki wa ndugu na hiyo roho iliwatawala umati wote katika safari barani. Hii roho ya kushtaki ya manung'uniko ni roho ya Shetani. Yeye ndiye mshtaki wa ndugu mbiguni na hii roho iliwaongoza umati wote katika safari yao barani. Tunakumbuka hakuna mwana Israeli ambaye alikubali hizo ahadi saba za Mungu lakini walichagua kumlaumu kwa mambo yao. Haya majaribu madogo yalitumiwa na Mungu kuwaruhusu Israeli kufanyisha imani yao mazoezi, lakini walionyesha hisia kamili za mioyo yao ilikuonyesha kutokuwa na shukrani na asante. Hakuna mwiisraeli aliyekuwa katika agano la milele na hakuna aliyejazwa na Roho ya Kristo. Hii inaonekana wazi katika sura inayofuta

> Mkutano wote wa wana wa Israeli ukasafiri, kutoka bara ya Sini kwa safari zao, kama Bwana alivyowaagiza, wakatua Refidimu; napo hapakuwa na maji, watu wanywe. (2) **Kwa hiyo hao watu wakateta na Musa,** wakasema, Tupe maji tunywe. Musa

akawaambia, Kwani kuteta na mimi? Mbona mnamjaribu Bwana? (3) Watu wakawa na kiu huko; nao **wakamnung'unikia Musa, wakasema, Mbona umetupandisha kutoka Misri, kutuua sisi na watoto wetu na wanyama wetu kwa kiu? (4) Musa akamlilia Bwana, akisema, Niwatendee nini watu hawa? Bado kidogo nao watanipiga kwa mawe**. Kutoka 17:1-4

Badala ya kumshukuru Musa kwa kumruhusu Mungu amtumie kwa kuwaongoza kutoka Misri, watu wakamshtaki kwamba alikuwa antaka kuwa uwa na pia wengine wakafikiria kumpiga mawe wa muuwe.

Hakuna sababu ambayo inayoshauri kwamba wanaisraeli walitubu dhambi zao mashtaka ya uongo au kuabudu sanamu ya kuchonga Misri. Hawakujazwa na Roho wa Mungu, lakini walijazwa na roho wa mashtaka, roho wa kutafuta anasa na starehe. Ni kwa hali hii ya fikira wana Israeli walimuahidi Mungu kumtii. Walijuwa ya kwamba Musa hakufanya hiyo miujiza yote kwa nguvu zake mwenyewe. Mashtaka ya kwa Musa yalikuwa yale ya kwanza ambayo walimuelekezea Mungu yanayopatikana katika kutoka 6:9 – chukizwa na hali yao ya utumwa na wakamlaumu Mungu kwayo. Hii chuki ilikuwa ndani ya mioyo yao wakati walimuahidi Mungu kufanya kilakitu ambacho Mungu aliwaahidi.

Bwana alijuwa ya kuwa hawakujazwa na Roho Yake na hawangeweza kutimiza ahadi. Alimchukuwa Musa mlimani ili hizo mbegu za chuki zidhihirike. Walidhania ya kwamba alikufa huko juu na chuki yao ikawa hai katika kuabudu miungu ya Misri.

Walawi, walikuwa kabila moja na Musa, Hawakuhusishwa katika kuabudu ndama ya dhahabu. Bila kulainishwa na mvuto wa Roho wa Mungu katika mioyo yao, Walawi wangelifikiria walikuwa bora kuliko ndugu zao.Hukuna sababu yakuwa walawi walitakaswa kwa Mungu. Walimnung’unikia Musa kama vile inavyoelezewa katika Kutoka 16. Walimuahidi Mungu kumtii pamoja na wengine na kwa sababu hii walikuwa katika fikira za Agano la Kale. Hii ni muhimu sana kuelewa, kama ilivyoonyeshwa katika ukurasa wa hapo awali – watu wakiwa katika Agano la Kale, Mungu ananenanao katika lugha ya mawazo ya fikira zao ilikufanya dhambi ifichuke zaidi kwa mwenye dhambi.

Tunahitaji kutia kikomo hapa na kutafakari ilikusoma kwa makini vile hukumu ya Mungu inavyotimika. Imeandikwa moja kwa moja katika amri za Mungu. Ndiyo njia ambayo Mungu analeta hukumu kwa watu.

> Mungu akanena maneno haya yote akasema,(2) Mimi ni Bwana, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa. (3) Usiwe na miungu mingine ila mimi.(4) Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. (5) Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; **nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao**, (6) nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu. Kutoka 20:4-6

Wakati Musa alimuomba Mungu amfunulie utukufu Wake kwake Bwana anasema kitu hicho hicho lakini tofauti kidogo.

> Bwana akashuka ndani ya lile wingu, akasimama pamoja naye huko, akalitangaza jina la Bwana. (6) Bwana akapita mbele yake, akatangaza, Bwana, Bwana, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; (7) **mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe; mwenye kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao, na wana wa wana wao pia, hata kizazi cha tatu na cha nne.** Kutoka 34:5-7

Je inamaanisha nini kuwapatiliza watoto uovu wa baba zao wanaonichukia? Kwanza, tujuwe wazi kwamba inakuja kwa kizazi ambacho kinaendelea kumchukia Mungu. Kumchukia Mungu ni kukataa ulinzi wake. Kwa hivyo kuwapatiliza uovu ni matokeo ya dhambi inayomwangukia mdhambi. Bibilia inatuambia hivi mara nyingi.

> Bwana amejidhihirisha na kutekeleza hukumu; **Amemnasa mdhalimu kwa kazi ya mikono yake.** Zaburi 9:16

> Nami, jicho langu halitaachilia, wala sitaona huruma; **lakini nitaleta njia yao juu ya vichwa vyao**. Ezekieli 9:10

Tunajua ya kwamba Israeli walikuwa wamekubali kutumia upanga kusuluhisha mambo yao. Kabla Israeli kuja mlima Sinai waliweza kuwaangamiza Waameleki vilivyo.

> **Musa akamwambia Yoshua, Tuchagulie watu, ukatoke upigane na Waamaleki;** kesho nitasimama juu ya kilele kile, na ile fimbo ya Mungu nitakuwa nayo mkononi mwangu.(10) Basi Yoshua akafanya kama Musa alivyomwambia, akapigana na Amaleki; na Musa na Haruni na Huri wakapanda juu ya kile kilima.(11) Ikawa, Musa alipouinua mkono wake, Israeli walishinda; na alipoushusha mkono wake, Amaleki walishinda.(12)Lakini mikono ya Musa ilikuwa mizito; basi wakatwaa jiwe, wakaliweka chini yake akalikalia. Haruni na Huri wakaitegemeza mikono yake, mmoja upande huu na mmoja upande huu; mikono yake ikathibitika hata jua lilipokuchwa.(13) **Yoshua akawaangamiza Amaleki na watu wake kwa ukali wa upanga.** Kutoka 17:9-13

Kama Musa aliamua peke yake kupigana na Waameleki au aliruhusiwa na Mungu kurudisha fikira za Israeli hatujaambiwa. Tunajuwa haikuwa mapenzi ya Mungu wana wa Israeli wa muuwe yoyote wakati walikuwa wakiteka nchi ya Kanani.

> Nitatuma utisho wangu utangulie mbele yako, nami nitawafadhaisha watu wote utakaowafikilia, nami nitawafanya hao adui zako wote wakuonyeshe maungo yao. (28) Nami nitapeleka mavu mbele yako, watakaomfukuza Mhivi, na Mkanaani, na Mhiti, watoke mbele yako. Kutoka 23:27-28

Kama Israeli wangelikubali ahadi saba za Mungu katika hilo agano wangelijazwa na Roho Wake. Kama Roho wa Mungu akimjaza mtu, hili linafanyika.

> naliinua macho yangu, nikatazama, na kumbe, mtu aliyevikwa nguo za kitani, viuno vyake vimefungwa dhahabu safi ya Ufazi; (6) mwili wake pia ulikuwa kama zabarajadi safi, na uso wake mfano wa umeme, na macho yake kama taa za moto, na mikono yake na miguu yake rangi yake kama shaba iliyosuguliwa sana, na sauti ya maneno yake kama sauti ya umati wa watu. (7) Nami, Danielii, nikaona maono haya peke yangu; **maana wale watu waliokuwa pamoja nami hawakuyaona maono haya; lakini tetemeko kuu liliwashika, hata wakakimbia ili kujificha.** Danieli 10:5-7

Hii ndiyo asili ya msaada wa Roho ambao ungelisaidia. Hawangelihitaji kufanya lolote. Maadui wao wangeliungama dhambi zao na kutubu, au wangelitoroka.

Ni huzuni Israeli hawakuwa na hii Roho. Walijazwa na manung'uniko na malalamiko na ndiyo maana hawakuwa na uwezo wa kuwafanya maadui wao wawatorokee. Walikuwa na lipi lakufanya? Walifanya kile walicho juwa ni chema, walichukuwa upanga wakaanza kuwauwa watu. Hakuwezi kuwa na hisia nzuri ukikabiliana na mwanadamu karibu, hakuna mapumziko ukimuona akianguka chini na uso uliosononeka, akihema kwa shida akiwa amelalia damu, akilia kwa uchungu au akivuta pumzi yake ya mwisho polepole. Hauwezi kusahau kisa kama hicho. Mtu yoyote ambaye anayemuuwa mwenziwe hawezi kupata Roho ya amani ya Kristo. Anapata roho iliyodhohofika ya uhuni - utoro.

Huyo mtu ana mfano usiomtakatifu uliochapishwa katika akili zake; mfano wa kutisha wakufanya kifo kwa mkono wake,kuleta ajali na umwagaji wa damu, ambapo kifo hicho kina mwagika kudhuru kina baba, kina mama, ndugu,kina dada, waume,wake ,watoto,familia na jamaa.

Bibilia inatuambia ya kwamba Kristo ni mtakatifu, asiye na lawama na asiye na dosari. Asiye na lawama inamaanisha hadhuru.

> Kwa kuwa ilitupasa tuwe na Kuhani Mkuu wa namna hii, yaani, aliye mtakatifu, asiye na lawama, asiye na dosari, aliyetengwa na wenye dhambi na kuinuliwa juu ya mbingu. Waebrania 7:26

Si rahisi kwa Roho ya Kristo anayeishi ndani ya mtu kuua au kuangamiza maisha. Kristo ni ufufuo na uhai. Kifo hakiwezi kuwa Yeye akiwakaribu. Anafufua wafu, hauwi. Watu wanaweza kuua wakiwa na fikira za Agano la Kale katika kimwili.

Ili Mungu awaonyeshe wanadamu wako katika Agano la Kale, atawarudishia mawazo yao ilidhambi iongezeke, anawapa nia yao kwa kioo Kwa upande mwingine wakati mtu yuko katika Agano Jipya anaona kitu tofauti. Hii ndiyo Musa aliona katika ukurasa huu  wakati Mungu alipomjaribu.

> Tena Bwana akamwambia Musa, Mimi nimewaona watu hawa, na tazama, ni watu wenye shingo ngumu (10) basi sasa niache, ili hasira zangu ziwake juu yao, niwaangamize, nami nitakufanya wewe uwe

> taifa kuu.(11) **Musa akamsihi sana Bwana, Mungu wake, na kusema, Bwana, kwa nini hasira zako kuwaka juu ya watu wako uliowaleta kutoka nchi ya Misri kwa uweza mkuu, na kwa mkono wenye nguvu?** Kutoka. 32:9-11

Musa alijaribiwa kukata tama kuhusu Israeli. Shetani alimjaribu ili awafanye wapotee na Mungu akamchunguza Musa na akarudisha hayo mawazo kama amri.

Kwa Musa kulikuwa na mbegu mbili ambazo zilimenyana kutawala kama vile Isau na Yakobo tumboni mwa Rebeka. Kama vile Musa alivyokuwa na Roho mzuri wa Mungu mlimani na uso wake uling'aa

Alionyesha tabia nzuri na akamsihi Mungu awahifadhi Waisraeli ambao waliomtendea mabaya. Alishinda mbegu za kimwili na akawa mshindi. *Jaribio hilo pia likawajia Walawi. Walikuwa kimwili si kiroho*. Mawazo yao kuhusu wale walioiabudu ndama ya dhahabu na waliokataa kutubu ilikuwa ni wafe. Kwa hivyo *Mungu kwa kupitia Musa akawarudishia mawazo yao*. Mungu lazima atowe kwa Walawi hisia zao za mauwaji. Kama hizi hisia zingelibaki zimefichika, zingeleta uharibifu mkubwa zaidi. Walawi usiku huo wakilala katika hema zao, mawazo yao yangelijazwa mifano mibaya ya waume kwa wake waliowakata kata katika umwagaji wa damu. Hii ndiyo makusudio ya mioyo yao, Mungu akawapa. Pia kwa nia zao za dhambi Mungu akaleta hukumu kwa waliokata kutubu. Na walikuwa wakimruhusu Shetani kwa kambi kwa uasi wao uliofika juu.

Baba yetu wa mbinguni amejawa na hekima. Anafanya na wanadamu kwa njia mbili za Agano. Kwanza kuwafunulia watu uovu wao ili wamgeukie Kristo na waokolewe kwa haki yake, na pia kuacha uovu wa wenye dhambi kuwaangamiza katika hukumu.

Wakati Musa alipojaribiwa na Bwana kuhusu kusimama nyuma na kuacha Israeli iteketezwe tunaona Agano Jipya njia ya kusuluhisha matatizo. Wakati Walawi walipopata maagizo ya kuwauwa wakosaji,wangelifanya vile Musa alivyofanya. Kwanza *wangeliungama manung'uniko ya kwa Musa na ujinga wa wakutaka kufanya ahadi ambazo Mungu aliwaahidi. Pia wangeliungama chuki yao ya huko Misri kukata kukubali Agano Jipya.Hapo ndipo wangelijazwa na Roho wa Mungu na waovu na waasi wangelitorokea maisha yao na pia kuuwana katika juhudi zao za kutoroka*. Musa alipeana

mwanzo na mtindo wa kufanya mambo.Walawi wangetafakari jinsi Musa alivyo suluhisha hiyo hali. Badala ya kutubu maning'uniko yao walichagua kupumzika katika kazi yao nzuri ya kutoinamia ndama ya dhahabu.Waliamua kuwauwa wengine badala ya kuungama dhambi zao.

Katika lugha ya Agano la Kale, Bwana alituma ujumbe katika kambi yote kwamba kuabudu sanamu haikubaliki. Bwana alipeana ujumbe kwa njia inayofahamika. Vifo vya watu elfu tatu viliweka kikomo kwa mioyo ya waovu ,lakini *mwishowe haiku saidia hata mmoja wa wale Walawi ;hakuna mmoja ambaye aliyeingia katika nchi ya ahad*i. Wote walianguka barani na kufariki.

Kati ya wote waliotoka Misri,ni Kalebu na Yoshua walioingia nchi ya ahadi. Kama vile Bwana anavyosema – aliwapatiliza uovu wa baba kwa kizazi cha wale wanao mchukia. Walawi bado walikuwa na mbegu ya chuki kwa Bwana, lakini walikuwa hawajuwi. Hii imedhihirishwa na kutoingia nchi ya Kanani.

Kwa sababu ya mwanga uliong'a kutoka usoni mwa Musa na kukubali kwake kuwafia waliomchukia, katika maandiko, ninauhaki adilifu kwamba Musa alikuwa na ufahamu kuhusu Chimbuko la Kioo, na vilile Mungu alivyofanya naye hapo awali katika sura ya thalathini na mbili ya Kutoka ndivyo alivyoamrishwa afanye na Walawi katika sura iliyofuata. Jaribio hilo likawajia wote ambao magoti ya hayakuinamia ndama wa dhahabu.

Hili chimbuko la kioo linaweza kutumika kwa njia sawa katika hadithi zingine za maisha ya Musa.

> Basi Israeli akakaa Shitimu, kisha watu wakaanza kuzini pamoja na wanawake wa Moabu; (2) kwa kuwa waliwaalika hao watu waende sadakani, sadaka walizowachinjia miungu yao; watu wakala chakula, wakaisujudu hiyo miungu yao. (3) Ikawa Israeli kujiungamanisha na Baal-peori; hasira za Bwana zikawaka juu ya Israeli. (4) Kisha Bwana akamwambia Musa, Watwae wakuu wote wa hao watu, ukamtungikie Bwana watu hao mbele ya jua, ili kwamba hizo hasira kali za Bwana ziwaondokee Israeli. Kutoka 25:4-5

Hii ni lugha ya kioo. Haya matendo si tabia ya Kristo na kwa hivyo neno la Bwana linaonyesha mawazo ya watu ilikuwaleta tobani. Ufungo wa kusoma hizi hadithi ni kulinganisha na matendo ya Kristo duniani. Yesu alipenda maadui zake na hakumuuwa yoyote. Alitunza amri ya Baba Yake inayosema "Usiuwe." Kwa hivyo amri hizi zinatolewa kwa kioo cha fikira za wanadamu

kusuluhisha vile hali ilivyo. Iwapo Musa alielewa au hakuelewa haibadili chimbuko la kioo vile Mungu ananena na mkusanyiko wa watu katika Agano la Kale.

Kuna hadithi nyingine ambayo tunastahili kuiangazia katika maisha ya Musa ambayo ikotofauti kidogo, hiyo ni hadithi ya Kora, Dathani na Abiramu. Nimuhimu kwa sababu Kora alikuwa wa kabila la Lawi; Wale ambao hawakuinamia sanamu ya ndama ya dhahabu.

Hadithi yake inatufahamisha kile kilichokuwa ndani ya mioyo ya wale walichukuliwa kama watakatifu wakati wa kisanga cha ndama wa dhahabu.

> Basi Kora, mwana wa Ishari, mwana wa Kohathi, mwana wa Lawi, akatwaa watu, pamoja na Dathani na Abiramu, wana wa Eliabu, na Oni, mwana wa Pelethi, waliokuwa wana wa Reubeni; (2) nao, pamoja na watu kadha wa kadha wa wana wa Israeli, watu mia mbili na hamsini, Wakuu wa mkutano, waliokuwa wateule wa mkutano, watu wenye sifa, wakainuka mbele ya Musa; (3) **nao wakakusanyika kinyume cha Musa na Haruni, na kuwaambia, Ninyi inawatosha, kwa kuwa mkutano wote ni mtakatifu, kila mmoja miongoni mwao, Bwana naye yu kati yao; n'nini basi kujitukuza juu ya mkutano wa Bwana?** (4) Musa aliposikia maneno haya, akapomoka kifudifudi; (5) kisha akanena na Kora na mkutano wake wote, akawaambia, Asubuhi Bwana ataonyesha ni kina nani walio wake, kisha ni nani aliye mtakatifu, tena ni nani atakayemkaribisha kwake; maana, yeye atakayemchagua ndiye atakayemsongeza kwake.(6) Fanyeni neno hili; twaeni vyetezo, ninyi Kora na mkutano wake wote; (7) vitieni na moto, mkaweke na uvumba juu yake mbele za Bwana kesho; kisha itakuwa ya kwamba mtu Bwana atakayemchagua, yeye atakuwa mtakatifu; inawatosha ninyi, enyi wana wa Lawi. (8) Musa akamwambia Kora, Sikizeni basi, enyi Wana wa Lawi; (9) **Je! Mwaona kuwa ni jambo dogo kwenu, kuwa Mungu wa Israeli amewatenga ninyi na mkutano wa Israeli, ili apate kuwakaribisha kwake; ili mfanye utumishi wa maskani ya Bwana, na kusimama mbele ya mkutano ili kuwatumikia;** (10) **tena ya kuwa amekuleta uwe karibu, na ndugu zako wote wana wa Lawi pamoja nawe? Nanyi, je! Mwataka na ukuhani pia?** (11) Kwa sababu hii wewe na mkutano wako wote mmekusanyika kinyume cha Bwana; na Haruni, je! Yeye ni nani hata mkamnung'unikia? Kutoka 16:1-11

Kora alimshtaki Musa kuwa na roho ya utawala na alikusudia kujiweka kiongozi wa watu. Haya mashtaka ama kweli yanaelekeza nia ya Kora kwa Musa. Ilifunuwa hisia za moyo wake. Kora ikionyesha mkusanyiko ni mtakatifu na Bwana yuko pamoja nao. Kwa nini aseme hivi?

Lazima tutazame visa kabla ya haya. Wajasusi kumi na mbili walirudi kutoka Kanani, na kumi waliingia wakaleta habari mbaya ambayo Israeli iliamini. Ni Yoshua na Kalebu walionyesha imani kwamba Mungu angeliwapeleka katika nchi ya ahadi. Watu waliitika kwa kutaka kumpiga na mawe Kakebu na Yoshua mpaka wafe. Kwa hayo makelele,Musa naye anajaribiwa hivyo hivyo kama hapo awali – Bwana anamjaribu Musa kwa kutaka kumfanya taifa kuu badala ya Israeli. Watu walikuwa waovu hadi ikawa ni jaribu kubwa la kuwa na nia ya kutaka kuwabadilisha na kuwa maliza kabisa.

> Bwana akamwuliza Musa, Je! Watu hawa watanidharau hata lini? Wasiniamini hata lini? Nijapokuwa nimefanya ishara hizo zote kati yao.(12) Nitawapiga kwa tauni, na kuwaondolea urithi wao, nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, kisha yenye nguvu kuliko wao. Hesabu 14:11-12

Kwa mara nyingine tena Musa anaingilia kati na kuwa tetea watu akionyesha Roho ya Kristo kama vile Bwana anvyonuia.

> Basi Musa akamwambia Bwana, Ndipo Wamisri watasikia habari hiyo; kwa kuwa wewe uliwaleta watu hawa kwa uweza wako, kutoka kati yao;(14) kisha watawaambia wenyeji wa nchi hii; wamesikia wao ya kuwa wewe Bwana u kati ya watu hawa; maana, wewe Bwana waonekana uso kwa uso, na wingu lako lasimama juu yao, kisha wewe watangulia mbele yao, katika nguzo ya wingu mchana, na katika nguzo ya moto usiku.(15) Basi kama wewe ukiwaua watu hawa mfano wa mtu mmoja, ndipo mataifa yaliyosikia habari za sifa zako watakaponena na kusema,(16) Ni kwa sababu yeye Bwana hakuweza kuwaleta watu hao kuwatia katika nchi aliyowaapia, kwa ajili ya hayo amewaua nyikani. (17) Basi sasa nakusihi sana, uweza wa Bwana wangu na uwe mkuu, kama ulivyonena, uliposema,(18) Bwana ni mpole wa hasira, mwingi wa rehema, mwenye kusamehe uovu na makosa, naye hatamfanya mwenye hatia kuwa hana makosa kwa njia yo yote; mwenye kuwapatiliza wana kwa uovu wa baba zao, katika kizazi cha tatu na cha nne. (19) **Nakusihi, usamehe uovu wa watu hawa, kama ukuu wa rehema yako**

> **ulivyo, kama ulivyowasamehe watu hawa, tangu huko Misri hata hivi sasa.** Hesabu14:13-19

Bwana aliwasahamehe Waisraeli ambao aliwazuia kuathirika saa hiyo kwa sababu ya dhambi ya uasi. Bwana anawarudishia na kuwaonyesha watu uamuzi wao na kile walichokuwa wakisema kwamba Mungu anajaribu kuwauwa barani.

> Waambieni, Kama niishivyo, asema Bwana, **hakika yangu kama ninyi mlivyonena masikioni mwangu, ndivyo nitakavyowafanyia ninyi;** (29) mizoga yenu itaanguka katika jangwa hili, na wote waliohesabiwa miongoni mwenu, kama jumla ya hesabu yenu, tangu waliopata umri wa miaka ishirini na zaidi, hao walioninung'unikia, (30) hakika yangu hamtaingia ninyi katika nchi, ambayo niliinua mkono wangu ya kwamba nitawaketisha humo, isipokuwa Kalebu mwana wa Yefune, na Yoshua mwana wa Nuni. Hesabu 14:28-30

Ni lazima tukumbuke kwamba hii hukumu ya kifo haikukusudiwa kuwaangamiza, ilikuwa ni utumishi wa kifo kuwafanya waje tobani. Kama wangelikubali hukumu na kuungama uovu wao bado wangelipata uzima wa milele kama vile Musa alivyo. Musa hakuingia nchi ya Kanani lakini alipata uzima wa milele. Wana wa Israeli wangelifanya hivyo iwapo wangelitubu.

Israeli walikumbwa na uovu wao, Shetani aliwachochea Kora, Dathani, na Abiramu. Walipinga uongozi wa Musa na wakamlaumu kuhusu yote yaliyo watendekea tangu watoke Misri. Kwa kupitia Musa, Mungu aliwaambia watu walikuwa waovu na hakika wangeona kifo. Hii ilikusudiwa kuwaleta tobani lakini walichaguwa kumlaumu Musa kwa sababu ya kutofaulu kwa kulivyo tendeka.

> je! Ni jambo dogo, wewe kutuleta kutoka nchi iliyojawa na maziwa na asali, ili kutuua jangwani, lakini pamoja na haya wajikuza mwenyewe uwe mkuu juu yetu kabisa?14 Kisha, hukutuleta katika nchi iliyojawa na maziwa na asali, wala hukutupa urithi wa mashamba, na mashamba ya mizabibu; je! Unataka kuwatoboa macho watu hawa? Hatuji. (15) Musa akakasirika sana, akamwambia Bwana. Usiikubali sadaka yao; mimi sikutwaa hata punda mmoja kwao, wala sikumwumiza hata mtu mmoja miongoni mwao. Hesabu 16:13-15

Musa alishtakiwa kwa kujifanya mwana wa mfalme juu yao, alijaribu kuwauuwa hawa watu, na achukuwe mali yao. Neno la kiebrania kasirika linaweza kutafsiriwa huzuni. Musa aliwafanyia hawa watu vitu vingi mpaka akataka kutoa uzima wake wa milele kwa sababu yao. Walakini mkusanyiko wote ulikubali udanganyifu na mashtaka ya Kora, Dathani, na Abiramu badala ya kutubu uovu wao. Hii kweli ilimdhuru Musa. Alisukumwa hadi mwisho kwa hili jaribu. Kora alikusanya mkusanyiko wote dhidi ya Musa na mpaka Bwana akaingilia kati.

> **Kisha Kora akakutanisha mkutano wote kinyume chao** mlangoni pa hema ya kukutania; na utukufu wa Bwana ukatokea mbele ya mkutano wote. Hesabu 16:19

Mara nyingine tena Musa anajaribiwa kuwacha watu waangamia au awatetee.

> Kisha Bwana akanena na Musa na Haruni, na kuwaambia, (21) Jitengeni ninyi mkaondoke kati ya mkutano huu, ili nipate kuwaangamiza mara moja, (22) Nao wakapomoka kifudifudi, wakasema, Ee Mungu, Mungu wa roho za wenye mwili wote, je! Mtu mmoja atafanya dhambi, nawe utaukasirikia mkutano wote? Hesabu 16:20-22

Mara nyingine tena Musa anabaki mwaminifu na anawatetea watu. Hiyo Roho ya thamani inaishi ndani ya Musa; kwa hivyo Musa alikuwa mwaminifu kuwatetea watu.Musa kisha anazungumzia mtu mmoja- Kora. Jaribio la enda kwa undani sana. Bwana anamuamuru Musa.

> Bwana akasema na Musa, na kumwambia, (24) Nena na mkutano, na kuwaambia, Ondokeni ninyi hapo karibu na maskani ya Kora, na Dathani, na Abiramu. (25) Basi Musa akainuka na kuwaendea Dathani na Abiramu; na wazee wa Israeli wakaandamana naye. (26) Akasema na mkutano, na kuwaambia, Nawasihi, ondokeni penye hema za hawa watu waovu, wala msiguse kitu chao cho chote, msiangamizwe katika dhambi zao zote. Hesabu 16:23-26

Hawa watu wako karibu kutoka nje ya ulinzi wa Mungu. Wakati amri ilitolewa kusonga mbali na hema yao, wangelitubu lakini walisimama kwa madharau mpaka mwisho wakitawaliwa na roho ya Shetani. Shetani aliwatawala hawa watu na sasa ilikuwa apate njia ya kuwaangamiza kisha Mungu alaumiwe.

> Basi wakaondoka hapo karibu na maskani ya Kora, na Dathani na Abiramu, pande zote; nao kina Dathani na Abiramu wakatoka nje wakasimama mlangoni mwa hema zao, pamoja na wake zao, na wana wao na watoto wao wadogo. (28) Musa akasema, Kwa jambo hili mtajua ya kwamba Bwana amenituma, ili nifanye kazi hizi zote; kwa kuwa mimi sikuzifanya kwa akili zangu mwenyewe. (29) Kama watu hawa wakifa kifo cha sikuzote, kama watu wote wafavyo, au kama wakipatilizwa kwa mapatilizo ya watu wote; hapo basi Bwana hakunituma mimi. (**30) Lakini Bwana akiumba kitu kipya, na hiyo nchi ikifunua kinywa chake na kuwameza, pamoja na wote walio nao, nao washukia shimoni wali hai; ndipo mtatambua ya kwamba watu hawa wamemdharau Bwana 31 Basi ilikuwa, hapo alipokwisha kusema maneno haya yote, nchi iliyokuwa chini yao ikapasuka; 32 nchi ikafunua kinywa chake, na kuwameza, na watu wa nyumba zao na wote walioshikamana na Kora, na vyombo vyao vyote.**33 Basi wao, na wote waliokuwa nao, wakashukia shimoni wali hai; nayo nchi ikawafunika wakaangamia kutoka mle mkutanoni. Hesabu 16:27-33

Hawa wafitini waliuliza ni haki ya Musa kuwaongoza. Walimshtaki kwamba alitaka kujifanya mwana wa mfalme juu yao. Mkusanyiko wote ulimgeukia Musa kwa sababu ya Kazi ya Koran a wenzake. Hebu tuangalia kwa makini kile Musa alichosema.

> Musa akasema, Kwa jambo hili mtajua ya kwamba Bwana amenituma, ili nifanye kazi hizi zote; kwa kuwa mimi sikuzifanya kwa akili zangu mwenyewe. (29) **Kama** watu hawa wakifa kifo cha sikuzote, kama watu wote wafavyo, au kama wakipatilizwa kwa mapatilizo ya watu wote; hapo basi Bwana hakunituma mimi. (30) Lakini Bwana akiumba kitu kipya, na hiyo nchi ikifunua kinywa chake na kuwameza, pamoja na wote walio nao, nao washukia shimoni wali hai; ndipo mtatambua ya kwamba watu hawa wamemdharau Bwana. Hesabu 16:28-30

Watu waliona sababu nyingi kwamba Bwana alikuwaakimuongoza Musa kwa yale yote yaliyotendeka Misri, bahari ya shamu, na mlima Sinai.Kulikuwa na sababu nyingi Musa alitumwa na Bwana.Miujiza uliofanywa na Bwana kulingana vile Musa alifanya ukapokewa na tashwishi.

Wakati Yesu alijaribiwa na Shetani kuhusu sehemu yake kama Mwana wa Mungu, alikataa kufanya miujiza kukabiliana na majaribu yaliyo husisha "*kama wewe ni*..

> Mjaribu akamjia na kumwambia, "**Kama** Wewe ndiye Mwana wa Mungu, amuru mawe haya yawe mikate." (4) Lakini Yesu akajibu, "Imeandikwa, 'Mtu haishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Mathayo 4:3-4

Baada ya Musa kufanya hayo yote, kama Yesu, *wote wakamwacha, wakakimbia*.Mariko 14:50. Wakati Musa alikuwa akiumia katika mwili wake, Shetani alimuita ateremke katika huu msalaba. Alijaribiwa kuitisha muujiza kuhifadhi cheo chake.Yesu hakujibu swali lililokuwa na ***kama*** kamwe.Hakutumia muujiza kuonyesha Yeye ni nani.Aliamini kabisa kile Baba yake alimwambia.

Yohana mbatizaji alikuwa ni mkuu wa manabii wote, alipata hilo jaribu akiwa korokoroni. Vile vile chimbuko la ***kama*** laonekana katika swali Yohana aliuliza wanafunzi wake wachunguze kuhusu Yesu.

> Yohana Mbatizaji aliposikia akiwa gerezani mambo ambayo Kristo **a** alikuwa akiyafanya, aliwatuma wanafunzi wake (3) ili wakamwulize, "Wewe ndiye yule aliyekuwa aje, au tumngojee mwingine?" Mathayo 11:2-3

Hakukuwa na muujiza kwa Yohana vile hakukuwa kewa Musa.Alienda katika kifo chake akiamini hakika kwamba Kristo ndiya Masihi. Wanafunzi wa Yohana walirudi kutoka kwa mkutano na Yesu wakampa Yohana dhibitisho aliyokuwa akitamani.

Wakati alipomwambia Musa awaarifu watu wasimame nyuma kotoka kwa Kora, Dathani na Abiramu, je, Musa alipuuza majukumu ambayo hakupewa wakati aliangazia swala la *kama*? Mungu alivyo lazimishwa kutoa ulinzi wa malaika wake kutoka kwa hawa watu waasi, Shetani alimjaribu Musa na swala la kama kuonyesha vile alipanga kuwaangamiza hawa makafiri. Kumbuka Shetani alikuwa amechukuwa utawala kamili wa hawa watu. Aliwasukuma kwa nguvu kukataa Roho ya Kristo iliwatubu. Yesu anatengeneza bali Shetani anaharibu na kwa kupitia tashwishi alizoweka katika fikira za Musa, Shetani aliweza kufunika kazi yake ya maangamizi kana

kwamba yatoka moja kwa moja kama hukumu ya Mungu. Ni udanganyifu wa hali ya juu bila Kristo kukaa ndani anaweza kudanganya hata wateule.

Hii ilikuwa jaribio la kuumiza mno kwa Musa na ni funzo kwetu. Musa alistahimili uzito wa uongo dhidi yake kwa mdaa mrefu sana na akawa anawatetea kila mara.Ilivyo kuja kwa huyu mmoja muovu na wenziwe ambao waliwageuza kila mtu, ni jaribio ambao watu wachache wamekumbana nalo tangu hiyo siku.

Kwa hivyo ni Shetani ambaye aliyefungua nchi na kuwameza hawa watu ili Mungu alaumiwe kwa kufanya hivyo. Paulo antupatia kidokezi kwa kile kilichotendeka kwa hili fungu.

> Msinung'unike kama baadhi yao walivyofanya, wakaangamizwa na mharabu. 1 Wakorintho 10:10

Neno mharabu, vile tulivyosema hapo awali, nyoka mwenye sumu. Koran a watu wake waliongoza manung'uniko dhidi ya Musa, na Paulo anasema nyoka mwenye sumu aliwaangamiza wote. Kumezwa kwa Kora na wenzake kulifanyika mbele ya wana wafalme 250. Hii iliwapatia mda wa kufikiria kwamba wako katika hatari kubwa na wanastahili kumkimbilia Mwokozi ili kumtoroka mharabu. Huzuni ni kwamba hawa kutubu na walikabidhiwa kwa Shetani kabisa.

> Kisha moto ukatoka kwa Bwana, ukawateketeza hao watu mia mbili hamsini waliofukiza uvumba. Hesabu 16:35

Wengi watalia "lakini inasema moto wa bwana" na watapuuza agizo la kulinganisha maandiko yote na kuonyeshwa Yesu Kristo ni Yule Yule jana, leo na hata milele!

Yesu, katika luka 9: 54 - 56, aliwaambia wanafunzi wake kwamba moto uliotoka mbinguni kumjibu Eliya sio roho ambayo anayofanya nayo kazi. Pia twajuwa kisa cha Ayubu kwamba "moto wa Mungu" ulikuja chini na kuteketeza kondoo na wajakazi wa ayubu.

> Huyo alipokuwa akali akinena, akatokea na mwingine, na kusema, **Moto wa Mungu umeanguka kutoka mbinguni** na kuwateketeza kondoo, na wale watumishi, na kuwaangamiza; mimi peke yangu nimepona, mimi tu, kukuletea habari. Ayubu 1:16

Tunajuwa Shetani alileta huu moto na kuwateketeza. Basi kama moto inaamanisha moto basi twajuwa vile huu moto ulivyo kuja, walakini, kama vile ilivyoelezewa katika ukurasa wa Malaika wa Mapigo. Huu moto ulikuwa kusadikishwa na Roho wa Mungu ambayo iliyowamulika na hofu katika mioyo yao, inayoonyeshwa kama umeme. Roho bila upole aligoga dhamiri za hawa watu kwa dhambi zao na akiwasihi watubu, lakini hawa kuamini Mungu ni mwenye rehema. Dhambi zao ziliwaangamiza. Tumeona hili chimbuko la moto kutoka mbinguni limetajwa katika aya nyingi za Bibilia .

Wakati wana wamfalme 250 walikata kutubu na Mungu alivyotowa ulinzi wa malaika wake, Shetani kwa haraka moto kuwateketeza au ilikuwa ni moto kutokana na kusadikishwa dhambi? Kwa kiasili tunaweza kupuuza kwamba moto uliowachoma hawa maakida uliwateketeza hadi wakageuka mavumbi lakini vile tunavyo jifunza kwa hadithi ya Nadabu na Abihu, moto uliowateketeza hukuchoma nguo zao.

> Kisha moto ukatoka hapo mbele za Bwana, nao ukawala, nao wakafa mbele za Bwana.3 Ndipo Musa akamwambia Haruni, Jambo hili ni hilo Bwana alilolinena, akisema, Nitatakaswa mimi katika hao wanikaribiao, nami nitatukuzwa mbele ya watu hao wote. Haruni akanyamaza kimya.(4) Musa akawaita Mishaeli na Elisafani, wana wa Uzieli mjombaye Haruni, na kuwaambia, Njoni karibu, mwachukue hawa ndugu zenu, mkawaondoe hapa mbele ya maskani, mwende nao nje ya marago. (5) Basi wakaja karibu, **na kuwachukua, hali wamevaa nguo zao, wakawachukua nje ya marago**; kama Musa alivyosema. Walawi 10:2-5

Kwa chimbuko au mambo ya busara yote tumejifunza kwamba kuna sababu nyingi katika maandiko ambayo ya onyesha kwamba si Mungu ndiye mharabu lakini Shetani ndiye. Ufahamu bora wa Agano ikiangaliwa sambamba na maisha ya Kristo makamilifu duniani inaonyesha hadithi za kikatili na chanzo – yeye aliye na uwezo wa kifo na huyo ni Ibilisi. Waebrania 2:14.

Musa alikuwa mtu mnyenyekevu na mpole sana aliyeishi hadi wakati wa Kristo. Makosa mengi amewekelewa kwa sababu ya kutoelewa agano zote mbili. Chini ya majaribu makali, alijaribiwa na haya yalimfanya Shetani kufunika kazi yake ya uharibifu. Haya majaribu yangeliweza kutushinda sisi, kwa hivyo hatuwezi kumhukumu Musa kwa yaliyotendeka. Na tunaona mtu

mmoja kuanguka kwa majaribu ya Shetani inaweza kuleta mgawanyiko mkubwa, hasa kama ni kiongozi ambaye amemuacha Kristo. Nimuhimu kufahamu masomo ilituone tabia ya Mungu katika maandiko haibadiliki. Ni Kristo tu ambaye anatupatia picha bora. Inatupasa kushukuru kwa huo mfano ilitusome Agano la Kale kwa mwanga wake mzuri, tukitambua ukweli wa unyenyekevu wa Baba yetu ambao Musa alikuwa mfano unaong'aa.

# 23. Eliya na Mpaka wa Mwisho

> Basi palikuwa na vita mbinguni: Mikaeli na malaika zake wakapigana na hilo joka, nalo joka pamoja na malaika zake likapigana nao.… Ufunuo 12:7

Mtindo wa shetani wa kuajiri ulihitaji propaganda dhidi ya Baba wa mbinguni ili kupata utii wa malaika. Utengano huu ulifaulu na theluthi ya malaika kupitia kwa uongo wake. Ufunuo 12:4,7. Shetani alionyesha itikadi zake za ukatili juu ya Mungu na basi kuwavuta malaika kwa upande wake. Malaika waliomfuata shetani hatimaye walimalizia katika serikali ya dhuluma waliokuwa wakidhani wanaikimbia. "Kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi." Yohana 8:34.

Shetani huficha nia yake ya kweli na kuonyesha kinyume kabisa cha kile amekuwa. Hekima yote, akili, na nguvu alizokuwa amepokea katika kuumbwa kwake na Mungu zilikuwa zimeingiwa na hila ya kito cha uongo wa kuuaminisha ulimwengu kumwabudu kama mkuu.

Mwanadamu alianguka katika mtego wa joka kupitia kwa hadithi ambazo shetani alimpa. Alikubali propaganda za shetani dhidi ya Mungu na wakamkumbatia joka, yule ambaye walifikiria wanamkimbia kutoka bustanini. Shetani alifanyika mwanzilishi wa mauti na nguvu za kifo kama tulivyogundua katika sura ya 3. Uongo wake mkuu ulikuwa kuwa Mungu

hasamehi. Ukweli wa hili ulidhihirishwa katika ukweli kuwa Adamu, Hawa, na kaini hawakuomba msamaha wa dhambi zao waliposogewa. Adamu alijifunza ujuzi wa kukwepa na upangaji kama silaha dhidi ya kutubu. Aligundua njia ya kufanya magoti kuwa ngumu ili yasijikunje na kuomba msamaha kutoka kwa Mungu. katika hali hii ya mawazo kila tendo la Mungu ambalo lingemfanya mwanadamu kuona shida yake kubwa limetafsiriwa kama juhudi ya Mungu kumuumiza au kumuangamiza. Hii ndio maana zawadi ya msalaba inafahamika na mwanadamu kama hasira ya Mungu ambayo inamfanya kuinuka na kumpiga Mwanawe. Kumbuka katika sura ya 20 tulisema:

> Hii ndio ugumu wa msalaba kufahamika.Unadhihirisha tabia ya kikatili ya Shetani na asili ya matokeo ya maisha ya dhambi na inahisi kana kwamba Mungu katika hasira kali ndiye anayelundika mateso kwa mwenye dhambi. Uso wa upendo wa Mungu umefichwa katika giza la hatia na yote yanayo hisiwa ni hofu ya kutisha ya aibu ya dhambi kupindukia *Agape*, Chapter 20, page 212.

> Kaini anahisi Hukumu yake ya kibinafsi ambayo ni matokeo ya dhambi yake.Anahisi kwamba dhambi yake ni kubwa mpaka hawezi kusamehewa. Lakini pia usemi wa kumrudishia Mungu haya na kumfanya awajibike kwa sababu ya matokeo haya.Hizi ndizo sehemu mbili za hukumu na kwa hivyo ni sehemu mbili za msalaba. *Agape*, Chapter 20, page 213.

Bibilia inaelezea mtindo huu wa kuonyesha sifa zetu juu ya Mungu kama mtu anayesoma Neno la Mungu na kisha kuuona uso wake halisi. Basi akijumuishwa kwa hili, uhalisia wa pande mbili za msalaba ukitumiwa katika mada ya maagano:

### kama hauelewi hatua mbili za mtindo wa maagano utahusisha mafichuo ya udhambi wa mwanadamu kama Mungu kuwa mwenye dhambi. Mungu katika sura ya mwanadamu, mbingu isiruhusu!

katika vitendo hivi inamaana kuwa hadithi za maandiko ambazo zinaeleweka kuonyesha ushindi mkuu wa Mungu kwa kweli zinatumika kuwa kushindwa kukuu kwa tabia yake kwa sababu zinasomwa katika mtazamo wa onyesho la sifa la mtu mdhambi.

Hadithi mbili kama hizo ambazo zinaingia katika nyanja hii ni ushindi wa Eliya juu ya Mlima Karmali na kutolewa kwa Isaka juu yam lima Moria. Tutaangazia hadithi ya Eliya katika sura hii na hadithi ya Ibrahimu katika sura ifuatayo. Hadithi ya Eliya imetumiwa na shetani kama moja wapo ya silaha yake ya propaganda dhidi ya Baba yetu wa mbinguni na tabia yake. kupitia kwa makadirio ya kioo shetani husababisha moto kuanguka kutoka mbinguni juu ya madhabahu ya Eliya nakupotosha hata ya mkini waliowateule. Imeaminika kimakosa kuwa Mungu yuko katika moto, upepo, na tetemeko wakati ambao sauti tulivu ndogo ya Roho wa Mungu imezamishwa katika propaganda za ukatili wa nyoka, ambaye uadui wake kwa Mungu unadhihirishwa katika nafsi za wanadamu zilizoanguka.

Iwapo tutarudi nyuma kama miaka 2600 na kusimama juu ya mlima Karmeli na Waisraeli wengine baada tu ya moto kushuka juu ya madhabahu ya Bwana na kuteketeza kafara, tunashuhudia eneo la makabiliano. Watu 850 wanauawa, watu waliongoza taifa katika ibada ya sanamu na vitendo vya machukizo yake. Watu hawa walikuwa wamebogoa ibada ya Mungu wa kweli na hata makachukua fursa ya kuwaua wale waliokuwa waaminifu kwa Yehova. Eliya, mtu wa Mungu, kisha anauchukuwa upanga wake na kuanza kazi ya kusafisha machukizo haya. Mtu baada ya mwingine anapitiwa kwa upanga, watu 850 wanaangushwa ardhini kwa kupumua pumzi yao ya mwisho.

> Eliya akawaambia, Wakamateni hao manabii wa Baali, asiokoke hata mmoja. Wakawakamata; na Eliya akawachukua mpaka kijito cha Kishoni, akawaua huko. 1 Wafalme 18:40

Upande wa mlima umejaa miili ya waabudu sanamu. Damu yao ikiloweka mchanga kame hadi jioni  wakati mbingu zilifunguka na kunyesha mvua. Mvua inaonekana kuwa ishara wazi ya kile kinachoonekana kuwa ni idhini ya mbingu ya mauaji yaliyotendeka siku hiyo.

Kabla ya kuendeleza sehemu hii ya hadithi, wacha tuangazia fungu kabla Eliya kufasiriwa kwenda mbinguni katika gari la moto.

> Ndipo mfalme akatuma akida wa askari hamsini pamoja na hamsini wake, wamwendee Eliya. Akamwendea, na tazama, ameketi juu ya kilima. Akamwambia, Ewe mtu wa Mungu, mfalme asema, Shuka. (10) Eliya akajibu, akamwambia yule akida wa hamsini, Ikiwa mimi ni mtu wa Mungu, na ushuke moto kutoka mbinguni, ukuteketeze

> wewe na hamsini wako. Moto ukashuka, ukamteketeza, yeye na hamsini wake. 2 Wafalme 1:9-10

Ni nini ambacho Eliya alikuwa amekifanya ili kusababisha kikosi cha askari 51 kumwendea? Mfalme wakati huo alikuwa amegonjeka na kuwatuma wajumbe kuuliza Baalzebub mungu wa Ekroni. Eliya aliwakamata na kuwaambia kuwa mfalme angekufa. Kiasili, mfalme hakufurahia kuhusu hili, na akawatuma watu wake kumshika Eliya.

watu hawa walipokuja kumchukua Eliya, aliamuru moto kushuka kutoka mbinguni uwateketeze. Tunaweza fikiria kuwa kikosi kifuatacho cha askari kitajifunza kutokana na yale yaliyotendeka na kujaribu njia mbadala ya kushauriana na Eliya. La kuhuzunisha, ni kuwa pia wao walikubana na moto kutoka mbinguni na wakafa. Watu 102 waliangamia kwa moto. Huyu anaonekana kuwa nabii shujaa ambaye anaweza ita moto kutoka mbinguni na kuangamiza adui wa Mungu. Baada tu ya hadithi hii tunasoma:

> Ikawa, walipokuwa wakiendelea mbele na kuongea, tazama! Kukatokea gari la moto, na farasi wa moto, likawatenga wale wawili; naye Eliya akapanda mbinguni kwa upepo wa kisulisuli. 2 Wafalme 2:11

Kwa watu wengi huu ni ushahidi wa kuwathibitishia kuwa Mungu alituma moto kutoka mbinguni na kuwateketeza askari hawa na kisha akamchukua mbinguni nabii wake shujaa. Hili ni tukio la kustajabisha, likiongezwa pamoja na ushindi wa Eliya juu ya manabii wa Baali katika mlima Karmeli, inaonekana kuwa ushindi wa ajabu kwa sababu ya ukweli.

Tukirudi katika onesho kamili la Baba katika Kristo tunapata ufafanuzi wa Uungu juu ya hadithi hizi.

> Wanafunzi Wake, yaani, Yakobo na Yohana walipoona hayo, **wakasema: “Bwana, unataka tuagize moto kutoka mbinguni ili uwaangamize?” (55) Yesu akageuka na kuwakemea, (56) nao wakaenda kijiji kingine**. Luka 9:54-56

> Ndipo Yesu akamwambia, **“Rudisha upanga wako mahali pake, kwa maana wote watumiao upanga watakufa kwa upanga.** Mathayo 26:52

> Yesu akajibu, "**Ufalme Wangu si wa ulimwengu huu.** Ufalme Wangu ungekuwa wa ulimwengu huu wafuasi Wangu wangenipigania ili nisitiwe mikononi mwa Wayahudi. Lakini kama ilivyo Ufalme Wangu hautoki hapa ulimwenguni." Yohana 18:36

Tunapotazama utukufu au tabia ya Bwana Yesu tunaona jambo tofauti na lile tunaona katika hadithi na Eliya. Wanafunzi walitaka kuiga Eliya lakini Yesu akawakemea na kuwaambia kuwa Roho wake sio wa kuangamiza au wa kazi kama hiyo. Yesu sio mwangamizi bali mkombozi. Kweli kwamba Yesu anazungumza moja kwa moja hadithi ya Eliya ya kushusha moto kutoka mbinguni na kuwateketeza watu, kutuambia kuwa huyu sio Roho wake, inamaanisha kuwa tunapaswa kuangalia kwa undani hadithi hii ili tujue kilichotendeka hasa.

kinachovutia ni kwamba tafsiri nyingi za kisasa zinaacha sehemu muhimu ya yale Kristo alisema:

> Wanafunzi Wake, yaani, Yakobo na Yohana walipoona hayo, wakasema: "Bwana, unataka tuagize moto kutoka mbinguni ili uwaangamize?" (55)Yesu akageuka na kuwakemea, Luka 9:54-55 (NIV)

Kuondolewa kwa kauli "sikuja kuangamiza roho za watu" katika NIV inamuache msomaji akishangaa kwa nini wanafunzi walikemewa. Inaweza kuwa tu ni suala la wakati au matumizi mabaya ya nguvu za Mungu. Kuwepo kwa kirai juu ya huduma ya Mwana wa Mungu sio kuangamiza, hakuzungumzi tu hitaji la wanafunzi bali pia vitendo vya Eliya.

Tunarejea kwenye asubuhi baada ya ushindi mkuu juu ya mlima Karmeli. Malikia Yezebeli ameudhika sana kuhusu yaliyotendeka na kutuma ujumbe kwa Eliya.

> Basi, Ahabu akamwambia Yezebeli habari ya mambo yote aliyoyafanya Eliya, na jinsi alivyowaua manabii wote kwa upanga. (2)Ndipo Yezebeli akampelekea Eliya mjumbe, kusema, **Miungu wanifanyie hivyo na kuzidi, nisipokufanya roho yako kesho, panapo wakati huu, kama roho ya mmojawapo wa hao.** 1 Wafalme 19:1-2

Eliya alikuwa shupavu katika kutangaza kuja kwa kiangazi kwa Mfalme Ahabu na katika miaka mitatu na nusu ambayo Ahabu alikuwa amejaribu kumtafuta

na kumuua. Alimwamini Mungu kumlinda na kumukilimia mahitaji yake. Baada ya Eliya kuwaua manabii wa bali jambo linatendeka na Eliya anakimbilia uhai wake.

> Naye alipoona hayo, **aliondoka, akaenda aihifadhi roho yake**, akafika Beer-sheba, mji wa Yuda, akamwacha mtumishi wake huko. (4) Lakini yeye mwenyewe akaendelea katika jangwa mwendo wa siku moja, akaenda akaketi chini ya mretemu. Akajiombea roho yake afe, akasema, Yatosha; sasa, Ee Bwana, **uiondoe roho yangu; kwa kuwa mimi si mwema kuliko baba zangu.** 1 Wafalme 19:3-4

Mbona Eliya amkimbie mwanamke huyu? Alikuwa amesimama juu ya mlima Karmeli akiwa peke yake wakati mfalme na makuhani wa Baaali wangemshika na kumuua wakati wowote. Eliya aliamini katika ulinzi wa Mungu wake. Lakini marekebisho ambayo Eliya alitarajia hayakutendeka. Watu hawakutubu kwa kuhusika katika ibada ya Baali. Moyo wake ulijawa na hofu na kuhisi likimlazimisha kuacha pahali pake pa kazi. Mbona mabadiliko ya ghafla katika Eliya? Sasa akiwa ameua, Eliya alikumbwa na hisia sawa na zile zilizomjia Kaini.

> Tazama, umenifukuza leo katika uso wa ardhi, nitasitirika mbali na uso wako, nami nitakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani; **hata itakuwa kila anionaye ataniua.** Mwanzo 4:14

Amri Kumi zikionyesha tabia ya Mungu zinasema wazi – *usiue*. Watu wanapo ua watu wengine hofu ya kifo inaongezeka nafsini. Kile unachotenda kwa wengine kinakufanya kuhofu kuwa jambo sawa litafanywa kwako. Hofu hii huongezeka kwa sababu shetani amepewa fursa kuu ya kujaribu na kunyanyasa. Kunahisia ya kutaka ulinzi ambapo majeshi au miji iliyozingilwa inaonekana muhimu zaidi katika kukabiliana na hofu hii.

Eliya alitamka maneno ya kuomboleza, "uiondoe roho yangu; kwa kuwa mimi si mwema kuliko baba zangu." Eliya alikuwa akipambana na nini ndani yake? Mbona akalemewa na kukatizwa tamaa hadi kwa kiwango cha kutaka kufa? Ukweli, matarajio yake ya juu ya mabadiliko hayakutendeka, bali yalimfanya kujilinganisha na baba zake, na kutaka kufa?

> **Eliya alikuwa mwanadamu kama sisi.** Akaomba kwa bidii kwamba mvua isinyeshe nayo haikunyesha juu ya nchi kwa muda wa miaka mitatu na miezi sita. Yakobo 5:17

Zingatia kile Eliya alimwambia Bwana alipoulizwa mbona alikimbia.

> Akafika kunako pango, akalala ndani yake. Na tazama, neno la Bwana likamjia, naye akamwambia, Unafanya nini hapa, Eliya? (10) Akasema, **Nimeona wivu mwingi kwa ajili ya Bwana Mungu wa majeshi; kwa kuwa wana wa Israeli wameyaacha maagano yako, na kuzivunja madhabahu zako, na kuwaua manabii wako kwa upanga;** nami nimesalia, mimi peke yangu; nao wanitafuta roho yangu, waiondoe. 1 Wafalme 19:9-10

Eliya analalamika kuwa, licha ya uaminifu wake, lazima ashuhudie huzuni ya kuona kuangamizwa kwa manabii wa Mungu kwa upanga, na kama inavyoonekana kuachwa peke yake. Kama Eliya angenyenyekeshwa kwa kupenda tamaa kama tunavyo, angejaribiwa kutafuta kulipiza kisasi kwa mauaji ya watu wa Mungu na labda wale waliokuwa marafiki zake wazuri? Unaweza jaribiwa na kulipiza kisasi kama rafiki wako wa karibu ameuawa? Inawezekana kuwa na nia hii ikifichika moyoni mwako, hata kufichika kwako wewe mwenyewe na kufunikwa kwa kujali kwa Mungu?

Eliya alipozulu maeneo ya maangamizi ya manabii wa Baali, aliona udhihirisho wa mbegu ya mauaji iliyokuwa nafsini mwake? Alifahamu kuwa hakuwa mwema kuliko baba zake? Wakati Yezebeli alitishia uhai wake, alikuwa na uhakika wa uhusiano wake na Mungu? Kama Adamu, Eliya alifuma katika mwitikio wa swali, “unafanya nini hapa?” mawazo kuwa kwa kweli yalikuwa makosa ya Mungu kuwa haya yote yalitendeka? Maelezo ya Eliya ni ya kujikinga; “nimefanya hili na nimefanya kile.” “Hali hii ni ya kutisha na niko peke yangu.”

Kwa baadhi ya watu aina hii ya uchunguzi kwa nabii shujaa ni kufuru. Kwa wale wanaotamani kuishinda dhambi, wanaona katika kile Eliya alipitia hali yao halisi ikidhihirishwa ili waweze kuagizwa kukabiliana na mgogoro wa Mwisho wa dunia. Ni muhimu kwetu kusoma hadithi hii kwa Nija ambayo itatufundisha, ili tutakapojipata katika mgogoro maishani mwetu na tudhihirishe sifa za tabia ambazo sio za Kikristo tuweze kushikilia na tusiombe kufa kwa kukata tamaa. Lazima tusome hadithi hii kwa undani wake na kufahamu funzo lake kwetu katika siku za mwisho. Roho wa Eliya

atashuka juu ya watu wa Mungu sio tu kuonya ulimwengu bali pia kuwaweka katika hali ya kuona hali yao halisi ya mauaji ikiwekwa wazi. Kama hautapata funzo, utakufa katika kukatishwa tamaa, au hata mbaya zaidi: utahalalisha tabia ya mauaji kama ghadhabu ya Mungu.

Tunaweza kuwa na uaminifu kuwa Eliya hakuwa katika Agano jipya wakati huo. Hisia ya Agano Jipya na kuandika tabia ya Mungu moyoni. Tabia ya Mungu inadhihirishwa katika Sheria ya Mungu.

> Hivyo basi, sheria yenyewe ni takatifu na amri ni takatifu na ya haki, tena ni njema.  Warumi 7:12

> Baada ya siku zile, hili ndilo agano  nitakalofanya na nyumba ya Israeli, asema Bwana, 'Nitaweka sheria zangu katika nia zao na kuziandika katika mioyo yao.  Nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu Wangu.:… Waebrania 8:10

Eliya anakimbilia mlimani Sinai na anaulizwa na Mungu, "unafanya nini hapa?" Eliya anajitetea. Anaeleza kuwa amekuwa mwaminifu kwa Mungu lakini kila kitu kilikuwa kikimwendea kinyume, na kwa hilo alikuwa peke yake, na kuwa utawala ulikuwa unajaribu kumuua. Mungu anaendelea kumuonyesha kuwa tatizo lilikuwa katika ufahamu wake.

> Akasema, Toka, usimame mlimani mbele za Bwana. Na tazama, Bwana akapita; upepo mwingi wa nguvu ukaipasua milima, ukaivunja-vunja miamba mbele za Bwana; lakini Bwana hakuwamo katika upepo ule; na baada ya upepo, tetemeko la nchi; lakini Bwana hakuwamo katika lile tetemeko la nchi; (12) **na baada ya tetemeko la nchi kukawa na moto;** lakini Bwana hakuwamo katika moto ule; na baada ya moto sauti ndogo, ya utulivu. 1 Wafalme 19:11-12

Tabia ya Mungu haikudhihirishwa katika maonyesho ya nguvu za maumbile. Kwa uwazi, hakuwa katika vitu hivi. Moto ulioshuka kutoka mbinguni na kuteketeza dhabihu ulitafsiriwa kama dhihirisho la nguvu iliyopelekea Eliya katika mauaji ya manabii wa Baali kwa upanga. Aliambiwa kuwa Mungu hakuwa katika moto. Hili linamaanisha nini? Mungu alituma moto lakini hakuwa katika moto? Mungu anamwambia Eliya, kwa athari, alijibu ombi aliloagizwa kuonyesha nani anamtumikia Mungu wa kweli. Jibu lilikuwa kwa namna ambayo hadhira iliielewa.

Waisraeli wote walikuwa katika Agano la Kale. Walichoshuhudia kilikuwa onyesho la nguvu kulingana na ufahamu wao wa jinsi Mungu anaweza tenda. Watu wote walitafsiri kutokana na kile waliona kuwa Mungu alikuwa katika moto huu. Mungu alimwambia Eliya kuwa hakuwa. Mungu alinenena na watu kwa kioo cha yale yaliyokuwa mioyoni mwao. Mungu kwa kweli alitenda muujiza wa moto *lakini haukuwa onesho la tabia yake mwenyewe.*

onyesho la nguvu kulitoa mbegu ya kisasi iliyokuwa ndani ya Eliya. Hii ndio kazi ya sheria katika Agano la Kale. Mungu angefanya dhambi itawale. Kwa njia sawa ambayo Yesu alimwambia mwanamke kuwa sio vizuri kuuchukua mkate wa mtoto na kuutupia mbwa, Baba yetu aliye mbinguni alitoa onyesho la nguvu ili kujaribu mioyo ya watu. Onyesho hili lilidhihirisha kilichokuwa ndani ya Eliya. Katika kioo Eliya anasikia amri ambayo moyo wake ulitamani – Amri ya kuwaangamiza manabii wa Baali. Ilidhihirisha Eliya kama muuaji sio mwema kuliko baba zake. Manabii wa baali wanaadhibiwa katika mchakato huo. Mungu anatenda kupitia Agano la Kale kutuma ujumbe kwa Waisraeli kuwa ibada ya sanamu ni mbaya, lakini tabia haioneshwi katika mchakato huu.

Muujiza wa upepo, tetemeko, na moto unatuonyesha kuwa Eliya hakuelewa tabia ya Mungu. Hata hivyo, Mungu alikuwa anataka kudhihirishia tabia yake mwenyewe ili Eliya aone tofauti na yake na atubu kwa sababu ya roho yake ya kisasi. Mungu alimuuliza Eliya swali tena ili kupata ungamo kutoka kwa Eliya.

> Ikawa, Eliya alipoisikia, alijifunika uso wake katika mavazi yake, akatoka, akasimama mlangoni mwa pango. Na tazama, sauti ikamjia, kusema, Unafanya nini hapa, Eliya? (14) Akasema, Nimeona wivu mwingi kwa ajili ya Bwana, Mungu wa majeshi; kwa kuwa wana wa Israeli wameyaacha maagano yako, na kuzivunja madhabahu zako, na kuwaua manabii wako kwa upanga; nami nimesalia, mimi peke yangu; nao wanitafuta roho yangu waiondoe. 1 Wafalme 19:13-14

Eliya anarudia ulinzi wake wa kwanza. Hili linaashiria kuwa hatambui maana ya matukio anayoonyeshwa. Eliya anafikishwa katika kikomo. Kama yesu alivyosema kwa wanafunzi, anasema kwa Eliya, “roho inataka lakini mwili ni dhaifu.” Eliya anaambiwa kuwa kazi yake itaisha karibuni.

> Bwana akamwambia, Enenda, urudi njia ya jangwa la Dameski; ukifika, mtie mafuta Hazaeli awe mfalme wa Shamu. (16) Na Yehu mwana wa Nimshi mtie mafuta awe mfalme wa Israeli; na **Elisha mwana wa Shafati wa AbelMehola mtie mafuta awe nabii mahali pako.** 1 Wafalme 19:15-16

Mbegu ya hofu kutokana na kuwaua manabii wa Baali ilisalia ndani ya Eliya. Nia ya kuua inadhihirishwa tena muda mfupi kabla ya Eliya kuchukuliwa, Eliya alipoitisha moto kutoka mbinguni juu ya wale waliokuja kumkamata. Tunajua kama Eliya alikuwa na hofu wakati hawa watu walikuja kumkamata?

> Malaika wa Bwana akamwambia Eliya, **Shuka pamoja naye; usimwogope.** Akaondoka, akashuka pamoja naye hata kwa mfalme. 2 Wafalme 1:15

Eliya bado alikuwa na hofu. Wakati akida wa hamsini mwanzo alimwita Eliya, alimwita "mtu wa Mungu" akida hakuwa na shuku kuwa alikuwa mtu wa Mungu.

> Eliya akajibu, akamwambia yule akida wa hamsini, **Ikiwa mimi ni mtu wa Mungu, na ushuke moto kutoka mbinguni, ukuteketeze wewe na hamsini wako.** Moto ukashuka, ukamteketeza, yeye na hamsini wake. 2 Wafalme 1:10

Mungu alimuonyesha Eliya kuwa hakuwa katika moto. Mbona Eliya akaitisha moto basi? Alikuwa na hofu. Ingewezekanaje kuwa moto ulishuka kutoka Mbinguni ukawala watu hawa? Chini ya huduma ya mfalme ambaye alikuwa amejitoa kwa huduma ya Baali, mungu wa Ekroni, ua wa ulinzi uliondolewa. Na alishusha moto juu ya watu hawa?

> Bwana akamwambia Shetani, Tazama, yote aliyo nayo yamo katika uwezo wako; lakini usinyoshe mkono wako juu yake yeye mwenyewe. Basi Shetani akatoka mbele za uso wa Bwana..... (16) Huyo alipokuwa akali akinena, akatokea na mwingine, na kusema, Moto wa **Mungu umeanguka kutoka mbinguni na kuwateketeza kondoo, na wale watumishi, na kuwaangamiza;** mimi peke yangu nimepona, mimi tu, kukuletea habari. Ayubu 1:12,16

Mbona shetani awateketeze watu ambao walikuwa wametumwa kumkamata nabii wa Mungu?

Hulazimisha maumivu juu ya nafsi ya mtu ili kupata imani ya adui. Mbinu 34 ya 36. *The Art of War* by Sun Tzu

Eliya alipokuwa katika hofu aliomba usaidizi wa muujiza ili kuthibitisha kuwa kweli alikuwa mtu wa Mungu, alimfungulia shetani milango ili kupiga. Katika kupiga watu wale chini ya uongozi wake, shetani aliushawishi ulimwengu kuwa Mungu aliwapiga watu hao na kuwaua.

Wanafunzi walichukua chambo na walikuwa na hamu ya kufuata mfano wa Eliya katika kuwaua Wasamaria.  Kupitia kwa mkakati huu, shetani alipata imani ya adui wake wa duniani. Walifanyika wenye roho yake kupitia kwa mikakati yake ya kuvutia. Ilimgharimu shetani watu 102, lakini akajishindia vita vya propaganda na lengo la kugeuza tabia ya Mungu, Mungu ambaye karibu wakristo wote ulimwenguni wanamkubali leo. Shetani, bila shaka, alifanya hili katika Umoja na roho wa kidunia wa mtu, ambaye katika hali yake halisi ya kutotubu anapenda kuwa na ghadhabu ya Mungu muumbaji, kwa sababu pengine ihalalishwe kwa ghadhabu yake mwenyewe, au ama humfanya ajihisi kuwa mkuu kwa Mungu kimaadili au humuimarisha katika uasi wake. Hadithi hii ya Eliya ni sehemu ya mpaka wa mwisho katika kukimbia mtego wa utandu wa uongo wa shetani ambao ameuweka kwa watu.

wakati mtu anaomba nguvu za Mungu katika kujikinga, ameingia katika mpito wa kufanya kazi na shetani. Mtu anaweza badilisha upande katika vita hivi vya kiroho bila ya kuwa na wazo ya kuwa amefanya hivyo.  Hatuwezi jua ukweli bila kuwa na maneno ya Yesu aliyoyanena kwa wanafunzi wake kuhusu moto huyu kutoka mbinguni, na kwa hivyo tutafungwa katika imani kuwa Mungu hutuma moto kutoka mbinguni kuua. Imani hii ya uongo itahakikisha kuwa tutajaribu kumtumikia kutokana na hofu, na wala sio upendo.

Baada ya siku arobaini jangwani Yesu alikuwa njaa sana. Shetani alimjaribu Yesu kufanya muujiza ili kujiokoa. Alisema, “kama wewe ni Mwana wa Mungu geuza mawe haya yawe mikate.” kwa kujibu Yesu alisema, “mtu hawezi ishi kwa mkate tu bali kwa kila neno litokalo kinywani mwa Baba.” Alikataa swali la *kama* la adui , na kushikilia neno la Baba yake. Wale wanaotaka kuishinda mikakati ya shetani, sehemu yake ikionyeshwa katika jua “Tzu’s ‘The Art of War’”, lazima wafahamu jinsi shetani hufanya kazi; hili halieleweki kupitia kwa kusoma vitabu vya kisufi vilivyoongozwa na shetani,

vinavyopanda mbegu ya ufisadi, ila kwa kupitia kwa hekima inayotoka kwa Mungu. Ni kwa kuruhusu Yesu kutuonyesha usumbufu wetu, tabia ya kijanja, kumruhusu kufanya mabadiliko ndani yetu na kisha kupitia kwetu. Hutupa maadili muhimu kwa msingi wa uhakika wa imani kamilifu katika Baba yetu – kama waridhi pamoja na Kristo tunayefuata pamoja naye roho sawa wa upendo wa kujikana nafsi unaoonyeshwa katika huduma ya Yesu duniani. Kwa wana wa Mungu:

> …Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo na kwa neno la ushuhuda wao. **Wala wao hawakuyapenda maisha yao hata kufa**. Ufunuo 12:11

Watu wa Mungu hawashindi shida zao kwa upanga na nguvu za mikono yao kuwaua watu. Hawapendi maisha yao hadi kwa kifo.

> Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo? Je, ni shida au taabu au mateso au njaa au uchi au hatari au upanga? (36) Kama ilivyoandikwa: **"Kwa ajili yako tunauawa mchana kutwa, tumehesabiwa kama kondoo wa kuchinjwa."** (37) **Lakini katika mambo haya yote tunashinda, naam na zaidi ya kushinda, kwa Yeye aliyetupenda.** Warumi 8:35-37

Basi Eliya angechukuliwaje mbinguni? Eliya ni aina ya wale katika siku za mwisho watakaochukuliwa mbinguni bila kuonja kifo.

> Angalieni, **nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya Bwana, iliyo kuu na kuogofya.** (6) Naye ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto wao, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, ili nisije nikaipiga dunia kwa laana. Malaki 4:5-6

Katika siku za mwisho, masalio wa Mungu watakabiliana na mnyama na sanamu yake katika roho ya Eliya. Warumi 11:2-5, Ufunuo 12:17. Masalio hawa watapitia majaribu sawa kama yale ya Eliya katika kukabiliana na mfalme wa dunia na maasi yake. Majaribu haya pia yanaonyeshwa katika hadithi ya Yakoko.

> Ole! Maana siku ile ni kuu, hata hapana inayofanana nayo, **maana ni wakati wa taabu yake Yakobo; lakini ataokolewa nayo.** (8) Na itakuwa katika siku ile, asema Bwana wa majeshi, nitaivunja nira yake itoke shingoni mwako, nami nitavipasua vifungo vyako; wala wageni hawatamtumikisha tena; Yeremia 30:7-8

Kabla ya Eliya kuchukuliwa, nira ya dhambi lazima ingevunjwa kikamilifu. Shuku ambayo Eliya alikuwa amenyenyekeshwa kwayo lazima ingeshindwa kabla ya kuenda mbinguni. Hadithi ya Eliya inashikanishwa na matukio ya Mwisho ya historia ya dunia.

> Huyu mnyama wa pili akafanya ishara kuu na za ajabu, **hata kusababisha moto kushuka toka mbinguni kuja duniani watu wakiona waziwazi. (14)Kwa sababu ya zile ishara alizokuwa amepewa uwezo wa kufanya kwa niaba ya yule mnyama wa kwanza, akawadanganya wakaao duniani**. Akawaamuru wasimamishe sanamu kwa heshima ya yule mnyama aliyekuwa amejeruhiwa kwa upanga lakini akaishi. (15) Akapewa uwezo wa kuipa pumzi ile sanamu ya yule mnyama wa kwanza, ili iweze kusema na kuwasababisha wale wote waliokataa kuiabudu hiyo sanamu kuuawa. (16) Pia alimlazimisha kila mmoja, mdogo na mkubwa, tajiri na maskini, mtu huru na mtumwa, atiwe chapa kwenye mkono wake wa kuume au kwenye kipaji chake cha uso, Ufunuo 13:13-16

Kuweka kwa hadithi ya Eliya ya moto kutoka mbinguni katika muktadha wa unabii wa Malaki 4:5-6 na Ufunuo 13:13-16. Kunaunganisha matukio ya siku za mwisho na alichokipitia. Hofu ndani ya Eliya lazima ingeshindwa, na ni kupitia kwa mchakato wa uchunguzi mkali wa nafsi ndio ambao Eliya alivunja nira kutoka begani mwake. Eliya alikuwa mtu wa maombi. Aliomba bila kukoma juu ya mvua katika mlima Karmeli, akishikilia imani, akisubiri hata wingu ndogo kama mkono wa mwanadamu lije. 1 Wafalme 18:41-45. Katika siku za mwisho watu wa Mungu wataomba bila kukoma katika wakati wa taabu ya Yakobo ili wapate ushindi dhidi ya mnyama na sanamu yake.

> Wakati huo Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwa na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo; na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile. Danieli 12:1

Mapito ya Eliya pia yanaonekena katika maisha ya Yohana Mbatizaji. Alikuwa na mgogoro mkubwa wa imani hata kabla auawe.

> Yohana Mbatizaji aliposikia akiwa gerezani mambo ambayo Kristo a alikuwa akiyafanya, aliwatuma wanafunzi wake (3) ili

> wakamwulize, **"Wewe ndiye yule aliyekuwa aje, au tumngojee mwingine?"** Mathayo 11:2-3

Yesu alimrejelea Yohana Mbatizaji kama  Eliya wa pili.

> Kama mko tayari kukubali hilo, yeye Yohana ndiye yule Eliya ambaye manabii walikuwa wamesema angekuja. Mathayo 11:14

Mgogoro wa imani ambao Yohana alipitia katika kuamini kuwa Yesu ni Masihi ulieneza mambo katika tabia yake ambayo ilihitaji kushindwa. Kama ilivyokuwa kwa Yohana Mbatizaji, Eliya alihitaji kuyashinda mambo haya. Katika hali iyo hiyo ngumu ya mateso, mioyo ya dhambi ya wanadamu hudhihirishwa, na katika hali hiyo Bwana yesu hufanya haki yake kuwa nyingi zaidi.

> Zaidi ya hayo, sheria ilikuja, ili uvunjaji wa sheria uongezeke. Lakini dhambi ilipoongezeka, neema iliongezeka zaidi. (21) Ili kwamba kama vile dhambi ilivyotawala kwa njia ya mauti, vivyo hivyo neema iweze kutawala kwa njia ya kuhesabiwa haki hata uzima wa milele katika Yesu Kristo Bwana wetu. Warumi 5:20-21

Eliya alienda mbinguni kwa kutegemea haki ya Masihi pekee. Hakuenda kama nabii shujaa wa kuwateketeza adui zake. Alienda kama mdhambi asiyeweza kujisaidia aaminiye tu neema ya Mungu katika ahadi ya mwana Kondoo.

Tunapounganisha hadithi ya Yakobo, Eliya, Yohana Mbatizaji, na roho ya Eliya kuwekwa wazi kwa watu wa Mungu katika siku za mwisho, tunaona kuwa watu wote watafikishwa katika kutubu ili kupokea taji la uzima. Wanafikishwa katika nafasi ngumu inayofunua mizizi ya dhambi ya udaifu wao wa hali ya binadamu.

Kazi hii ya kutubu haionekani kwa wasomi wa Bibilia katika maisha ya Eliya, lakini maneno ya Yesu yanaashiria kuwa roho wa kwanza ndani ya Eliya hakuwa roho wa Kristo. Lazima angetubu kwa hili kabla kunyakuliwa kutokee. Ukosefu wa imani kwa Mwana wa Mungu kwa Yohana Mbatizaji pia kulimaanisha kuwa alihitaji kutubu ili apokee uzima wa milele. Yale watu hawa wawili waliyapitia, yatarudiwa na masalio wa siku za mwisho. Wengine watanyakuliwa mbinguni bila kuonja kifo (1 Wathessalonika 4:15-17) lakini watapitia wakati wa shida ili kusafisha uchafu ulioko mioyoni mwao. Baadhi

watakatwa vichwa kama Yohana Mbatizaji. Lakini wote wanafikishwa katika kiwango cha kutubu yale ambayo hayahitaji kutubiwa.

> Kwa maana huzuni ya kimungu huleta toba iletayo wokovu na wala haina majuto. Lakini huzuni ya kidunia husababisha mauti. 2 Wakorintho 7:10

Kwa Yakobo, kujiamini kwake, kujikinga, tabia ya udanganyifu hatimaye kulisalimishwa baada ya usiku wa pambano na Mwana wa Mungu, kukataa kumuacha aende hadi alipopata hakikisho la mibaraka ya Mungu na uaminifu kamili wa Mungu ambao ulimlisha maisha yake yote. Mwanzo 48:15.

Kwa Eliya, miili ya watu 952 iliyotapakaa juu ya ardhi katika matukio hayo mawili, ilitoa ushahidi wa roho ya kisasi na hofu iliyokuwa ndani yake bila ya yeye kujua.

Kwa Yohana mbatizaji, alihatarisha kuwa na shaka juu ya kazi ya Masihi jambo ambalo lingewaathiri maelfu ya watu. Lakini wote walishinda hali zao kwa kutubu na kuamini tu uhalali wa Mkombozi wetu. Jambo sawa litashuhudiwa kwa watu wa Mungu katika siku za Mwisho. Ni mpaka wa mwisho. Hakuna nabii shujaa; kuna Kristo tu na ndiye aliyesulubishwa. Kuna haki katika Kristo tu kwa wokovu. Mungu alifanya mambo makuu kwa manabii hawa wawili lakini jambo kuu zaidi lilikuwa kuwafahamisha hitaji lao; wenyewe la wokovu kama hakuna tofauti na mtu mwingine.

Tunaposhika kwa *kweli ukweli huu – hakuna mwenye haki*, hakuna hata mmoja – basi uongo wa shetani utakosa nguvu juu yetu.

Shetani anataka watu wasome Bibilia kwa juujuu na kuamini kuwa matendo ya nabii yakionyesha tabia yake ya ukatili yanaweza fahamika kuwa tabia ya Mungu. Mungu anapoleta watu kupitia kwa Agano la Kale kujitazama, shetani huwashawishi watu kukadiria udhaifu wa vitendo vya binadamu vikiwekwa wazi kama onesho la tabia ya Mungu. Mchakato huu wa kutangaza kuwa takatifu vitendo vya watu, kuwa wako katika mapenzi ya moja kwa moja ya Mungu, hutekeleza tu kusudi la kuhalalisha roho wa kisasi, ukatili, na kuwaondoa adui wako.

Wacha tumtazame Kristo pekee kama mfano kamili wa Baba. Kwa kusoma tabia yake pekee tutakuwa na uhakika kuwa tunapata sauti ndogo tulivu ya Mungu sio iliyochanganywa na upepo, mitetemeko, na moto. Tusimuumize

Mungu kwa kumuelewa visivyo, kwa kuwa katika hili ukweli hukataliwa na kudharauliwa na wanadamu. “Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; Na pamoja na matajiri katika kufa kwake**; Ingawa hakutenda jeuri**, Wala hapakuwa na hila kinywani mwake.” Isaya 53:9

## 24. Ibrahimu na Chukizo la Ukiwa

> Ikawa baada ya mambo hayo Mungu alimjaribu Ibrahimu, akamwambia, Ee Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa. 2 Akasema, Umchukue mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria, ukamtoe sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia. Mwanzo 22:1-2

Baada ya hayo yote ambayo tumeangazia inapaswa kuwa wazi kwamba kifungu hiki kinaweza somwa kwa namna mbili tofauti. Namna moja inadhihirisha upendo wa Mungu kwa njia ya kustajabisha; Ibrahimu kumtoa Mwanawe Isaka kunatoa mfano wa upendo wa Mungu kuwa tayari kumtoa Mwanawe kwetu ili tuweze kuona na kuamini jina (tabia) ya Mwana wa Mungu na tuokolewe. Kwa kinyume, tukiangalia kwa kioo cha Agano la Kale tunaona sura ya Mungu akijaribu uaminifu wa Ibrahimu kupitia kwa jaribio ambalo haliwezi onekana kuwa bora na hitaji la Ibrahimu kumuua mwanawe katika ubaya.

Mbona Mungu amwagize Ibrahimu kumtoa mwanawe wa ahadi kama sadaka ya kuteketezwa? Ombi hili linaonekana kupataka kikamilifu katika dhana ya hasira ya Mungu ambayo huhitaji kuridhishwa kwa kifo. Hivi ndivyo dini zote za kipagani zinafanya kazi; kutuliza Mungu wako kupitia dhabihu ni moyo wa kipagani. Mbona Bibilia inaonekana kumuonyesha Mungu katika nuru hii?

Kwanza, wacha turudi nyuma na tuangalie mwanzo wa dhabihu katika maandiko.

> Bwana Mungu akawafanyia Adamu na mkewe mavazi ya ngozi, akawavika. Mwanzo 3:21

Hatujaambiwa jinsi ngozi ilikuja kuwepo. Kinachowezekana sana ni kuwa mnyama au wanyama walikuwa wafe ili ngozi ipatikane. Mungu angeweza kuziumba ngozi hizi bila kifo cha mnyama lakini huu ni uvumi tu kwa kuwa katika fungu hili hatujaambiwa. Kifungu cha kwanza kinachozungumza kuhusu sadaka kinapatikana katika sura inayofuata ya Mwanzo.

> Ikawa hatimaye Kaini akaleta mazao ya ardhi, sadaka kwa Bwana. (4) Habili naye akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama. Bwana akamtakabali Habili na sadaka yake; Mwanzo 4:3-4

Hadithi hii inaashiria kuwa sadaka ilihitajika na bila sadaka ya mwana kondo ibada haingechukuliwa kwamba imekubalika.

> **Bali Kaini hakumtakabali, wala sadaka yake. Kaini akaghadhibika sana,** uso wake ukakunjamana. (6) Bwana akamwambia Kaini, Kwa nini una ghadhabu? Na kwa nini uso wako umekunjamana? (7) **Kama ukitenda vyema, hutapata kibali?** Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangoni, nayo inakutamani wewe, walakini yapasa uishinde. Mwanzo 4:5-7

Hivyo basi, inaonekana kuwa Mungu alihitaji wanadamu kutoa sadaka ya Wanyama kama sehemu ya ibada. Kukataa kwa Kaini kuleta mnyama kama sadaka kulienea hadi kwa hatua ya mauaji ya kwanza. Kilicho cha muhimu sana ni kuwa wakati Kaini hangetambua sadaka ya mwana kondo, alipata kibadala katika mauaji ya nduguye kukidhi ghadhabu yake mwenyewe.

Hili ni muhimu kwa hadithi ya dhabihu ya Isaka kwa sababu hili pia lilikuwa pendekezo la sadaka ya mwanadamu kwa kusudi la upatanisho. Kama kwa mkao wa Mungu kwa dhabihu, tunagundua yafuatayo kwa mvuto kubwa.

> Ee Bwana, Mungu wangu, umefanya kwa wingi Miujiza yako **na mawazo yako kwetu; Hakuna awezaye kufananishwa nawe;** Kama ningependa kuyatangaza na kuyahubiri, Ni mengi sana hayahesabiki. (6) **Dhabihu na matoleo hukupendezwa nazo,**

> **Masikio yangu umeyazibua, Kafara na sadaka za dhambi hukuzitaka.** Zaburi 40:5-6

Mwandishi wa zaburi aliyeongozwa anasema kuwa Mungu hakuhitaji dhabihu. Kisha anatoa tangazo la ajabu kuwa Mungu hakuomba au kuamuru sadaka ya kuteketezwa na sadaka ya dhambi. Mwanzoni wazo hili linaonekana kuwa halipatani kabisa na yale ambayo yameandikwa katika sehemu zingine za Agano la Kale. Maagizo ambayo Mungu alimpa Musa na maelezo wazi juu ya jinsi sadaka ingewasilishwa inaonekana kweli kuonyesha kuwa hili ndilo Mungu alihitaji. Ila tunasoma tena:

> **Maana sikusema na baba zenu, wala sikuwaamuru kwa habari za sadaka za kuteketezwa na dhabihu, siku ile nilipowatoa katika nchi ya Misri**; (23) lakini naliwaamuru neno hili, nikisema, Sikilizeni sauti yangu, nami nitakuwa Mungu wenu nanyi mtakuwa watu wangu; mkaende katika njia ile yote nitakayowaamuru mpate kufanikiwa. (24) Lakini hawakusikiliza, wala kutega sikio lao, bali walikwenda kwa mashauri yao wenyewe, na kwa ushupavu wa mioyo yao mibaya, wakaenda nyuma wala si mbele. Yeremia 7:22-24

Hili linaonekana kupingana kabisa. Nabii Yeremia anaandika kwa muongozo ya kuwa Mungu hakuwaagiza Waisraeli kuhusu sadaka ya kuteketezwa na dhabihu. Lakini maandiko ya Musa yanapeana amri nyingi kuhusu hili.

> Bwana akanena na Musa, na kumwambia, (2) Haya, nena na wana wa Israeli, uwaambie, Kama mtu ye yote akifanya dhambi pasipo kukusudia, katika neno lo lote ambalo Bwana amelizuilia lisifanywe, na kutenda neno lo lote la maneno hayo; (3) kama kuhani aliyetiwa mafuta akifanya dhambi, hata analeta hatia juu ya watu; ndipo na atoe kwa ajili ya dhambi yake aliyoifanya, na kumsongeza kwa Bwana ng'ombe mume mchanga mkamilifu, kuwa ni sadaka ya dhambi. (4) **Naye atamleta huyo ng'ombe na kumweka mlangoni pa hiyo hema ya kukutania,** mbele za Bwana; naye ataweka mkono wake kichwani mwake ng'ombe, na kumchinja huyo ng'ombe mbele za Bwana. Walawi 4:1-4

> Kisha Bwana akanena na Musa, na kumwambia, (2) **Waagize hao wana wa Israeli, uwaambie, Matoleo yangu, chakula changu cha sadaka zangu zisongezwazo kwa moto, za harufu ya kupendeza kwangu mimi, mtaangalia kuzisongeza kwangu**

> **wakati wake upasao.** (3) Nawe utawaambia, Hii ndiyo sadaka isongezwayo kwa moto mtakayomsongezea Bwana; wana-kondoo waume wa mwaka wa kwanza wakamilifu, wawili kila siku, wawe sadaka ya kuteketezwa ya sikuzote.(4) **Mwana-kondoo mmoja utamsongeza asubuhi, na mwana-kondoo wa pili utamsongeza jioni;** Hesabu 28:1-4

Tunajikumbusha moja wapo ya hoja kuu za sura ya 21 ya kitabu hiki.

### … katika Agano la Kale au hali halisi, amri anazopeana ambazo ziko katika vita na maisha ya Yesu duniani zinatoa dhibitisho la kioo cha Uungu kazini.

Wacha turejee katika kipindi ambacho Mungu alimsogea Adamu katika Bustani ya Edeni. Mungu alimuuliza Adamu kama alikuwa amekula tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Adamu hatubu juu ya matendo yake, lakini badala yake anamshtaki Mungu kwa kusababisha tatizo. Adamu hagundui kuwa moyoni mwake kuna mbegu za mauaji. Kwa kutii ushauri wa nyoka, Adamu amekumbatia roho wa nyoka ambaye alikuwa muuaji tangu mwanzo. Yohana 8:44. Ili Adamu kutubu dhambi zake, alihitaji kuanza kufahamu kile alichokitenda kwa kula tunda.

Tulijadili ukweli huu katika sura ya 19 – *Alijeruhiwa kwa Makosa yetu.* Tunarudia hoja hii:

> Adamu na Hawa walipoanguka dhambini walikuwa kama asili ya Shetani. Kristo ambaye alikuwa ndani yao alichomwa na kupondwa kama meno yanayosaga mbegu.Ni roho ya Kristo ndani ya mwanadamu ambayo inampatia uhai. Yeye ndiye nuru ambayo imwangaziayo kila mtu anayekuja ulimwenguni, Yohana 1:9. Kama Kristo angelimuacha Adamu kabisa basi angefariki. Roho ya Kristo ndani ya Adamu ilipondwa lakini Kristo hakujitoa, ijapokuwa ilimletea maumivu makali kukaa.Katika mateso ya Kristo, mwamba, ulitowa maji ya kiroho yakumfanya Adamu aishi. *Agape,* Chapter 19, page 198, 199.

Adamu hakuwa anajua kuwa alikuwa na mbegu ya ukatili ndani yake. Hakufahamu kuwa matukio ya kusulubiwa kwa Kristo ambayo yangewekwa wazi miaka 4000 baadaye yalipata chanzo hiki ndani yake. Mungu

alimuonyesha Adamu tatizo lilikuwa nini ili Adamu afahamu hali yake ya kukata tamaa na kuitikia roho wa Kristo na kutubu.

mfumo wa kutoa dhabihu ulikuwa kioo cha yale watu wana hisi kuhusu Kristo. Mfumo wa kutoa dhabihu na shule kuu ya kuwaleta watu kwa Kristo, lakini kama tulivyoonyesha awali, watu wanaonyesha kioo hiki nyuma kwa Mungu na kuweka tabia zao juu yake. Hivyo basi karibu ulimwengu wote unaamini kuwa Mungu huhitaji dhabihu na kama matokeo watu kwa kujua au kwa kutoandika wanaamini kuwa Mungu alimuua Mwanawe.

Ibrahimu alilelewa Babeli – inchi ya Wakaldayo. Mwanzo 11:31. Alikulia katika utamduni wa kutoa kafara ya wanadamu. Kanuni ambayo ilikuwa imewekwa wazi katika Kaini alipomuua nduguye ilikuwa fadhila mahususi ya kila dini ya kipagani. Uchinjaji wa mamilioni ya wanyama na maelfu ya watu yote yanashinikiza kutoka kwa moyo mdanganyifu wa mwanadamu ukionyesha nyuma kwa Mungu hali ya ghadhabu yake mwenyewe. Badala ya kukubali kuwa dhabihu ni onesho lake mwenyewe na hali yake ya kujinyima, watu hugeuza dhabihu kama kitu kinachohitajika na Mungu ili kumridhisha.

> Naye Samweli akasema, je! Bwana huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu Sawasawa na kuitii sauti ya Bwana? Angalia, kutii ni bora kuliko dhabihu, Na kusikia kuliko mafuta ya beberu. 1 Samweli 15:22

Ibrahimu alikuwa amekosa kumwamini Mungu kuwa angempa mwana wa ahadi ayiyemtaka. Alimwomba Mungu kumkubali Eliezeri, mjakazi wake mwaminifu. Mwanzo 15:2. Kisha Ibrahimu akasikiliza pendekezo la mke wake la kupata mtoto kupitia kwa mjakazi wake Hagai, aliyemza Ishmaeli.

Ukosefu wao wa imani ulileta mazingira hasi ya familia, na Ibrahimu analazimika kumfukuza Hagai na Ishmaeli kutoka nyumbani kwake. Katika hali yake ya kukata tamaa Ibrahimu anagundua udhaifu wake. Jaribu la kutodhabihu ya kitu ili kumtuliza Mungu linaongezeka. Uzoefu wote wa utotoni, ukichanganyika na mbegu ya Adamu ya kuridhi udunia, ilimsukuma Ibrahimu kutafuta upatanisho kupitia kwa kutuliza.

Ni katika muktadha huu ambapo Mungu anaweka tatizo la Ibrahimu katika kioo. Amri inatolewa kama onesho la mawazo yake katika suala la kutuliza. Wakati huo huo tunagundua kwa makini kuwa Mungu hakika hakumwambia

Ibrahimu amuue mwanawe, Isaka. Mungu alimwambia amtoe Isaka kama sadaka ya kuteketezwa. Amri ilitoa uwezo wa kuisoma kwa njia mbili tofauti.

Yesu alipozungumza kwa Mwanamke aliyeomba bintiye aponywe, Yesu alisema “sio haki kuchukua chakula cha watoto na kukipa mbwa.”

Hakumwita mbwa.  Alinena wazo lililokuwa akilini mwa wanafunzi na alijua Wayahudi walifikiria kumhusu. Alimuelewa kuwa alisema kuwa alikuwa mbwa katika mwitikio wake, lakini aliweza kumwambia kwa urahisi kuwa alikuwa mtoto wa Mungu.

Jambo sawa linatendeka katika hadithi ya Ibrahimu. Mungu alimwambia Ibrahim utu kumtoa mwanawe kama sadaka ya kuteketezwa. Hakumwambia kwa uwazi kumuua mwanawe. Kwa kufikiria hili linaweza kuwa ni kwa Ibrahimu kufa moyo katika hamu yoyote ya mtoto iliyokuwa kinyume na mapenzi ya Mungu. Kwa sababu ya jinsi Ibrahimu alilelewa na kwa sababu ya mawazo yake ya kutuliza, Ibrahimu alielewa kuwa Mungu alitaka amuue mwanawe. Mungu alijua hili lingetendeka. Ilikuwa muhimu kuonyesha ndani ya Ibrahimu nusu ya ufahamu wa kuelewa kwake kwa kiwango cha kumuamini Mungu kabisa. Ni mwendo wa ajabu wa kumleta Ibrahimu katika Agano Jipya la imani katika roho na kweli, kupitia kwa utukufu wa Agano la Kale. 2 Wakorintho 3:7-9

> Ndipo malaika wa Bwana akamwita kutoka mbinguni, akasema, Ibrahimu! Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa. (12) Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee. (13) Ibrahimu akainua macho yake, akaangalia, na tazama, kondoo mume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka. Basi Ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo, akamtoa awe sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe. Mwanzo 22:11-13

Kama tutatoa katika hadithi hii kuwa Mungu hataki kutulizwa kupitia kwa kuwaua watoto wetu lakini badala yake kupitia kwa Mwanawe, basi bado tupo kwa ndani katika upagani sio mbali Sanaa kutolewa katika mfano wa Aztecs wa Merekani ya Kati. Tofauti tu ni Mwana wa nani Mungu anataka afe; kuwa Mwana wa Mungu anafaa zaidi na ni dhabihu ya thamani ikilinganishwa na dhabihu ya wapagani.

Hamu ya kumtuliza Mungu kupitia kwa kutoa dhabihu imekuwa ni huzuni daima kwa Mungu kwa karne. Hapendezwe na mtu kumtuliza kwa kuchinja wanyama.

> Nuhu akamjengea Bwana madhabahu; akatwaa katika kila mnyama aliye safi, na katika kila ndege aliye safi, akavitoa sadaka za kuteketezwa juu ya madhabahu. (21) Bwana akasikia harufu ya kumridhisha; Bwana akasema moyoni Sitailaani nchi tena baada ya hayo kwa sababu ya wanadamu, maana mawazo ya moyo wa mwanadamu ni mabaya tangu ujana wake; wala sitapiga tena baada ya hayo kila kilicho hai kama nilivyofanya. Mwanzo 8:20-21

kusoma fungu hili kwa juu kunamfanya mtu kufikiria kuwa Mungu anatulizwa na dhabihu. Harufu nzuri inayoingia katika pua la Bwana inamfanya kuahidi kuwa hatalaani ardhi tena. Ukweli ni kuwa neno *harufu* bila shaka ni neno *ruach*. Ni neno kuu ambalo kwalo kunapata neno Roho, au Roho wa Mungu. Neno hili linamaanisha:

> Mzizi usiosahilishawa mno; **kuvuma** vizuri**, yaani, pumzi;** pekee (sawasawa) kutoa harufu au (kwa maana tambua (kwa mfano tazamia, furahia): - kubali, harufu, X mguso, fanya ufahamu wa upesi.

Kupumua kunaweza kuwa ndani au nje. Kupumua nje kuna ashiria kupeana kitu. Kupumua ndani kuna ashiria kupokea kitu. Katika mwanzo wa fungu la 21 ni neno na. kiunganishi hiki hakipatikani kwa Kiebrania. Mungu hakutulizwa na dhabihu ya wanyama. Alikubali kutubu kwa Nuhu ambaye kupitia kwa kitendo hiki alikusudia kusema, “ najua kwamba sifai kwangu binafsi na nina hatia ya mauaji ya Mwanao.” Bwana kwa rehema zake anapuliza Roho wake juu ya dunia na rena ya neema yake inafanya kutuma uhai kujaa duniani. Tunaposoma Bibilia kwa nuru ya Kristo, vifungu hivi vyote vya utulizo wa giza vinaanza kung’a katika uso wa Kristo. 2 Wakorintho 4:6.

Kaini alichukua kanuni za ibada ya utulizo hata mbali zaidi kuelekea ibada ya maumbile. Aliondoa kondoo ambaye alikuwa mfano wa moyo wake wa mauaji na akapeana matunda na mboga. Katika kitendo hiki cha kutuliza Mungu, vitu vya ardhi vilikuwa mkombozi wake. Kaini aliongeza katika ibada hii mauaji ya nduguye na kwa hivyo mwanzo wa ibada ya kipagani ilianza. Katika ibada ya kipagani hili lilikuwa wazi kupitia kwa kuabudu katika mashamba ya miti ikijumuishwa na kafara ya watu. Aina hii ya ibada ilikuwa

huzuni ya *daima* au *kila siku* ya Mungu. Shetani alipotosha ukweli wa thamani sana uliokuwa umeundwa kufunzwa katika dhabihu na akawafanya watu kutafuta kumtuliza Mungu.

> Vunjeni kabisa mahali pote walipokuwa wakiitumikia miungu yao mataifa mtakayoyamiliki, juu ya milima mirefu, na juu ya vilima, na chini ya kila mti wenye majani mabichi; (3) nanyi zivunjeni madhabahu zao, zibomoeni nguzo zao, na maashera yao yateketezeni kwa moto, na sanamu za kuchonga za miungu yao zikateni; na jina lao lifutilieni mbali na mahali hapo. (4) Wala msimfanyie hivyo Bwana, Mungu wenu. Kumbukumbu 12:2-4

Njia ambayo Waisraeli wangeweza kuharibu pahali pa juu pa upagani ilikuwa kuondoa mawazo ya ibada ya kutuliza na kuruhusu Mungu kuwapulizia juu yao Roho wake (sio kunusa moshi kutoka kwa dhabihu zao).

Walidhani kuwa Mungu alikuwa kama mmoja wao tu; walidhani kuwa walikuwa wanampa Mungu kile alichoagiza: damu, ushahidi wa uhai uliotolewa dhabihu kuridhisha kiu ya Uungu. Lakini Mungu alisema angepeana damu.

> Kwa kuwa uhai wa mwili u katika hiyo damu; **nami nimewapa ninyi hiyo damu** juu ya madhabahu, ili kufanya upatanisho kwa ajili ya nafsi zenu; kwani ni hiyo damu ifanyayo upatanisho kwa sababu ya nafsi. Walawi 17:11

Kama wangeisikiza sauti ya Mungu, wangebomoa madhabahu haya yaliyoishi katika akili zao wenyewe.

> Ingawa tunaishi duniani lakini hatupigani vita kama ulimwengu ufanyavyo. (4) Silaha za vita vyetu si za mwili, **Bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome. (5) Tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu** na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo, 2 Wakorintho 10:3-5

Ushahidi kuwa Waisraeli hawakuepuka kikamilifu kanuni ya ibada ya kumtuliza inaoneshwa katika ukweli kuwa Mahali pa Juu palisalia Israeli karibu wakati wote, hata kwa wafalme wakamilifu machoni pa Bwana.

> **Sulemani** naye akampenda Bwana, akienda katika amri za Daudi babaye, ila hutoa dhabihu na **kufukiza uvumba katika mahali pa juu**. 1 Wafalme 3:3

> **Lakini mahali pa juu hapakuondoshwa**; ila moyo wake **Asa** ulikuwa mkamilifu kwa Bwana siku zake zote. 1 Wafalme 15:14

> Tena, wana wa Israeli wakafanya kwa siri mambo yasiyokuwa mema juu ya Bwana, Mungu wao, wakajijengea mahali pa juu katika miji yao yote, kutoka mnara wa walinzi hata katika miji yenye boma. (10) **Wakajisimamishia nguzo na maashera juu ya kila mlima mrefu, na chini ya kila mti wenye majani mabichi; (11) wakafukiza uvumba huko katika kila mahali pa juu, kama mataifa walivyofanya,** ambao Bwana aliwafukuza mbele yao; wakaunda mambo mabaya, ili wamkasirishe Bwana; (12) wakatumikia sanamu, ambazo Bwana aliwakataza, akasema, Msitende jambo hili. 2 Wafalme 17:9-12

Wafalme wawili walipaondoa pahali pa juu: Hezekia and Yosia.

> **Alipaondoa mahali pa juu, akazibomoa nguzo, akaikata hiyo** Ashera; akaivunja vipande vipande ile nyoka ya shaba aliyoifanya Musa; maana hata siku zile wana wa Israeli walikuwa wakiifukizia uvumba; naye akaiita jina lake Nehushtani 2 Wafalme 18:4

> **Na nyumba zote pia za mahali pa juu palipokuwa katika miji ya Samaria,** wafalme wa Israeli walizozifanya, ili kumkasirisha Bwana, Yosia aliziondoa, akazitenda kwa mfano wa mambo yote aliyoyatenda katika Betheli. 20 Akawaua na makuhani wote wa mahali pa juu waliokuwako huko, juu ya madhabahu, akateketeza mifupa ya watu juu yake; kisha akarejea Yerusalemu. 2 Wafalme 23:19-20

Kitabu cha sheria pia kilipatikana katika utawala wa Yosia na wakaanza tena kuzishika sheria na kuhifadhi sherehe za Bwana. 2 Mambo ya Nyakati 35:1. La kuhuzunisha, Yosia alikufa katika vita dhidi ya mfalme wa Misri na Waisraeli wakarejerea upagani tena katika ibada yao. Muda mfupi baada ya hili walipelekwa mateka katika nchi ya Babeli. Hamu ya Waisraeli ya kuabudu miungu ya kutulizwa karibu nayo inawekwa wazi katika maono ya Ezekieli.

> Akanileta mpaka ua wa ndani wa nyumba ya Bwana, na tazama, mlangoni pa hekalu la Bwana, kati ya ukumbi na madhabahu,

> **walikuwako watu kama ishirini na watano, wamelipa kisogo hekalu la Bwana, na nyuso zao zimeelekea upande wa mashariki, nao wanaliabudu jua, kwa kuuelekea upande wa mashariki**. Ezekieli 8:16

Ni mshangao kidogo kuwa kama taifa la Israeli na hasa viongozi wao walishikwa mateka kwa kuabudu jua kama mataifa ya kipagani ambayo hatimaye wangeshikwa mateka halisi na mataifa ya kipagani. Wakiwa katika mateka ya Babeli, Danieli anaomba kuelewa kitakachotendeka kwa watu wa Mungu. Katika maono ya Danieli sura ya saba anaona mfululizo wa wanyama wachafu wakitoka baharini kutawala ulimwengu. Watu wa mungu wanadhulimiwa na kuteswa na falme hizi zinazotawala. Watu wa Mungu wanatawanywa kwa kuteswa huku, lakini haya yanatendeka kwa sababu ya Waisraeli kukataa kupaondoa pahali pa juu pa ibada ya misingi ya kutuliza na kutubu tu kwa ajili ya dhambi zao na kukubali haki ya Mungu katika Masihi.

> Tena ikiwa baada ya hayo yote hamtaki kunisikiza, bali mwaenenda kwa kunishikia kinyume; (28) ndipo nami nitakwenda kwa kuwashikia ninyi kinyume katika ghadhabu yangu; **nami nitawaadhibu mara saba kwa dhambi zenu**. (29) Nanyi mtakula nyama ya miili ya wana wenu, na nyama ya miili ya binti zenu mtaila. (30) **Nami nitapaharibu mahali penu palipoinuka, na kuziangusha sanamu zenu za jua,** nami nitaitupa mizoga yenu juu ya mizoga ya sanamu zenu; na roho yangu itawachukia. (31) Nami nitaifanya miji yenu iwe maganjo, na **mahali penu patakatifu nitapatia ukiwa;** wala sitasikia harufu ya manukato yenu yapendezayo. (32) Nami nitaitia hiyo nchi ukiwa; na adui zenu watakaokaa huko wataistaajabia. (33) **Nanyi nitawatapanya-tapanya katika mataifa,** nami nitaufuta upanga nyuma yenu; na nchi yenu itakuwa ni ukiwa, na miji yenu maganjo. Walawi. 26:27-33

Ni zaidi ya wigo la kitabu hiki kujishugulisha na mara saba inayotajwa hapa lakini haina uhusiano wa unabii kwa urejesho wa injili ya kweli kwa watu wa Mungu.

Ulikuwa mpango wa Mungu Israeli kuwa kiongozi wa mataifa na kuwa mataifa yaliyoizunguka yangekuja Israeli kujifunza kuhusu Mungu wa kweli na njia zake. Kama tu wangeisikia sauti yake na kutambua agano la milele na kugeuka kutoka kwa theolojia yao ya kutuliza. Hakungehitajika kuwa na hizi

falme kuu za kipagani kuinuka kwa njia ambayo ziliinuka. Falme hizi zilikuwa ni ukuzaji wa moyo wa dhambi wa mwanadamu ili kwamba wanadamu watambue dhuluma na ukatili wa njia za mwanadamu.

> Tangu mwaka wa kumi na tatu wa kutawala kwake Yosia, mwana wa Amoni, mfalme wa Yuda, hata siku hii ya leo, miaka hii ishirini na mitatu, neno la Bwana limenijia, nami nimesema nanyi, nikiamka mapema na kusema; lakini ninyi hamkusikiliza. (4) **Naye Bwana ametuma kwenu watumishi wake wote, hao manabii, akiamka mapema na kuwatuma, lakini ninyi hamkusikiliza, wala hamkutega masikio yenu, msikilize.** (5) Akasema, Rudini sasa, kila mtu na aiache njia yake mbaya; uacheni uovu wa matendo yenu, mkae katika nchi ambayo Bwana aliwapa, ninyi na baba zenu, tangu zamani za kale na hata milele; (6) wala **msiwafuate miungu mingine, ili kuwatumikia na kuwasujudia, wala msinikasirishe kwa kazi ya mikono yenu; basi, mimi sitawadhuru ninyi kwa dhara lo lote. (7) Lakini ninyi hamkunisikiliza, asema Bwana; ili mnikasirishe kwa kazi ya mikono yenu, na kujidhuru nafsi zenu.** (8) Basi Bwana wa majeshi asema hivi, Kwa kuwa hamkuyasikiliza maneno yangu, (9) angalieni, nitapeleka watu na kuzitwaa jamaa zote za upande wa kaskazini, asema Bwana, nami nitatuma ujumbe kwa Nebukadreza, mfalme wa Babeli, mtumishi wangu, nami nitawaleta juu ya nchi hii, na juu yao wakaao ndani yake, na juu ya mataifa haya yote yaliyopo pande zote; nami nitawaangamiza kabisa, na kuwafanya kitu cha kushangaza, na kitu cha kuzomewa, na ukiwa wa daima. Yeremia 25:3-9

Falme nne zilizoinuka katika maono ya Danieli zilikuwa, Babeli, Waamedi na Wajemi, Ugiriki, na Roma. Falme hizi zote zilikuwa na hekalu la kuabudu ambamo dhabihu ilitolewa mbele ya miungu. Kati ya vita vya shetani dhidi ya Mungu ni propaganda ya daima ya kutuliza kupitia kwa dhabihu. Dhabihu yao ilitolewa kila siku. Kimeandikwa juu ya silinda ya Cyrus (538 -529BC) ni maandishi yanayozungumza kuhusu dhabihu yao ya kila siku kwa miungu yao.

> "**Kila siku** alipanga na katika uadui, aliruhusu sadaka ya mara kwa mara kutolewa; aliteua - alianzilisha katika mji." Imenukuliwa katika F.L Sharp, *Antiochus or Rome,* page 40.

Nukuu hii inataja wakati ambao sadaka zilidakizwa. Hili linatwambia kuwa walikuwa na dhabihu za kila siku kama sehemu ya huduma yao. Danieli alipoendelea kushangaa juu ya maisha ya mbeleni na kuteswa kwa watu wake alishangazwa hadi kwa kiwango cha kufa moyo, akiwa kwenye maono alisikia viumbe wawili wakizungumza:

> Na katika moja ya pembe hizo ilitokea pembe ndogo, iliyokua sana, upande wa kusini, na upande wa magharibi, na upande wa nchi ya uzuri. (10) Nayo ikakua, kiasi cha kulifikilia jeshi la mbinguni; ikaangusha chini baadhi ya jeshi lile, na ya nyota, ikazikanyaga. (11) Naam, ikajitukuza **hata juu yake aliye mkuu wa jeshi hilo, ikamwondolea sadaka ya kuteketezwa ya daima, na mahali pa patakatifu pake pakaangushwa chini** (12) Na jeshi likatolewa kwake pamoja na sadaka ya kuteketezwa ya daima, kwa sababu ya makosa; nayo ikaiangusha kweli hata chini; ikatenda ilivyopenda, na kufanikiwa. (13) Ndipo nikamsikia mtakatifu mmoja akinena, na mtakatifu mwingine akamwuliza huyo aliyenena, **Haya maono katika habari ya sadaka ya kuteketezwa ya daima, na lile kosa lifanyalo ukiwa, yataendelea hata lini, kukanyagisha patakatifu na jeshi?** (14) Akamwambia, Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa. Danieli 8:9-14

Hatutamani kukwamishwa katika undani wote wa kifungu hiki. Hoja muhimu tunayotaka kutoa hapa ni kuwa mfumo wa kila siku wa kuabudu kama ulivyofanywa na wapagani ungetupiliwa mbali katika umbo lake la kipagani na kubadilishwa na kuenziwa katika mfumo wa Kikristo. Nguvu zilizojitokeza katika anguko la ufalme Roma zilichukua dhabihu ya Kristo na kuipa sura ya kwa lugha ya adhabu ya badala. Sadaka ya Kristo ingetolewa ulimwenguni kama kituliza cha Mungu mwenye hasira ambaye alihitaji adhabu ya kifo. Hii ndio sehemu ambayo sio ngumu kuielewa. Ujumbe wa injili ambao unahubiriwa katika makanisa mengi kwa kweli unavyanzo vyake katika mwongozo wa dhana za kipagani za ibada.

Danieli alipokuwa akitafakari kitisho cha kutendeka kwa mambo haya alizidiwa.

> Na maono ya hizo nyakati za jioni na asubuhi yaliyosemwa ni kweli; lakini wewe yafunike maono hayo; maana ni ya wakati ujao baada ya siku nyingi. (27) **Na mimi, Danielii, nikazimia, nikaugua siku**

> **kadha wa kadha; kisha nikaondoka, nikatenda shughuli za mfalme; nami naliyastajabia yale maono, ila hakuna aliyeyafahamu.** Danieli 8:26-27

Alipokuwa akitafuta ufahamu wa jinsi haya yatatendeka, Malaika Gabrieli alitumwa kwa Danieli kumwelezea zaidi kuhusu maono ya awali. Gabrieli kwanza anampa Danieli pahali pa kuanzia pa unabii kuhusu majuma sabini yatakayoleta Masihi mwana wa Mfalme. Kisha Gabrieli anasema jambo muhimu sana:

> Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja; **na kwa nusu ya juma hiyo ataikomesha sadaka na dhabihu; na mahali pake litasimama chukizo la uharibifu;** na hivyo, hata ukomo, na ghadhabu iliyokusudiwa imemwagwa juu yake mwenye kuharibu. Danieli 9:27

Fungu hili linazungumza juu ya kazi ya Kristo duniani. Kwa kifo cha Yesu, dhabihu ya wanyama haikuwa tena sehemu ya ibada ya kumwabudu Mungu. Kristo alipokufa, pazia la hekalu lilipasuka katikati hivyo kuonyesha mwisho wa mfumo wa kutoa kafara halisi.

Hata hivyo, kuna maana ya ndani ya kifungu hiki ambayo haijaeleweka na wengi. Tunajua kuwa baada ya Yesu kufa msalabani, kafara ya wanyama ilizidi kutolewa hata kama haikuwa na umuhimu. *Ukweli wa ndani wa kazi ya Yesu ni kuwa, kukomesha kutolewa kwa dhabihu sio jambo la kuonekana tu*. <u>Ukweli wa msalaba utakapoeleweka kwa usahihi basi kanuni za theolojia ya kutuliza zitakoma mioyoni mwa waumini.</u> Wakati ukweli, agano la milele litafahamika, watu wataacha kumkaribia Mungu kupitia kwa mtindo wa dhabihu ya kumtuliza. Huu ni ukweli wa ndani wa maana ya fungu kuwa *atafanya dhabihu na matoleo kukoma*. Neno ndogo *kwa* linaweza fasiriwa *dhidi*. Wakati agano la milele linapendwa kikamilifu kabisa basi theolojia ya kutuliza itakoma, na ukweli wa thamani utatenda kinyume cha kuenea kwa machukizo yaliyoifanya injili ukiwa wa tabia ya kweli ya Mungu ya upendo. Kitabu kinaweza andikwa tu juu ya jambo hili lakini uhusiano uko wazi. Ufahamu wa kweli wa msalaba utafichua na kushinda machukizo yanayoleta ukiwa.

Leo hii watu wengi wanapozungumza kuhusu msalaba wa Kristo, wanazungumza katika muktadha wa ghadhabu ya Mungu kuridhishwa. Mawazo haya hupelekea kwenye machukizo ambayo huufanya moyo ukiwa.

Hisia yoyote ambayo mtu anayo kwa Mungu inafanywa ukiwa kisiri wanaporuhusu wazo kuwa Mungu anaweza ua Mwanawe ili kuridhisha hasira yake. Nafsi inaachwa kame na mawazo kuwa Mungu angeweza kutunga amri ya kifo ambayo kuuawa kwa Mwanawe tu kungeiridhisha. Mafunzo ya Katoriki ni maelezo kamili ya mfumo huu wa kutuliza. Kwa kuhudhuria Misa aghalabu kila Jumapili, ukiungama dhambi zako kwa kuhani wa duniani, ukiamini katika utatu, na kutegemea uhalali wa watakatifu wa Katoriki, unaweza epuka ghadhabu ya Mungu ya moto wa jahanamu ya milele.

Ukweli ni huu tu:

Dhabihu na sadaka inakomeshwa kwa kweli kwa wale ambao Masihi anathibitisha agano.

Ondoleo rahisi la dhabihu ya mnyama katika ndani yake haiondoi hamu ya kumtuliza Mungu kupitia dhabihu hizi. Kama Ibrahimu, leo tunasikia sauti ikituita tukiwa karibu kutia kisu ndani ya uhusiano wetu bora kabisa tukidhani kuwa hili litamtuliza Mungu.

Kwa maana wahubiri wote wa injili wanaozitoa familia zao kuhubiri ujumbe wanahisi wameitwa kushiriki, isikie sauti – " sihitaji kutulizwa! Matendo yako katika kuhubiri hayakulipia dhambi zako. Taaluma yako ya toleo la mafundisho yanayosababisha haja ya kutenga wengine kama wazushi wa kubaguliwa na kuhukumiwa kunaweza koma."

Baba yetu wa mbinguni anataka tuwe huru kwa mawazo yetu ya kipagani. Anataka tuamini kwa kweli kuwa anatupenda – anatupenda upendo wa agape. Hakuna chochote tunaweza fanya au sema ili kumfanya atupende zaidi ya vile anavyotupenda. Soma mawazo haya ya kupenya ya mtunzi wa Kikristo:

> Wazo la suluhu au dhabihu ni kuwa kwamba kuna ghadhabu inayo tulizwa. Lakini zingatia hoja kuwa ni sisi ambao tunahitaji dhabihu, na wala sio Mungu. Hutupa dhabihu. Wazo kuwa ghadhabu ya Mungu lazima isuluhishwe ili kwamba tuweze kupata msamaha halipati idhini yoyote katika Bibilia. Ni upuuzi wa juu kusema kuwa Mungu ameghadhabika sana na watu na hawezi kuwasamehe ila tu wametoa kitu cha kutuliza ghadhabu yake, na kwa hivyo yeye

> mwenyewe hutoa karama yeye mwenyewe, ambayo kwayo anatulizwa…
>
> Wazo la kilimwengu, ambalo mara nyingi linashikiliwa na wale wanaojiita wakristo, ni kuwa watu lazima watoe dhabihu kutuliza ghadhabu ya mungu wao. Ibada yote ya kimataifa na hongo kwa miungu yao ili kuwapendelea…
>
> Mateso yaliyotendwa kwa inchi za walioitwa wakristo kwa wakati uliopita na hata kwa kisi hadi sasa, ni miinuko tu ya wazo hili la kipagani la suluhu. Viongozi wa kikanisa wanadhani kuwa wokovu ni kwa matendo na kuwa watu kwa matendo wanaweza kulipia dhambi, na kwa hivyo wanamtoa yule ambaye wanamfikiria ni muasi kama kafara kwa mungu wao wala sio kwa Mungu wa kweli, kwa sababu hatulizwi kwa dhabihu kama hiyo. E. J Waggoner, *Present Truth*, Aug 30, 1894.

Kama sisi ni waaminifu na tunaona ukweli wa tabia ya Baba yetu ya upendo, itaanza kuzua hisia ya ndani ya maana ya kutubu.

> Maana nataka fadhili wala si sadaka; na kumjua Mungu kuliko sadaka za kuteketezwa. Hosea 6:6

Mfumo wa dhabihu ya kutuliza ni moja wapo ya sehemu ya mwisho katika ulinzi wa mwanadamu dhidi ya kukubali majukumu yetu ya kujiunga na shetani na malaika wake katika mauaji ya Mwana wa Mungu. Tutakapovuka mpaka wa mwisho hili ndilo litakalo tendeka.

> Nami nitawamwagia watu wa nyumba ya Daudi, na wenyeji wa Yerusalemu, roho ya neema na kuomba; nao watamtazama yeye ambaye walimchoma; nao watamwombolezea, kama vile mtu amwombolezeavyo mwanawe wa pekee; nao wataona uchungu kwa ajili yake, kama vile mtu aonavyo uchungu kwa ajili ya mzaliwa wake wa kwanza. Zakaria 12:10

Uchungu wa nafsi kuwa Adamu angetoa dhabihu kwa Mungu kwa mwitikio wa dhambi yake, leo unaweza kuwa wetu katika nuru ya tabia ya upendo wa Mungu. Mungu hahitaji dhabihu ya kumtuliza na sadaka ili kumridhisha. Hii ndiyo dhabihu ambayo huhitaji:

> Dhabihu za Mungu ni roho iliyovunjika; Moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu, hutaudharau. Zaburi 51:17

> Maana yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele; ambaye jina lake ni Mtakatifu; asema hivi; Nakaa mimi mahali palipoinuka, palipo patakatifu; tena pamoja na yeye aliye na roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao waliotubu. Isaya 57:15

Kama uko tayari kuyachunguza maandiko kwa makini katika mwanga wa kanuni za kitabu hiki, utapata ukweli wa maneno ya Yesu kwa Philipo:

> Yesu akamjibu, "Filipo, nimekaa nanyi muda huu wote hata usinijue? Mtu ye yote aliyeniona Mimi, amemwona Baba… Yohana 14:9

kwangu mimi binafsi, ni furaha kuu kuamka kila asubuhi na fikira ya upendo tefu wa Baba wa Mbinguni. Naguswa kwa ndani kwa kuwa amekuwa tayari kumtuma Mwanawe ili kutuonyesha jinsi alivyo kwa kweli. Licha ya hatari kuwa wanadamu wangefurukuta kila kitu, Yesu alikuja kwa kujitolea kutuonyesha Baba na kuwa tuweze kujua kwamba yeye sio adui yetu; Ni Baba yetu, Baba yetu wa thamani apendaye wanawe. Hakuna lugha inayoweza kueleza kina cha upendo wake wa kujikana nafsi- upendo wa Agape kwetu.

Nitumaini langu kuwa tutajumuika pamoja kuingia patakatifu pa amani kamilifu na kusikia maneno haya yote kwa utimilifu wake.

> Nayo sauti kutoka mbinguni ikasema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa, ambaye ninapendezwa sana naye." Mathayo 3:17
>
> Kwa hiyo tunamsifu Mungu kwa huruma zake kuu alizotumiminia kwa sababu sisi ni wa Mwanae Mpendwa. Waefeso 1:6

Ndani ya kila mmoja wetu ni hamu ya Amani, utulivu na dhibitisho la kupendwa. Ni jinsi gani jamii ya mwanadamu inaweza ukaribia uhalisia huu? Na maendeleo haya yote katika teknolojia ulimwengu wetu yanaingia ndani zaidi katika ubinafsi na ukatili.

Maisha ya Kristo ambaye alitembea duniani miaka 2000 iliyopita yanatupa mfano wa upendo wa kujikana nafsi ambao umeleta amani kwa mamilioni yasiyohesabika. Kwa watu wengi upendo huu mzuri huangamizwa na hata kuharibiwa na hadithi nyingi ambazo zimenakiliwa katika kurasa za Bibilia zikielezea uhusiano wa Mungu na watu katika historia yote ya mwanadamu.

Mungu wakati mwengine huonekana kuwa mkatili kabisa na muuaji aamuruye sio tu kifo cha majeshi ya adui  bali pia watoto wao wachanga. Huonyesha kwa utaratibu wa kuogofya kuwa amekasirika na kujawa na ghadhabu. Zaidi ya hili kifo cha msalaba ni kwa wengi kuchafuliwa na mawazo kuwa Mungu huhitaji kifo kwa wale wanaomuasi.

Kwa walio na mvuto kwa neno la Mungu, tofauti kati ya maelezo ya Mungu na maisha ya Kristo imesababisha baadhi ya madai ya Yesu kuwa gumu Zaidi kutatua. Ila katika kipindi fulani akinena kwa mmoja wa wafuasi wake Yesu alisema, "Iwapo umeniona umemwona Baba."

Hili linawezekanaje? Inaweza kuwa ukweli kuwa Mungu kwa kweli ni mwenye huruma, neema na ukarimu kama inavyodhihirishwa katika maisha ya Yesu? utata huu unaweza tatuliwa katika kusalia waaminifu kwa neno la Andiko? Unashikilia mikononi mwako ufunguo wa kufungua after hii.